Hakimiliki © Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

KUWAWEZESHA VIONGOZI WA KANISA

▪AFRIKA MASHARIKI▪

MARKO—SEHEMU YA 1

Mwandishi

Jonathan M. Menn

B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., Kornell Law School, 1977
M.Div., Trinity Evangelical Divinity School, 2007

Equipping Church Leaders-East Africa
3701 N. Gillett St., Appleton, WI 54914
(920) 731-5523
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

2021

Wanazuoni wengi wanafikiri Marko ndiyo injili ya kwanza kuandikwa. Baba wa imani Papias anataja uandishi wa kitabu hiki kuwa wa Marko, na anasema taarifa zake alizipata kutoka kwa Petro mtume. Hilo halikutiliwa shaka na kanisa la kwanza, na hata taarifa mbalimbali zinaonesha hivyo. Kitabu hiki ni cha kivitendo. Ni moja ya injili zenye kufanana (synoptic) zingine zikiwa ni pamoja na Mathayo na Luka, kwasababu injili hizi tatu zina simulizi nyingi zinazofanana, katika mtiririko ule ule, na mara mara kwa kutumia maneno yale yale. Ingawa ndicho kitabu kidogo kuliko injili zingine, mara nyingi kinatoa simulizi za kina, zenye desturi za Kiyahudi zilizotolewa maelezo kwa ajili ya Wamataifa wasomaji. Marko anaonesha jinsi Yesu anavyotimiza unabii wa AK wa Masihi ajaye na, kama Marko anavyoeleza katika mistari ya kwanza kabisa ni, “Mwana wa Mungu.”

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

I. Utangulizi……... 2

A. *Mwandishi*…….. 2

B. *Tarehe*……. 2

II. Muundo na Mukhtasari…… 2

A. *Muundo* …….. 3

B. *Mukhtasari* ……. 3

C. *Sehemu za mada* …… 3

III. Ufafanuzi wa Marko ……. 5

1:1-8: Mwanzo wa Injili na Yohana Mbatizaji**…….... 5**

1:9-13: Ubatizo wa Yesu na kujaribiwa kwake na Shetani**…… 9**

1:14-15: Kutangazwa kwa Ufalme**…….. 11**

1:16-20: Kuitwa kwa wanafunzi wa kwanza**…… 13**

1:21-45: Uponyaji na kutoa pepo**……. 14**

2:1-12: Yesu amponya aliyepooza**…… 18**

2:13-17: Kuitwa kwa Lawi**…….. 22**

2:18-22: Yesu na Kufunga: umuhimu wa Kristo**……. 28**

2:23-28: Kula Masuke siku ya Sabato**……. 30**

3:1-6: Yesu anaponya siku ya Sabato**…….. 31**

3:7-12: Yesu anaponya wengi wenye kuonewa na walio na pepo wachafu**…….. 32**

3:13-19: Kuchaguliwa kwa Kumi na Wawili**…….. 33**

3:20-35: Kutokuamini, upinzani, na familia ya kweli ya Kristo**…….. 34**

4:1-34: Yesu anafundisha kwa mifano**…….. 39**

4:35-41: Yesu atuliza bahari**…… 42**

5:1-20: Yesu anamponya Mgerasi mwenye pepo**…….. 44**

5:21-43: Binti Yairo na mwanamke mwenye kutokwa na damu**……. 46**

6:1-6: Yesu wa Nazarethi**……. 49**

6:7-13, 30-32: Kumi na wawili wanatumwa na kurudi**……. 51**

6:14-29: Hatma ya Yohana Mbatizaji**…….. 53**

6:33-44: Yesu awalisha 5000 **……..... 55**

6:45-56: Yesu anatembea juu ya maji na kuponya kule Genesareti**……..... 56**

7:1-23: Mapokeo na kinachomtia mtu najisi**……. 58**

7:24-37: Yesu anamponya binti wa Msirofoinike na kiziwi**…… 61**

8:1-10: Yesu awalisha 4000 **…….. 64**

8:11-21: Mafarisayo wanataka ishara na wanafunzi hawaelewi**…….. 66**

8:22-26: Yesu amponya kipofu**……..... 68**

BIBLIOGRAFIA……. 68

MWANDISHI…….. 73

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

I. Utangulizi

A. *Mwandishi*

Marko, kwa jina lingine katika Biblia anajulikana kama "Yohana ambaye pia aliitwa Marko" (**Mdo 12:12, 25; 15:37**). Alikuwa kijana wa kiume wa mwanamke maarufu aliyeitwa Mariamu wa Yerusalemu (**Mdo 12:12**), kwasababu watu wengi walikuwa wamekusanyika katika nyumba yake wakati Petro alipokuwa amefungwa kule Yerusalemu, na Petro alifika hapo baada ya kutolewa gerezani kimiujiza (**Mdo 12:1-19**). Pia alikuwa mjomba wa Barnaba (**Kol 4:10**), ambaye pia alikuwa mtu mwenye kipato (**Mdo 4:36-37**). Marko aliambatana na Paulo na Barnaba katika safari ya kwanza ya kimishenari (**Mdo 13:5, 13**) lakini akawaacha, na kupelekea Paulo kumkataa katika safari yake ya pili ya kimishenari, na kusababisha kutengana kwa Paulo na Barnaba (**Mdo 15:36-40**). Baadaye Paulo na Marko wanaelewana. Marko alikuwa na Paulo wakati wa kufungwa kwake kule Rumi kwa mara ya kwanza (**Flm 24; Kol 4:10**), na Paulo kipekee alituma Marko aje wakati wa kufungwa kwake Rumi kwa mara ya pili (**2 Tim 4:11**).

Katika *Historia yake ya Kikanisa,* Eusebius anasema hivyo kuhusiana na uandishi wa injili ya Marko: "Kuhusiana na hili mzee mmoja wa kanisa pia alisema: Marko, baada ya kuwa mkalimani wa Petro, aliandika kwa usahihi, ijapo siyo kwa mtiririko, kila alichoweza kukumbuka ambacho Kristo alisema na kutenda. Kwasababu hakuwahi kumsikia Bwana wala kumfuata lakini baadaye, kama nilivyosema, alimfuata Petro, ambaye aliyaleta mafundisho yake kwa namna iliyoweza kugusa mahitaji ya wasikilizaji wake, lakini akiwa hana nia ya kutoa moja kwa moja mafundisho ya Bwana kama yalivyokuwa, hivyo Marko hakufanya kosa lolote kwa kadiri alivyoyakumbuka. Kwasababu alikuwa makini kwa jambo moja, asiache lolote kati ya yale aliyokuwa amesikia, asije akatoa maelezo yeyote ya uongo. "Mambo haya yanahusiana na maelezo ya Papias kuhusu Marko." (Eusebius 1890: 3.39.15) "Mzee" hapa yawezekana ni mtume Yohana, ambaye kutoka kwake Papias (Askofu wa Hierapolis) alijifunza.

"Kwamba Marko aliandika Injili ya pili kwa kushawishiwa na Petro, au kama kumbukumbu ya yale aliyosikia kutoka kwake, ni mapokeo ya jumla ya zamani. . . . Justin mfia dini anataja Injili ya Marko kwa jina la "kumbukumbu . . . ya Petro" (*Dial. c. Tryph.* 106)." (Ibid.: 2.15n.390). Irenaeus, Tertullian, Clement wa Alexandria, Origen, na mababa wengine wa kanisa wanathibitisha kuwa Marko ndiye mwandishi wa Injili ya Marko na kwamba alikuwa na uhusiano wa karibu na Petro (Carson and Moo 2005: 173). Ushahidi fulani wa ndani ya Injili ya Marko unaonesha hivyo, ikiwa ni pamoja na: umaarufu wa Petro katika kitabu; na nuru ya msimamo mkali wa kipekee ambayo mitume, na hasa Petro alikuwa nayo (ambayo inaashiria kuwa ni mtume Petro tu ndiye aliyekuwa na msimamo huo mkali); ukweli kwamba Injili ya Marko inafuata mtindo unaofanana na ule unaoonekana katika ujume wa Petro katika **Mdo 10:36-41**; na ukweli kwamba katika **1 Pet 5:13** Petro anamuita Marko *"mwanangu",* hayo huonesha uhusiano wa karibu kati yao.

Mapokeo mengi ya kanisa yanaonesha kuwa, baada ya kifo cha Petro na Paulo kule Rumi, Marko alielekea Alexandria, Misri, akaanzisha kanisa huko, na kuleta watu wengi kwa Kristo, na aliuwawa huko katika mwaka wa 68 BK (McBirnie 1973: 254-57; Eusebius 1890: 2.16.1n.394).

B. *Tarehe*

Injili ya Marko imepachikwa tarehe za miaka ya 40, 50, 60, na 70 BK (angalia pia Carson and Moo 2005: 179-82). Mjesuit wa kispanish kasisi wa kikatoliki, mtaalamu wa magombo ya zamani na msomi wa maandiko ya Biblia, Jose O'Callaghan Martinez, alidai kuwa vipande vya namna ya karatasi za zamani (papyrus) vilivyopatikana kule Qumran miongoni mwa magombo yaliyovumbuliwa katika bahari ya chumvi vilikuwa ni sehemu za Injili ya Marko. Kama ndivyo, namna hizo za karatasi za zamani, "zilizokubaliwa kwa kutumia njia za kisayansi kwamba zimekuwepo katika maktaba kule Palestina mwaka wa 50 BK., zinaonesha kuwa Injili ya Marko inaweza kuwa ilishakuwepo karibu miongo kadhaa baada ya kifo cha Yesu" (McBirnie 1973: 251). Wasomi wengi hupinga madai ya O'Callaghan (Carson na Moo 2005: 179-80; "Jose O'Callaghan Martinez" 2021: 7Q5). Matokeo yake, wasomi wengi hukipa kitabu cha Marko tarehe kuanzia katikati ya miaka ya 50 hadi 60 BK.

II. Muundo na Muhtasari

D. A. Carson na Douglas Moo wanaonesha umuhimu wa Marko kama mwandishi wa Injili hii: Marko ndiye mtengenezaji wa Injili hii katika muundo wa kifasihi—akichanganya mada za kiwasifu na zile za [kimahubiri] (kerygmatic) ambazo kwa ukamilifu zinawasilisha hisia za maana ya upekee wa mhusika katika historia ya binadamu, Yesu wa Nazarethi, mwana wa Mungu. Njia mpya za kuangalia maandiko ya Marko zimeonesha ufundi na nguvu ya Marko kisimulizi. . . . Kwa kuwakumbusha wakristo kwamba wokovu wao unategemea kufa na kufufuka kwa Kristo, Marko hatenganishi imani ya kikristo na uhalisia wa matukio ya

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kihistoria." (Carson and Moo 2005: 192)

A. ***Muundo***

Kama ilivyooneshwa hapo juu, mpangilio wa Marko unaenda sambamba na mahubiri ya Petro katika **Mdo 10**:

Mdo 10	Marko
"habari njema" (**mst. 36**)	"mwanzo wa habari njema" (**1:1**)
"Mungu alimpaka mafuta Yesu wa Nazarethi kwa Roho Mtakatifu" (mst**. 38**)	Kuja kwa Roho Mtakatifu juu ya Yesu (**1:10**)
"akianzia kule Galilaya" (**mst. 37**)	Huduma kwa Wagalilaya (**1:16–8:26**)
"Alizunguka huko na huko akitenda mema na kuwaponya wote waliokuwa wameonewa na ibilisi" (**mst. 38**)	Huduma ya Yesu ilikazia uponyaji na kutoa pepo (**1:16–8:26**)
"Sisi ni mashahidi wa kila kitu alichofanya . . . kule Yerusalem" (**mst. 39**)	Huduma kule Yerusalemu (sura ya **11-14**)
"Walimuua kwa kumtundika msalabani" (**mst. 39**)	Mkazo ni katika kifo cha Kristo (sura **15**)
"Mungu alimfufua kutoka kwa wafu siku ya tatu" (**mst. 40**)	"Amefufuka! Hayuko hapa" (**16:6**)

Muundo wa kitabu chenyewe unaweza kugawanywa katika sehemu kuu mbili kama ifuatavyo:

Utangulizi (**1:1-13**): Yahana mbatizaji; ubatizo wa Yesu; Yesu kujaribiwa na shetani kule jangwani.
Huduma ya wazi kule Galilaya (**1:14–8:26**): kuitwa kwa wale kumi na wawili; mafundisho; miujiza na uponyaji; mkazo ni katika upekee wa Yesu
Kuelekea Yerusalemu na kuendelea (**8:27–16:20**): kutabiri kwa kifo chake, ufufuo, na kurudi kwake mara ya pili; kubadilika; mafundisho na uponyaji; huduma kule Yerusalemu; kusalitiwa, kukamatwa, kusulubiwa, kuzikwa na kufufuka

B. ***Muhtasari***

Kitabu cha Marko kimsingi kinaweza kugawanywa katika sehemu mbili: **1:1–8:26** na **8:27–16:20**. Sehemu hii ya nusu ya kwanza inakazia huduma ya Yesu kule galilaya, ikiwa ni pamoja na kutangaza ufalme, kuwachagua wanafunzi wake kumi na wawili, huduma na kifo cha Yohana mbatizaji, na mafundisho ya Yesu na miujiza, ambayo yanaleta upinzani kutoka kwa viongozi wa dini na kutokuamini miongoni mwa wengi, lakini pamoja na hayo yanasaidia kujibu swali *"Huyu basi ni nani?"* (**4:41**).

C. ***Sehemu za kitabu***

Kitabu hiki kinaweza kuwekwa katika sehemu zifuatazo:

I. Utangulizi (1:1-13)
- **A.** Huduma ya Yohana Mbatizaji (**1:1-8**)
- **B.** Ubatizo wa Yesu (**1:9-11**)
- **C.** Kujaribiwa na Shetani (**1:12-13**)

II. Huduma ya Yesu Galilaya (1:14–8:26)
- **A.** Kutangaza ufalme (**1:14-15**)
- **B.** Kuita wale kumi na wawili (**1:16-20**)
- **C.** Uponyaji na kutoa pepo (**1:21-45**)
  1. Yesu anafundisha katika sinagogi na kumponya mtu aliyekuwa na pepo (**1:21-28**)
  2. Anamponya Mkwe wa Petro (**1:29-31**)
  3. Anaponya watu wengi waliopagawa na pepo na wagonjwa (**1:32-34**)
  4. Yesu anahubiri kule galilaya (**1:35-39**)
  5. Kuponywa kwa Mkoma (**1:40-45**)
- **D.** Kupingwa kwa Yesu kunaanza na kupata nguvu (**2:1-3:6**)
  1. Yesu anamponya aliyepooza (**2:1-12**)
  2. Kuitwa kwa Lawi (Mathayo) (**2:13-17**)
  3. Yesu na kufunga: umuhimu wa Kristo (**2:18-22**)
  4. Yesu na Sabato (**2:23–3:6**)
     a. Kula masuke siku ya Sabato (**2:23-28**)
     b. Yesu anaponya siku ya Sabato (**3:1-6**)
- **E.** Yesu anawaponya wengi waliokuwa hawawezi na wenye pepo wachafu (**3:7-12**)

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

F. Kuchaguliwa kwa kumi na wawili (**3:13-19**)
G. Kutokuamini, upinzani, na familia ya kweli ya Kristo (**3:20-35**)
1. Familia ya kidunia ya Yesu wanafikiri ana wazimu (**3:20-21**)
2. Waandishi wanamtuhumu Yesu kuwa amepagawa na pepo (**3:22-30**)
3. Kristo anabainisha familia yake ya kweli (**3:31-35**)
I. Yesu anafundisha kwa mifano (**4:1-34**)
1. Mfano wa mpanzi na aina za udongo (**4:1-20**)
2. Kilichofichika kitafunuliwa, na kwa kipimo upimacho utahukumiwa (**4:21-25**)
3. Mfano wa mbegu, kukua, na mavuno (**4:26-29**)
4. Mfano wa mbegu ya haradali (**4:30-34**)
J. Yesu atuliza bahari (**4:35-41**)
K. Kutoa pepo na uponyaji (**5:1-43**)
1. Mgerasi mwenye pepo (**5:1-20**)
2. Binti Yairo na mwanamke aliyetokwa damu (**5:21-43**)
L. Yesu kule Nazareth (**6:1-6**)
M. Wale kumi na wawili wanatumwa na kurudi (**6:7-13, 30-32**)
N. Hatma ya Yohana Mbatizaji (**6:14-29**)
O. Miujiza: kulisha watu 5,000; Yesu kutembea juu ya maji; na uponyaji (**6:33-56**)
1. Kulishwa 5000 (**6:33-44**)
2. Yesu kutembea juu ya maji (**6:45-52**)
3. Uponyaji kule Genesareti (**6:53-56**)
P. Mapokeo na utambulisho wa watu (**7:1-23**)
1.Yesu anapingana na Mafarisayo juu ya mapokeo (**7:1-13**)
2. Yesu anasema kuwa unajisi unatoka ndani (**7:14-23**)
Q. Anatambulisha huduma kwa mataifa (**7:24–8:10**)
1. Kumtoa pepo binti wa mama Msirofoenike kule Tiro (**7:24-30**)
2. Uponyaji wa Kiziwi Dekapoli (**7:31-37**)
3. kulishwa watu 4000 Dekapoli (**8:1-10**)
R. Kujaribiwa, kutokufahamu, na uponyaji (**8:11-26**)
1. Mafarisayo wanaomba ishara (**8:11-13**)
2. Wanafunzi washindwa kuelewa (**8:14-21**)
3. Kuponywa kwa mtu kipofu (**8:22-26**)

III. Utambulisho wa Yesu na hatma yake vinafunuliwa (**8:27–9:13**)
A. Yesu ndiye Masihi (Kristo) (**8:27-30**)
B. Yesu atauwawa lakini atafufuka tena (**8:31-33**)
C. Gharama ya uanafunzi (**8:34-38**)
D. Kugeuka sura (**9:1-13**)

IV. Njia ya kwenda Yerusalemu (**9:14–14:9**)
A. Uponyaji wa kimiujiza wa kijana aliyepagawa na pepo (**9:14-29**)
B. Mafundisho kuhusu kifo chake/ufufuo, uanafunzi, na talaka (**9:30–10:16**)
1. Yesu atabiri kufa na kufufuka kwake (**9:30-32**)
2. Nani mkuu katika Ufalme (**9:33-37**)
3. Asili ya uanafunzi (**9:38-50**)
4. Yesu anafundisha kuhusu talaka (**10:1-12**)
4. Yesu abariki watoto wadogo (**10:13-16**)
C. Mtawala kijana tajiri (**10:17-31**)
D. Mafundisho kuhusu kifo chake/ufufuo na uanafunzi (**10:32-45**)
1. Kwa mara nyingine Yesu anatabiri kufa na kufufuka kwake (**10:32-34**)
2. Yakobo na Yohana wanataka kupewa kipaumbele (**10:35-40**)
3. Asili ya uanafunzi wa kweli na msingi wa kupata kipaumbele (**10:41-45**)
E. Kuingia Yerusalemu (**10:46–11:11**)
1. Yesu amponya Batimayo kipofu akiwa njiani kuelekea Yerusalem (**10:46-52**)
2. Kuingia Yerusalemu kwa msafara wa ushindi (**11:1-11**)

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

V. Huduma ya Yesu kule Yerusalemu (**11:12–13:37**)
- **A.** Dalili za umasihi wa Yesu (**11:12-26**)
  1. Kulaani mtini (**11:12-14, 20-26**)
  2. Kufukuza wabadilishaji wa pesa hekaluni **1:15-19**)
- **B.** Mamlaka ya Yesu, mifano, na mafundisho (**11:27–12:44**)
  1. Kutiliwa shaka asili ya mamlaka ya Yesu (**11:27-33**)
  2. Mfano wa wakulima wa mizabibu (**12:1-12**)
  3. "Mpe Mungu yaliyo ya Mungu" (**12:13-17**)
  4. Ufufuo na ndoa katika ufufuo (**12:18-27**)
  5. Amri iliyo kuu (**12:28-34**)
  6. Kristo ndiye Bwana (**12:35-37**)
  7. Maonyo dhidi ya unafiki wa waandishi (**12:38-40**)
  8. senti mbili ya mjane (**12:41-44**)
- **C.** Mafundisho katika mlima wa mizeituni (**13:1-37**)

VI. Maandalizi ya kufa; Kusalitiwa; kusulubiwa; na kufufuka (**14:1–16:20**)
- **A.** Yesu apakwa marhamu ya gharama (**14:1-9**)
- **B.** Yuda kumsaliti Yesu (**14:10-11**)
- **C.** Chakula cha mwisho cha jioni (**14:12-31**)
- **D.** Katika Bustani ya Gethsemane (**14:32-42**)
- **E.** Kusalitiwa kwa Yesu na kukamatwa (**14:43-52**)
- **F.** Kushtakiwa mbele ya Sanhedrin na Pontio Pilato (**14:53–15:20**)
  1. Sanhedrin (**14:53-72**)
  2. Pontio Pilato (**15:1-15**)
  3. kudhihakiwa na askari (**15:16-20a**)
- **G.** Kusulubishwa na kuzikwa (**15:20b-47**)
- **H.** Kufufuka (**16:1-8**)
- **I.** Kuonekana baada ya kufufuka (**16:9-20**)

III. Ufafanuzi wa Marko

1:1-8: ***[1]Mwanzo wa Injili ya Yesu kristo, Mwana wa Mungu. [2] Kama ilivyoandikwa katika Isaya nabii, " Tazama, namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakayeitengeneza njia yako, [3]sauti ya mtu aliaye nyikani: 'Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake,'" [4] Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi. [5] Wakamwendea nchi yote ya uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao. [6] Na Yohana alikuwa amevaa singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake, akala nzige na asali za mwitu. [7] Akahubiri akisema, Yuaja nyuma yangu aliye na nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuinama na kuilegeza gidamu ya viatu vyake. [8] Mimi naliwabatiza kwa maji, bali yeye atawabatiza kwa Roho mtakatifu."***

mst. 1-8—Mwanzo wa Injili na Yohana Mbatizaji

Injili ya Yesu kristo—ni nani na alikuja kufanya nini—ametabiriwa mamia ya miaka mingi katika AK. Katika sehemu hii, Marko anabainisha jinsi nabii hizo zilivyotimia.

1. **mst. 1—**Injili

"Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, mwana wa Mungu" ina maanisha kwamba hii ni habari ya uzinduzi wa Injili, lakini mwisho wake bado haujafika. Yesu anazungumzia wakati wa mwisho huo (kurudi mara ya pili kwa Kristo katika **Marko 13** (mara nyingi huitwa hotuba katika mlima wa mizeituni). Matokeo yake, **mst. 1** unaweza ukaonekana kama unaorejea au kichwa cha habari cha kitabu chote. Kwa upande mwingine, R. A. Guelich anaonesha kuwa "kanuni ya kawaida ya kiyahudi katika kunukuu mambo ya kiroho, 'kama ilivoandikwa na,' . . . mara zote inaunganisha kile kilichotangulia na kile kinachofuata" (Guelich 1992: 513). Kwa maneno mengine, **mst 1** haukupaswa uishie na kituo bali koma. Matokeo yake, kwa kuwa ahadi ya Isaya inataja kuja kwa Yohana mbatizaji, "mwanzo" unaweza kutazamwa kama "hatua ya mwanzoni ya huduma" ya Yesu, ikiwa ni pamoja na huduma ya Yohana Mbatizaji, kubatizwa kwa Yesu, kujaribiwa kwake na Shetani kule jangwani, na labda mahubiri yake ya mwanzoni katika **1:14-15** (angali Carson na Moo 2005: 169; Guelich 1992: 513). Sehemu iliyosalia ya *"Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu"* inakuwa basi ni simulizi kuhusu

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

Yesu katika sehemu iliyobakia ya kitabu.

Injili ni *"Injili ya Yesu Kristo."* Hakutangaza tu Injili bali yeye aliivaa injili: Yesu *ndiye* Injili. Neno "Injili" lenyewe ni neno la Kigiriki (*euaggelion*) lenye maana ya "habari njema" (Danker 2000: *euaggelion,* 402; Green na McKnight 1992: 282). "Neno la Kigiriki 'Injili' (ev-angelion) lilitofautisha ujumbe wa Wakristo na ule wa dini zingine. 'Ev-angel' lilikuwa na maana ya tukio kubwa la kihistoria, kama vile ushindi katika vita au kushika nafasi kwa mfalme mpya, kulikobadilisha hali ya wasikilizaji na kutaka muitikio wao. Kwahiyo Injili ni habari za kile ambacho Mungu ametenda katika kutufikia. Siyo ushauri kuhusu nini tunalazimika kutenda ili kumfikia Mungu." (Keller n.d.: "The Gospel," 1) Kwa maneno mengine, injili inahusu Yesu ni nani na nini ametenda.

Kipekee, Mungu ni mtakatifu, mwenye haki, na mwema (**Mwa 18:25; Kut 34:6-7; Law 11:44; Ayubu 34:10-12; Zab 5:4; 136:1; 145:17; Hab 1:13; Rum 1:18; Yak 1:13**). Ijapo wanadamu wa kwanza (Adam na Ev) waliumbwa bila dhambi, walichagua kumfuata Shetani na kumuasi Mungu na hivyo wakapata asili ya dhambi (**Mwa 3:1-19**). Matokeo yake, kila mwanadamu tangu wakati wa adamu na eva amekuwa akizaliwa katika hali ya uharibifu wa kimaadili unaojulikana kama dhambi ya ndani; dhambi hii ya ndani ni "sheria" au nguvu itendayo dhambi ndani ya kila mtu (**Rum 7:5, 8-11, 14-24; Gal 5:17; Ebr 3:12-13**). Inapelekea hali ya dunia yote kutambua kadiri watu wanavyoendelea katika maisha. (**Mwa 8:21; Zab 51:5; 143:1-2; Yer 17:9; Mrk 7:20-23; Rum 3:9-18, 23; 5:12-14; 7:14-24**). Biblia kwa usahihi inatuelezea matokeo ya hili: *"mshahara wa dhambi na mauti"* (**Rum 6:23;** angalia pia **Mwa 2:17; Ezek 18:4, 20; Rum 5:12**). Kwa kuwa Mungu ni matakatifu, hawezi kuvumilia dhambi (**Hab 1:13; Rum 1:18**). Mungu pia ni wa haki: "Kutokana na hali yake ya utakatifu na asili ya ukamilifu Mungu hawezi kugeuzia mgongo uharibifu wa mwanadamu kitabia, kana kwamba si kitu kwake . . . Kama Mungu atabakia katika hali yake ya asili ya dhambi, makosa yote yapasa yaadhibiwe." (Alexander 2008: 130, 131)

Kama wanadamu watakaa katika hali inayokubaliwa na Mungu na kufurahia uzima wa milele, dhambi yao lazima ishughulikiwe. Hili linazalisha tatizo kubwa. Kwasababu Mungu mwenyewe ni mtakatifu na mkamilifu, hicho ndicho kipimo anachotupimia (**Mat 5:48**). Matatizo ya wanadamu ni kwamba hatuwezi kamwe kufikia kiwango cha Mungu cha utakatifu na ukamilifu kwa nguvu zetu wenyewe. Kwanza, "mtu akisha tenda dhambi, hawezi tena kamwe kuwa mkamilifu." (Sproul 2002: 94). Pili, hata matendo yetu mazuri yamechafuliwa na dhambi. Hakika, kama tunatenda matendo mema ili tuepuke adhabu ya Mungu na kuzimu, hilo peke yake hufanya matendo yetu mema kuwa *kutokuwa "*mema" kwasababu kama msukumo wetu ni kuepuka kuzimu kwa kufanya "matendo mema" basi matendo hayo, kwa maana yake halisi, ni ya kibinafsi, na kujiangalia kibinafsi, jambo ambalo ni dhambi. Tatu, hakuna kiasi cha matendo mema kinachobadilisha asili ya dhambi na udhaifu wa moyo mwenye dhambi. Hivyo, matendo mema hayabadilishi uharibifu, wenye dhambi kuwa wenye haki, wasio na dhambi; ndani yao kabisa wanabakia wenye dhambi. Hata hivyo, Mungu ni wa upendo na hataki yeyote aangamie (**Ezek 18:23; 33:11; 2 Pet 3:9; 1 Yh 4:8**).

Injili ni habari njema kwamba Mungu ametutendea kile ambacho tusingeliweza kutenda wenyewe. Mungu alifanyika mtu katika Yesu Kristo. Yesu aliishi maisha tuliyopaswa kuishi *kama mtu*; alimtii Mungu Baba kwa ukamilifu katika kila jambo; *"alijaribiwa katika mambo yote kama tunavyojaribiwa, wala hakutenda dhambi"* (**Eb 4:15**). Hilo lilimpa nafasi ya kustahili kuwa mwakilishi wetu, kuchukua dhambi yetu na kuadhibiwa adhabu ambayo tulipaswa kulipa lakini tusingeweza (**Rum 8:1-4; 2 Kor 5:21; Gal 3:13; Kol 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; 1 Pet 2:24**). Wakati huo huo, Yesu alikuwa Mungu. "Hivyo basi Mungu hakuweka maumivu kwa mwingine, bali pale msalabani yeye mwenyewe aliyabeba maumivu, ukatili, na uovu wa dunia. . . . Huyu ni Mungu aliyefanyika mtu na kutoa damu ya uhai wake ili kuheshimu haki ya kimaadili na upendo wa rehema ili aweze kuharibu uovu wote bila kutuharibu sisi. . . . Kwanini *ilikuwa* ni lazima Yesu afe ili kutusamehe sisi? Kulikuwa na deni la kulipwa—Mungu mwenyewe alililipa. Kulikuwa na adhabu ya kupokea—Mungu mwenyewe aliipokea. . . . Msalabani haki wala rehema havikupotea—Vyote vilitimizwa kwa pamoja. Kifo cha Yesu kilikuwa cha lazima kama Mungu angechukulia haki yake kama ilivyo na bado audhihirishe upendo wake kwetu." (Keller 2008: 192-93, 197) Kufufuka kwa Yesu kutoka kwa wafu na kupaa kurudi kwa Baba kulithibitisha Yesu ni nani na kile alichofanya ndiyo kitovu cha injili. Marko analiangazia hili katika kitabu chake chote.

Marko pia anaanza kwa kuweka wazi kwamba Yesu Kristo ni *"Mwana wa Mungu."* John Carter anasema, "Mada ya msingi ya kitheolojia katika injili ya Marko inajikita katika kumueleza Yesu kama mwana wa Mungu, aliyethibitishwa na Baba (1:11, 9:7), na mapepo (3:11, 5:7), na jemadari wa kirumi (15:9), na Yesu mwenyewe (13:32; 14:36, 61-62). Nguvu ya kimamlaka ya Mwana wa Mungu inadhihirishwa katika mamlaka ya mafundisho yake (1:22, 27), nguvu zake za kuponya magonjwa na ulemavu (1:30-31, 40-42; 2:3-12; 3:1-5; 5:25-34; 7:31-37; 8:22-26; 10:46-52), Nguvu yake kamili juu ya nguvu za kipepo (1:23-27; 5:1-20; 7:24-30; 9:17-27), nguvu zake juu ya asili (4:37-39; 6:35-44, 47-52; 8:1-10), na mwisho, nguvu zake juu ya mauti (5:21-

24, 35-43). Marko alitumia ushuhuda wa kutoka kwa mtu wa kwanza (ambaye inaaminika alikuwa ni Petro) kuthibitisha kwamba kwa nguvu hizi ufalme wa Mungu umewajia watu katika Yesu Kristo. Muitikio pekee unaoweza kukubalika kwa maarifa kama hayo lazima uwe kumwendea Yesu kwa imani." (Carter 2003: 7-8)

2. **mst. 2-3—**Nukuu kutoka Malaki na Isaya

Mistari 2 unanukuu **Mal 3:1 na mst. 3** unanukuu **Isa 40:3**. Injili ya Marko inatofautiana na injili ya Mathayo na Luka katika jambo hili kwamba, tofauti na injili hizo haanzi na orodha ya uzao wa kibinadamu. Tofauti na Yohana ambaye pia hataji "uzao" wa kiungu wa Yesu. Badala yake, Marko mara moja huanza na kile ambacho tungeweza kukiita "uzao wa injili", yaani, anaacha kila kitu ambacho siyo muhimu kwa kusudio lake lakini anatangaza kwamba *"huu ndio mwanzo wa injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu"* na halafu anaonesha namna injili ya Yesu Kristo ilivyotabiriwa katika AK. Marko anasema kwamba maneno ya **Mal 3:1** na **Isa 40:3** yanatimizwa kwa ujio wa Yohana Mbatizaji. Kadhalika, **Mat 3:3; Lk 3:4** inatumia **Isa 40:3** kwa Yohana Mbatizaji. Yohana Mbatizaji mwenyewe alitambua kwamba alikuwa akitimiza **Isa 40:3**, kwasababu katika **Yh 1:23** ananukuu mstari huo kuwa unamhusu.

Katika **Mat 11:10; Lk 7:27** Yesu mwenyewe alitumia **Mal 3:1** kwa yohana Mbatizaji na kumlinganisha na Eliya ambaye alitabiriwa kuwa angekuja kabla ya *"siku ya bwana iliyo kuu na ya kutisha"* (**Mal 4:5;** angalia **Mat 11:14; Mk 9:11-13;** angalia pia **Lk 1:17**). Mavazi ya Yohana Mbatizaji yalifanana na ya Eliya (linganisha **Mk 1:6** na **2 Fal 1:8**). Kama kutimizwa kwa **Mal 3:1** na **Isa 40:3** na kama Eliya aliyetabiriwa, inaweza usemwa kuwa Yohana Mbatizaji alikuwa nabii wa mwisho wa manabii wa AK. Hata hivyo, kutimizwa kwa unabii wa AK na ule wa kutangaza kuwa Masihi amekuja, kulishika nafasi ya mpito ya kuingia katika AJ (angalia **Mat 11:9-13; Lk 16:16**).

Huduma ya Yohana Mbatizaji ilikuwa jangwani, na nukuu kutoka katika **Isa 40:3** inamtaja mpaza sauti *"nyikani."* "Kwa Isaya, jangwani kunakuwa mahali pa kuanzia mwanzo mpya. Jangwa la Isaya ni kinyume cha jangwa la Sinai. Jangwa la Sinai kulikuwa mahali pa uasi, kushindwa, kufa kwa Mwana wa Mungu Israeli. Lakini katika Isa. 40 na sura zinazoendelea, jangwani ni mahali pa shangwe, utele, uhai na baraka kwa Israeli wa Mungu. Katika Isa. 40, jangwa linakuwa mahali pa kuanzia kutoka, kwa watu wa Mungu. . . . Sasa, katika Mk. 1:2-4, Yohana Mbatizaji anaonekana kuashiria uzinduzi mpya wa kutoka ulioonesha na Isaya. . . . Hapa, katika Yesu, ndiyo Israeli wa Mungu ambaye anaweza kuingia jangwani na kuinyamazisha laana ya dhambi. Hapa, katika Yesu, ndiye Israeli wa Mungu ambaye anaweza kutamalaki jangwani na kuteka mateka vitu vya yule mwenye nguvu. Jangwani, Israeli huyu hatashindwa kwa kutokuamini, huyu Israeli hatatamani nyama za Misri; Huyu Israeli hatamtumikia mwingine isipokuwa Mungu peke yake." (Dennison 1994: n.p.) Hivyo, licha ya kutumia **Mal 3:1** na **Isa 40:3** kumuunganisha Yohana Mbatizaji, sehemu muhimu zaidi ya mwanzo wa injili ya Marko ni kumtambulisha Yesu Kristo (**mst. 1**) kuwa ndiye *"Bwana"* (**mst. 3**), yaani, ndiye Mungu mwenyewe.

3. **mst. 4-8—**Huduma ya Yohana Mbatizaji

Mistari 4 unasema *"Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi."* Jangwa, toba, na ubatizo vyote ni vitu vinavyotuelekeza kwa Yesu na Injili.

- Jangwani palikuwa mahali ambapo Mungu huwaleta watu wake kuzindua kizazi kipya (**Isa 35:1-10; Hos 2:14-23**).
- Neno la Kigiriki la "toba" ni *metanoia,* ambalo lina maana ya kubadili nia na muelekeo kutoka katika maovu na kugeukia mema, kutoka dhambini na kumgeukia Mungu (Zodhiates 1992: *metanoia,* 970-72). Toba inatarajiwa kujidhihirisha yenyewe katika kubadilika kwa mwenendo. (**Mdo 26:20**). Yohana mwenyewe aliliweka wazi hili alipowaambia watu waliomjia *zaeni matunda yapasayo toba"* **Mat 3:8; Lk 3:8**) na alitoa mifano halisi ya kile alicho maanisha (**Lk 3:10-18**). Michael Spencer anasema kwamba toba iliyohubiriwa na Yohana Mbatizaji "ilikuwa tendo la kuanza maisha upya katika uhalisia mkuu wa ufalme uliokuwa unawakaribia. Hakuna chochote katika yale ambayo Mungu huwataka watu wake katika ufalme ambacho ni kubadilika kidogo au kubadili upande wa pili wa jani.' Huku ni kubadilika kabisa kunakojikita katika kila kitu ndani ya ufalme unaokaribia na kufanya kila maamuzi kutokana na mtazamo huo wa ufalme. Ukristo wa kisasa unahitaji kukumbuka kile anachohubiri Yohana tunapofikiria Yesu anataka nini kwa wafuasi wake." (Spencer 2008: The Forerunner)
- Ubatizo unamaanisha kusafishwa. **Ezek 36:25** inasema, *"nitawanyunyizia maji safi, nanyi mtakuwa safi mbali na uchafu wenu wote, na mbali na vinyago vyenu vyote."* Ubatizo pia una maana pia ya kifo cha maisha ya kale na mwanzo wa maisha mapya (**Rum 6:3-4**). Ubatizo, tofauti na taratibu za kutahiriwa za Agano la Kale, hufungua njia mpya ya kutakaswa na maisha mapya kwa wote—wanawake na wanaume—wote sawa. Spencer anaonesha, "Ubatizo haukuwa kitu ambacho Wayahudi wangeweza kukifikiria kwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

wepesi. Waongofu wa kiyahudi walibatizwa na Wayahudi wengine. . . . Alichowaitia Yohana kilikuwa ni hatua ya unyenyekevu halisi kwa Wayahudi waliokuwa na kiburi: kushushwa hadi katika nafasi ya waongofu. Kuja kama wageni, kama mtu mchafu na asiyesafika. Njia ya kuingia katika ufalme ni njia ya unyenyekevu kuanzia mwanzo." (Spencer 2008: The Forerunner) Hata hivyo, ni wazi kwamba "Yohana analiona hili kama kutakaswa kwa maji kunakotangulia kusafishwa/ kujazwa/kuoshwa na kitakasa chenye nguvu zaidi kuliko vyote-Roho Mtakatifu wa Mungu. Mistari 8 unaonesha kwamba ubatizo wa maji siyo mwisho, lakini kibao cha kutuelekeza, picha ya uhalisia ulio mkubwa zaidi na wenye kina.." (Ibid.)

Sehemu yote hii ya huduma ya Yohana Mbatizaji inamuonesha akijikita kwa yule aliyekuwa anakuja baada yake na ufalme ambao Yesu atauzindua. Hili linaonekana katika uhalisia wa jangwani, toba, na ubatizo tuliozungumzia hapo juu. Kwa nyongeza, Yohana mwenyewe alisema kwamba *"Baada yangu anakuja mwenye nguvu zaidi kuliko mimi, ambaye sistahili kumwinamia na kulegeza gidamu za viatu vyake"* (**Mk 1:7**) na *"mimi nawabatiza kwa maji, lakini yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu"* (**Mk 1:8**). Mahali pengine, anasema, *"Ni lazima yeye [Kristo] aongezeke, na mimi lazima nipungue"* (**Yh 3:30**). Kwa maneno Mengine, kusudi kuu la Yohana lilikuwa ni kutoa suti nzuri ambaye Yesu ataiitikia na kuipa maneno ya maisha yatakayoimbika, kifo na ufufuo." (Ibid.)

MASWALI YA KUJADILI

1. Neno "Injili" kimsingi lina maana ya "habari njema" ni "habari njema" gani za Yesu zinazozungumziwa hapa?

2. Yesu anatajwa kama "Mwana wa Mungu." Maneno haya yanaweza yakachukuliwa yanamaanisha nini kwa wasioamini Mungu yupo au mtu asiye na uhakika wowote wa uwepo wa Mungu? Kwa mtu wa kizazi kipya? Kwa Yesu mwenyewe?

3. Kwa kuzingatia nuru ya mistari kadhaa katika sura ya 1, kwanini unafikiri kwamba Marko hakuingiza uzao wa Yesu, tofauti na injili zingine mbili za Mathayo na Luka?

4. Yohana mbatizaji ameitwa na baadhi ya watu "mtu wa mwisho wa Agano la Kale." Kwa upande mwingine, inaweza kusemwa kwamba ni "mtu wa kwanza wa Agano Jipya." Unajua nini hasa kuhusu Yohana Mbatizaji? Siyo tu katika kitabu cha Marko, lakini katika Biblia yote, kuna mifanano mingi ya kuvutia (na tofauti pia) kati ya Yohana Mbatizaji na Yesu–ni nani, watu wa namna gani, walisema na kufanya nini. Tengeneza orodha mbili: moja ya mifanano; nyingine ya tofauti zao.

5. "Toba" ni nini (**mst. 4**)?

6. "Ubatizo" kama ibada au desturi ulikuwa wa kipekee mno na muhimu katika huduma ya Yohana Mbatizaji kiasi kwamba, ni tofauti na yeyote katika Biblia, anajulikana na kutambulishwa na tendo hilo (hata hivyo, anaitwa "Yohana mbatizaji"). Umuhimu wa ubatizo uliendelezwa na Yesu ambaye aliwaagiza wanafunzi wake *"kufanya wanafunzi kwa mataifa yote, mkiwabatiza kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu"* (**Mat 28:19**). Ubatizo una umuhimu na nafasi gani, na ni kwa njia gani muhimu unatofautiana na desturi iliyokuwepo ya Kiyahudi ya kutahiriwa?

7. Unafikiri nini kuhusu msimamo mkali wa Yohana Mbatizaji kuhusu mavazi, chakula na mtindo wa maisha ulikusudiwa kufundisha nini?

8. Ni kwa njia gani Yohana Mbatizaji anadhihirisha roho na kanuni ya Injili katika maneno aliyosema na alivyoishi?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

1:9-13: ***9 Ikawa katika siku zile, Yesu alikuja kutoka Nazareth ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani. 10 Mara alipopanda kutoka majini , akaona mbingu zinapasuka, na Roho, kama hua, akishuka juu yak; 11 na sauti ikatoka mbinguni, wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe." 12 Mara Roho akamtoa aende nyikani. 13 Akawako huko siku arubaini, hali akijaribiwa na shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu, na malaika walikuwa wakimhudumia.***

mst. 9-13—Ubatizo wa Yesu na kujaribiwa kwake na Shetani

Kabla ya Marko kuandika kumbukumbu yeyote ya maneno ya Yesu, kwa kifupi anarudia kueleza ubatizo wa Yesu na kujaribiwa kwake na shetani kule jangwani. Matukio yote haya mawili yalikuwa ya kimfano. Mbali na mengine, matukio haya huonesha kwamba, Yesu—Masihi wa Israeli aliyeahidiwa na mwokozi wa ulimwengu—anahuisha tena historia ya Israeli na wanadamu, tofauti ikiwa kwamba Yesu anafaulu pale ambapo Israeli na Adamu walishindwa.

1. **mst. 9-11—**Ubatizo wa Yesu

Mathayo anatueleza kwamba Yohana alijisikia *"nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu" Lakini Yesu akajibu akamwambia, "kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote."* (**Mat 3:14-15**) Yohana alikuwa anaonyesha kuwa anatambua hali ya kutokuwa na dhambi ya Yesu, kwa kuwa ubatizo ulikuwa ni alama ya toba na kujitoa kwa Mungu na ufalme wake. Kwa kujinyenyekesha hadi kubatizwa, Yesu alikuwa anaachia hadharani kila kitu kwa Mungu. Zaidi ya hayo, ijapokuwa hakuwa na dhambi, kwa kukubali kubatizwa "Yesu asiye na dhambi alikuwa akijitambulisha kama mmoja wa waisraeli waliokuwa na dhambi ambao walihitaji kuungama dambi zao na kubatizwa. Kujitambulisha kama mmoja wao ikiashiria kujitambulisha kwake kikamilifu na wenye dhambi wote pale atakapozichukua dhambi zao msalabani." (Poythress 1991: 253) Wakati huo kwa nafasi ya juu kabisa *"atahesabiwa pamoja na wakosaji"* (**Isa 53:12**). Kama alivyoanzisha ubatizo kama alama ya nje kwamba tu wafuasi wake, Yesu alionesha utayari wake kuachilia taasisi zote za kiungu na kufanya kila kitu ambacho anataka tufanye.

Yohana Mbatizaji anaonesha kwamba alimbatiza Yesu ili kujihakikishia utambulisho wa kimasihi (**Yh 1:31**, *"Mimi mwenyewe sikumtambua, lakini kwa kusudi hili nalikuja nikibatiza kwa maji, ili apate kufunuliwa kwa Israeli"*). Ubatizo wa Yesu ulitumika kama kuwekwa wakfu huduma yake hadharani, utambulisho wake kama Masihi, na uhusiano wake na Mungu. Hilo linathibitishwa katika **mst. 10-11** inayosema *"Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka, na Roho, kama hua, akishuka juu yake. Na sauti ikatoka mbinguni, wewe ndiwe mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe."* Maneno hayo yana maana. Kwanza Mungu alitangulia kumuita Israeli "mwanawe" wakati wa kutoka misri (**Kut 4:22—***"Israeli ni mwanangu, mzao wa kwanza").* **Mat 2:15** ananukuu **Hos 11:1,** *"Kutoka huko nalimwita mwanangu"* na kuyahusisha na Yesu. Lugha hii inaonesha ni kiasi gani historia ya AK ya Israeli inavyoandikwa upya na Yesu. Ubatizo wa Yesu pia unaandika upya kuvuka Bahari ya shamu na mto Yordani (ambako ndiko alipobatiziwa), na kuingia katika nchi (**Kut 14:13-22; Yosh 3:14-17;** angalia **Mat 3:13-17; Mk 1:9-11; Lk 3:21-22; Yh 1:31-34**). Zaidi ya hayo, kutambulishwa kwa Yesu kama mtoto wa Mungu kunaonesha kuwa yeye anatimiza Agano la Daudi, Masihi, mpakwa mafuta, na mtumishi wa Bwana aliyetabiriwa (angalia **2 Sam 7:14; Zab 2:7; Isa 42:1; 52:13–53:12; Mdo 13:33**). Kupasuka kwa mbingu ni mwangwi wa lugha ya **Isa 64:1** (*"Laiti ungepasua mbingu na kushuka")* kama tulivyoona katika **1:1-3**, "kama Isa. 40 na Mal. 3 anavyoonesha matarajio yake ya kuja siyo mtu wa kimasihi tu, bali Mungu mwenyewe, kadhalika Isa. 64. Yesu hatambulishwi kama wakala tu wa Mungu, lakini kwa namna isiyo wazi kama uwepo halisi wa Yahwe." (Watts 2007: 122) Hapa Mungu ameshuka katika umbo la mtu-Yesu, na Roho na Baba wanamshuhudia Mwana. Lugha ile ile ya kupasua inatumika tena kuhusiana na kusulubiwa kwa Yesu wakati *"pazia la hekalu lilipopasuka vipande viwili, kutoka juu hadi chini."* (**Mk 15:38**). Kupasuka kwa mbingu (huduma ya hadharani ya Yesu).

Isa 61:1 Alisema kuwa Roho wa Bwana angekuja juu ya Masihi na kumpaka mafuta ya Huduma. Kupakwa huko kulidhihirishwa hadharani na Roho kushuka juu ya Yesu kama hua. Yesu alithibitisha kupakwa mafuta huko katika **Lk 4:18** (akinukuu **Isa 61:1**). Katika sauti iliyotoka juu, Mungu analeta pamoja vifungu kadhaa vya AK kumtambulisha Mwana; "Zab 2:7 inazungumza kuhusu mwana wa kifalme, Isa. 42:1 anazungumzia mtumishi anayempendeza Mungu atakayeteswa, na Mwa. 22:2 kuhusu Mwana mpendwa anayetolewa. Mada zote hizi za AK zinamzungumzia Yesu wakati huu." (Spencer 2008: The Baptism) Hivyo, ubatizo wa Yesu ni wa kimfano na una maana kubwa—unafunua utambulisho wake na kuonesha huduma yake. "Katika injili ya Marko, Mungu kuwa Mwana wa Mungu kunatangazwa na ufunuo wa ubatizo. Kimaigizo, kwa haraka—sauti, hua, mbingu kupasuka—yote yanatangaza kwamba sasa ufalme wa Mungu umefika; sasa, kuanzia wakati huu hapa Yordani, ufalme wa Mungu umefika; sasa, mwanzo wa mambo mapya umeanza—mwanzo mpya katika historia ya ukombozi kwa tukio—kuja—kwa mwana wa Baba. Kutoka kunatimizwa

katika Yesu; safari ya jangwani inakamilika katika Yesu; kupita katika maji kunatimia kaika Yesu. Hakika, ufalme wa kieskatolojia wa Mungu umekaribia." (Dennison 1994: n.p.)

Sehemu moja zaidi ya ubatizo wa Yesu*"Kutimiza haki yote"* ni kwamba ametimiza masharti ya kuingia katika ukuhani. Alikuwa kuhani kwa mfano wa Melkizedek (**Zab 110:4; Eb 5:8-10; 6:20**). Makuhani walitoa dhabihu kwa Mungu kwa niaba ya watu; Yesu mwenyewe alifanyika dhabihu kwa dhambi zetu (**2 Kor 5:21; 1 Pet 2:21**). Katika AK, kuhani alitakiwa kusafishwa kwa maji (**Kut 29:4; Law 8:6**) na kupakwa mafuta (**Kut 29:7; Law 8:12**). Ubatizo wake katika maji na kupakwa mafuta ya Roho Mtakatifu vinadhihirisha kwamba Yesu ametimiza masharti lakini kwa kina zaidi kuliko walivyofanya makuhani wa AK—hatimaye ubatizo wa maji ulikuwa ukiashiria kifo na ufufuo (**Rum 6:3-5**), na Roho mtakatifu ndiye uhalisia unaowakilishwa na mafuta ya kupakwa. Alihitaji pia kufikia umri wa miaka 30 (**Hes 4:3**; angalia **Lk 3:23;** Price 2018: n.p.).

2. **mst. 12-13—**Kujaribiwa na Shetani

Mara Roho akamtoa aende jangwani" (**mst. 12**). "Kuna picha inayooneshwa hapa kwa wakristo wote. Kwanza, kuna mahali pa utii. Kisha kuna Baraka ya kuhakikishiwa kuwa nimekuwa mtoto wa Mungu. Kisha kuna kutolewa na kwenda mahali pa kujaribiwa na kupimwa. Hii ni kazi ya Mungu kama ilivyo Baraka ya ubatizo. Marko anawaambia wasomaji wake wazi kwamba kupimwa kwao na majaribu ni sehemu ya uzoefu kama watoto wa Mungu. Yesu alipitia njia hiyo hiyo" (Spencer 2008: The Temptation)

Muunganiko huu kati ya majaribu ya Yesu na yetu ni wa kina kuliko hata mawazo ya Spencer yanavyoweza kuonesha. Yesu anaitwa "Adamu wa mwisho" na "mtu wa pili" katika **1 Kor 15:45, 47**. Katika kujaribiwa kwake, Yesu alikuwa anashika nafasi ile ile ya majaribu aliyokabiliana nayo Adamu katika bustani ya Edeni: Wote Adamu na Kristo walijaribiwa na Shetani. Adamu alijaribiwa akiwa katika bustani, Yesu alijaribiwa akiwa jangwani. Adamu alijaribiwa kwa tunda, alikuwa akilijaribu neno la Mungu, na alishawishiwa na kule kuwa kama Mungu (**Mwa 3:1-6**); Yesu alijaribiwa kwa mkate, alijaribiwa kumjaribu Mungu, na alijaribiwa kwa ushawishi wa kupewa ufalme na fahari yake (**Mat 4:1-10; Lk 4:1-12**). Kule bustanini, Adamu alikuwa amezungukwa na alitawala wanyama, Yesu alikuwa amezungukwa na wanyama wa porini. Adamu alishindwa katika kujaribiwa na Shetani, Yesu alishinda majaribu ya shetani. Kwasababu alishindwa, malaika walilinda njia ya kuufikia mti wa uzima ili Adamu asiweze kula kutoka kwake (**Mwa 3:24**); kwasababu Yesu alishinda, malaika walimhudumia (**Mk 1:13**).

Majaribu ya Adamu na Kristo ni vielelezo kwetu. Swala lililoko mbele ya Adamu, Kristo na sisi ni kujua neno la Mungu na kuchagua kama tutamfuata au la. Kitovu cha dhambi ya Adamu (na yetu) ni "uharibifu wa kile kilichokuwa chema katika kutumiwa kwa matamanio binafsi ya mwanadamu kwa kiumbe kumpuuza muumbaji. Uchaguzi wa kusikiliza sauti ya Mungu unafanyiwa biashara kwa faida binafsi" ukisukumwa na kujitegemea na matamanio ya kibinadamu. (Faro 2021: 116) Kwa kujaribiwa kama "Adamu wa mwisho" na "mtu wa pili," Yesu alikuwa akituonesha jinsi ya kushinda majaribu. Ufunguo ni kwamba, tofauti na Adamu na sisi, Yesu hakutenda kutoka katika matamanio yake lakini mara zote alitenda na kunena kulingana na mapenzi ya Baba (linganisha **Mwa 3:1-6; Mat 16:23; Mk 8:33** na **Mat 26:39; Mk 14:36; Lk 22:42; Yh 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14;10**). Kule jangwani, "ni mdhaifu kama tulivyo wadhaifu, na bado alipinga na kutuonesha jinsi ya kupinga. (Ef 6:10ff) Ushindi wake juu ya kila jaribu ni tumaini kwa kila mtu anayeomba kutoka katika mashindano yaliyopo." (Spencer 2008: The Temptation) Hatimaye, **Eb 2:18** inasema *"Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa."* Ukweli kwamba Yesu *"aliteseka alipojaribiwa"* unaashiria kwamba kuteswa kwake kulikuwa kwa hali ya juu kuliko tunavyoweza kuteseka tunapojaribiwa. Sababu ni kwamba Yesu alipinga majaribu *katika njia yake yote hadi mwisho, bila kushindwa na jaribu.* Kwa ujumla hatufanyi hivyo. Majaribu yanapokuwa makubwa, huwa tunajiachia na kuyaruhusu yatubebe. Yesu hakuwahi kufanya hivyo. Matokeo yake, mara zote alipata uzoefu wote kwa ukamilifu uliohitajika. Ushindi wake unaweza kuwa wetu tunapodumisha kuwa karibu naye, kujua neno lake na mapenzi yake, kupata nguvu ya Roho Mtakatifu, na kumtii katika kila jambo.

Majaribu ya Yesu pia kwa mifano huelezea historia ya Israeli. Siku arubaini za Yesu kule jangwani (**Mat 4:1-2**) ni sehemu ndogo ya miaka arubaini ambayo Israeli walikaa jangwani. Kama Mungu alivyowaongoza Israeli jangwani (**Kut 13:17-18, 21**), Roho Mtakatifu alimuongoza Yesu jangwani (**Mat 4:1; Mk 1:12; Lk 4:1**). Ingawa Marko hataji majaribu, Mathayo na Luka wanataja. Majaribu ambayo Yesu alikabiliana nayo kule jangwani (**Mat 4:1-11; Lk 4:1-13**) yalienda sambamba na majaribu ya Israeli jangwani. "Katika jaribu la kwanza na itikio la Yesu kuna mambo kadhaa ya kuvutia na yenye maana na yanayofanana yakijikita katika mada moja ya uana wa Yesu na wa taifa la Israeli. Wote ni 'wana' (Kumb. 8:5; linganisha na Mat. 4:3, 6); wote 'wanaoongozwa' (Kumb. 8:2; linganisha na Mat. 4:1); wote wanapelekwa jangwani/nyikani (Kumb. 8:2; linganisha na Mat. 4:1); na wote wanapata njaa (Kumb. 8:3; linganisha na Mat. 4:2)." (Burke 2006: 173-74n.55) Pale ambapo Israeli hakuridhishwa na ile mana aliyowapa Mungu (**Hes 11:1-6**), Yesu alijaribiwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kubadilisha mawe kuwa mkate (**Mat 4:3; Lk 4:3**). Mbeleni, baada ya kuwalisha watu 5000, Yesu anajilinganisha na mana waliyokula Israeli kule jangwani akisema, *"Mimi ni chakula kilichoshuka kutoka mbinguni"* (**Yh 6:1-14, 41, 48-58**). Ambapo Israeli wanamjaribu Mungu kule Masa na Meriba wakidai uthibitisho wa uwepo na nguvu zake (**Kut 17:1-7**), Yesu alijaribiwa kuruka kutoka katika mnara wa hekalu kumlazimisha Mungu kuheshimu ahadi yake (**Mat 4:5-6; Lk 4:9-11**). Pale Israeli walipomuacha Mungu na kugeukia ndama ya kuyeyushwa (**Kut 32:1-6**), na baadaye kumwabudu Baal (**Hos 2:1-13**), Yesu alijaribiwa kuanguka na kumsujudia Shetani (**Mat 4:8-9; Lk 4:5-7**). Zaidi ya hapo, Yesu aliyakabili majaribu kwa kunukuu moja kwa moja kutoka katika muhtasari wa historia ya Israeli kule jangwani (**Kumb 8:3; 6:13, 16**). "Kuchaguliwa kwa maandiko mawili kutoka katika sehemu ndogo ya AK kunaonesha kuwa aliona mfanano wa kitheolojia kati ya uzoefu wa Israeli na uzoefu wake mwenyewe. Israeli amerudiwa 'kama mtu anavyomrudi mwanawe' (Kumb. 8:5), lakini hata hivyo hakujifunza somo vizuri. Sasa Yesu, anatangwazwa upya 'mwana wa Mungu' kule Jordani, uana huo umejaribiwa kwa namna ile ile. Lakini pale Israeli aliposhindwa, Yesu alithibitisha kuwa mwana wa Mungu. Katika yeye ahadi ya Israeli inatimizwa." (France 1975: 67)

MASWALI YA KUJADILI

1. Yapi yalikuwa ni makusudi ya kubatizwa kwa Yesu na namna ulivyokuwa uzoefu muhimu katika maisha yake na muhimu katika kuzindua ufalme wa Mungu?

2. Bila kujali injili zingine, ni majaribu gani ambayo Yesu angelikumbana nayo, siyo tu kule jangwani lakini pia katika maisha yake yote?

3. Kama Yesu alimshinda Shetani pale msalabani na katika kufufuka kwake, kwanini bado tunakumbana na majaribu?

4. Unapokutana na majaribu, inakusaidia kujua kwamba Yesu alikutana nayo pia? Kwanini au kwanini sivyo?

- Inaleta tofauti kwa jibu lako unapofikiria majaribu yaliyokushinda (yakiwemo yale ambayo ulikuwa *ukijua* na *ukaweka nia* kushindwa hata kama ulikuwa unajua kuwa kile unachokwenda kutenda siyo sawa, kimekatazwa na maandiko, na kilimhuzunisha/ kulimkasirisha Mungu)?

5. Kusema kweli Biblia inaweka wazi kwamba Yesu, hakuwahi kutenda dhambi—lakini *angeliweza* kutenda dhambi wakati alipokabiliwa na majaribu yake? Je, **Eb 2:18**, ambayo inaoneshwa kuwa Yesu *aliteseka* wakati wa kujaribiwa kwake, aliyavumilia? Kama ndivyo, kwa namna gani? Kama hufikirii hivyo, kwanini, na kwa maana hiyo, **Ebr 2:18** ina maana gani?

6. Soma majaribu matatu yaliyoandikwa katika **Mat 4:1-10**, na kisha fikiria yafuatayo: Kuna *kanuni* au *msingi* gani kwa kila jaribu?

- Ni kwa namna gani kila jaribu linahusiana na ufalme wa Mungu na dhima ya Yesu?

- Yapi yangeliweza kuwa matokeo muhimu (kwa Yesu, dhima yake, na ufalme) kama Yesu angeshindwa katika kila jaribu?

1:14-15: ***[14] Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri habari njema ya Mungu, [15]akisema, wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamni injili."***

mst. 14-15—Kutangazwa kwa Ufalme

Injili ya Yohana inaonesha kuwa kimsingi Yesu alianza huduma kule Yudea na karibu na mto Yordani kabla Yohana Mbatizaji hajatiwa gerezani. Haya yalitokea wakati Yesu akiwa "anaongezeka" na Yohana "anapungua" (**Yh 3:30**). "Ni wazi mitume hawakuwa naye wakati wote katika kipindi hiki isipokuwa mara chache" (Cheney 1969: 37). Hata hivyo, katika **mst. 14**, Marko anatuonesha kwamba Yohana alikamilisha kazi aliyokuwa amepangiwa na Mungu kama mtangulizi. Yohana alifungwa na Herode Antipa, mtawala wa Galilaya, kwasababu Yohana amemshutumu Herode kwa kumuoa Herodia, ambaye alikuwa mke wa Filipo ndugu yake wa baba mmoja mama mbalimbali (**Mat 14:3; Mk 6:17-18; Lk 3:19-20**) Kwa namna isiyo ya kawaida, tukio hili lilimfanya Yesu kwenda Galilaya (Jimbo la Herode). Kule Galilaya Yesu anawachagua wale kumi na

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

wawili wawe pamoja naye wakati wote, na ujumbe wake unaanza kupata nguvu.

Mistari 15 unatoa muhtasari wa ujumbe wa Yesu. Mpango wa Mungu ulikuwa kwamba *"hata ulipowadia utimilifu wa wakati,Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe wale waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate hali ya kuwa wana"* (**Gal 4:4-5**). Matokeo yake, katika **mst. 15** Yesu anatangaza, *"Wakati umetimia."* Alithibitisha hili katika **Lk 4:21** aliposoma kutoka **Isa 61:1-2a** kuhusiana na kuja kwa Masihi na kisha akasema, *"Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu."* Matokeo yake, **2 Kor 1:20** inasema kwamba ahadi zote za Mungu zilitimizwa katika Yesu.

Hili lina maana kubwa kwetu. Kama Paulo anavyoliweka katika **2 Kor 6:2**, *"Tazama, wakati uliokubalika nalikusikia, siku ya wokovu nalikusaidia; tazama, wakati uliokubalika ndio sasa."* Hili linaturudisha kwenye tangazo la Yesu **Mk 1:15** kwamba *"ufalme wa Mungu umekaribia."*Wakati Yesu alipotoa mapepo, aliwaambia Mafarisayo, *"Ufalme wa Mungu umewajilia"* (**Lk 11:20**). Katika **Lk 17:20-21** anaongezea, *"Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; wala hawatasema, Tazama, upo huku, au kule, kwa maana ufalme wa Mungu umo ndani yenu."* Inawezekanaje hili, wakati tungali tunaogelea dhambini na katika uovu, na mambo mengi ya kidunia ni kinyume na Kristo na utawala wake? Hiki kinachoonekana kuwa na utata kinaelezewa na asili ya ufalme wa Mungu ya "tayari/bado", yaani ingawa ufalme wa Mungu na utawala wa Kristo umezinduliwa na kutambulika kikanuni (ufalme "tayari"), haujafunuliwa kikamilifu lakini unasubiri ukamilifu wa mbeleni katika utukufu wake kamili (ufalme "bado").[1]

Maana ya msingi wa maneno kwa Kiebrania katika AK na Kigiriki katika AJ yaliyotafsiriwa "ufalme" ni "utawala wake, Ukuu wake …. siyo upeo au watu" (Ladd 1959: 19-21; angalia **Zab 103:19; 145:11, 13; Mat 6:33; Mk 10:15; Lk 19:11-12**). Kwa maana moja, ufalme wa Mungu ni wa milele. Mungu amekuwepo wakati wote, yupo sasa, na wakati wote atabaki kuwa mkuu na mtawala juu ya kila kitu (**Mwa 1:1; Ayb 12:9-10; Zab 103:19; Isa 44:24-28; 66:1-2; Dan 4:34-37; 6:26-27; Mat 5:34-35; Mdo 4:27-28; 7:49-50; Ef 1:11**).

Hata hivyo, kwa maana nyingine ni uhalisia wa kiroho uliopo na ambao unafikika sasa. Asili ya ufalme imetofautiana na matarajio ya waisraeli na hata wanafunzi wa Yesu (pale mwanzoni). Yesu alikazia kuwa ufalme wa Mungu ni wa kiroho (**Yh 3:5-8**) na unaweza kupatikana kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili (**Yh 3:3**). Hii ndiyo maana Yesu alisema, *"Tubuni na kuiamini injili"* (**Mk 1:15**). Tayari tumeshazungumzia toba hapo nyuma kuhusiana na ubatizo wa Yohana Mbatizaji. *"Kuiamini injili"* kwa upande mwngine wa shilingi wa toba. Mtu anaweza kusema kwamba kuna sehemu tatu za ukweli kuhusu imani inayookoa: (1) Kuna sehemu ya akili—lazima mtu aamini Yesu ni nani na amefanya nini (angalia **Mdo 2:22-24, 32, 36; Rum 1:1-4; 10:9; 1 Kor 15:1-8**); (2) kuna sehemu ya kitabia—tabia zetu, matendo yetu, maisha yetu ni ushahidi wa kama imani tunayokiri ni halisi (angalia **Mat 28:18-20; Yh 14:23-24; Ef 2:8-10; Yak 2:14-20**); na (3) kuna sehemu ya kiibada—upendo na kujitoa kwa Kristo ndio ukweli muhimu, na imani inayookoa (angalia **Yh 15:4-15; 17:3; 21:15-17**). Michael Spencer anaelezea asili ya kweli ya "kuamini" kunakookoa kama ifuatavyo: "Kuamini katika Agano Jipya kunafanana zaidi na namna ya imani tunayoihusisha na mambo tunayojifunga nayo. Ndoa ni mfano mzuri. Watu wanaopeana maisha kila mmoja kwa mmwenzake "humwamini" mwingine kwa moyo wao wote, hatma yao na umiliki wao. . . . Imani katika Yesu isiyoendelea siyo imani ya kweli. Saburi ni moja ya tabia ya imani. Imani inaweza kuwa safari ndefu yenye kona nyingi na vilima, mabonde na majira ya kutokuwa na matunda, lakini imani halisi huendelea kuamini katika Yesu na kutafuta kumfuata. Biblia haiahidia raha kwa yule huamini lakini haendelei. . . . Toba na kuamini lazima viende pamoja. Hivyo, mtu anaponiuliza afanye nini aweze kwenda mbinguni, huwa ninatoa jibu la uwazi na ukweli: Kubali una dhambi, tubu na kuyatoa maisha yako yote kwa kadiri ujuavyo kwa Yesu." (Spencer 2020: The Response)

Kutangaza ufalme ilikuwa ni shabaha ya msingi ya mafundisho ya Yesu (**Mat 4:17, 23; 9:35; Lk 4:43**) na mifano yake (**Mat 13:1-50; 21:28-22:14; 25:1-13**). Aliwaagiza wanafunzi wake kutangaza ufalme wa Mungu (**Lk 9:1-6; 10:1-12**). Kabla na baada ya kifo cha Kristo, "ufalme wa Mungu" ulikuwa ndiyo *"injili yenyewe"* (**Lk 9:2, 6**) na *"injili ya neema ya Mungu"* (**Mdo 20:24-25**). **Mdo 28:23-31** inaweka sawa *"ufalme wa Mungu"* na *"wokovu wa Mungu."* Yesu aliweka wakfu kanisa lake kuwa mwakilishi wa kimwili wa ufalme wa duniani (**Mat 16:18-19**). Kama ndivyo, inatupasa kutunza vizuri akilini mwetu kwamba uwepo wa ukristo kwa ujumla wake ni kutumia injili katika kila eneo la maisha yetu. Tunaanza na Kristo kama uumbaji mpya kwa ajili yetu, na tunasonga mbele kufikia lengo, ambalo ni kufanywa kuwa kama yeye alivyo katika uumbaji mpya duniani kote." (Goldsworthy 1991: 233) Hii ndiyo ile "tayari" ya ufalme.

[1] Uwakilishi wa "Tayari"/"na bado" vimejadiliwa na wafafanuzi wengi. Angalia kwa mfano, Hoekema 1979: 13-22; Venema 2000: 12-32; Vos 1979: 38 (helpful diagram). Yameakisiwa katika zile heri za **Mat 5:2-10**: **mst. 2, 10** iko katika wakati ulipo; thawabu zingine zote ziko katika wakati ujao. "Tofauti hii ni muhimu, kwa kuwa inakazia kwamba ingawa ufalme wa Mungu (utawala wa Kristo) ni uhalisia uliopo, kilele cha cha ufalme huo kinasubiri kurudi kwake katika utukufu" (Alexander 2008: 95).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

Kwa maana nyingine ufalme wa Mungu ni wa kieskatolojia. Baadhi ya aya zinazungumzia ufalme wa Mungu kama upeo wa mbeleni ambao utakuja tu wakati Kristo atakapokuja (**Mat 7:21; Mk 9:47; 10:23; 14:25**). Kwa maneno mengine, ufalme wa Mungu ni ndiyo shabaha ya kihistoria ya kieskatolojia, wakati maadui wote wa Mungu watakapokuwa wameshindwa, uovu wote kutokomezwa, na Mungu kutawala pamoja na watu wake katika haki kamilifu, furaha na wema (**Dan 2:44; Zak 14:9; Mat 6:9-10; 1 Kor 15:20-28; Uf 21:1-22:5**). Kwa hali hii, ufalme wa Mungu ni wa mbeleni (**Mat 7:21; Mk 9:47; 10:23; 14:25; Lk 21:27-31; 22:15-16; Ef 5:5; 2 Tim 4:18; 2 Pet 1:11**). "Ni urithi ambao Mungu atawapa watu wake wakati Kristo atakapokuja katika utukufu [**Mat 25:34; 1 Kor 15:50; Ef 1:14, 18; Kol 3:24**]" (Ladd 1959: 17). Hayo ni ile "bado" ya ufalme. Ile "tayari" na "bado" ya ufalme wa Mungu vina uhusiano: "Baraka ya kizazi kilichoko ni ahadi na muhuri wa Baraka kuu ijayo" (Hoekema 1979: 22).

1:16-20: ***[16] Naye alipokuwa akipita kando ya bahari ya Galilaya, akamwona Simioni na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. [17]Yesu akawaambia, njoni mnifuate, name nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. [18]Mara wakaziacha nyavu zao wakamfuata. [19]Akaendelea mbele kidogo, akamwona Yakobo wa zebedayo, na Yohana nduguye, nao pia walikuwa chomboni, wakizitengeneza nyavu zao. [20]Mara akawaita, wakamwacha baba yao Zebedayo ndani ya chombo pamoja na watu wa mshahara, wakaenda wakamfuata.***

mst. 16-20—Kuitwa kwa wanafunzi wa kwanza

Katika siku za Yesu, watu wakitamani kuwa wanafunzi wa mwalimu au rabi walikuwa wakimwendea na kumuomba kuwa wafuasi (angalia **Mat 8:19**). Hata hivyo, kwa Yesu, Yesu yeye alichukua hatua katika kuanzisha na kustawisha mahusiano na wanafunzi (angalia **Mat 4:18-19; Mk 1:16-17; 2;14; Lk 5:9-11, 27; Yh 1:42-43**). Tukio lililoandikwa na Marko siyo la kwanza Yesua likuwa ameshakutana na Petro, Yakobo na Yohana. **Yh 1:35-51** inaonesha kwamba Simioni (Petro), Andrea, Philipo, na Nathanaeli walikuwa wamekutana na Yesu, wakati fulani baada ya ubatizo wa Yesu, labda karibu na Mto Yordani. Hilo linaweza kuelezea kwanini Petro, Andrea, Yakobo, na Yohana wote waliacha mashua zao mara moja Yesu alipowaita *"Nifuateni"*

Kuitwa kwa wanafunzi hawa wa mwanzoni kunatuonesha kitu fulani muhimu kuhusu uanafunzi. Kwanza, hakuna tofauti kati ya uongofu na uanafunzi (**Mat 28:18-20**). Katika aya nyingi, Yesu aliita watu kumfuata kama wanafunzi wake na kujadili uhalisia wa kuwa mwanafunzi (angalia **Mat 4:18-22; 5:3-16; 10:24-25; 12:46-50; Mk 3:31-35; Lk 6:40; 8:19-21; 9:23-24, 57-62; 14:25-33; Yh 8:31-32; 13:34-35; 15:1-8, 18-20**). Neno la Kigiriki la "mwanafunzi" ni *mathētēs.* "*Mathētēs* katika Agono Jipya lina maana zaidi ya mwanafunzi au anayejifunza. Ni mtu anayeambatana na kupokea maelekezo anayopewa na kuyafanya kanuni ya mwenendo wake." (Zodhiates 1993: *mathētēs,* 936) Pili, uanafunzi ni jambo la kimabadiliko. Mwitikio wa Petro, Andrea, Yakobo na Yohana—*"waliondoka . . . na kumfuata"*—Inaendana na wito wa Yesu wa *"kutubu na kuamini."* Wanafunzi hao wa mwanzoni waliacha shughuli zao na familia zao—na kipato chao na usalama wao pia—na kumfuata Yesu. Baadaye, Petro alisema, *"tumeacha vyote na kukufuata"* (**Mk 10:28**). Kuna mahusiano ya moja kwa moja ya wito wa Yesu wa *"tubuni na kuiamini injili"* (**Mk 1:15**) na kuja kufanyika mwanafunzi. Kusema kweli, msingi wa uanafunzi ni uelewa wa kina na kuikubali injili na yote yanayoendana nayo: "Injili ni kwa ajili ya wanafunzi, siyo kwa ajili ya wenye dhambi tu; inaokoa na kubadilisha watu katika mahusiano, siyo mtu peke yake tu. . . . Uanafunzi unahusu kumtegemea Yesu, kuiamini injili yake. Ingawa hili linaweza kuonekana rahisi sana, tatizo ni kwamba sisi sote tungali tuna shida kuelewa maana ya kumtegemea Yesu au kuiamini injili kunaonekanaje. . . . [Agizo Kuu] hulenga kutangaza injili kwa wale ambao hawajawa wanafunzi bado na kuifundisha injili kwa wale waliokwish kuwa wanafunzi. Yesu anatanguliza injili, ambayo inalenga kufanya na kukuza wanafunzi. Haiti watu kuinjilisha kwanza, na kuwafanya kuwa wanafunzi kama kitu cha pili kinachojitegemea. Uinjilisti na uanafunzi msingi wake ni injili. . . . Yesu alitangaza injili ile ile kwa makutano ambayo aliifundisha kwa wanafunzi. Hakuwaweka wanafunzi wake kipekee, katika darasa la nyongeza ya injili ili kujifunza masomo ya daraja la juu. Injili ni kwa ambao ni wa daraja la chini na wale wa daraja la juu kwasababu hakuna anayehitimu katika injili. Yesu alifundisha injili ile ile ya ufalme kwa wenye dhambi na watakatifu. Kwanini? Kwasababu ajenda yake ndiyo suluhu pekee kwa matatizo yetu yote ya dhambi, tuwe wakristo au wasio wakristo. Wote wanahitaji kusamehewa, kupatanishwa, na kurejeshewa nguvu ya injili ya kuwawezesha kumfahamu na kumfurahia Mungu, siyo mara moja lakini maisha yote." (Dodson 2012: 17, 19, 36, 38)

Michael Spencer anaonesha kuwa tunavyoitikia wito wa Yesu, kama walivyoitikia wanafunzi wa kwanza, lazima iwe ni "kuyaacha maisha yetu kabisa na kuchukua maisha mapya. Tunaposoma majina haya [ya wanafunzi wa kwanza], tunatambua kuwa hawa walikuwa ni wanaume wenye familia na majukumu ya lazima na bili za kulipa kama sisi tulivyo, pamoja na hayo walibadilishwa na Yesu kiasi kwamba waliacha vyote na

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kumfuata. Yesu alielewa hali hiyo ilimaanisha nini. Aliwaambia wanafunzi wake wahesabu gharama (Lk 14:28ff) na wasimfuate huku wamegawanyika nia zao. (Mat 8:18-22)" (Spencer 2009: The Calling) Mwanafunzi wa kweli huweka upendo wake na kujitoa kwake kwa Yesu juu ya kila kitu na kila mtu, hata maisha yake mwenyewe, (**Lk 14:26**). Anaongeza kusema, "Leo ni jambo linalojulikana sana kuzungumzia "kumpokea Yesu" na "kumuomba Yesu aingie katika moyo wako." Maneno haya hayapatikani katika Biblia na yanaueleza Ukristo katika maana ambayo ina mapungufu. Kristo anatuita kumfuata. Tujifunze kutoka kwake. Tumuige. Tuambatane naye. Hatuwezi kumaliza kuelezea maana ya kumfuata Yesu" (Ibid.)

MASWALI YA KUJADILI

1. "Ufalme" wa Mungu ni nini?

2. Ufalme *unakaaje* leo (hasa kwa kuzingatia udhihirisho wa uovu duniani)?

3. Yesu alisema *"Iaminini Injili"* Hii ina maana gani?

- Kuhusiana na hili, leo hii watu wanalionaje neno "amini?"

- Unafikiri Yesu alifikiri nini kuhusiana na neno hilo?

4. Yesu alisema *"nifuate."* Ina maana gani kumfuata Yesu?

5. "Kumpokea Yesu" au "kumuomba aingie katika moyo wako" hayapatikani katika Biblia. Maneno haya yana mapungufu kwa namna gani katika kuelezea maana ya kuwa mkristo?

- Kuhusiana na hili, unafikiriaje wazo la kwamba unaweza ukampokea Yesu kama *"mwokozi"* na siyo *"bwana"*

6. Ni kweli Yesu amekuita? Kama ndivyo, umewahi kujiuliza *kwanini* alikuita?

1:21-45: ***[21]Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi, akafundisha. [22] Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi.[23]Na mara palikuwapo ndani ya sinagogi lao mtu mwenye pepo mchafu; akapaza sauti, [24] akisema, Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! Umekuja kutuangamiza? [25] Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke. [26] Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka. [27]Wakashangaa wote, hata wakaulizana, wakisema, Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wamtii! [28]Habari zake zikaenea mara kotekote katika nchi zote kandokando ya Galilaya. [29]Na mara walipotoka katika sinagogi, walifika nyumbani kwa Simoni na Andrea, pamoja na Yakobo na Yohana. [30]Naye mkwewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa kitandani, hawezi homa; na mara wakamwambia habari zake. [31]Akamkaribia, akamwinua kwa kumshika mkono, homa ikamwacha, akawatumikia. [32]Hata kulipokuwa jioni, na jua limekwisha kuchwa, walikuwa wakimletea wote waliokuwa hawawezi, na wenye pepo.[33]Na mji wote ulikuwa umekusanyika mlangoni. [34] kaponya wengi waliokuwa na maradhi mbalimbali, akatoa pepo wengi, wala hakuwaacha pepo kunena, kwa sababu walimjua. [35]Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko. [36]Simoni na wenziwe wakamfuata;***
37 nao walipomwona wakamwambia, Watu wote wanakutafuta.[38]Akawaambia, Twendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nalitokea. [39]Akaenda akihubiri katika masinagogi yao, katika nchi yote ya Galilaya, na kutoa pepo. [40]Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, Ukitaka, waweza kunitakasa. [41]Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika. [42]Na mara ukoma wake ukamtoka, akatakasika. [43]Akamkataza kwa nguvu, akamwondoa mara, [44]akamwambia, Angalia, usimwambie mtu neno lolote, ila enenda zako ukajionyeshe kwa kuhani, ukatoe alivyoamuru Musa kwa kutakasika kwako, iwe ushuhuda kwao. [45]Lakini akatoka, akaanza kuhubiri maneno mengi, na kulitangaza lile neno, hata Yesu asiweze tena kuingia mjini kwa wazi; bali alikuwako nje mahali pasipokuwa na watu, wakamwendea kutoka kila mahali.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mst. 21-45—Uponyaji na kutoa pepo

Yesu alianzia huduma yake wazi wazi kule Galilaya, ambako alikuwa mkazi. Galilaya iko kaskazini mwa Israeli, karibu na bahari ya Galilaya. Huduma yake iliambatana na uponyaji, kutoa pepo, na kufundisha. Ilikuwa kule Galilaya ambako aliwaita wanafunzi wake.

1. **mst. 21-28—**Yesu anafundisha katika Sinagogi na kumponya mtu aliyekuwa na pepo mchafu

Mat 4:13 anaandika kwamba Yesu alipokwenda Galilaya baada ya Yohana Mbatizaji kukamatwa, aliweka makazi yake kule Kapernaumu, "Kapernaumu ulikuwa mji mkubwa na muhimu kule Galilaya, makao makuu ya serikali na biashara na mahali barabara za kimataifa zilikutana. . . . Akiwa amealikwa kufundisha katika Sinagogi kubwa katika mji maarufu halikuwa jambo lililotendeka bila kufikiriwa vema au kuonekana kuwa na umuhimu. Hili ni dodoso linaloashiria kuwa tayari Yesu alikuwa ameshajipatia umaarufu kama mwalimu na labda kama mtenda miujiza." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Teacher")

"Waandishi" hawakuwa watu walionakili tu sheria lakini walikuwa "wasomi wa siku hizo, waliofunzwa kitaaluma katika kutafsiri na matumizi ya sheria" (Wessel 1984: 627). Waandishi wangefundisha na kutafsiri maandiko, kama wasomi wa siku za leo, kwa kunukuu tafsiri zingine na mamlaka. Yesu alikuwa tofauti. Alifundisha kama mtu mwenye mamlaka iliyotokea ndani mwake ya kutoa maana ya maandiko. Mtindo wake wa kufundisha unaweza kuonekana katika hotuba yake ya mlimani ambapo kwa kurudia mara kadhaa alisema, *"mmesikia ikisemwa [yaani katika Maandiko] . . . lakini mimi nasema"* (**Mat 5:21-22, 27-28, 31-32, 33-34, 38-39, 43-44**). Zaidi, alipofundisha katika sinagogi kule Nazarethi, baada ya kunukuu **Isa 61:1-2a**, ndipo alitamka, *"Leo maandiko haya yametizwa masikioni mwenu"* (**Lk 4:21**). Hatushangazwi na hili, kwasababu tunaelewa Yesu alikuwa nani: "Njia pekee tunayoweza kufikiria aina hii ya mafundisho yenye mguso ni kuwaza kwamba wakristo wangemwitikiaje mtu ambaye angesema: 'sawa, najua bibilia inasema hivi na vile, lakini nasema …" (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Teacher") Haishangazi kuona kuwa watu *"walishangazwa na mafundisho yake, kwakuwa alifundisha kama mwenye mamlaka, na siyo kama waandishi"* (**mst. 22**)

Zaidi ya hayo, vitendo vya Yesu vilidhihirisha kuwa alikuwa na mamlaka ya kufundisha kama alivyofanya (**ms. 27**). Ijapokuwa wengi katika makusanyiko inawezekana hawakujua Yesu alikuwa nani, mapepo yalijua. Yalijua alikuwa *"mtakatifu wa Mungu"* (**mst. 24**). Walijua kuwa kuja kwa huyu mtakatifu wa Mungu kungeleta hukumu na kuharibiwa, ndio maana waliuliza, *"Umekuja kutuangamiza?"* (**mst. 24**; angalia pia **Mat 8:29; Mk 5:7; Lk 8:28-31**) Hata hivyo, mapepo hawakujua habari ya ile asili ya ufalme "tayari lakini bado" na ukweli kwamba Kristo angekuja mara mbili: Mara ya kwanza katika unyenyekevu, mara ya pili katika ushindi na hukumu.[2] Kwa kuzitoa roho chafu, Yesu alikuwa ikionesha kuwa alikuwa na mamlaka juu ya "mamlaka, nguvu za anga, giza hili la leo, na nguvu za uovu katika ulimwengu wa roho" (**Ef 6:12**; see **Mat 12:22-29; Mk 3:22-27; Lk 11:14-22**). Kwa kifupi, "wewe na mimi tunapokutana na Yesu uso kwa uso katika maisha yetu tunahitaji kuelewa kile ambacho watu wa wakati wake walielewa: Huyu siyo mtu wa kawaida. Huyu ni mtu wa kipekee kabisa. Huyu ni mtu anayefundisha kwa mamlaka, kama Mungu mwenyewe. Huyu ni mtu anayekabili maovu na yanamtii kama Mungu mwenyewe." Huyu ni mtu (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Teacher")

Mwisho, wakati mapepo walipomtambua Yesu kama *"mtakatifu wa Mungu"* (**mst. 24**), Yesu alimkemea, akisema *"kaa kimya!"* (**mst. 25**) Yesu aliamuru hivyo mapepo na mahali pengine pia katika injili. (angalia kwa mfano, **Mat 8:4; 9:30; 16:20; 17:9; Mk 1:25, 34, 44; 3:12; 5:43; 7:36; 8:30; 9:9; Lk 4:41; 9:21**). Kwani alifanya hivi? Inawezekana kukawa na sababu kadhaa. Kwanza, yawezekana hakutaka utambulisho wake utangazwe na mapepo. Pili, Inawezekana hakutaka kuwa maarufu mapema hivyo asije akapoteza mwelekeo wa dhima yake, aonekane si zaidi ya mponyaji na mtoa pepo. Tatu, baada ya Yesu kuwalisha watu 5000, Yohana anaandika kwamba watu *"watu walitaka kuja na kumkamata kwa nguvu ili kumfanya mfalme"* (**Yh 6:15**). Kwa maneno mengine, Yesu alizungukwa na watu waliokuja kumtazama kama aliyetosheleza mahitaji yao ya kimwili (angalia **Yh 6:26-27**), kisiasa au hata kuwa kiongozi wa kijeshi. Hayo hayakuwa dhima yake. Badala yake, Yesu alijua kuwa utambulisho wake ulihusiana kwa karibu sana na msalaba. Ndiyo maana alikuja duniani, na lilikuwa jambo ambalo haliwezi kusimulika wala kuelezeka. Kama mwandishi mmoja alivyosema, "kwa kuwa ilikuwa ni kwa njia ya kifo chake kwamba Yesu angeokoa watu wake, kwamba kifo kilikuwa ni lazima kabla ya utambulisho wake halisi kujulikana. Kama utambulisho huu ungewekwa wazi kabla ya kifo chake, mgogoro mkubwa zaidi ungelitokea kutokana na msingi wa kutokuelewa Masihi angekuwaje" (Carter 2003: 9) Hata wanafunzi wake hawakuelewa umuhimu wa kusulubiwa. Ilikuja

[2] Kutoelewana huku ni sawa na kutoelewana kwa wanafunzi wenyewe ambao kwa wazi walifikiri kwamba kuharibiwa kwa hekalu, kuja kwa Yesu, na mwisho wa nyakati ilikuwa ni tukio moja tata (angalia **Mat 24:3; Mk 13:4; Lk 21:7**) Ile asili ya ufalme ya "tayari " na "bado" imejadiliwa katika Menn 2021: 23-25.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kueleweka kwao baada ya kufufuo kwake.

2. **mst. 29-34—**Yesu awaponya wengi

Uponyaji huu unafunua nguvu ya Yesu isiyo ya kawaida. Maneno "wote" au "wengi" (**mst. 32, 34**) yanaonesha kwamba uponyaji wa mtu aliyepagawa na pepo katika **mst. 21-28** halikuwa tukio la tofauti na kwamba Yesu alikuwa na nguvu za kuponya magonjwa ya kawaida kadhalika na kuwa na mamlaka juu ya pepo. Uponyaji wa Yesu ulikuwa wa papo kwa papo, wa jumla, na uliodhihirika. Hapakuwa na maswali kwamba alikuwa wa kipekee katika nguvu zake na mamlaka. Yesu, nguvu ya kizazi kijacho "alitokea" katika kizazi hiki; nguvu zake dhidi ya mapepo na magonjwa ya kimwili vilidhihirisha kwamba *"ufalme wa Mungu umekaribia"* (**Mk 1:15**). "Miujiza ya uponyaji katika Marko ipo kama sehemu ya ujumbe: ufalme wa Mungu umefika kwa njia ya Yesu. Magonjwa na kuchakaa kimwili vilikuwa mojawapo ya matokeo ya dhambi tuliyo iona katika Mwanzo 3. Kwa kulinganisha, miujiza ya Yesu inadhihirisha nguvu ya ufalme wa Mungu katika kupindua matukio haya ya dhambi na kuharibu kazi za shetani." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Healer")

Umaarufu wa kwanza wa Yesu kama mponyaji ulikuwa na maana kivitendo. Kwanza, kwakuwa wanadamu ni muunganiko wa nafsi-mwili, maradhi ya kimwili humgeuza mtu kuangalia "ndani" yaani, mambo mengine yote hujipima kwa kujilinganisha na maradhi ya mwili. "Miujiza hii ya uponyaji huonesha kuwa Yesu analeta kitu fulani katika maisha mazima ya mtu. Ufalme wa Mungu ni habari njema kwa kila eneo la maisha yetu." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Healer") Uponyaji wa Yesu kwa wagonjwa sio tu ulidhihirisha mamlaka yake na nguvu lakini pia uliwawezesha kuacha kuangalia hali zao za kimwili ili kuitikia wito wa Yesu kuhusiana na hali zao za kiroho.[3] Pili, mwitikio wa mkwe wa Petro kwa uponyaji wake *("akamkaribia, akamwinua kwa kumshika mkono, homa ikamwacha, akawatumikia,"* **mst. 31**) unadhihirisha muitikio wa wanafunzi wote wa kweli: pale Yesu anapogusa maisha yetu, tunamtumikia, na tunafanya hivyo kwa kuwatumikia wengine.[4]

3. **mst. 35-39—**Yesu anafundisha kule Galilaya

Mis. **35-39** inaonesha "upande mwingine wa shilingi" wa mahusiano kati ya yale ya kimwili na yale ya kiroho. Ingawa kuponya mwili wa mtu kunaweza kukafungua mlango wa kuisikiliza injili, kwa kuwa tungali ni viumbe wa kimwili wanaoishi katika dunia ya kimwili, mambo ya kimwili yanaweza yakazidi yale ya kiroho. Kama Michael Spencer anavyotuonesha, "Msomaji wa injili hutoka humo na mawazo kwamba kibinadamu karibu Yesu angezidiwa na idadi ya wale waliokuja kupata uponyaji" (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Healer").

Yesu alitambua hatari hii. Matokeo yake, mara baada ya kuponya na kutoa wengi pepo, *"akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko"* (**mst. 35**). Alifanya jambo hilo hilo mara tu baada ya kulisha watu 5000 (**Mk 6:46**). Walter Wessel anatuonesha kuwa jambo ambalo Yesu alikutana nalo na kushangaa baada ya wengi kuponywa, kutolewa pepo, na watu 5000 kulishwa lilikuwa "mwitikio usio na kina na wa juu juu wa watu kwa Yesu." Wanavutiwa tu na yale aliyokuwa anaweza kutenda katika kuponya mateso yao ya kimwili. Kwahiyo Yesu anatafuta nguvu ambayo hutolewa na baba kwa njia ya ushirika. Wanafunzi . . . wanafikiri Yesu atapendezwa kujua kwamba kila mtu alikuwa akimtafuta (mst. 37). hawaelewi kwamba hali inayojulikana sana ya kutokuwa na kina katika kumkubali ilikuwa ndiyo sababu hasa alijitenga na kwenda kuomba." (Wessel 1984: 629)

Mistari 38-39 inatuonesha kwamba, bila kujali umuhimu wa jinsi alivyojali mahitaji yao ya kimwili, Yesu alijua kuwa dhima yake ilikuwa muhimu sana kuliko hayo. Makutano walimtaka Yesu kurudi au kubakia alikokuwa. Angefanya hivyo, watu wengi wangeliponywa kimwili kwa muda—lakini kamwe tusingekuwa na mwokozi. Kwahiyo, aliwaambia wanafunzi wake, *"Twendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nalitokea"* (**mst. 38**). Ni lazima kanisa lisisahau somo hili. Ni lazima lijihusishe na mahitaji ya kimwili ya watu. Hata hivyo, ni lazima kufanya hivyo kwa muktadha wa kudhihirisha ukweli unaobadilisha na uhalisia wa injili.

4. **mst. 40-45—**Yesu anamtakasa mwenye ukoma

Uponyaji wa mkoma katika kifungu hiki (angalia pia **Mat 8:2-4**) unaonesha bado upande mwingine wa mahusiano ya kimwili—kiroho, mahusiana ya kuingiliana mwili-roho. "Yesu alikuwa na uelewa wa kina. Alikuwa na uwezo usio wa kawaida wa kuona ndani kabisa ya watu na kujua walitaka nini, au kama waliamini

[3] Muunganiko wa karibu kati ya kimwili na kiroho ni lazima usisahauliwe na kanisa katika misheni zake kwa dunia. Muunganiko huu umejadiliwa kwa kina kiasi fulani katika Menn 2016 na Menn 20017.

[4] Siyo tu kwamba Petro alikuwa ameoa, lakini hata wale wanafunzi wengine kadhalika walikuwa wameoa (**1 Kor 9:5**).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kweli, lakini waliogopa kusema. . . . Kwa mkoma katika Marko 1:40-45 angeliweza kupaza sauti yake, 'Uwe mzima . . . lakini nisimsogelee. Huwa sipendi kuwaona wakoma.' Hakufanya hivyo. Yesu alimsogelea na kumgusa. Mguso wa Yesu si lazima ulikuwa wa uponyaji wa kimwili. Ilikuwa ni muhimu kuponywa mihemko yake. Unafikiria mtu huyu alijisikiaje alipoguswa? Mkoma alikuwa mtu wa kutengwa, lilikuwa jambo la kawaida akionekana anatembea mtaani watu walitawanyika kumpisha, na kusema, 'najisi—najisi!' Yesu alijua kuwa mtu huyu hakuwa tu na mwili wenye ugonjwa lakini alikuwa na ugonjwa mwingine sawa na huo wa kujifikiria tofauti. Alihitaji kuguswa ili kuponywa kikamilifu. Hivyo, Yesu aliitikia kama alivyofanya siku zote, kumponya mtu kila eneo." (Pippert 1979: 37-38)

Yesu alinukuu kutakaswa kwa wakoma kama alama iliyoonesha kuwa alikuwa masihi wa kweli wa Israeli, aliiyekuwa analetwa, na ufalme wa Mungu ulikuwa unazinduliwa. "Unabii wa kurudi kutoka uhamishoni, na kurudi kwa YHWH sayuni, ulishuhudia alama ya matukio haya yakionesha kurejeshwa kwa uumbaji, kwa kuangalia uponyaji wa wagonjwa. [mf. **Isa 35:1-10:** *"Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba."*]: . . . Tunaweza kwa kujiamini kwamba Yesu alikusudia 'matendo yake makuu' ya uponyaji yachukuliwe kama alama ya kutimiza matarajio haya." (Wright 1996: 428-29) Wakati Yohana Mbatizaji aliposhangazwa na yale Yesu aliyokuwa akifanya na kuhoji kama kweli Yesu alikuwa ndiye aliyetarajiwa, Yesu alijibu kwa kuonesha asili ya alama ya matendo yake: *"Yesu akajibu akawaambia, Nendeni mkamweleze Yohana mnayoyasikia na kuyaona;vipofu wanapata kuona, viwete wanakwenda, wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa habari njema. Naye heri awaye yote asiyechukizwa nami."* (**Mat 11:4-6; Lk 7:22-23**)

Mguso wa Yesu kwa mkoma unaashiria jambo muhimu kuhusiana na uungu wa Yesu. Kulingana na sheria, kumgusa mkoma au kitu kingine "najisi" watu wangemfanya mtu huyo kuwa najisi (**Law 5:3**; angalia pia **Law 13:45-46; Hes 5:1-4; 19:22**). Hata hivyo, "Yesu alipomgusa mkoma, ukoma haukuhamia kwa Yesu. Yesu ndiye mtakatifu na mponyaji. Nguvu ya kuponya na kutakasa, hutiririka kutoka kwa Yesu kwenda kwa mkoma kuushinda ugonjwa. Ukoma hauna uwezo wa kumshambulia Yesu. . . . Yesu anathibitisha kuwa na nguvu na mamlaka maalum. Kama Emanueli, ni mtakatifu. Utakatifu hutiririka kutoka kwake kuponya walioambukizwa na ana mamlaka ya kutangaza kutakasika kwa aliyetakaswa. Yesu hakuhitaji kupitia mchakato wa kujitakasa. Injili haiandiki chochote kwamba Yesu yeye binafsi alifuata aina yeyote ya kujitakasa. Kama mtakatifu, asingeliweza kunajisika kwa kumgusa mkoma. . . . Ingawa Yesu hanajisiki kwa kumgusa mkoma, utakatifu hutiririka kutoka kwake kwenda kwa mkoma. Sheria ya kujitakasa inapata utimilifu wake katika yeye" (Viljoen 2014: 6)[5]

Hili, kwa upande mwingine, lina maana ya kuwasilisha injili kwa Waislamu na wengine ambao huangalia maswala ya kuwa safi na kunajisika. Bruce Sidebotham anajadili jambo hili: "Kule Indonesia rafiki aliuliza kwanini Wakristo hukazia kwamba Yesu ni Mungu na kwamba alisulubiwa. Badala ya kujaribu kumshawishi rafiki yangu kwamba wote ni wenye dhambi na kwamba dhambi zote lazima ziadhibiwe kwa kifo, niligundua kile ambacho tayari alikuwa anakifahamu, kwamba wenye mwili wote ni wanajisi na kwamba hata kabla ya kuzaliwa ni wenye uchafu wanaohitaji kusafishwa. Nilielezea mawazo yangu ya kutokuona faida katika desturi za kidini katika kututakasa kiasi cha kutosho kustahili kuingia mbinguni, kwasababu uchafu hauwezi kujisafisha wenyewe kama vile giza lisivyoweza kujifanya nuru. Nilisema kwamba kama vile mshumaa unavyofukuza giza kutoka chumbani mwetu kwa kuingia katika chumba hicho, Mungu huondosha maovu katika mwili wa mwanadamu kwa kufanyika mwili. Kwa maneno mengine, kitu kile kile Waislamu wanachowapinga Wakristo,—Mungu kujifananisha na uumbaji wake, ndicho kinacholeta suluhu kwa matatizo mengi ya msingi ya binadamu kama Waislamu wanavyoyatambua." (Sidebotham 2002: 4) Ingawa Waislamu wanapinga wazo kwamba Yesu si Mungu katika mwili, "Asili ya miujiza ya Yesu – kuponya vipofu kwa mate yake na wakoma kwa kuwagusa bila kuambukizwa, na ingawa kaburi la nabii linaweza kuwa takatifu mate yake yatabaki kuwa yananuka kama ya mtu mwingine awaye yote." (Ibid.). Wakati Yesu (na mate yake) yanabakia kuwa safi na matakatifu, jambo ambalo lina maanisha kuwa hawezi kuwa mwanadamu wa kawaida.

Swala la Yesu kuamuru watu wakae kimya (**mst. 44**) lilijadiliwa hapo juu kuhusiana na **mst. 21-28**. Hapa, mkoma aliyeponywa alitenda kwa kufuata asili ya mwanadamu na kutoa habari za uponyaji wake licha ya

[5] "Simulizi inahitimisha na Yesu kumuagiza mtu achukue sadaka yake na kwenda kujionesha kwa kuhani. Inapasa ijulikane kuwa sehemu ya kwanza na ya pili ya taratibu za kutakaswa, kama zilivyoelezwa katika Walawi 14:2–9, zimewekwa pembeni. Yesu tayari alikuwa ameshaondoa uchafu kutoka kwa yule mtu (sehemu ya kwanza ya kutakaswa), na tayari alikuwa amemtangaza yule mtu kuwa yuko safi (sehemu ya pili). Kilichokuwa kimesalia ilikuwa ni sadaka ya sehemu ya tatu, ili kwamba kuhani aweze kumruhusu kupata ushirika kamili wa kijamii na kiroho." (Viljoen 2014: 6) Mkoma aliyeponywa kwenda kwa kuhani, ingekuwa ni ushahidi wa wazi wa Yesu kuponya hata magonjwa mabaya ya kuchukiza na ingeamsha fahamu kuweza kuuona utambulisho wa kipekee wa ukuhani wa Yesu, nguvu, na mamlaka yake.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kuwa Yesu alimwambia asiseme. Hili lilikuwa na madhara ya kuzuia upeo wa huduma ya Yesu kwa watu. Hata hivyo, sifa zake zilivuma kiasi kwamba licha ya kujitenga, *"watu walimfuata kutoka kila mahali"* (**mst. 45**).

MASWALI YA KUJADILI

1. Kama "dhambi ni dhambi," kwanini Yesu alikuwa na maneno makali kwa waandishi, mafarisayo, na waalimu wa sheria kuliko wenye dhambi "wa kawaida"?

2. Kwanini Yesu mara nyingi aliwaamuru watu na pepo kukaa kimya baada ya kutenda muujiza?

3. Jadili mahusiano ya kimwili - kiroho/mwili-nafsi.

4. Kwanini uponyaji ulikuwa sehemu muhimu ya huduma ya Yesu. Ni kwa namna gani uponyaji wake uliathiri vibaya huduma yake?

5. Uponyaji na miujiza ya Yesu ilikuwa na umuhimu gani kama alama?

6. Yesu aliwezaje kumgusa mkoma bila kunajisika?

7. Yesu anapotugusa—ama kwa kutuponya au vinginevyo—tunapaswa kuitikiaje?

2:1-12: ***[1]Akaingia Kapernaumu tena, baada ya siku kadha wa kadha, ikasikiwa ya kwamba yumo nyumbani. [2]Wakakusanyika watu wengi, isibaki nafasi hata mlangoni; akawa akisema nao neno lake. [3]Wakaja watu wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne. [4]Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo; na wakiisha kuivunja wakalitelemsha godoro alilolilalia yule mwenye kupooza. [5]Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako. [6]Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao, [7]Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu? [8]Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? [9]Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? [10]Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza), [11]Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako. [12]Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe!"***

mst. 1-12—Yesu amponya aliyepooza

Tukio hili linaanzisha upinzani dhidi ya Yesu na huduma yake, unaoishia katika kifo chake. Hakika, tukio hili na matukio machache yanayofuata katika huduma ya Yesu yanatumika kuwaunganisha waandishi, Mafarisayo, na Maherode (ambao hapo awali walikuwa hawapatani) dhidi ya Yesu *"ili kumwangamiza"* (**Mk 3:6**).

Kuna angalau maeneo sita katika uponyaji wa Yesu kwa aliyepooza tunayohitaji kuyaangalia. Kwanza, tukirejea kwamba katika **Mk 1:38** Yesu alisema, *"Twendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nalitokea"* Sasa amerudi kapernaumu—ambako ni wazi kulikuwa ndio kituo chake cha kuifikia Galilaya (angalia **Mat 4:12-17**)—na *"alikuwa akiwahubiria Neno"* (**Mk 2:2**).

Pili, mtu aliyepooza aliletwa kwa Yesu na watu wanne marafiki zake. Yesu aliwaona. Michael Spencer anatoa mawazo yake hivi, "Haikuwa imani ya yule aliyepooza tu, lakini pia imani ya marafiki zake inasifiwa. Kwa sehemu kubwa Ukristo wa magharibi una hamasa za kibinafsi na hupinga "imani ya kijumuiya.' Lakini nafikiri kibiblia haiwezekani kuongelea imani nje ya imani ya kijumuiya inayoamini kabla hatujatenda, hutulea kadiri tunavyoamini, hutusaidia kadiri tunavyoamini na huamini wakati tunapojikwaa katika kutokuamini. Agano la Mungu na 'watu' wake ni agano na jumuiya lisilopuuza imani binafsi, lakini huliambatanisha agano la Mungu na jumuiya kama kitovu cha utendaji wake katika kushughulika na binadamu. Yote haya hukazia kwanini ni muhimu kwa kila mkristo kuwa sehemu ya jumuiya ya waamini." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Forgiver of Sins")

Tatu, jambo la kuzingatiwa linapatikana katika **mst. 5** unaosema, *"Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako."* Kwakuwa yule mtu alikuwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

amekuja kuponywa kimwili kupooza kwake, bila shaka alitarajia Yesu kusema neno kama vile *"kijana, imani yako imekuponya—uwe mzima!"* Kusema kweli inawezekana aliyepooza alijisikia kuvunjika moyo Yesu aliposema, *"Kijana, dhambi zako zimesamehemewa."* (Yawezekana alifikiri, "hilo ni zuri, lakini Yesu, ni wazi kuwa nimekuja kuponywa kupooza kwangu.") Yesu alijua hilo. Lakini pia alijua kuwa yale tunayotaka sana yanaweza kuwa siyo tnayohitaji zaidi. Mtu huyu—na sisi—tatizo la msingi lilikuwa siyo hali yake ya kimwili, lakini hali yake ya kiroho. Yesu alikuwa hasemi kwamba hali ya kimwili ya yule mtu haikuwa muhimu. (maana hata hivyo Yesu atamponya.) Hata hivyo, kila kitu kuhusu maisha yetu katika mwili huu, ikiwa ni pamoja na kupooza, njaa au shibe, ugonjwa au afya, umasikini au utajiri, na hata maisha yenyewe, ni duni ukilinganisha na mahitaji yetu ya wokovu na kusamehewa dhambi zetu. Matokeo yake, kitovu cha kisa hiki ni muendelezo wa mamlaka ya ufalme wa Yesu kwa jambo hilo muhimu la mwisho katika maisha ya mwanadamu – kusamehewa dhambi. Dhambi ndilo tatizo la msingi la mwanadamu, tatizo linalotawala katika kitabu cha Mwanzo 1-11 na huongoza katika mpango wa Mungu ukianzia na Abrahamu na kuendelea katika Biblia yote. Ufalme wa Mungu ni mashambulizi ya himaya anayodai Shetani iliyoshikiliwa na nguvu ya dhambi. Wokovu ni ushindi wa Mungu dhidi ya dhambi na ushindi huu hudhihirishwa kwanza na kwa umuhimu katika msamaha. Mahitaji muhimu zaidi ya mwanadamu ni ile hatia tuliyo nayo mbele za Mungu mtakatifu iondolewe. Tukio kama hili haliwezekani kwa nguvu za mwanadamu peke yake. Hatuwezi kujisamehe wenyewe au kutenda mema ya kutosha kumshawishi Mungu atusamehe. Mungu hutoa msamaha kwa rehema na neema, akihamasishwa na kazi ya Mwanawe aliyefanyika mtu, msalaba na ufufuo. Mungu sasa anaweza kuwasamehe wenye dhambi kwasababu adhabu yao imelipwa na haki yake kuridhishwa kabisa. Agano lote la Kale lilizungumzia mwelekeo huu na Yesu sasa anatangaza msamaha kama zawadi ya bure. Hizi ni habari muhimu sana za Injili." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Forgiver of Sins")

Hili linatupeleka katika sehemu muhimu ya nne ya jambo hili, yaani, muitikio wa waandishi: mwanzo wa upinzani wa viongozi wa kidini dhidi ya huduma ya Yesu. Kile ambacho Yesu alisema kwa yule aliyepooza (na kile alichokuwa anakaribia kutenda) kiligonga swala la *Yesu ni nani.* Kama Yesu ni binadamu tu, basi waandishi walikuwa sahihi waliposema katika **mst. 7**, *"Kwanini mtu huyu anaongea hivyo? Anakufuru! Ni nani anayeweza kusamehe dhambi isipokuwa Mungu tu?"* Kwa usahihi walitambua hili, kulingana na sheria, ni utoaji sahihi wa dhabihu ndio uliokuwa una nafasi ya kusamehewa, lakini kutoa msamaha kwa kutoa tamko tu kusema kweli ni kitu kinachostahili kufanywa na Mungu peke yake. Hakika, kwa kumwambia yule mtu (ambaye hajawahi kukutana naye) *"dhambi zako zimesamehewa"* Yesu kwa kusema hivyo, ilileta maana kwamba mtu yule amemtenda dhambi *Yesu mwenyewe.*

Hatimaye dhambi zote ni kinyume na Mungu kwasababu sheria ya Mungu yatoka kwake na inaakisi asili yake; kwahiyo, kutenda dhambi kwa kuiasi sheria yake ni kumkwaza yeye binafsi. Zaidi ya hayo, kutenda dhambi dhidi ya watu wengine ni kutenda dhambi dhidi ya Mungu kwasababu watu wameumbwa kwa sura ya Mungu (**Mwa 1:26-27; 9:6; Yak 3:9-10**); dhambi hufikia kilele chake katika kudhalilisha na kuchafua sura ya Mungu na hapo hufunua mwenye dhambi anamfikiriaje Mungu mwenyewe. Hali hii inafanana na pale mtu anapofanya jambo la jinai dhidi ya mtu mwingine; mhalifu hatendi jinai kwa mtu mwingine lakini anavunja sheria ya nchi. Hivyo, ni serikali ndiyo humshitakia aliyevunja sheria, siyo aliyefanyiwa kosa. Kwa kudai kumsamehe mtu aliyepooza, Yesu hapo alikuwa anatangaza kwamba alikuwa Mungu aliyekuja duniani kama mtu. C. S. Lewis alionesha umuhimu wa Yesu kudai anaweza kusamehe dhambi—dhambi yeyote: "Sote tunaweza kuelewa jinsi mtu anavyoweza kusamehe mabaya aliyotendewa. Unanikanyaga kiatu changu na ninakusamehe, unaiba pesa zangu na ninakusamehe. Lakini tumtazame vipi mtu ambaye hajaibiwa, hajakanyagwa, ambaye anatangaza kukusamehe kwa kuwakanyaga vidole vya watu wengine na kuiba pesa za watu wengine? . . . Na hili ndilo Yesu alilofanya. Aliwaambia watu kuwa dhambi zao zilikuwa zimesamehewa, na hakuhitaji kusubiri hadi awasiliane na waliokosewa ambao watakuwa wameumizwa na dhambi hiyo bila shaka. Bila kusita anaonekana kama na yeye ni sehemu ya waliokosewa, mtu aliyekosewa kwa makosa yote. Hili linaleta maana ikiwa tu hakika alikuwa Mungu ambaye sheria yake imevunjwa na ambaye upendo wake umejeruhiwa na kila dhambi. Katika kinywa cha kila mnenaji ambaye si Mungu, maneno haya yangemaanisha kile ambacho naweza kukiita tu ujinga na kujikweza kusikostahili kabisa kwa yeyote katika hitoria." (Lewis 1996: 55)

Tano, mwitikio wa Yesu kwa waandishi ulidhirisha kwamba, kusema kweli, alikuwa Mungu aliyekuja kama mtu. Katika **mst. 8**, Yesu alifunua kuwa alijua siri na mawazo ya watu katika mioyo na akili zao. "Hii siyo kusoma sura tu au lugha ya mwili, bali udhihirisho wa maarifa ambayo ni mtu tu mweye uungu anaweza kuwa nayo; namna ya maarifa yenye kuchunguza mawazo ya wanadamu na nia zao yanayomruhusu Mungu kutufahamu kama tulivyo na kutuhukumu kwa unyofu." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Forgiver of Sins") Katika **mst. 9-12**, Yesu anatoa hakikisho bayana kwamba ana mamlaka ya kumsamehe mtu dhambi, na hapo akadhihirisha kuwa alikuwa Mungu: *"[9]Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa*

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? [10]Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza), [11]Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako. [12]Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe!".

Yeyote angeweza *kusema* maneno *"dhambi zako zimesamehewa."* Lakini mtu angejuaje kuwa dhambi zake zimesamehewa, kwakuwa msamaha hauonekani na ni wa kiroho? Hii ndiyo maana Yesu alidhihirisha mamlaka yake ya kusamehe (na hivyo akadhihirisha yeye ni nani hasa) kwa kufanya jambo ambalo lisingewezekana kwa yeyote kulifanya isipokuwa Mungu: mara na kwa ukamilifu aliyepooza akaponywa kwa kutamkiwa neno tu. Hata hapa, kuna mengi yanayoendelea kuliko tunavyoweza kuona. Ijapokuwa watu walishangazwa na kumtukuza Mungu walipomuona yule mtu aliyeponywa, hawakutambua kwa kina kwanini ni Yesu tu angeliweza kutamka maneno *"dhambi zako zimesamehewa"* na kwanini *"ili mpate kujua kwamba mwana wa mtu ana mamlaka duniani ya kusamehe dhambi"* Sababu ni msalaba. Ni ukweli kwamba Yesu alijua kuwa anakabiliwa na msalaba kulipa dhambi ya Yule aliyekuwa amepooza kwamba hilo lilimwezesha kusema *"dhambi zako zimesamehewa"* Mamlaka ya kusamehe dhambi yanamaanisha mamlaka ya kushughulikia matokeo ya dhambi. Ni Yesu peke yake angeliweza kufanya hivyo pale msalabani. Kwa kuwa hatma ya magonjwa, madhaifu, kupooza na kifo ni matokeo ya dhambi (angalia, kwa mf. **Mwa 2:17; Ezek 18:20; Rum 5:12-14**), Yesu alikuwa anadhihirisha mamlaka yake juu ya dhambi na madhara yake katika ulimwengu wa kimwili, ili kwamba wote waone na kujua kwamba "Kwa Yesu hakuna mipaka ya mamlaka yake katika eneo lolote la maisha. Anaweza kuisemesha dhambi, ugonjwa, uonevu wa kipepo, hatia, kujisikia kuhukumiwa – chochote kinachotufunga—na kutuweka huru na wakamilifu" (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Forgiver of Sins"). Hili limeoneshwa pia katika **mst. 11** wakati Yesu alipomwambia yule mtu, *"Nakuambia, inuka, chukua godoro lako na uende."* Neno "inuka" asili yake ni neno la Kigiriki *egeirō,* ambalo mahali pengine katika injili ya Marko na Agano jipya ni neno linalofahamika sana lenye maana ya "ufufuo." Kufufuka kwa Yesu kutoka kwa wafu na kupaa kurudi kwenda kwa Baba kunahalalisha Yesu ni nani na kuonesha kuwa Baba alikubali dhabihu ya Kristo mwenyewe pale msalabani kwa ajili yetu. Kwasababu Yesu ni "uzao wa kwanza", wa ufufuo, anatuhakikishia kwamba, wakati wa kurudi kwake, wote walio wake (akiwemo aliyekuwa amepooza) watafufuliwa pia (angalia **1 Kor 15:23**).

Kwa maneno mengine, Ili Yesu amsamehe yule mtu ilimaanisha kuwa Yesu mwenyewe itamlazimu afe badala ya yule mtu na kulipa gharama ya dhambi zake. Gleason Archer anaeleza hivi, "Mungu kama Mungu asingeweza kutusamehe kwa dhambi zetu isipokuwa dhambi zetu ziwe zimelipiwa; vinginevyo yeye mwenyewe angekuwa mfidiaji au mteteaji wa uvunjifu wa sheria yake takatifu. Ilikuwa katika kuwa mtu tu katika Kristo kwamba Mungu angeliweza kukamilisha ondoleo la dhambi za mwanadamu kikamilifu; kwa kuwa ni mtu tu, binadamu halisi, angeliweza kuwakilisha wanadamu kikamilifu. Lakini mkombozi wetu ilimbidi awe Mungu, kwa kuwa ni Mungu tu angeliweza kutoa dhabihu yenye thamani ya milele, kufidia adhabu ya moto wa kuzimu ambao dhambi zetu zilistahili, kulingana na madai ya haki ya haki ya kiungu." (Archer 1982: 323)

Anselm wa Canterbury anaeleza hivi: Kwasababu mwanadamu *hawezi* kulipa deni lake likamilifu kwa Mungu, hakuna mwingine isipokuwa Mungu *anaweza* kulipa kikamilifu. Lakini binadamu ndiye *aliyepaswa* kufanya hivyo. Kwa hiyo, kama ikiwa lazima, kama inavyoonekana, kwamba ufalme wa mbinguni unafanywa na watu, na hili haliwezi kutekelezeka isipokuwa utoshelevu tuliotangulia kusema umekamilishwa, ambao hakuna mwingine isipokuwa anayeweza kuufanya, na siyo mwingine isipokuwa binadamu ndiye anayestahili kuufanya, ilikuwa muhimu kwa Mungu-mtu kuchukua nafasi hii. . . . Kwahiyo, ili kwamba Mungu-mtu aweze kutekeleza hili, ni muhimu kwamba awe Mungu kamili na mtu kamili. Ili kuleta ondoleo hili la dhambi. . . . Hivyo, basi, ni muhimu kwamba Mungu-mtu anakuwa amekamilika katika kila moja ya asili hizo, haiwezi kupungua kwamba asili hizi ziungane na kuwa katika nafsi moja, kama vile mwili na nafsi vinavyoishi pamoja kwa kila binadamu; kwa kuwa kinyume cha hayo, haiwezekani kwamba mtu huyo huyo awe Mungu kamili na mtu kamili." (Anselm 1903: II:6-7) Yesu peke yake ndiye mwenye sifa hizi.[6]

Ni katika muunganiko huu wa ajabu wa Mungu na mtu katika Kristo unaomwezesha Mungu kupatiliza na kustahimili msalaba. Yesu aliishi maisha tuliyopaswa kuishi *kama mtu:* alimtii Mungu Baba kikamilifu katika mambo yote; *"alijaribiwa katika mambo yote tunayojaribiwa, lakini hakutenda dhambi"* (**Eb 4:15**). Hili lilimfanya astahili kutuwakilisha, kuchukua dhambi zetu katika mwili wake na kulipa adhabu ambayo vinginevyo tulipaswa kulipa lakini tusingeliweza (**Rum 8:1-4; 2 Kor 5:21; Gal 3:13; Kol 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; 1 Pet 2:24**). Kama Timothy Keller anavyosema, "Hivyo, Mungu hakuweka maumivu kwa mwingine, lakini

[6] Kristo ni mtu kamili na kama Mwana wa Mungu imeelezwa katika Menn 2020 hapo juu, sehemu ya **2.VI. Muitikio wa mtazamo wa Kiislamu wa Yesu: Yesu ni "Mwana wa Mungu"**.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

pale msalabani alibeba maumivu, ukatili, na uovu wa dunia juu yake mwenyewe. Kwahiyo, Mungu wa Biblia siyo kama miungu inayodai damu zetu ili ghadhabu zao zitulizwe. Badala yake, huyu ni Mungu anayefanyika mwanadamu na kutoa damu yake mwenyewe ili kuheshimu haki ya kimaadili na upendo wa rehema ili aweze kuharibu uovu wote bila kutuharibu sisi. . . . Kwanini Yesu *alilazimika* kufa ili aweze kutusamehe? Kulikuwa na deni la kulipwa—Mungu mwenyewe alililipa. Kulikuwa na adhabu iliyotupasa—Mungu aliichukua mwenyewe. . . . Msalabani haki wala rehema havishindwi—vyote vinakamilishwa kwa pamoja. Kifo cha Yesu kilikuwa muhimu kama Mungu angechukulia haki inavyopasa na bado aoneshe upendo kwetu." (Keller 2008: 192-93, 197) John Stott anahitimisha, "Kiini cha dhambi ni mtu kujiweka katika nafasi ya Mungu, wakati kiini cha wokovu ni Mungu kujiweka katika nafasi ya mtu. Mwanadamu hujiingiza mwenyewe kinyume cha Mungu na kujiweka mahali anapostahili Mungu tu; Mungu hujitoa dhabihu kwa ajili ya mtu na kujiweka mahali ambapo ni mtu tu ndiye anastahili kuwepo. Mtu hudai sifa anazostahili Mungu peke yake; Mungu anakubali fidia inayopaswa kutolewa na mtu tu." (Stott 1986: 160)

Mwisho, katika **mst. 10**, matamko ya Yesu, *"Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi"*yanaleta maana zaidi watu walivyoweza kuelewa wakati huo au wakati huu. Yesu anaitwa "mwana wa Adamu" karibu mara 80 katika injili; ni utambulisho wake unaojitokeza zaidi. Maneno *"Mwana wa Adamu"* yanatukumbusha **Dan 7:13-14** *("Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye <u>mfano wa mwanadamu</u> akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. **14**Naye akapewa mamlaka, na utukufu, na ufalme, ili watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, wamtumikie; mamlaka yake ni mamlaka ya milele, ambayo hayatapita kamwe, na ufalme wake ni ufalme usioweza kuangamizwa").* Katika **Uf 1:13-14** Yohana alipokea ufunuo kutoka kwa Yesu, ambaye anamuelezea kama "*mfano wa Mwana wa mtu … [ambaye] kichwa chake na nywele zake vilikuwa vyeupe kama sufu, kama theluji."* Picha hizo zimechukuliwa kutoka katika maono ya Danieli katika **Dan 7:9, 13**. Hata hivyo, katika maono ya Danieli (**Dan 7:9**) ilikuwa ni katika "*siku za kale*" ambapo *"mavazi yalikuwa meupe kama theluji na nywele nyeupe kama sufu nyeupe"* Kwa muktadha huu, "Mwana wa Mtu ni Mungu, asiye na kikomo katika hekima na utakatifu." (Johnson 2001: 59) Hivyo, popote Yesu alipotumia maneno *"Mwana wa mtu"* alikuwa anatangaza kwamba yeye ndiye, hakika, Mungu anakuja duniani *kama mtu.*

Hakika, Yesu kutumia maneno "Mwana wa Mtu" kujitambulisha kunaleta maana mpya katika maneno hayo na kufunua utambulisho wa kina zaidi wa uhalisia wa utambulisho wa Yesu na wa Mungu kuliko watu walivyoweza au wanavyoweza kutambua. "Kulingana na Daniel 7:9-22 Mwana wa Mtu ilikuwa ni sura ya mbinguni ya mtu atakayeshiriki katika kuhukumu siku ya mwisho; hata hivyo, Yesu anaongezea maana zaidi katika cheo hicho kwa kudai kuwa Mwana wa Mtu yampasa pia ateseke. Hivyo, Yesu anaunganisha pamoja na mtumishi wa Mateso (Isa. 52:13-53:12 [angalia **Mat 17:12; 20:25-28; Mk 10:42-45; Lk 22:25-27; Yh 3:14**])." (Schreiner 1989: 818) "Kifo na kuinuliwa kwa mtumishi wa Bwana ni njia ambayo Mungu huonesha utukufu wake na kudhihirisha uungu wake duniani. . . . Mtumishi, katika kushushwa kwake na kuinuliwa kwake, siyo mtu anayetofautishwa na Mungu, lakini, katika kushushwa kwake na kuinuliwa kwake, kunahusu utambulisho wa Mungu wa kipekee" (Bauckham 1998: 49, 51). Hivyo, neno, "Mwana wa Mtu" huonesha (pamoja na matamko mengine mengi ya Yesu) asili halisi ya Mungu alivyo. Kama Richard Bauckham anavyoeleza, "Yesu anafunua utambulisho wa kiungu—Mungu ni nani hasa—katika kushushwa na pia katika kuinuliwa, na katika muunganiko wa haya mawili. Utambulisho wa Mungu mwenyewe unafunuliwa katika Yesu, maisha yake na msalaba wake, kama hakika ilivyo katika kuinuliwa kwake, kwa namna ambayo ni endelevu na inayoendana na Agano la Kale na uelewa wa Kiyahudi kuhusu Mungu, lakini pia ni mpya na ya kushangaza." (Ibid.: viii)

<u>MASWALI YA KUJADILI</u>

1. Ni nafasi gani unafikiri imani ya kijumuiya inapaswa kuchukua katika maisha ya waamini?

- Ni kwa namna gani maisha yako yameguswa na imani ya kijumuiya?

2. Yesu anajua mawazo yetu yote (**ms. 8**). Ni tofauti gani inaweza kuletwa (au inapaswa kuletwa) na hili kwako?

3. Ni kwa namna gani tukio hili la mtu aliyepooza linaelezea uungu wa Yesu?

4. Kwanini Yesu pekee ndiye aliye na mamlaka ya kusamehe dhambi?

5. Ni kwa namna gani Yesu anafunua asili halisi ya vile Mungu alivyo?

6. maneno “Mwana wa Mtu” yana mhusu nani na yana maana gani?

2:13-17: ***[13]Akatoka tena, akaenda kando ya bahari, mkutano wote ukamwendea, akawafundisha. [14]Hata alipokuwa akipita, akamwona Lawi wa Alfayo, ameketi forodhani, akamwambia, Nifuate. Akaondoka akamfuata. [15]Hata alipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake, watoza ushuru wengi na wenye dhambi waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata. [16]Na waandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi? [17]Yesu aliposikia aliwaambia, “Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi.”***

mst. 13-17—Kuitwa kwa Lawi

Tukio hili tena linaanza na mafundisho ya Yesu (angalia pia **Mk 1:14, 38; 2:2**). Anaweza akawa anafundisha kutokea kwenye mashua iliyokuwa karibu na pwani kama katika **Mk 4:1** au anafundisha akiwa anatembea (**Mk 2:14**; angalia **Lk 24:13-15, 25-28**). **Ms. wa 13** unaonesha kuwa, ingawa viongozi wa kidini walikuwa wanaanza kumpinga Yesu, makutano walikuwa wangali wakimwendea. **Mistari 14-17** inakazia kuitwa kwa Lawi, mtoza ushuru, kuwa mwanafunzi wa Yesu.[7] Kama ilivyokuwa katika kuponywa yule mtu aliyekuwa amepooza katika **mst. 1-12,** tukio hili ni muhimu na linafunua mengi kuhusu mambo manne muhimu: asili ya Yesu, ufalme, na injili; hitaji letu la neema ya Mungu na msamaha; asili ya kina ya kuzaliwa kwetu mara ya pili (kama inavyowakilishwa na Lawi); na asili ya wapinzani wa Yesu. Kwasababu kuna mtiririko wa kimantiki kwa mpangilio huo, huu ndio mpangilio tutakao fuata katika kuzungumzia kifungu hiki.

1. Asili ya Yesu, Ufalme na injili.

Pale ambapo **mst. 1-12** inazungumzia moja kwa moja swala hili la Yesu ni **mst. 14-17** inatuambia asili ya injili, ufalme, maadili ya Yesu, na mahusiano na watu. Kama Michael Spencer anavyoliweka, “Kama ukristo uko sahihi katika kukiri kwake kwamba Yesu ni Mungu Muumbaji, aliyekuja katika mwili, basi namna Yesu alivyowachukulia watu huenda ni sehemu muhimu ya ujumbe wa injili. Kwanini? Kwasababu hili litaonesha jinsi Mungu anavyojisikia kuhusu mimi! Ni sehemu ya kibinafsi sana ambayo injili inasema kwa yeyote miongoni mwetu.” (Spencer 2020: “Reconsider Jesus – Calling the Tax Kollector”)

Mwito wa Yesu kwa Lawi una maana ya kipekee kwamba “katika Palestina ya karne ya kwanza, watoza ushuru walidharauliwa. Hilo lilitokana na sababu kadhaa: Warumi waliuza vibali vya kukusanya kodi kwa wale waliotoa dau kubwa. Mara baada ya mkusanyaji kodi kulipa robo yake kwa Warumi, angeweza kubakia na kilichosalia. Kwasababu hiyo, watoza ushuru walikuwa siyo waaminifu kabisa na wakati mwingine walikusanya mara mbili (au zaidi) ya kile kilichodaiwa. Pia, watoza ushuru walionekana kuwa ni washirika wa mamlaka iliyokuwepo. Myahudi wa kawaida anaweza asiwe mkereketwa, lakini kwa hakika alikuwa mzalendo na ilikuwa ni rahisi kumchukia mtu aliyewapa kisogo watu wake mwenyewe, kwa ajili ya kuwatumikia Warumi. Kuwa na mahusiano na Warumi pia ilimaanisha kwamba mtoza ushuru kwa taratibu za kidini alikuwa najisi, na alihesabiwa miongoni mwa “watu wasio na dini” waliotengwa na jamii. Hivyo, haishangazi kundi hili kushirikiana na makahaba na “wenye dhambi.” Kundi lao la kijamii lilikuwa na mipaka dhidi ya makundi mengine ya kidini na waliotengwa.” (Spencer 2020: “Reconsider Jesus – Calling the Tax Kollector”)

Kifungu hiki kinaelezea kwamba Yesu “hana upendeleo.” Neema ya Mungu haiwahusu matajiri tu, wenye nguvu, wenye mali, au wasomi (ingawa baadhi ya hao, kama vile Nicodemo na Yusufu wa Arimathayo, walipokea neema hiyo). Badala yake, neema ya Mungu huwafikia watu wa aina zote kwa usawa, bila kuweka tofauti: wanawake na wanaume; wadogo kwa wakubwa; masikini kwa matajiri; wadhaifu wa wenye nguvu; wasiosoma kwa wasomi; wagonjwa na wenye afya; wenye sura mbaya na wenye sura nzuri; wanaopendeka na wasiopendeka; hata *“watoza ushuru*” (**mst. 16-17**). Kwamba Yesu “hana upendeleo” limeoneshwa wazi katika *“kukaa kwake mezani nyumbani kwa [Lawi]”* (**mst. 15**). Hilo lina maana zaidi kuliko tunavyoweza kutambua angalau kwa njia mbili:

- Kwanza, Kula chakula lilikuwa jambo la kina sana katika ukarimu na kukubalika. Ilikuwa ni mwaliko wa urafiki na ushirika, uliokwenda zaidi ya kula chakula tu. Wasomi wengi wa leo hutafsiri kuamini kwa Yesu kwamba kitendo hiki, kwa upande wa Yesu, kilikuwa ni zaidi ya jambo lililoangaliwa kumhusu yeye; wanaamini lilikuwa kitendo cha makusudi, kilichofanywa hadharani, kutangaza ujumbe mkali ulio tofauti kuhusu ufalme wa Mungu na Mungu wa ufalme.” (Spencer 2020: “Reconsider Jesus – Calling the Tax

[7] Lawi ni sawa na Mathayo (angalia **Mat 9:9; 10:3; Mk 3:18; Lk 5:27-28; 6:15; Mdo 11:13**). Walter Wessel anasema, “Lawi huenda lilikuwa jina lake la kupewa na Mathayo (‘zawadi ya Mungu’) jina lake la kitume” (Wessel 1984: 634).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

Collector") Yesu hakuwa anatoa neema ya juu juu tu kwa "mtoza ushuru na mwenye dhambi" halafu akae mbali naye. Badala yake, alikuwa anaonesha urafiki wa kweli, na kukubalika halisi kwa watu waliokuwa wametengwa na wale wenye kuheshimika katika jamii.[8]

Hili linatuambia mengi kuhusu asili ya ufalme na injili. Ni somo ambalo sote twapaswa tujifunze. Petro alilazimika kujifunza somo hili katika **Wagalatia 2**. **Gal 2:11-14** inasema, *"[11]Lakini Kefa alipokuja Antiokia, nalishindana naye uso kwa uso, kwa sababu alistahili hukumu. [12]Kwa maana kabla hawajaja watu kadha wa kadha waliotoka kwa Yakobo, alikuwa akila pamoja na watu wa Mataifa; lakini walipokuja wao, akarudi nyuma akajitenga, huku akiwaogopa waliotahiriwa. [13]Na hao Wayahudi wengine wakajigeuza pamoja naye, hata na Barnaba pia akachukuliwa na unafiki wao. [14]Walakini, nilipoona ya kuwa njia yao haiendi sawasawa na ile kweli ya Injili, nalimwambia Kefa mbele ya wote, Ikiwa wewe uliye Myahudi wafuata desturi za Mataifa, wala si za Wayahudi, kwa nini unawashurutisha Mataifa kufuata desturi za Wayahudi?"* Mistari hii huonesha kwamba injili hugusa kila eneo la maisha yetu, ikiwa ni pamoja na nani tuna kula pamoja naye. Paulo aliliona kwamba, bila kujali nia yao, vitendo na matokeo ya kile Petro na wengine walichofanya kilichoma katika moyo wa injili yenyewe.

Katika **Mdo 10** Petro alikuwa ameonyeshwa kuwa Mungu hana upendeleo kati ya Wayahudi na Wamataifa. Hata ameshuhudia hili katika **Mdo 11** kwa Wayahudi waliokuwa wamempinga kwa kula pamoja na Wamataifa wasiotahiriwa. Wakati Petro alipokutana na Paulo kule Yerusalemu, alikubaliana na mafundisho ya Paulo (**Gal 2:1-10**). Pamoja na hayo, Sasa, Petro alikuwa akikana injili ile ile aliyokuwa akiihubiri kwa namna alivyokuwa anaishi. Shabaha ya nje ya Petro haikuoana na ile ya ndani, mambo yaliyofichika aliyoamini. Matokeo yake, Paulo kwa wazi akamwita "mnafiki." Kwa kuwa hili halikuwa jambo la faragha kati ya Petro na Wamataifa fulani lakini kanisa lote liliathirika na asili yenyewe ya injili ilikuwa mashakani, Paulo hakwenda kwa Petro kwa faragha (kulingana na **Mat 18:15-16**) lakini alimkabili hapo hapo *hadharani* (angalia **Ef 5:11; 1 Tim 5:20**). Petro alikuwa akionyesha kujitenga, kwa namna ya ubaguzi wa kikabila kinyume na injili. Hii ndiyo maana Paulo hakumshambulia kwa misingi hiyo kwamba Petro alikuwa akionesha ubaguzi wa kikabila, au rangi, au chuki, au kwa namna ya kuumiza, ingawa vitendo vyake viliashiria hayo yote. Badala yake, Paulo aliyaelekeza mashambulizi yake kwenye kiini halisi cha jambo, ambalo ni kwamba Petro alishindwa *"kuwa muwazi kuhusu ukweli wa injili"* (**mst. 14**). Biblia ya NIV inatafsiri kama ni kushindwa*"kuendana na ukweli wa injili."* Petro aliikana injili kwa kuwatenga Wamataifa katika kushiriki kikamilifu kwa usawa maisha ya kanisa. Alikuwa pia akiwanyima kujiamini kikamilifu katika *maisha yake ya faragha* (yaani, kwa wale aliokula nao) kwasababu ya ukweli kwamba walikuwa Wamataifa. Kusema kweli, ijapokuwa alijua vema kuliko wengine, Petro alikuwa anaifanya injili ionekane ni ya "Wayahudi peke yao." Hili ni kinyume chake kabisa cha vuguvugu zima la historia ya wokovu na hupelekea kupindua Agano Jipya na kulirejesha Agano la Kale.

Mk 2:14-17 na **Gal 2:11-14** ni maandiko muhimu sana kwa kanisa la leo. Swala linalotukabili linaweza lisiwe ni nani tunakula naye. Maswala yanayofanana na hili hutokea wakati wowote wakati kanisa au mkristo binafsi anaponyimwa uanachama, nafasi ya uongozi, ushirika, au usawa kamili kwasababu za kikabila, uzawa, hali ya kiuchumi, au sababu ingine inayofanana na hii. Hili lilikuwa tatizo kubwa siyo tu kule Galatia lakini pia katika kanisa la kwanza kule Yerusalemu (angalia **Mdo 6:1; Yak 2:1-13**); inaendelea kuwa tatizo kubwa kwa kanisa duniani kote leo. Hili linaakisiwa katika kukosekana kwa ushirika miongoni mwa madhehebu. Inaeleweka, sote tunawaza kuwa theolojia yetu ndiyo sahihi na ya wale wasiokubaliana nasi ndiyo ina makosa. Hata kama tuko sahihi katika theolojia yetu, hata hivyo, tunaweza tukawa sahihi kwa namna ile ile ambayo Petro alikuwa sahihi: imani yake ya ndani kuhusu kuwa kitu kimoja Wayahudi na Wamataifa katika Kristo ilikuwa sahihi, lakini kwa kuwa hakutafsiri imani hiyo ya ndani katika uhalisia wa vitendo chanya kuhakikisha kuwa Wamataifa wanatendewa kwa haki, Petro, alikuwa mnafiki ambaye *"hakuwa muwazi kuhusu ukweli wa injili."* Kwa hilo, alikuwa amegeuza urithi wake wa Kiyahudi na desturi kuwa sanamu. Hii ni hatari. Injili ni *ukweli,* na ukweli kimsingi huathiri nanmna tunavyoishi kadhalika na nini tunaamini. Kama makanisa (na mtu binafsi) hawatajichunguza na kubadilisha matendo yao kuwaleta

[8] Hili ni muhimu zaidi kuliko tunavyoweza kutambua. Wakati "watoza ushuru na wenye dhambi" waliokula na Yesu katika **mis. 15-16** ni wazi imekuwa utaratibu wa kidini hakufuatwa, wasioamini wa kati huo walikutana na Yesu, Yesu kula na watu kulienda mbali zaidi ya kula na "watoza ushuru na wenye dhambi.' Katika **Uf 3:20**, kwa mfano, Yesu anasema, *"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kuufungua mlango, nitaingia kwake, nami nitakula pamoja naye, na yeye pamoja nami."* Yatupasa kukumbuka kwamba Yesu alisema maneno haya kuhusiana na kuongea na kanisa la kule Laodikia. Kwa maneno mengine, anachosema, ni kwamba hata katika kanisa lenyewe, ijapo kuna watu wanaohudhuria mara kwa mara, wanatoa sadaka mara kwa mara, na wanaoonekana kwa n je kuwa ni Wakristo, kummbe, *sio* Wakristo, hawajazaliwa mara ya pili kiuhalisia, *hawajaokoka,* hawajaingia katika mahusiano ya karibu naya upendo na Yesu Kristo mwenyewe. Tutajadili hili zaidi hapo chini kuhusiana na "kaka mkubwa" katika mfano wa Yesu katika **Lk 15**.

katika kuoana na yale yanayoletwa na injili, hukumu ya Mungu siku ile ya hukumu inaweza kutukuta kama watu ambao hatukuwa waamini waaminifu au makanisa kabisa lakini tulikuwa wanafiki na waabudu sanamu.

- Pili, kama Yesu alivyomsamehe mtu yule aliyepooza katika **mst. 1-12** inatuelekeza kwenye ukweli kwamba Yesu mwenyewe angelichukua dhambi za mtu yule msalabani, hivyo, ile karamu au chakula ambacho Yesu alishiriki na Lawi na marafiki zake ilikuwa ni kutuonesha "karamu ya kimasihi" na "chakula cha harusi ya mwana kondoo" katika **Uf 19:6-9**. Hili limetabiriwa katika **Isa 25:6** (*"Na katika mlima huu Bwana wa majeshi atawafanyia mataifa yote karamu ya vitu vinono, karamu ya divai iliyokaa juu ya urojorojo wake, karamu ya vinono vilivyojaa mafuta, karamu ya divai iliyokaa juu ya urojorojo wake, iliyochujwa sana"*). Karamu ni kwa *"watu wote"*bila kutofautisha. Hili limeakisiwa pia katika Ufunuo, ambako inasema kwamba *"kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi"* (**Uf 5:9-10**; angalia pia **7:9**). Hata hivyo, katika **Mat 8:11-12** Yesu anaweka wazi maonyo kwamba alichosema kwa Waandishi na Mafarisayo hakikuwa mzaha katika **Mk 2:17**. Katika Mathayo Yesu alisema, *"Nami nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa mbinguni; bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno."* (angalia pia **Mat 21:28-32; 22:1-14; Lk 13:22-30; 14:7-24**) Kwa maneno mengine, wakati neema ya Mungu inawafikia watu wa aina zote, ni wale tu waliounganishwa na Yesu Kristo kwa imani watakaoshiriki "karamu ya kimasihi" na "chakula cha harusi ya Mwana kondoo." Wale wanaomkataa Kristo watakuwa mahali ambapo kutakuwa na *"kulia na kusaga meno."*

2. <u>Hitaji letu la Neema na msamaha wa Mungu.</u>

Matamko ya Yesu kwa Waandishi na Mafarisayo katika **mst. 17** (*"Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi."*) yanaakisi sehemu nyingine muhimu ya injili na ufalme. Ambapo **mst. 1-12** inaonesha Yesu ni nani na kwamba yeye pekee ana uwezo na mamlaka ya kusamehe watu, **mst. 17** unafunua *hitaji* letu la msamaha. Mungu ni mtakatifu, mwenye haki, na mwema (**Mwa 18:25; Kut 34:6-7; Lawi 11:44; Ayb 34:10-12; Zab 5:4; 136:1; 145:17; Hab 1:13; Rum 1:18; Yak 1:13**). Kwasababu Mungu mwenyewe ni mtakatifu na mkamilifu kimaadili, hicho ndicho kiwango anachotushikilia (**Mat 5:48**). Yesu anavyotofautisha kati ya "wenye afya" na "wagonjwa," "wenye haki" na "wenye dhambi" inatuonesha ukweli kwamba *wote* ni "*wagonjwa*"; *wote* ni "wenye dhambi."[9]

Ingawa mwanadamu wa kwanza (Adamu na Eva) waliumbwa bila dhambi, walichagua kumfuata Shetani na kumuasi Mungu na kwasababu hiyo wakawa wenye dhambi (**Mwa 3:1-19**). Matokeo yake, kila mwanadamu ni mwenye dhambi kwa kuwa Adam na eva wamezaliwa katika hali ya uharibifu wa kimaadili unaojulikana kama dhambi ya asili; dhambi hii ya asili ni "sheria' au nguvu ambayo iko hai ikitenda kazi ndani ya kila mtu (mf., **Mwa 6:5; Zab 51:5; Yer 17:9; Rum 3:9-18, 23; Rum 7:5, 8-11, 14-24; Gal 3:21-22; 5:17; Ebr 3:12-13**). Inatuingiza katika hali ya dunia yote kujitambua kama wadhambi kadiri tunavyoendelea na maisha (**Mwa 8:21; Zab 51:5; 143:1-2; Yer 17:9; Mk 7:20-23; Rum 3:9-18, 23; 5:12-14; 7:14-24**). Kama Paulo alivyoonesha katika **Rum 3:10-12**, *"Hakuna mwenye haki hata mmoja. [11]Hakuna afahamuye; Hakuna amtafutaye Mungu. [12] Wote wamepotoka, wameoza wote pia; Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja."* "ugonjwa" wa dhambi yetu siyo jambo dogo linaloweza kutoweka lenyewe; ni la kuleta mauti (angalia **Ef 2:1**, *"mlikuwa <u>wafu</u> katika makosa na dhambi zenu"* na **Rum 6:23**, *"mshahara wa dhambi ni mauti"*; angalia pia **Mwa 2:17; Ezek 18:4, 20; Rum 5:12**).

Kwa ufupi, tatizo letu liko ndani mwetu, katika mioyo yetu (yaani, ndani ya utu wetu), na hatuwezi kubadilisha miyo yetu sisi wenyewe (**Mat 15:16-20; Mk 7:14-23**). Tatizo la wanadamu ni kwamba kamwe hatuwezi kufikia viwango vya Mungu vya utakatifu na ukamilifu sisi wenyewe, kwa kuwa "mara mtu anapotenda dhambi, haiwezekani tena milele kuwa mkamilifu" (Sproul 2002: 94). Hakika, hata matendo yetu mema yana vinasaba vya dhambi. Kama tunatenda matendo mema, hata kama kwa sehemu ili tupate kibali cha Mungu au kuepuka adhabu ya Mungu na kuzimu, hilo peke yake lafanya matendo yetu kuwa *siyo* "mema," kwasababu nia yetu ni ya ubinafsi na kujijali, hilo lenyewe ni dhambi. Zaidi ya hayo, hakuna kiwango cha matendo mema kinachoweza kubadilisha asili ya dhambi na matamanio ya dhambi katika moyo. Hivyo, matendo mema hayabadilishi uharibifu, watu wenye dhambi kuwa wenye haki, wasio na dhambi; ndani kabisa, wanabakia watu wenye dhambi. Kwa kuwa hakuna kiasi cha shauku, utashi, desturi, dhabihu, au matendo

[9] Katika kutofautisha kwake kati ya "wenye afya" na "wagonjwa," "wenye haki" na "wenye dhambi," Yesu *hakumaanisha* kwamba Mafarisayo walikuwa "wenye afya" na "wenye haki" na hawahitaji wokovu anaouleta. Hilo linaonekana wazi katika kushughulika nao katika AJ lote. Kwa mfano, katika **Yohana 8** Yesu alisema kwamba walikuwa watumwa wa dhambi (**Yh 8:34**), hawakuwa wana wa Abrahamu (**Yh 8:39),** na walikuwa wana wa ibilisi (**Yh 8:44**).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mengine yanayoweza kubadilisha tatizo la msingi la uharibifu wetu wa ndani na hali yetu ya dhambi katika mioyo yetu, hakuna desturi, dhabihu, 'matendo mema," au matendo mengine ambayo kamwe yanaweza "kutuletea haki yetu" au "kutupa nafasi" ya kuingia mbinguni, wokovu, au kibali kwa Mungu (**Gal 2:16**).

Hii ndio maana Yesu alilazimika "kutuita" (**mst. 17**); hatuwezi kupata kibali kwa Mungu na kuuingia ufalme sisi wenyewe. Injili ni habari njema ambayo, katika Kristo, Mungu amefanya kwa ajili yetu kile ambacho tusingeweza kutenda sisi wenyewe. Kwasababu Yesu aliishi maisha tuliyopaswa kuishi na *"alijaribiwa katika mambo yote kama sisi, bila kutenda dhambi"* (**Ebr 4:15**), yeye peke yake alistahili kuwa mwakilishi wetu, kuchukua juu yake mwenyewe dhambi zetu na kulipa adhabu ambayo tulipaswa kulipa lakini tusingeweza (**Rum 8:1-4; 2 Kor 5:21; Gal 3:13; Kol 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; 1 Pet 2:24**). Kufufuka kwa Yesu kutoka kwa wafu na kupaa kurudi kwa Baba kulithibitisha alikuwa nani na kuonesha kwamba Baba alikubali dhabihu yake pale msalabani kwa ajili yetu. Hivyo, wokovu ni—na unawezekana tu—*kutolewa* na Mungu kwa watu kama *zawadi* ya *neema* yake. Wokovu —unaweza *kupokelewa* na watu kwa *imani* peke yake katika Kristo. Kama **Ef 2:8-9** inavyosema, *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.* Kuokolewa ina maanisha kutubia dhambi zetu, kukubali kwa imani kile Kristo alichofanya kwa ajili yetu, na kumgeukia Kristo kama Bwana wa maisha yetu, (**Mat 11:28; Mk 1:14-15; Yh 1:12; 3:16; 17:3; Mdo 26:20; 1 Yh 1:8-9** Katika Kristo tunakuwa huru mbali na hatia na hukumu ya dhambi kana kwamba tumejilipia gharama kamili ya dhambi zetu (**Rum 6:3-7; Gal 2:20**). Kusema kweli, tunapomgeukia Kristo kwa imani, siyo tu kwamba anajitwisha dambi zetu yeye mwenyewe na kulipa gharama ya dhambi zetu ambayo tulipaswa kulipa, lakini pia anatupatia haki yake ili tustahili kusimama mbele za Mungu (**Isa 53:5-6, 10-11; Rum 10:4; 2 Kor 5:21; Ebr 2:17-18; 1 Pet 2:4; 3:18**).

3. <u>Asili ya msingi ya uhalisia wa kuzaliwa mara ya pili</u>

Mistari 14 unasema, *"Hata alipokuwa akipita, akamwona Lawi wa Alfayo, ameketi forodhani, akamwambia, Nifuate. Akaondoka akamfuata."* Gundua kwamba Yesu ndiye aliyemfikiria Lawi na kumuita; Lawi hakuwa anamtafuta Yesu. Hiki ni kielelezo cha utaratibu wa wokovu: Mungu ndiye msingi—lazima afanye upya mioyo yetu kwanza; ndipo tunaweza kuitikia kwa imani na utii. Timothy Keller anaeleza, "Dini [yaani, dini yeyote isipokuwa ukristo] hutenda kazi kwa kanuni ya "nina tii—kwahiyo ninakubaliwa na Mungu.' Lakini kanuni inayotenda kazi kwa injili ni 'ninakubaliwa na Mungu kwa njia ya kile alichofanya Kristo—kwahiyo nina tii.'" (Keller 2008: 179-80)

Wito wa Lawi unawakilisha, labda vizuri zaidi kuliko katika visa vingine, asili ya msingi ya maana ya kuzaliwa mara ya pili. Kuna angalau sababu mbili katika hili. Walter Wessel anaonesha kwamba, "kulikuwepo na mambo mengi yaliyokuwa mbele ya Lawi katika kupokea changamoto ya Yesu. Wavuvi wangaliweza kurudi kirahisi kuvua samaki (kama ambavyo baadhi ya wanafunzi walifanya baada ya kusulubiwa kwa Yesu [angalia **Yh 21:3**]), lakini kwa Lawi nafasi ya kurudi katika kazi yake ingelikuwa ndogo sana. Kazi ya mtoza Ushuru ilifikiriwa kama njia ya hakika ya kupata utajiri kwa haraka." (Wessel 1984: 634) Kwa nyongeza, kama tulivyojadili hapo juu, watoza ushuru walidharauliwa na, kimsingi, walifikiriwa na Wayahudi wengine kuwa wasaliti kwa Israeli. Kwa kumfuata Yesu, Lawi atakuwa anaachana na washirika wake katika serikali yake na mahusiano ya kijamii na kujiungamanisha na kundi la watu ambao wangeweza kumdharau. Atakuwa akijifunza maisha mapya mageni kabisa kwa kila mtu aliyewahi kumfahamu au kuwa naye. Hiyo ni hatua kubwa sana! Hata hivyo Lawi alichukua hatua hiyo.

Inavutia kuona kwamba Agano Jipya lina mifano ya "watoza ushuru na wenye dhambi" ambao kwa uwazi kabisa walitambua asili haswa ya wokovu na nini kilimaanishwa katika maisha yao. Zakayo—mtoza ushuru mwingine—anaeleza hivi. Kwa mara nyingine tena, Yesu alimuona na *"kumpokea kwa furaha"* (**Lk 19:6**). Kama katika **Mk 2:16**), watu waliomuona Yesu akiwa na Zakayo "walinung'unika" na kusema, *"amekwenda na kuingia katika nyumba ya mwenye dhambi"* (**Lk 19:7**). Hata hivyo, ni muitikio wa Zakayo uliofunua kwa kina ni kiasi gani alielewa asili ya wokovu katika kugeuza maisha **Lk 19:8** inasema, *"Zakayo akasimama, akamwambia Bwana, 'Tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimenyang'anya mtu kitu kwa hila namrudishia mara nne'".* Sheria ilimtaka kila mtu kutoa fungu la kumi, yaani kutoa 10% (angalia **Law 27:30-33; Kumb 12:18; Hes 18:21-24**). Kama mtoza ushuru, Zakayo bila shaka alikuwa mtu tajiri. Alitambua kuwa 10% ilikuwa si kitu kwake. Pia alitambua kuwa, kwa kumfuata Yesu Kristo, alikuwa sasa chini ya "sharia ya Kristo." Matokeo yake, alijitolea kutoa mali zake kwa masikini. Zaidi ya hayo, sheria ya AK ilimtaka mtu kurudisha kiasi cha 120% tu na siyo 400%, kwa habari ya wizi au kumdhulumu mtu (angalia **Law 6:2-5; Hes 5:7**). Licha ya hayo Zakaria alijitolea na kuamua kurudisha kiasi cha mara nne cha kile alichomdhulumu mtu. Urudishaji wa kiasi kikubwa hivyo ulionesha wazi kwa nje kuwa moyo wake ulikuwa umebadilika. Na fikiria kuhusu msukumo wake wa ndani: Msukumo wa ndani wa Zakayo ulikuwa ni

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kumpendeza Bwana. Ona matamko yake, *"Bwana, tazama!"* (au, *"Bwana, angalia!")* ni kama mtoto mdogo anaposema "Mama, Angalia!" au "Baba, Angalia! Ona ninachofanya!" Zakayo alikuwa akifanya alichodhani kuwa kitampendeza Bwana. Hiyo inapaswa kuwa ndiyo hali yetu pia.

Mfano kama huo unapatikana katika **Lk 7:36-50**. Hapo, *"mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi"* (**mst. 37**) alileta chupa ya marimari yenye marhamu na *"Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kumdondoshea miguu machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu-busu miguu yake na kuipaka yale marhamu"* (**mst. 38**). Simioni, Farisayo ambaye Yesu alikuwemo chakulani akawa akijisemea kwamba *"ni mwenye dhambi"* (**mst. 39**). Ndipo Yesu akamwambia Farisayo mfano na kuhitimisha akisema, *Kwa ajili ya hayo nakuambia, Amesamehewa dhambi zake ambazo ni nyingi, —kwa kuwa amependa sana. Lakini asamehewaye kidogo, huyo hupenda kidogo"* (**mst. 47**). Kama ukweli huu ulivyokuwa kwa Zakayo, mwanamke huyu alijua asili ya mageuzi ya maisha yaletwayo na wokovu, na alidhihirisha hilo kwa vitendo. Alikwenda kwa nyumba ya Farisayo akijua alimuonaje, alijinyenyekesha na kujifedhehi mwenyewe kwa kubusu miguu ya Yesu na kuifuta kwa nywele zake, na kutoa marimari yenye marhamu ya bei kubwa,[10] yote hayo kwa kumpenda na kumshukuru Yesu.

Inakuwa hivyo, "Watoza ushuru na wenye dhambi" wanaonesha imani yao bila mipaka kwasababu wanaelewa kina cha maana ya mabadiliko ya maisha hayo mapya katika Kristo. Ambao ni mlinganisho wa wazi kati ya maisha waliyokuwa nayo na yale wanayoitiwa na kuwezeshwa sasa kuyaishi. Tunaliona hilo katika **Lk 18** katika mfano wa Yesu kuhusu Farisayo na Mtoza ushuru waliokwenda hekaluni kuomba. Wakati kimsingi Farisayo alijiinua mwenyewe, "Mtoza ushuru, akiwa amesimama mbali, hata asiweze kuinua macho yake mbinguni, bali kujipiga kifuani, akisema, 'Mungu, unirehemu mimi, mwenye dhambi!'" (**Lk 18:13**) Michael Spencer anahitimisha kwa kusema, "Tunachopata kutokana na haya yote kinashangaza hasa. Ukristo siyo dini ya kujifanya wenyewe tukubalike kwa Mungu. Kama tunaamini tumekubalika kwake, basi tumepishana naye. Badala yake, Ukristo ni mahusiano ambapo moyo wa Mungu humuelekea mwenye dhambi, aliyevunjika, aliyekataliwa na kutengwa. Mungu husimama na wenye dhambi na kula pamoja nao, akituonya sisi ambao ni washika dini kwamba, kwa kujitangaza kuwa tu salama, tunasimama katika hatari ya kutokusikia sauti ya Muumba ikituita kwake. Mtazamo kama huu hauondoi haja ya Ukristo kuhusisha utakatifu wa Mungu na hukumu juu ya dhambi, hili likiwa ni jambo la msingi katika Biblia. Lakini tukisema kuwa tunamuona Mungu kama alivyojifunua katika Yesu, basi tutakuwa tunadai kuwa tunamuona Mungu ambaye rehema zake zinawatafuta wenye dhambi halisi waliojikwaa katika utakatifu wake, akiwa pia amebeba gharama ya kuwaokoa. Haya ndiyo yanayoletwa na msalaba, na hili ndilo ambalo mtume Paulo anasema kwamba msalaba ni upuzi kwa dunia lakini ni nguvu kwa wale wanaookolewa." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – Calling the Tax Collector")

4. <u>Asili ya wapinzani wa Yesu</u>

Mistari 16 unatuambia kwamba *"waandishi na Mafarisayo, walipoona alikuwa anakula na wenye dhambi na watoza ushuru, waliwaambia wanafunzi wake, 'Mbona anakula na watoza ushuru na wenye dhambi?'"* Ingawa mwito wa Yesu kwa Lawi na kula pamoja naye na wenye "dhambi" wengine ulifunua uthaminishaji na vipaumbele, mwitikio huu wa waandishi na Mafarisayo ulifunua hali yao ya ndani na vipaumbele vyao. Hata hivyo, mwitiko wao siyo wao peke yao; bali, mwitikio wao uliakisi hali ya ndani ya watu wengi, angalau miongoni mwa wale "walioheshimika" zaidi na watu walioshika dini. Ni hali ya dunia, kama **1 Sam 16:7** inavyosema, *"Wanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo."* Tatizo siyo tu kule "kuangalia kwetu kwa nje," lakini kwamba pia huwa *tunachagua* sana neno la "muonekano wa nje" la kuangalia au kulisimamia. Hivyo waandishi na Mafarisayo wao waliona tu kwamba Yesu alikuwa anakula na "watoza ushuru na wenye dhambi." *Hawa*kufikiria ukweli mwingine kwamba maisha ya watu hawa yalikuwa yameingia katika mchakato wa kina wa kubadilishwa na Yesu. Wala hawakufikiria sababu zinazowezekana kuwa ziliwasukuma watu kuishi maisha ya "dhambi" au juhudi mbalimbali walizofanya ili kubadilisha hali yao au hali zilizo wasukuma kijamii kuiga maisha kama hayo. Hali yao iliakisi ubaguzi uliooneshwa na watu wa dini katika **Yak 2:1-13** kwa mtu tajiri, mwenye mavazi mazuri dhidi ya masikini, aliyekuwa amejivalia ovyo. Hata hivyo, kama Douglas Moo alivyoona, kwamba *kanuni* anayojadili Yakobo inahusu "kutokumchukulia mtu yeyote kwa misingi ya anavyoonekana kwa nje—iwe kabila, utaifa, utajiri, au namna alivyo vaa" (Moo 1989: 1155).

Hali ni ya ndani zaidi kuliko tunavyoiona kwa nje na kuwapendelea watu "kama tunavyojipendelea." Ni hali ambayo watu wote wanaweza kubebwa nayo, hasa kwa watu ambao wanaheshimika na watu wa dini ambao

[10] Kama kibweta cha marimari kilikuwa kama manukato katika **Mat 26:6-13** na **Yh 12:1-8** kingekuwa na thamani ya dinari 300, yaani, sawa na mshahara wa mwaka mzima.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

"siyo watoza ushuru." Kwa kawaida ni hali ya ndani inayosema, "nimetimiza sheria, na wewe pia inakupasa kutii"; nimefanya kazi kwa bidii na kujipatia kitu fulani, na wewe pia unapaswa kufanya hivyo; Nimekwenda kanisani na kulipa fungu langu la kumi; kwahiyo Mungu anapaswa kunibariki, lakini (umasikini) wako, (hali yako mbaya kimwili, maisha yako mabovu) ni makosa yako mwenyewe—huna wa kumlaumu, kwahiyo, usinifuate kuomba msaada."

Hali hii inadhihirishwa na kaka mkubwa katika mfano wa "mwana mpotevu" katika **Lk 15:11-32**.[11] Mfano huu wengi tunaufahamu. Ni muhimu kutambua kwamba, mwanzo mwa mifano mitatu Aliyoisimulia Yesu katika **Luka 15** (mfano wa "mwana mpotevu" ni wa tatu), alikuwa anaongea na makundi mawili ya watu *"watoza ushuru na wenye dhambi"* na *"Mafarisayo na waandishi"* (**Lk 15:1-2**). Timothy Keller anatuonesha haya, "Aina hizi mbili za watu zinaendana na ndugu wawili wa kiume katika mfano uliofuata. Watoza ushuru na wenye dhambi ni kama yule kaka mdogo katika mfano huo. Wamekuwa wakijihusisha na matendo maovu, na maisha yasiyo na maadili ya kidini (ms.13). Wameasi desturi za kimaadili za familia zao. Hata hivyo, Mafarisayo na waandishi wa sheria, ni kama kaka mkubwa katika mfano huo. Wametunza desturi za kimaadili ya kukua kwao. Wamejitoa hasa kujifunza na kutii Neno la Mungu. Mara kwa mara wanaomba na kuabudu." (Keller n.d.: "The Two," n.p.)

Katika mfano huu, "Yesu anatuonesha baba wa watoto wawili, na wote wametengwa sawa katika moyo wake. Mmoja amedhihirishwa kutengwa kwake kwa kukimbilia nchi za mbali, lakini kaka mkubwa yeye ni hasira tu sawa na mgeni kwa baba. Baba lazima 'atoke' kumwendea kila mmoja wao kumsihi aingie ndani (mst. 20, 28). Lakini hapa kuna sehemu muhimu. Mmoja wa wanawe ni mtu mzuri sana, na mwingine ni mwovu sana, lakini mwishoni, ni yule mwovu ndiye anaingia katika sherehe ya baba yake na kucheza na huenda anayeonekana kuwa huenda asishiriki ni yule kijana mzuri." (Ibid.) Lakini kwanini kaka mkubwa abakie nje badala ya kushiriki sherehe. Kaka mkubwa anatuambia: "ni kwasababu miaka yote hii nimekutumikia na sijawahi kukuasi... (mst.29). Siyo ubaya wake unaomweka nje, bali 'wema' wake. Siyo dhambi zake zinazomtenga na sherehe ya baba bali 'haki' yake. Kaka mkubwa mwishoni anakuwa mpotevu, siyo kwa kudharau aliyoyatenda bali kwasababu ya hayo." (Ibid.)

Kwa maneno mengine, hakuna njia moja tu ya kuwa mbali na Mungu, bali njia mbili, tunajua ni njia moja ni kuvunja sheria ya Mungu na kuishi maisha ya anasa kama yule kijana mdogo. Njia nyingine ya kutuweka mbali na Mungu ni *kutunza sheria yake* kama yule kijana mkubwa. Kwanini kaka mkubwa alikasirika hivyo? Keller anaeleza kwa kifupi: "Anajisikia ana haki ya kumwambia baba cha kufanya kuhusiana na vazi, pete, na ndama. Inaonesha kuwa alijisikia vibaya baba yake alivyotawala mali zake sawa tu na mdogo wake. Kijana mdogo alikwenda zake aepushe mali zake na kutawaliwa na baba yake, lakini kaka mkubwa alibaki nyumbani na "hakuwahi kuasi" utaratibu wa kufanya jambo lile lile. Katika mioyo yao wote walifanana. Wote walikuwa wanajaribu kuepuka utawala wa baba, wote hawakupendezwa na utawala wake na waliasi. Lakini mmoja alifanya hivyo kwa kuvunja sheria yote ya baba, na mwingine kuzitunza sheria." (Ibid.)

Hili ni muhimu kwetu kujua kwa kuwa, ingawa kuna baadhi ya "kaka wadogo" katika kanisa, watu wengi katika kanisa hawakuwa makahaba, walevi wa madawa ya kulevya, wezi, au wauaji; walio wengi kanisani ni watu wa dini kwa kuwalinganisha, watu wanaoheshimika wanajitahidi kutunza taratibu na kufanya yaliyo sawa. Swala, hata hivyo, ni *msukumo wa ndani:* Tofauti kati ya mtu wa dini na mkristo wa kweli ni kwamba mtu wa dini hutii ili ampate Mungu. Mtu wa dini anatii ili amshawishi Mungu, amtawale, amweke katika nafasi wanayodhani wanamdai. Kwahiyo, licha umakini wao katika maswala ya maadili na dini, kusema kweli wanajaribu kujiokoa wenyewe. Wakristo, wanaojua kuwa wameokolewa kwa neema na hawawezi kamwe kumtawala Mungu, wanamtii kwa shauku ya kupenda na kumpendeza na kumweka karibu yeye aliyewaokoa." (Ibid.)

Jambo tunalopaswa kutambua ni kwamba, kama tunavyoona katika mfano wa **Luka 15**, na mwitikio wa Mafarisayo katika mazungumzo ya Yesu na "watoza ushuru" katika AJ, ni kwamba ni rahisi kuwaleta kwa Yesu "akina kaka wadogo" kuliko kaka wakubwa." Yesu na injili wanakuwa na mvuto zaidi kwa kaka mdogo, kwasababu wao hutambua kwa urahisi hali zao za kupotea na uhitaji wao kuliko kaka mkubwa. Ni kwasababu kaka wakubwa hutunza sheria na wanaheshimika na wamefanikiwa kiasi kwamba hawatambui mahitaji yao kabisa. (au ugumu wa mioyo yao wenyewe). Hivyo, yatupasa tusikie maonyo ya Kristo na kufundisha watu wetu kwamba *"watoza ushuru na makahaba wanawatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu. Kwa sababu Yohana alikuja kwenu kwa njia ya haki, ninyi msimwamini; lakini watoza ushuru na makahaba walimwamini, nanyi hata mlipoona, hamkutubu baadaye, ili kumwamini."* (**Mat 21:31-32**)

[11] Kusema kweli mfano unapaswa kuitwa mfano wa baba na vjana wawili wa kiume, kwa kuwa kunamengi ya kusemwa kuhusu baba na kijana mkubwa kama ilivyo kwa kijana mdogomwana ("mpotevu").

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

MASWALI YA KUJADILI

1. Inakuwaje, kama chochote, chaweza kufanya uamuzi wa Lawi kuwa na uzito zaidi kuliko, kwa mfano uamuzi wa Petro, Yakobo au Yohana?

2. Kama Yesu ni Mungu katika mtu, basi namna alivyowatendea watu laweza kuwa sehemu muhimu zaidi ya ujumbe wa injili. Unafikiri hilo ni kweli? Kwanini au kwanini hufikiri hivyo?

- Yesu aliwachukuliaje watu?

- Kwanini ni muhimu kwamba tuone alivyowachukulia watu?

3. Leo, Wakristo wengi wanaonekana kufikiri na kutenda kama Yesu (kama angekuwepo leo hapa) huenda angeonekana kanisani au huenda kwenye mgahawa ambao hauuzi pombe (tofauti na kwenda kwenye baa), na kwamba marafiki zake wangekuwa wahubiri, na siyo makahaba. Unafikiri tungemkuta Yesu wapi? Kama ni mahali fulani "pasipo heshimika" kama kanisani au kwenye mgahawa usiouza pombe, uko tayari kwenda huko?

4. Leo, nani anaonekana kama "mtoza ushuru"? Inakuwaje tukionekana tuna jambo na mtu kama huyo?

5. *Kula* na watoza ushuru kuna mashiko gani?

6. Wakati wa Yesu, watu waliokataliwa katika jamii walimwendea Yesu kwa wingi kwasababu walijua alikuwa upande wao na aliwapenda na kuwasamehe. Je wengi waliotengwa katika jamii leo wanakimbilia kanisa kwasababu wanajua liko upande wao na linawapenda na kuwasamehe? Kwanini au kwanini siyo hivyo?
- Kama siyo hivyo, kwani nini siyo hivyo, na nini kinapaswa kifanyike?

7. Jadili "njia mbili za kuwa mbali na Mungu" yaani, kuwa kama kaka mdogo katika **Lk 15** na kuasi sheria dhidi ya kuwa kama kaka mkubwa na kuzitii.

- Kama tukielewa hili, kwanini iwe vigumu kuwaleta "kaka wakubwa" kwa Kristo?

- Ni kwa namna gani kuelewa aina mbili za wakaka—na ukweli kwamba huenda watu wengi kanisani wako upande wa "kaka mkubwa"—huathiri namna tunavyohubiri na kuwasilisha injili?

2:18-22: ***[18] Nao wanafunzi wake Yohana na Mafarisayo walikuwa wakifunga; basi walikuja, wakamwambia, Kwani wanafunzi wa Yohana na wanafunzi wa Mafarisayo hufunga, bali wanafunzi wako hawafungi? 19Yesu akawaambia, Walioalikwa arusini wawezaje kufunga maadamu bwana-arusi yupo pamoja nao? Muda wote walipo na bwana-arusi pamoja nao hawawezi kufunga. [20]Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana-arusi, ndipo watakapofunga siku ile. [21]Hakuna mtu ashonaye kiraka cha nguo mpya katika vazi kuukuu; ikiwa ashona, kile kipya kilichotiwa huliharibu lile vazi kuukuu, na pale palipotatuka huzidi. [22]Wala hakuna mtu atiaye divai mpya katika viriba vikuukuu; ikiwa atia, ile divai mpya itavipasua viriba vile, divai ikamwagika, vile viriba vikaharibika. Bali hutia divai mpya katika viriba vipya."***

mst. 18-22—Yesu na kufunga: umuhimu wa Kristo

Katika mtiririko huu wa matukio ya huduma ya Yesu, hili ndilo jambo moja ambalo hakupingwa au kuhojiwa na wapinzani wake. Badala yake, watu walioona kwamba wanafunzi wa Yohana walifunga na Mafarisayo walifunga, lakini wanafunzi wa Yesu hawakufunga, walijiuliza kwanini kuwe na tofauti hiyo.[12] Hata hivyo, walichomaanisha katika swali lao kiko katika kulaumu Mafarisayo, hasa kwamba Yesu alikuwa anavunja desturi. Hivyo, swali na jibu la Yesu vinaturudisha kwenye swala lililoibua mambo katika **mst. 1-12**, yaani Yesu ni nani, na pia katika swala lililoibuliwa **mst. 13-17**, Yesu anafanya nini.

[12] Katika **Mat 9:14-17** na **Lk 5:33-39**, matukio yote, kama yale ya **Mk 2**, Mara baada ya kuitwa kwa Lawi. Katika Mathayo, wale walioliza swali walitambuliwa kama wamafunzi wa Yohana Mbatizaji. Katika Luka, inasema "wali"muuliza; hiyo "wali" haikubainishwa kipekee, lakini waandishi na Mafarisayo walitajwa, kwa kuwa walikuwa wametajwa kabla hapo.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

1. Kufunga katika AK

Katika sheria kufunga kulihitajika tu siku ya upatanisho (**Law 16:29, 31; 23:27-32; Hes 29:7**). Baada ya kutoka uhamishoni, kufunga kwa aina zingine nne zaidi zilitekelezwa (**Zak 7:5; 8:19**). Mifungo wakati mwingine iliitwa na viongozi na manabii katika kuitikia tukio maalumu, kama vile nyakati za hatari za kitaifa, toba au unyenyekevu (**2 Nyak 20:3; Ezra 8:21-23; Neh 1:4-11; Yer 36:9; Yoeli 1:8-2:17**). Mifungo pia ilifanyika kibinafsi kwa sababu mbalimbali (**2 Sam 12:15-23; 1 Fal 21:27; Zab 69:1-15, 35:13-14, 109:4-21**).

2. Yesu na kufunga: Yesu kama Bwana harusi

Yesu alifunga wakati wa majaribu yake kule jangwani (**Mat 4:2**). Ijapo hakukana kufunga, hakuwapa wanafunzi wake maagizo yeyote au ushauri wa desturi ya kufunga. Moja ya sababu ya hili inaonekana katika jibu la Yesu katika **mst. 19** kwa swali kuhusu kwanini wanafunzi wake walikuwa hawafungi. Michael Spencer anatuonesha, "Kipindi kimoja ambacho kufunga kulikatazwa ilikuwa ni wakati wa sherehe za harusi. Maadamu kwa majuma mawili bibi harusi na bwana harusi walizungukwa na kusherehekea na marafiki, waliojulikana kama 'watoto' wa bwana harusi. Kwa watu wengi, sherehe hii ilikuwa ndiyo sherehe kubwa zaidi katika maisha yao na lilikuwa ni tukio la shamra shamra kwa jamii yote. Huzuni ilipigwa marufuku na kufunga kungeonekana kituko na usaliti. Hadhira ya kwanza ya Yesu katika karne ya kwanza wangecheka wazo kama hilo. Yesu anajilinganisha na bwana harusi. Bibi harusi anaweza akawa amengoja kwa miaka kuja kwa bwana harusi wake kumchukua kwenda kwa familia yake, kama Wayahudi walivyoingojea ahadi ya yeye aliyehidiwa. Kipindi hiki wakati Yesu yupo na analeta shangwe na kujisikia vizuri kunakotokana na ufalme wa Mungu siyo wakati wa kufunga, bali ni wakati wa kuzama katika shangwe na furaha ya tukio hilo." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Bridegroom and The New Wine") Yesu alitenda kama hivyo katika **mst. 14-16** katika kusherehekea na Lawi na "wenye dhambi."

Mungu amejilinganisha na bwana harusi katika **Isa 62:5**. Sasa Yesu anasema, "*mimi* ni bwana harusi" (angalia pia **Mat 9:15; Lk 5:34-35; Yh 3:28-29**). Kwa kujiita mwenyewe bwana harusi, hapo Yesu alikuwa anasema alikuwa ndio utimilifu wa kila kitu AK kilisema kuhusu AJ. Wright anaonesha theolojia ya kina ya jibu la Yesu: "Kufunga katika kipindi hiki hakukuwa, kwa ajili ya Wayahudi, ilikuwa ni njia ya kujiadibisha, sehemu ya kuonesha kujitoa. Ilihusika na hali ya leo ya Israeli: alikuwa bado yungali uhamishoni. Kwa usahihi zaidi, ilihusika zaidi kuadhimisha kuharibiwa kwa Hekalu. Ahadi ya Zakaria kwamba mafungo yatageuzwa kuwa sherehe [**Zak 8:19**] inaonekana kuja kuwa kweli wakati YHWH atakaporejesha Baraka ya watu wake. Hilo, hasa, ndilo Yesu kwa namna ya fumbo alimaanisha [kuhusiana na wanafunzi wake kutokufunga na viriba vipya]. Kwa maneno mengine, sherehe imepamba moto, na hakuna anayetaka kuona uso wa huzuni harusini. Hiki siyo kipande cha 'mafundisho' juu ya 'dini' au 'maadili'; wala siyo hotuba ya ukweli usio na mwisho. Ni madai kuhusu eskatolojia. Muda umetimia; uhamishoni basi; bwana harusi anakaribia. Yesu alitenda kimafumbo kusherehekea badala ya kufunga, kunaleta wazi madai yake yaliokuwa na utata kwa uma, kwamba katika kazi yake tumaini la Israeli lilikuwa linabainishwa; kwa usahihi zaidi, kwamba katika kazi yake *Hekalu lilikuwa linajengwa upya.*Wale waliokuwa wamezoelea kuishi uhamishoni zaidi kiasi kwamba hawakuweza kusikia ujumbe wa ukombozi walikuwa viziwi hasa." (Wright 1996: 433-34)

Katika **mst. 20** Yesu anatoa angalizo, *"Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana-arusi, ndipo watakapofunga siku ile."* Huenda hili ni dokezo lililojificha la kusulubiwa kwake kulikokuwa kunakaribia na kupaa kwake kurudi kwa Baba. Tukidhani ndivyo ilivyokuwa, yapasa kutia akilini mwetu mambo kadhaa tunapofikiria swala la kufunga leo. Kwanza, hali yetu siyo sawa na ile waliyokuwa nayo wanafunzi ambapo Yesu alikuwa pamoja nao kimwili. Matokeo yake, **mst. 20** unapendekeza kwamba kufunga kwa Wakristo kunakubalika leo. **Mdo 13:1-3** na vitabu vya maandiko ya kanisa la kwanza yajulikanayo kama *Didache* (c. 70-110), sec. 8.1 yanaonesha kwamba kanisa la kwanza lilikuwa na kawaida ya kufunga. Pili, kufunga kunaweza kukawa nidhamu ya kiroho kwa mtu binafsi kujitoa kwa Mungu, kwa ajili ya kumtafuta Mungu, kutafuta mapenzi yake, na kutafuta uhusiano wa karibu naye, na sababu zingine kama hizo; kufunga pia kunaweza kuwa na faida mbalimbali za kiafya (angalia Wallis 1968: *passim*). Hata hivyo, kufunga, kama jambo la kinidhamu kama mengine, kunaweza kukafanyika namna ya sheria au kutusababisha tufikiri kwamba wale tunaofunga tunawazidi wale wasiofunga. Hiyo ndiyo iliyokuwa hali ya Mafarisayo katika **Lk 18:12** waliomwambia Mungu, "tunafunga mara mbili kwa juma." Yesu anasema ni kujiinua mwenyewe (**Lk 18:14**; angalia pia **Mat 6:16-18**). Kama Spencer anavyosema, "Ukristo unahitaji desturi ambazo zinaweza kuleta maana na zinaweza kutengeneza hali yetu ya kiroho, lakini wakati huo huo tunahitaji kuwa waangalifu kuepuka namna yeyote ya sheria, kujitaabisha, au namna mpya ya matambiko ya zamani. Tunapozungumzia kuhusu kufunga, kutoa fungu la kumi, au desturi zingine za kiroho ni lazima tukumbuke kwamba ni kwa njia pekee ya Yesu na alichofanya kinachotupa kibali mbele za Mungu. Tunampokea Roho Mtakatifu kwa imani, siyo kwa nguvu zetu au matambiko." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Bridegroom and The New Wine") Mwisho, wakati Yesu

akiwa hayupo pamoja nasi kimwili kama alivyokuwa na wanafunzi wa mwanzoni, siyo tu kwamba yuko nasi lakini yuko *ndani* yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu (**Yh 14:16-18**; angalia **Mdo 2:1-4; 1 Kor 3:16; Gal 4:6**). Matokeo yake, maisha ya Kikristo hayapaswi kutawaliwa na huzuni au uso mzito isipokuwa na shangwe na amani (angalia, kwa mfano., **Yh:27; Gal 5:22-23; Flp 4:4-7**). "Shangwe ya Wakristo siyo mihemko ya kujifanya, bali itikio la mtu mzima – roho, akili, utashi, mwili na mihemko – kwa uwepo wa kweli ya Mungu." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Bridegroom and The New Wine") Roho hutuongoza, hutuelekeza, hututia nguvu, na kuwasiliana nasi. Hebu tumkaribie na kuwa na ushirika wa karibu naye, na kama kufunga kunasaidia kukuleta karibu naye, basi vema.

3. <u>Kiraka katika vazi kuukuu na mvinyo mpya katika viriba vya kale</u>

Katika **mst. 21-22**, vielelezo vya Yesu vya kiraka katika vazi kuukuu na mvinyo mpya katika viriba vya kale vilikuwa vitu vinavyojulikana katika hadhira yake. Kielelezo cha **mst. 21** kinaonesha kuwa, "kama mtu atajaribu kushona nguo iliyokwisha sinyaa kwa kutumia kipande kipya cha nguo, kile kiraka kipya hatimaye kikianza kusinyaa kitaharibu kile kilichokwisha sinyaa, kwasababu kilichokwisha sinyaa hakina tena uwezo wa kuvutika" (Sproul 2021: n.p.). Kuhusiana na **mst. 22**, "Katika siku za Yesu, watu walitumia ngozi za wanyama—kama vile ngozi za mbuzi—kuwekea vimiminika. Vinywaji vilivyochacha kama vile mvinyo hutanuka, na kwa kuwa kiriba cha kale kitakuwa kilisha tanuka hadi mwisho wake, mvinyo mpya ungekipasua kule kiliposhonwa. Hii ndio maana mvinyo mpya ulihitaji kuhifadhiwa katika viriba vipya. Kadiri mvinyo ulivyotanuka, kiriba kilitanuka ili kutoa nafasi zaidi ya kuuhifadhi." (Jesus Film Project 1995-2021: "New wine and old wineskins") Na Yesu alikuwa anasema, kwa kumponya yule aliyepooza kwa neno lake tu na kwa kula na "watoza ushuru na wenye dhambi," alikuwa akionesha kwamba Mungu "hafungwi na desturi, bali huwafikia wenye dhambi kwa namna ya kushangaza. Haikuwa sheria ya Kiyahudi au ya Mungu wa Kiyahudi au moyo wa Myahudu mwenye msimamo mkali ambaye Yesu alimzungumzia; ilikuwa ni ule utii kwa namna ya dini isiyotembea na Mungu kufikia mambo na tumaini la mbeleni, badala yake ilikwenda kinyume nyume na kukaa katika desturi na, matokeo yake, kuwafunga watu katika dhambi zao za zamani. Yesu hakuja kukarabati mfumo kama huo. Hakuja kumimina mvinyo mpya katika kiriba cha kale. Dini za kidesturi mara zote watachana na kuondoa kipande wakati wa kazi yenye nguvu ya Roho Mtakatifu katika ufalme. Mugu anatenda kazi katika ufalme wake, akivunja kuta, akiweka watu huru, akiponya walioumizwa, ikiwa ni pamoja na waliokataliwa. . . . Yesu alikuwa anawakabili wote waliokuwa wanamfahamu kwa mambo muhimu ya kuchagua kuhusu mahusiano na Mungu yalipaswa kuwa ya namna gani na Mungu mwenyewe anafananaje. . . . Tunapaswa kutambua kwamba ile nguvu ya kupasua, kuchana ni matumizi yanayoendelea. Mahali popote, kwa mfano ambako asili ya kibinadamu na ya anguko, inatawala, Injili huleta uhai wenye nguvu na maisha mapya. Hii ni sehemu ya Agizo letu la kwenda duniani kama chachu, kama mbegu mpya, kama wasafiri na wageni, kama nuru gizani. Na mara tunapokuwa duniani, tunawakilisha siyo ya kale, bali mapya, Kristo na ufalme wake." (Spencer 2020: "Reconsider Jesus – The Bridegroom and The New Wine")

<u>MASWALI YA KUJADILI</u>

1. Kwanini tuwe na shangwe wakati bwana harusi wetu yuko mbinguni?

2. Wakristo mara nyingi hukaa upande wa "ya zamani" na siyo "mapya." Wanafanyaje hivyo? Ni "upya" gani ambao Mungu angependa kuleta katika dunia yetu: kibinafsi, familia yako, katika shughuli yako kanisani kwako?

3. Kama unafunga, unafungaje na ni faida zipi umekuwa ukizipata kutokana na kufunga?

4. Una mapendekezo yeyote kwa ajili ya kusaidia watu wasigeuze kufunga kuwa namna ya sheria?

<u>2:23-28:</u> [23] Ikawa alipokuwa akipita mashambani siku ya sabato, wanafunzi wake walianza kuendelea njiani wakivunja masuke. [24] Mafarisayo wakamwambia, Tazama, mbona wanafanya lisilokuwa halali siku ya sabato? [25] Akawaambia, "Hamkusoma popote alivyofanya Daudi, alipokuwa ana haja, na kuona njaa, yeye na wenziwe? [26] Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, zamani za kuhani mkuu Abiathari, akaila mikate ile ya Wonyesho, ambayo si halali kuliwa ila na makuhani, akawapa na wenziwe?" [27] Akawaambia, "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato. [28] Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia."

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mst. 23-28—Kula masuke siku ya Sabato

Kulingana na **Kumb 23:25**, sheria iliruhusu kung'oa masuke ya ngano katika shamba la jirani. Hata hivyo, "sheria ya mdomo" ilizuia jambo hilo kufanyika siku ya Sabato. Jibu la kwanza la Yesu kwa Mafarisayo lilirejea kile Daudi alichokuwa amefanya, kama kinavyoandikwa katika **1 Sam 21:1-6**, ambapo Daudi hahukumiwi na AK.[13] Yesu anaonekana kutengeneza hoja yenye sura tatu kwa kutumia reje ya Daudi. Kwanza, "kwa kuwa Daudi hakuhukumiwa, kwanini mnanihukumu mimi?" Pili, swala la Daudi halikuwa kung'oa tu masuke na kupuguchua ngano lakini "ilikuwa tuhuma mbaya zaidi ya kula *mikate ya wonyesho*, ambayo, baada ya kuwekwa mbele za Mungu, ilizuiliwa kutumiwa na watu wote, isipokuwa ingeweza kutumiwa na makuhani tu" (Cole 1989: 129); Matokeo yake, hakuna msingi wa kumhukumu Yesu au wanafunzi wake.[14] Tatu, Wanadamu wanashika nafasi ya kwanza kabla ya desturi za kimapokeo za sheria.

Katika **mst. 27-28** Yesu anagusa swala la msingi zaidi la asili ya Sabato yenyewe na uhusiano wake na Sabato. Katika **mst. 27** maneno ya Yesu kwamba *"Sabato iliwekwa kwa ajili ya watu, na siyo watu kwa ajili ya Sabato"* kimsingi anasema kwamba "Mafarisayo, kwa misimamo yao mikali, iliyokusudiwa kuepusha uwezekano wowote wa kuvunja sabato, wameishia kuifanya sabato mzigo usiovumilika (linganisha na Mt. 23:4). Sasa walikuwa wamesahau kabisa kwamba asili ya sabato ilikuwa ni rehema za Mungu kwa viumbe vyake." (Cole 1989: 129)

Mistari 28 unakazia hoja kuu ya Yesu kwamba swala la msingi siyo katika kipi kinaweza kufanywa au kutokufanywa siku ya sabato, lakini swala muhimu ni utambulisho wake; swala la msingi linahusu Kristolojia. Anaanza kwa kujiita tena "mwana wa mtu," kama alivyofanya katika **2:10**. Hivyo, kwa mara nyingine tena anatangaza utambulisho na mamlaka kama Mungu aliyekuja dunini kama mtu. Hapo ndipo Yesu aliposema yeye ni *"Bwana wa Sabato"* (**Mk 2:28;** angalia pia **Mat 12:6; Lk 6:5**). Mafarisayo walidai kwamba wanafunzi wa Yesu walikuwa wana hatia ya kung'oa masuke ya ngano siku ya Sabato. Yesu anasema kuwa "wanafunzi hawana hatia *kwasababu* [yeye] kama mwana mtu ni Bwana wa Sabato" (Carson 1982: 67). Kwa kusema hivyo, Yesu alikuwa anatangaza "ukuu wake juu ya Sabato na, hivyo, ana mamlaka ya kubatilisha au kurekebisha sheria ya Sabato" (Moo 1984: 17). Ni Mungu tu ndiye aliye na mamlaka juu ya sabato na mamlaka ya kubatilisha au kurekebisha Sheria ya Sabato. Alitoa madai kama hayo ya kulingana na Mungu katika **Yh 5:17-18** alipomponya mtu siku ya sabato na kumwambia *"chukua godoro lako uende,"* kinyume na sheria ya Sabato. R. T. France anatoa hoja kwamba Yesu "anajifunua hatua kwa hatua kama [Bwana] katika mafundisho na vitendo vyake, kuhusiana na nguvu ya kiroho na uponyaji wa kimwili, katika kutangaza msamaha wa dhambi, na hata (*kai*) katika kuhusiana na taasisi takatifu mno ya Sabato. Elimu ya Ktistolojia ingewekwa kwa shida juu zaidi ya hapa." (France 2002: 148) Madai yake ya kuwa Bwana wa Sabato "siyo tu ni madai mazito ya kimasihi, lakini yanaibua uwezekano wa mabadiliko ya mbeleni au tafsiri ya Sabato" (Carson 1982: 66).[15] Madai ya Yesu kuwa *"Bwana wa Sabato"* yana uhusiano siyo tu na mwenendo wake lakini pia yanaathiri mwenendo wa wengine. Kama tutatambua Yesu ni nani, basi tunakabiliwa na uchaguzi: ama kujitoa kwake na kumtii (kama walivyofanya wengi ambao walichukua magodoro yao na kutembea) au kumpinga (kama waandishi na Mafarisayo).

3:1-6: ***[1] Akaingia tena katika sinagogi; na palikuwako huko mtu mwenye mkono uliopooza;***
2 wakamvizia ili kuona kama atamponya siku ya sabato; wapate kumshitaki. [3] Akamwambia yule mtu mwenye mkono uliopooza, Simama katikati. [4] Akawauliza, Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya? Kuponya roho au kuiua? Wakanyamaza. [5] Akawakazia macho pande zote kwa hasira, akiona huzuni kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao, akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako. Naye akaunyosha; mkono wake ukawa mzima tena. [6] Mara wakatoka wale Mafarisayo, wakawa wakifanya shauri juu yake pamoja na Maherodi, jinsi ya kumwangamiza.

mst. 1-6—Yesu anaponya siku ya Sabato

Tukio hili la mwisho kati ya matukio matano yaliyoandikwa kuanzia **2:1–3:6** yanahitimishwa na

[13] Rejea ya **mst. 26** kwa Abiathari inaibua ugumu fulani, kwa kuwa **1 Sam 21:1** inasema kwamba baba yake Abiathari Ahimeleki, alikuwa kuhani wakati huo. Maneno ya Kigiriki ya **mst. 26** hayamaanishi kusimamia kabisa kwamba Abiathari alikuwa kuhani mkuu lakini yana maana pana zaidi (angalia Cole 1989: 129n.2; Blomberg 1986:147-48). Further, AK lenyewe linaonekana kuunganisha, kuchanganya, au kutumika pamoja Ahimeleki kama Abiathari (linganisha na **1 Sam 22:20** na **2 Sam 8:17; 1 Nyak 18:16; na 24:6**).

[14] Hiki ndicho kinachojulikana kama hoja ya *a fortiori* (yaani, hoja kutoka kwa yenye nguvu kwenda kwa iliyo dhaifu), kwa mfano, kama humwamini mtoto wako kuendesha baiskeli kwa usalama, basi kwa *a fortiori*, hutamwamini kuendesha gari.

[15] Jinsi Yesu alivyotimiza na kuingiza Sabato ya AK na inajadiliwa kwenye Menn 2021: 89-91.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

Mafarisayo na Maherode kushauriana juu ya namna ya kumuangamiza Yesu. Sasa siyo tu wanafunzi wa Yesu wanaofanya jambo siku ya Sabato kama ilivyokuwa katika tukio la hapo nyuma, lakini ni Yesu mwenyewe. Zaidi ya hayo, uponyaji anaoufanya Yesu siku ya sabato siyo nyumbani kwa mtu kama katika **2:1-12** lakini ilikuwa katika sinagogi. Zaidi tena, ukichukulia kwamba alimwambia mtu aliyepooza mkono kusimama na kuja mbele, Yesu anaonekana alimponya kwa makusudi mtu huyu kama *changamoto* kwa wale waliokuwa wanamtazama ili wamshitaki.

Swali la Yesu katika **ms. wa. 4** (*"Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya? Kuponya roho au kuiua?"*) akirudia kanuni iliyoko nyuma ya Sabato ambayo aliitaja katika **2:27**: *"Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato."* Jibu, ambalo Mafarisayo walilijua lakini wasingekubali, kutenda *(mema . . . kuokoa maisha."* Mathayo anavyoelezea tukio hili, Yesu anaweka wazi kwa kutoa mfano, *"[11]Akawaambia, Ni mtu yupi miongoni mwenu mwenye kondoo mmoja, na yule kondoo ametumbukia shimoni siku ya sabato, asiyemshika akamwopoa? [12]Je! Mtu ni bora kuliko kondoo mara ngapi? Basi ni halali kutenda mema siku ya sabato.'"* (**Mat 12:11-12**) *ukimya* wa Mafarisayo, pamoja na kwamba walijua jibu sahihi kwa swali la Yesu, liliwapelekea "kufanya madhara." R. Alan Cole anaeleza hivi, "kumuacha mtu mwenye shida kungemfanya aendelee kuwa mlemavu; hili ni wazi lingekuwa sawa na kumdhuru" (Cole 1989: 132). Ukimya wa Mafarisayo ni sawa na "kupita pembeni" kwa kuhani na Mlawi katika mfano wa Yesu wa Msamaria mwema (**Lk 10:29-37**). Kwa maneno mengine, *"kushindwa* kutenda mema wakati tunaweza kunaonekana ni kutenda uovu; na *kutokuokoa* maisha wakati tunaweza ni kama kuua maisha."

Katika **mst. 5** unasema kwamba Yesu alikuwa amekasirika na kuhuzunishwa kwa wakati mmoja. Alikasirika kwasababu Mafarisayo walikuwa wamebeba uuaji katika mioyo yao na, kama Luka anavyoelezea tukio hili anatuambia, *"alitambua mawazo yao"* (**Lk 6:8**). Alihuzunishwa kwasabu ya *"ugumu wa mioyo yao"* (**v. 5**). Yesu alijua kuwa hitaji halisi la wanadamu siyo dini, desturi au ujinga, lakini moyo wa mwanadamu wenyewe (angalia **Yer 17:9**), na ni Yesu tu anayeweza kubadilisha mioyo yetu na kutupatia "moyo wa nyama" badala ya "moyo wa jiwe" (**Ezek 36:26**). Uponyaji huu unaweka alama ya mabadiliko katika huduma ya Yesu, kwasababu Mafarisayo walitaka kukaa na mioyo yao migumu badala ya kumfuata Yesu. Hivyo, *(waliondoka mara na kuitisha mkutano na Maherode dhidi yake, jinsi ya kumwangamiza)."*

MASWALI YA KUJADILI

1. Yesu alidai kuwa Mungu katika mwili na "Bwana wa Sabato" bado lawama kubwa dhidi yake ilikuwa kwamba *hakuwa mtunza dini kwa kiwango cha kuridhisha!* Hili lina maanisha nini kwetu kama wafuasi wa Yesu?

2. Unafikiria nini juu ya matamko, *"kushindwa* kutenda mema wakati tunaweza kunaonekana ni kutenda uovu; na *kutokuokoa* maisha wakati tunaweza ni kama kuua maisha."

3:7-12: ***[7] Naye Yesu akajitenga, yeye na wanafunzi wake, akaenda baharini. Mkutano mkuu ukamfuata, kutoka Galilaya, na Uyahudi, [8]na Yerusalemu, na Idumaya, na ng'ambo ya Yordani, na pande za Tiro na Sidoni, mkutano mkuu, waliposikia habari za mambo yote aliyokuwa akiyatenda, wakamwendea. [9]Akawaambia wanafunzi wake ya kwamba chombo kidogo kikae karibu naye, kwa sababu ya mkutano, wasije wakamsonga. [10]Maana aliponya wengi, hata wote waliokuwa na misiba wakamrukia wapate kumgusa. [11]Na pepo wachafu, kila walipomwona, walianguka mbele yake, wakalia wakisema, "Wewe ndiwe Mwana wa Mungu". [12]Akawakataza sana, wasimdhihirishe.***

mst. 7-12—Yesu anawaponya wengi wenye kuonewa na pepo wachafu

Kwa namna mbalimbali, sehemu hii inafanana na **1:21-34**. Ingawa Marko hatuambii kwanini Yesu alijitenga, Mathayo anaonesha kuwa ilikuwa ni kwasababu Yesu alijua kuna njama ya kumuua (angalia **Mat 12:15**). **Mistari 7-10** inaonesha kuwa, licha ya upinzani wa waandishi na Mafarisayo, mkutano mkubwa kutoka sehemu mbalimbali, ndani na nje ya Israeli, bado walimfuata, inawezekana kwa sehemu kubwa ni kwasababu ya huduma yake ya uponyaji. Rejea ya kwenye mashua katika **mst. 9** inarudiwa katika **4:1** na inaonesha kivitendo kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kufundisha makutano makubwa na bado akawa salama. Yesu alipoona mkutano mkubwa *"aliwahurumia, kwasababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji"* (**Mk 6:34**). Hata hivyo, hakuvutiwa hasa na ukubwa wa mkutano *"kwasababu yeye mwenyewe alitambua kilichoko ndani ya mtu"* (**Yh 2:23-25**). Anachojali Yesu ni kina cha mtu katika kujitoa kwake (angalia, kwa mfano, **Mat 10:37-39; Mk 8:34-38; Lk 14:25-33; Yh 6:53-66**). Kama ndivyo, ijapo Yesu alitambua mkutano waweza kugeuka na kuwa chochote, kwamba wengi wao walihudhuria ili kuona miujiza au kulishwa, na siyo kuishia kuwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

wanafunzi wake, hata hivyo alifundisha na kuwaponya. Zaidi ya hayo, ingawa Yesu aliweza kuonesha huruma za upendo kwa makutano, hakupunguza ukali wa ujumbe wake kuhusu jinsi ya kuingia katika ufalme na maana ya kuwa katika ufalme. Hii ndiyo maana, katika **Yh 6:66**, watu wengi waliokuwa wakimfuata waliondoka wasiendelee kumfuata. Huu ni mstari mzuri kwa kanisa kujifunza: jinsi ya kuwafikia watu wa kila namna na kuonesha upendo kwa vitendo, ambao wanaweza wasiwe watu wa kupendeka, na bado hakupunguza nguvu ya injili na maana yake kwa maisha yetu ili kupata mkutano mkubwa. **Mistari 11-12** inaenda sambamba na **1:24-25** kwamba roho wachafu walitambua Yesu ni nani na hadharani walimtambulisha kama mwana wa Mungu, hata hivyo Yesu aliwakemea na kuwaamuru wasifanye hivyo.

MASWALI YA KUJADILI

1. Kama Kanisa, tunahitaji kufanya au kubadilisha nini katika yale tunayofanya ili tutembee katika njia aliyotembea Yesu, yaani, kutokana na kuwafikia kwa matendo ya upendo watu wa kila namna, ambao wanajiona hawawezi kupendwa, bila kupunguza nguvu ya injili na maana yake katika maisha yetu?

3:13-19: ***[13]Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea.[14]Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, [15]tena wawe na amri ya kutoa pepo. 16 Akawaweka wale Thenashara; na Simoni akampa jina la Petro; [17]na Yakobo, mwana wa Zebedayo, na Yohana nduguye Yakobo, akawapa jina la Boanerge, maana yake, wana wa ngurumo; [18]na Andrea, na Filipo, na Bartholomayo, na Mathayo, na Tomaso, na Yakobo wa Alfayo, na Thadayo, na Simoni Mkananayo, [19]na Yuda Iskariote, ndiye aliyemsaliti.***

mst. 13-19—Kuwachagua Kumi na Wawili

Luka anatuambia kwamba, kabla ya kuwachagua wale kumi na wawili, Yesu alitumia usiku mzima katika maombi (**Lk 6:12**). Kama katika matendo yake mengine na misemo, kuchagua kumi na wawili kulikuwa na maana ya kina ya kitheolojia. Yesu kuanzisha kanisa katika msingi wa wanafunzi kumi na wawili/ mitume kumi na wawili kuliashiria kwamba alikuwa anaanzisha Israeli mpya ya kiroho. Uchaguzi wa Yesu wa wanafunzi kumi na wawili/mitume kumi na wawili (**Mat 10:1-2; Mk 3:13-19; Lk 6:12-26**) ni alama ya makabila kumi na mbili ya Israeli" (Goppelt 1982: 108). Yakobo analitambua hili kwa kuanza waraka wake *"kwa kabila kumi na mbili waliotawanyika"* (**Yak 1:1**). Barua hii kwa vyovyote waliandikiwa *Wakristo* (angalia **Yak 2:1**). "katika kutumia maneno [*ai dōdeka phulai; "kabila kumi na mbili"*], mwandishi anawatazama wanaopokea ule waraka kama Israeli wa kweli. Kanisa limechukua heshima ya cheo hicho kama asili yake, kwa kuwa ni kazi ya masihi kustawisha upya makabila kumi na mbili (Yr. 3:18; Ezek. 37:19-24; Zab. Sol. 17:28), na Wakristo wanajitambua kama warithi halisi wa imani ya kiyahudi (Rum 4; 1 Kor. 10:18; Gal. 4:21-31; Flp. 3:3)." (Davids 1982: 63) Cole anabainisha mambo kadhaa yanayofanana kati ya Israeli wa AK na makabila kumi na mbili na mitume kumi nambili: "Kama Israeli wa zamani alivyokuwa na 'mababa waanzilishi' kadhadhalika Israel mpya; hata baadhi ya majina yanafanana. Katika yule wa kale na mpya, kuna Simioni, na Lawi kadhalika Yuda. Milinganisho mingine ambayo hatujaijua inaweza ikawepo pia, kwa Andrea na Filipo kwa hakika walikuwa na majina ya kiebrania katika dini na pia majina ya kigiriki. . . . na kama kulivyokuwepo na kabila pendwa, Benjamin, kadhalika kuna mwanafunzi aliyependwa, Yohana, na, katika Israeli mpya, wote ni makuhani na wafalme (Uf. 1:6), kama hasa ilivyokuwa kwa Israeli wa kale (Kut. 19:6). (Cole 1989: 135-36n.3)

Kwamba Yesu alikuwa anazindua Israeli mpya, wa kweli, wa kiroho katika wale kumi na wawili inathibitishwa na Yerusalemu Mpya. Katika malango kumi na mbili ya Yerusalemu mpya kumeandikwa *"majina kumi na mbili ya makabila kumi nambili ya Israeli"*(**Uf 21:12**), Lakini katika mawe kumi nambili ya msingi wa Yerusalemu Mpya kuna *"majina kumi nambili ya mitume wa Mwana kondoo"* (**Uf 21:14**). Kwa kufanya hivi, Ufunuo unatutangazia muunganiko muhimu kati ya Israeli wa Agano la Kale na wafuasi wa Yesu na mitume wake kama Israeli mpya, wa kweli, na wa kiroho (angalia Walker 1996: 239). Inavutia, ijapokuwa mtu anaweza kuwaza kuwa "msingi" wa Yerusalemu Mpya unapaswa kuwa Israeli wa Agano la Kale, kwa kuwa ndiye aliyetangulia kwanza, ni majina ya mitume kumi na wawili ndiyo yako kwenye msingi. Hili linaonesha kuwa Kristo na Injili ndio msingi wa Yerusalemu Mpya.

Mitume wenyewe walitambua umuhimu wa "12": Katika **Mdo 1:12-26** walihitimisha kwamba ilikuwa ni lazima kujaza nafasi ya Yuda Iskariot kama mtume. Kwa nyongeza, ijapokuwa Paulo alikuwa mtume (angalia, kwa mfano., **Rum 1:1; 1 Kor 1:1; 9:1**), AJ (na Paulo mweneyewe) wanatambua tofauti ya utume wa Paulo na wale "kumi na wawili" (angalia **Mdo 6:2; 1 Kor 15:5, 8**). Hili linaweza kuhusishwa na ukweli kwamba huduma ya Paulo kimsingi ilikuwa ni kwa ajili ya Mataifa (angalia **Mdo 9:15; 13:46; 18:6; Gal 1:16; 2:7**), ambapo Petro, anayeonekana kuwa kiongozi na msemaji wa wale kumi na wawili, kimsingi alikuwa

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mtume kwa Wayahudi (angalia **Gal 2:7-8**).

Baada ya kusema hayo, "lilikuwa kundi la watu wa aina yake ambao Bwana wetu aliwachagua kuwa wanafunzi wake. Wanne kati yao walikuwa wavuvi, mmoja mtoza ushuru aliyechukiwa, mwingine mwanachana wa chama chenye msimamo mkali. Hao wengine sita hatujui chochote. Wote walikuwa watu wa kawaida. Hapakuwepo na mhubiri au mtaalamu wa maandiko katika kundi zima. Hata hivyo ni kwa kundi la wanaume hawa Yesu alianzisha kanisa lake na kusambaza habari njema hadi mwisho wa dunia." (Wessel 1984: 643)

MASWALI YA KUJADILI

1. Katika matukio kadhaa Yesu alijitenga na watu (angalia pia **Mk 6:31, 46; 7:24; 14:34-35**). Kuna umuhimu gani kwako kujitenga na watu mara kwa mara?

- Ni wakati gani unahisi hitaji hili?

- Una mkakati gani kuongezea nguvu betrii yako (kiroho, kimwili, kiakili, na kimhemko)?

2. **Mistari 14-15** inaonesha kuwa Yesu aliwaita kumi na wawili ili waende duniani sawa kabisa na yeye mwenyewe alivyofanya, kwa mamlaka yale yale aliyokuwa nayo. Hili lina maana gani kwa maisha yetu, kwa namna tunavyohusiana na watu, n.k.?

3. Ni nini, kama kipo, kinachowakilishwa na hali ya kiishara ya Yesu katika kuwachagua mitume 12 ambacho kinatuambia jinsi ambavyo sisi kama (kanisa) tunavyopaswa kuwa?

4. Ni nini, kama kuna chochote, ambacho asili na tabia ya mitume inatufundisha (kama kanisa) itupasavyo kuwa?

3:20-35: ***[20]Mkutano wakakusanyika tena, hata wao wenyewe wasiweze hata kula mkate. [21]Jamaa zake walipopata habari wakatoka kwenda kumkamata; maana walisema, Amerukwa na akili. [22]Nao waandishi walioshuka kutoka Yerusalemu wakasema, Ana Beelzebuli, na, Kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo. [23]Akawaita, akawaambia kwa mifano, Awezaje Shetani kumtoa Shetani? [24]Na ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, ufalme huo hauwezi kusimama; [25]na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama. [26]Na kama Shetani ameondoka juu ya nafsi yake, akafitinika, hawezi kusimama, bali huwa na kikomo. [27]Hawezi mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu, na kuviteka vitu vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu; ndipo atakapoiteka nyumba yake. [28]Amin, nawaambia, Dhambi zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; [29]bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele, [30]kwa vile walivyosema, Ana pepo mchafu. [31]Wakaja mamaye na nduguze; wakasimama nje, wakatuma mtu kumwita. [32]Na makutano walikuwa wameketi, wakimzunguka, wakamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako wako nje, wanakutafuta. [33]Akawajibu, akisema, "Mama yangu na ndugu zangu ni akina nani?" [34]Akawatazama wale walioketi wakimzunguka pande zote, akasema, "Tazama, mama yangu na ndugu zangu! [35]Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na** *mama yangu."*

mst. 20-35—Kutokuamini, upinzani, na familia ya kweli ya Kristo

Sehemu hii inaanza kwa kuzungumzia kuhusu familia ya Yesu ya kidunia, kisha inajadili tuhuma za waandishi dhidi yake, na kumalizia na familia ya Yesu ya kidunia na tafsiri ya Yesu kuhusu ipi anaitazama kama familia yake ya kweli.

1. Familia ya kidunia ya Yesu wanafikiri ana wazimu

Mara nyingi tunasahau kuwa Yesu alitokea katika familia na alikuwa na kaka na dada (wa kambo).[16] Wakati wa huduma ya Yesu duniani, ndugu zake hawakumwamini (**Yh 7:5**) na , kama **mst. 21** unavyotueleza, hata walifikiri alikuwa na wazimu. Jambo la kugundua hapa ni kwamba kila mtu—kuanzia na viongozi wa dini hadi kwa familia yake—hawakujua Yesu ni nani. Kwahiyo hatupaswi kuwashangaa watu tunaowaletea habari za Yesu wakishindwa kuelewa au kuamini, na hatupaswi kushangaa wakati watu wa familia yetu wakishindwa kutuelewa au kutuamini, hata kufikiri kwamba hatuna akili kwa kumfuata Yesu. Yesu mwenyewe alitangulia

[16] Zaidi kuhusu ndugu wa kiume na wa kike wa Yesu, angalia yaliyojadiliwa katika **mst. 31-35**, hapo chini.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kusema itakuwa hivyo (angalia **Mat 10:34-36; Lk 12:51-53**). Upendo kwa familia, kuambatana na familia ni jambo lenye nguvu, lakini Yesu anatuita kumpenda na kuambatana naye zaidi, hata zaidi ya familia zetu za kidunia. (**Mat 10:37-39; Lk 14:26-33**).

2. Upinzania wa viongozi wa dini na "kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu"

Viongozi wa kidini walivuka mipaka hata kufikiri kwamba Yesu alikuwa na wazimu. Walikuwa maadui zake na walimtuhumu kuwa *amepagawa na pepeo wa Beelzebuli,"* na kusema *"kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo´* (**mst. 22**; angalia pia **Mat 12:31-32; Lk 12:10; Yh 10:20**).[17] Tuhuma hizo kimantiki ni za kipuzi, kama Yesu anavyoonesha katika **mst. 23-27**. Hata hivyo, tuhuma hizi zilikuwa mbaya zaidi kimantiki kuwa za kipuzi. Dhana ya Yesu kuhusisha "kumkufuru Roho Mtakatifu" ni kule waandishi kuhusisha kazi ya Kristo ya uponyaji na kutoa pepo kwamba ni kazi ya ibilisi, ijapokuwa kila mtu mwenye ufahamu timamu angeliweza kuona kuwa ni kazi njema, *wao wenyewe walitambua* kuwa kile alichofanya Yesu kilikuwa kitu chema (angalia **3:1-5**), na walijua kwamba Yesu hasa alikuwa anaharibu kazi za Shetani (**3:23-27**). Ni muhimu kuona kuwa wakati waandishi walipoleta tuhuma zao dhidi ya Yesu *kwa hakika walijua au walipaswa kujua alikuwa ni nani.* Yesu hakuwaficha viongozi wa dini alikuwa nani: wakati wa kubatizwa kwake Roho alishuka kwa wazi juu yake kama hua (**1:10**); Sauti ya Mungu kutoka mbinguni ikatangaza, *"Huyu ni Mwanangu Mpendwa"* (**1:11**); Roho mara akamchukua jangwani (**1:12**); Yesu aliwaambia viongozi wa dini kwamba angeweza kufanya yale tu ambayo baba anafanya kwa kumsamehe kwa maneno tu na kisha kuthibitisha hivyo kwa kwa kumponya mtu aliyepooza (**2:5-12**); alikuwa anasema ndiye *"Mwana wa Mungu"* (**2:10**); alikuwa anasema ndiye bwana harusi (**2:19**); alikuwa anasema ndiye *"ndiye bwana wa Sabato"* (**2:28**); alikuwa anasema ndiye mwenye nguvu ambaye angeweza kumfunga Shetani na kuthibitisha hivyo kwa kutoa pepo mara kwa mara (**3:27**; angalia **Mk 1:4-8** wakati Yohana Mbatizaji alipotabiri kuja aliye na *'nguvu zaidi kuliko mimi"*).[18] Waandishi walikuwepo wakati Yesu alipokuwa akimponya mwenye kupooza katika **Mk 2:1-12**. Walitambua kuwa ni Mungu peke yake anayeweza kusamehe dhambi kwa maneno yake na hivyo wakamtuhumu Yesu kwa kukufuru alipomsamehe yule mtu. (**2:7**). Lakini alipomponya yule mtu kimwili, **mst. 12** unasema kwamba *"wote walishangaa na kumtukuza Mungu."*Labda, iliwahusu waandishi pia ambao walikuwa *"hawajawahi kuona kitu kama hichos"* (**mst. 12**). "kulikuwa na jambo moja tu lililopungua; kama Yesu alitoa pepo, ingewezekana hivyo tu ikiwa alikuwa anamiliki nguvu na mamlaka yenye uwezo zaidi kuliko ya Shetani. Nguvu kubwa zaidi namna hiyo, kwa Wayahudi, ingekuwa ni nguvu ya Mungu tu (Lk. 11:20). Kwa upande mwingine hii ilimaanisha kuwa utawala wa Shetani kwa dhambi na mauti ulikuwa umefikia mwisho, na kwamba utawala wa Mungu tayari ulikuwa umeanza, katika mioyo na akili za watu ambao Yesu Kristo amewatakasa na kuwakomboa kutoka katika nguvu za Shetani." (Cole 1989: 142; see also **John 10:21**)

Katika maelezo ya Mathayo kuhusu mapambano haya, Yesu hasa anasema kwamba anafanya hayo kwa nguvu ya Roho Mtakatifu: *"Lakini ikiwa ni kwa Roho wa Mungu natoa pepo, basi ufalme wa Mungu umewajilia"* (**Mat 12:28**). Kwa kudai kuwa kazi ya Roho ilikuwa ni kazi ya Shetani, viongozi wa dini walikuwa wanarudia historia ya mababa zao, kama inavyoandikwa na Isaya: *"Lakini wakaasi, wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu; kwa hiyo akawageukia, akawa adui, akapigana nao"* (**Isa 63:10**). ndipo Isaya anaendele na maombi kwamba Mungu *"angepasua mbingu na kushuka"* (**Isa 64:1**) kuwasaidia watu wake. C. K. Barrett anatuonesha kitu, "Maombi ya nabii yalikuwa yamejibiwa. Mungu alikuwa amepasua mbingu; alikuwa ameshuka . . . kwa mfano wa Roho . . . juu ya Yesu [**Mk 1:10**], ambaye mara alichukua hatua kama Musa, kuwakomboa watu wake. Matendo yake makuu yamejulikana. Mapepo walimtambua kuwa alikuwa mkuu. Lakini kazi hii mpya ya Mungu ilipokelewa kwa namna ile ile kama ile ya zamani. Watu badala ya kuikaribisha waliiasi, na kuhuzunisha (kukufuru) Roho wa Mungu, kama Marko anavyoandika. . . . Kwa kuwa hili ni tendo la mwisho la wokovu la Mungu, kieskatolojia, wale wanaokataa kabisa wanaweza, kulingana na lilivyo, wasipate wokovu." (Barrett 1958: 105)

Inaonekana kwamba matendo ya Yesu ya kula na "watoza ushuru na wenye dhambi," kusema kwamba kufunga (ambako Mafarisayo walifanya mara mbili kwa juma) hakuhitajiki tena kwakuwa alikuwepo, kuwaruhusu wanafunzi wake kuvunja sheria ya mdomo na "kufanya kazi" siku ya Sabato, na kuponya hadharani mtu mwenye kupooza mkono siku ya Sabato, katika sinagogi, kinyume na kile viongozi wa dini walichoona ni halali, yalisababisha viongozi wa dini kumtuhumu Yesu kuwa alikuwa anaongozwa na Shetani. Robert

[17] Beelzebuli wakati mwingine inatafsiriwa Beelzebub. Beelzebuli ni muundo wa zamani wa kiebrania wa Baalzebub, ambalo lina maana ya "Bwana wa inzi," na ni neno lililopinduliwa kutumika kama kejeli Baalzebuli, ambalo lina maana ya "Bwana Baal au Mheshimiwa Baali" (Cole 1989: 140; Stoops 1993: 70). "Kwa kiaramaiki, Beel-zebul linaweza kuwa lilipewa maana ya 'Bwana wa kinyesi.'" (Stoops 1993: 70).

[18] "Maelezo kuhusu Shetani kama "mwenye nguvu" [*ho ischuros*, **Mk 3:27**] yanapata mshindani katika maelezo yule anayebeba 'Roho Mtakatifu' kama 'aliye na nguvu zaidi' [*ischuroteros,* **Mk 1:7**]" (Lane 1974: 143n.92).

Deffinbaugh anaeleza, “Swali halisi halikuwa hasa, ‘anathubutuje kudai ni Mungu?’ lakini ‘anathubutuje kudai ni masihi na bado anatupuuza, wakati anashirikiana na watu najisi?’ Ni wazi viongozi wa Kiyahudi walikuwa wamepuuzwa.” (Deffinbaugh n.d.: Background [2]) Kama Jeffrey Gibson anavyoongeza kusema, “Kwa hakika, kilichowavunja moyo kilikuwa kwamba siyo mtu yeyote, lakini ‘mtakatifu wa Mungu’ aliyebeba sura ya mambo haya” (Gibson n.d.: II). Yesu alitambua hili (**Lk 7:34**, *“Mwana wa Adamu amekuja, anakula na kunywa; nanyi mwasema, Tazama, mlafi huyu, na mnywaji wa divai, rafiki wao watoza ushuru na wenye dhambi!’”*; angalia pia **Mat 11:19**). Kwa maneno mengine, alijua Yesu alikuwa nani, walijua kuwa tuhuma kwamba alikuwa amepagawa na Beelzebuli zilikuwa za uongo, lakini hata hivyo kwa makusudi walimtuhumu ili kumuangamiza.[19] Kusema kweli, katika **3:6** walishaamua kumuangamiza Yesu; ndiyo maana walileta tuhuma hizi katika **3:22** zilikuwa ni sehemu tu ya mpango wao (Deffinbaugh n.d.: Background [4], “Viongozi wa Kiyahudi waliazimia kumwangamiza Yesu [**mst. 6**] kabla hawajapata sababu nzuri ya kuwawezesha kutekeleza hilo. . . . Hizi [tuhuma katika **mst. 22**] siyo matamshi yaliyotamkwa tu bila kufikiriwa bali yaliyofikiriwa vema na viongozi wa dini waliokuwa tayari wameshamkataa Yesu kama Masihi”).

Viongozi wa kidini huenda kwa kujua walimuacha waliyemjua kuwa ndiye masihi aliyetumwa na Mungu, na kumtuhumu kuwa anatawaliwa na Shetani, kwasababu Masihi kama huyo masihi wa aina hiyo hakuendana na uelewa wao kwamba Masihi angepaswa kufanya nini.[20] Walishindwa kupokea ukweli kwamba Mungu angekuwa kinyume na ile picha ambayo mara zote wamefikiria. Masihi kama huyu na pia Mungu alitishia tamaa yao ya nafasi za juu na mamlaka (angalia **Yh 11:48**, *“Tukimwacha hivi, watu wote watamwamini; na Warumi watakuja, watatuondolea mahali petu na taifa letu.”)*.[21] Matokeo yake, ingawa walijua kivingine, kwa makusudi walichagua kumfanya Yesu aonekane kama mchawi na nabii wa uongo na mtenda miujiza anayeelezwa katika **Kumb 13:1-5**. Jambo baya zaidi ni kwamba “wakati bwana halisi wa Nyumba anapotoa pepo wachafu, walimkiri kuwa Mtakatifu wa Mungu/Mwana wa Mungu [**1:24**; angalia pia **Mat 17:9; Mk 1:34; 3:11; Lk 4:41**], lakini wale walihusika kwa mambo ya utakaso wa Israeli na nyumba ya Mungu wanamtuhumu kuwa ana pepo mchafu (3:30)” (Watts 2007: 150).

Ilikuwa ni kwasababu Mafarisayo hawakukosea bila kujua lakini wakijua kuwa walichokuwa wanasema kuhusu Yesu ni uongo kwamba, katika **mst. 29**, Yesu anasema, *“Bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele.”* Anasema kwamba ni kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu kwasababu, kama waandishi waliokuwa wanajua vema, Yesu alikuwa haongozwi na Shetani bali Roho Mtakatifu na ni Roho Mtakatifu aliyemfunua Kristo duniani. Kukufuru ni sawa na kupoa.[22] Hakuna yeyote anayekuwa katika hali hiyo bila kujua au kwa ajali, lakini kila mmoja kwa kudhamiria kwa makusudi. Kama Walter Grundmann anavyosema, “Dhambi hii inatendwa wakati mtu anapotambua dhima ya Yesu kwa Roho Mtakatifu lakini akaichafua na kuipinga” (Grundmann 1964: 304; angalia pia Bremer 1993: 91-92). Je dhambi hii inahusu siku tulizo nazo, kwakuwa Yesu hayuko tena duniani na hatuwezi kumuona kimwili akitenda miujiza kama walivyomshuhudia waandishi na Mafarisayo? Naamini inatuhusu, kwasababu tungali na maelezo

[19] Mfano wa Yesu wa mkulima wa zabibu katika **Mk 12:1-12** unaweka wazi kwamba viongozi wa walitenda wakijua kwa hakika Yesu alikuwa nani.

[20] Frank Powell anatujulisha kwamba viongozi wa dini “walikuwa wakimtafuta Masihi ambaye angelikuwa ‘kama Musa,’ au ambaye, atakuwa kama mmoja wa mashujaa wakuu wa kitaifa na nyota Judas Maccabeus (B.C. 167-161), kwa mkono wenye nguvu na mkuu angewaokoa kutoka kwa watesi wao; yeye ambaye ataleta ukombozi mkuu kiasi kwamba Nchi ya Ahadi itarejeshwa mikononi mwao bila ushindani; yeye ambaye atafuatwa na kila tukio la nguvu na utukufu kama manabii walivyonene. Hakuna mwingine angewaridhisha. Yesu hakutimiza hata moja wapo ya hayo. Yesu ahkuwa shujaa na, kwa namna yeyote, hakutoa ishara ya kuwa tayari kuongoza uasi dhidi ya Warumi. Kinyume chake, alikuwa mtu wa amani. Ufalme wake ‘haukuwa wa dunina hii.’ Hakuwakana Warumi; lakini kwa hakika aliwakana—viongozi wa Wayahudi. . . . Zaidi ya hayo, Yesu alifundishwa kuwa alikuwa na misheni kwa Wamataifa kadhalika kwa Wayahudi. Kwa makadirio ya viongozi mtu kama huyo asingeweza kuwa Myahudi wa “kweli” au Masihi. Katika uelewa wao Yehova hakuwa na mpango kabisa na Wamataifa.” (Powell 1954: 90-91)

[21] Hili limeoneshwa pia katika **Mk 11:15-19** Yesu “alipotakasa hekalu” kwa kuwatoa wale waliokuwa wakifanyia biashara zao hekaluni, akapindua meza za wabadilishaji wa pesa, hakuruhusu yeyote kufanya chochote hekaluni, nay eye mwenyewe alifundisha hekaluni. **Mistari 18** unasema kwamba kuhani mkuu na waandishi walifikiria kumuangamiza *“kwasababu walimuogopa”* Ni wazi vitendo vya Yesu vilikuwa tishio la mamlaka yao na kwa vyovyote viliwaletea hasara kubwa kifedha” (Wessel 1984: 728). Hata hivyo, nyuma ya hayo, kulikwa na matarajio kwamba kama mkutano ungemfuata Yesu, nafasi ya viongozi na mamlaka hapo mbeleni itapotea, kwa kuwa Yesu alikuwa akionesha wazi kuwa huduma ya hekaluni, kama ilivyokuwa ikifanywa na viongozi wale, ilikuwa haikubaliki kwa Mungu. Zaidi sana, **mst. 17** Yesu alinukuu kutoka **Yer 7:11**, ambao ni mazungumzo ambapo Mungu anawakemea viongozi wa Israeli na kuahidi kuwaondoa mbele ya uso wake.

[22] B. M. F. van Iersel analinganisha kumkufuru Roho Mtakatifu na kupoa kiroho, kama ilivyotajwa katika **Ebr 6:4-6** (van Iersel 1980: 27-28).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

na ushuhuda wa Yesu katika Biblia na Roho Mtakatifu bado anatenda kazi akimfunua Kristo duniani leo. Tukichukulia hali yetu, Hermann Beyer anasema kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu "kunaonesha kukataa nguvu ya wokovu na neema ya Mungu kwa wanadamu kwa kujua na kwa makusudi. Ni mtu yule anaye jiweka kinyume na msamaha ndiye asiyehusika na hilo." (Beyer 1964: 624) R. Alan Cole anaelezea kama "dhambi ya kujitakia ya kipofu, ambaye tena na tena anakataa nuru ya Roho, anapinga kazi ya Roho, na kujihesabia haki kwa kufanya hivyo kwa kumwelezea Yesu tofauti na alivyo. Kwa maana mtu kama huyo, hakuna tena msamaha, kwa kuwa anaikataa njia pekee ya msamaha ambayo Mungu ameiweka." (Cole 1989: 142) William Smith analiweka hivi: "kwa kifupi ni mtu aliyepata nuru kwa Roho akaijua kweli kuhusu Kristo na kuona matendo makuu ya Roho Mtakatifu kupitia kwake, halafu anamwacha Kristo, anaikataa injili, na kuishi kama adui wa Kristo." (Smith 2004: n.p.)[23]

Ieleweke kuwa "kukufuru Roho Mtakatifu" siyo "tukio la mara moja, kwamba likishatendeka, haliwezekani tena kubatilishwa. Siyo kutoa maneno ya kejeli kuhusu Yesu au Roho Mtakatifu. Bali, ni msimamo anaoshikilia mtu kuhusu Yesu unaokana nguvu za Roho Mtakatifu akitenda kazi ndani ya Yesu. . . . Katika injili ya Luka, matamko yanayohusu dhambi ya milele na kumkufuru Roho Mtakatifu yanatokea katika muktadha wa kumkiri Yesu mbele ya watu wengine (12:8-10). . . . Luka anaunganisha kumkana Yesu na kumkufuru Roho Mtakatifu, muunganiko ambao unamuingiza Petro akilini alipomkana Yesu baada ya kukamatwa kwake. . . . Petro alitenda kile ambacho chaweza kikaonekana kama dhambi isiyosameheka, kumbe kwa njia ya neema na upendo wa Yesu bado amehifadhiwa ndani ya zizi. Mwisho, hatuna nguvu za kujilinda tusitende dhambi ambayo hatutahitaji kutegemea msamaha wa rehema za Mungu kwa njia ya Kristo, ambaye 'yupo hai siku zote kutuombea.'" (Thompson 1999: 82)[24]

3. <u>Yesu anaelezea familia yake ya kweli</u>

Sehemu hii inaishia na rejea nyingine ya Yesu kuhusu familia yake ya kidunia. Hili halikutokea kama kwa ajali kwasababu, baada ya kuwaziwa kuwa ana wazimu na kutuhumiwa kuwa anatoa pepo kwa nguvu ya ibilisi, Yesu anaelezea familia yake ya kweli ni ipi. **Mistari 31** inamlenga *"mama yake na ndugu zake."* Biblia mara kwa mara inasema kwamba Yesu kwa uchache alikuwa na ndugu wa kiume wanne (Yakobo, Joseph, Simioni, na Yuda wanatajwa) na kwa uchache alikuwa na dada wawili (angalia **Mat 12:46-47; 13:53-56; Mk 3:31-32; 6:3; Lk 8:19-20; Yh 2:12; 7:3, 5, 10; Mdo 1:14; 1 Kor 9:5; Gal 1:19**).[25] Kwasababu ya mtazamo wao kwamba Mariamu alikuwa bikira, Wakatoloki wa Rumi wanashikilia kwamba ndugu wa kiume wa Yesu walikuwa binamu. Hata hivyo, "kifungu pekee ambapo ndugu wa kiume wa Yesu hawahusishwi na mama yake ni Yohana 7:3, 5, 10. Uhusiano unaotajwa wa mama wa Yesu unaonekana kumaanisha kwamba wanaotajwa ni watoto wa mama mmoja." (Zodhiates 1993: *"adelphos,"* 80) Zaidi ya hayo, ukweli kwamba Yesu alikuwa ndiye mkubwa wa "kaka"hao halisi (na siyo mabinamu) "unaungwa mkono na *prima facie* linalo maanisha mzao-wa kwanza', *prōtotokos,* katika Lk. ii. 7. Luka asingeweza kutumia neno hili, kama angejua kuwa Mariamu hajazaa watoto wengine, kwa kuwa neno *monogenes* (lililotumika katika Lk. vii. 12, viii. 42 lenye kumaanisha mtoto 'pekee') lilitumika. Tunapaswa pia kuona kuwa katika hali ya kawaida ya maana za maneno katika Mt. i. 25 'hakumjua hadi alipopata mtoto wake wa kwanza' ni kwamba, baada ya uzao huo, mahusiano ya kawaida ya kindoa yaliendelea na watoto wengine walizaliwa." (Tasker 1982: 22-23)

Ingawa, kama tulivyoona, familia yake ya kidunia hawakumwamini, waliamini baada ya ufufuo wake. Wote walikuwemo katika ile orofa siku ile ya Pentekoste (**Mdo 1:14**). Yesu alimtokea binamu yake Yakobo baada ya ufufuo (**1 Kor 15:7**), na Yakobo akawa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu (**Mdo 12:17**); alishika nafasi muhimu katika ule mkutano wa Yrusalemu, kwa kuwa mwenyekiti wa kikao hicho na kutangaza yaliyoamriawa (**Mdo 15:13-29**). Alijulikana kama mmoja wa "nguzo" za kanisa (**Gal 2:9**). Binamu yake Yuda alikuwa ndiye aliyeandika waraka wa Yuda (**Yuda 1**; angalia pia **Mat 13:55** [Neno la Kigiriki la Yuda ni

[23] La kuvutia ni hili kwamba hatimaye ilipofika wakati wa kumuondoa Yesu, viongozi walijua kuwa wasingeweza kuleta madai yao kuwaYesu alikuwa amepagawa na Beelzebul au anafanya kazi kwa nguvu za kipepe. Matokeo yake, katika **Yh 10:33**, ingawa walijua vema, uelewa wao kuhusu Mungu na Masihi wakoje na wafanyeje kuliwafanya viongozi wa Kiyahudi kukazia madai yao kwamba amekufuru (*"Wayahudi wakamjibu wakisema, 'siyo kwa kazi njema tunakwenda kukupiga mawe bali kwa kukufuru, kwasababu, wakati wewe ni mtu, unajifanya kuwa Mungu'";* angalia pia **Mat 9:2-3; Lk 5:20-21; Yh 5:17-18; 8:58-59**). Huo ndio msimamo walioushikilia hata wakati wa kuleta mashtaka yao mbele ya baraza la Sanhedrin (**Mat 26:57-66; Mk 14:61-64; Lk 22:67-71**). Hivyo, msimamo wao uliishia katika hali sawa na ya watu wa leo wanaomkataa Yesu kama Bwana, yaani, anaweza asiwe Shetani, lakini kwa hakika siyo Masihi wala siyo Mungu."

[24] C. E. B. Cranfield rightly anasema, "Ni swala lenye umuhimu kwamba tunaweza kusema kichungaji kwa kujiamini kwa yeyote ambaye ameshikwa na hofu kuu kwamba ametenda dhambi hii, kwamba ukweli kwamba anateseka ni ushahidi wa hakika hajatenda dhambi hii" (Cranfield 1972: 142).

[25] Yule aliyedhaniwa kuwa ndiye baba yake, Yususfu, hatajwi, ikidhaniwa kuwa labda hakuwa hai.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

‘Judas”).

Licha ya upendo wa kawaida na mguso kwa familia za kidunia, katika **mst. 34-35** Yesu anaeleza wale ambao anawafikiria kuwa ndio hasa familia yake: *“Akawatazama wale walioketi wakimzunguka pande zote, akasema, Tazama, mama yangu na ndugu zangu! Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu.”* Yesu alitambua kwamba familia za kidunia, hata kama ni nzuri kiasi gani zinapita; familia yake na ufalme wake ni wa milele. Katika hali yake ya asili, familia za kidunia hazina ukombozi; ni familia yake tu ndiyo inayojengwa na waliokombolewa. Kuna msemo usemao, “Damu ni nzito kuliko maji.” Yesu anasema, Hilo laweza kuwa kweli, lakini damu ya kidunia haiwezi kumpa mtu uzima wa milele—ni *damu yangu tu* inayompa mtu uzima wa milele.”

Kwa kifupi, familia yetu ya kiroho katika Kristo ni muhimu zaidi kuliko familia zetu za kimwili; hakika, Roho ni muhimu zaidi kuliko chochote cha dunia hii. Hii ndiyo maana Yesu alilinganisha upendo wetu na kwa familia zetu za kidunia na maisha yetu ya kidunia: upendo wetu wa asili kwa familia zetu na maisha yetu ya kidunia yanapaswa kuchukiwa ukilinganisha na upendo wetu kwa Yesu (**Mat 10:37; Lk 14:26**). Kutokea msalabani, Yesu alionesha kwamba kumfuata ni muhimu zaidi kuliko kusikiliza familia zetu za kidunia. Kama kijana mkubwa, ilikuwa ni wajibu wake kumwangalia mama yake; alipokuwa hana uwezo wa kufanya hivyo, alitua jukumu hilo kwa wadogo zake. Hata hivyo, wakati akiwa anasulubiwa, kaka zake wa kidunia hawakumwamini. Matokeo yake, kutokea msalabani Yesu alimpa mwanafunzi wake Yohana jukumu hilo, kama **Yh 19:26-27** inavyosema: *“Basi Yesu alipomwona mama yake, na yule mwanafunzi aliyempenda amesimama karibu, alimwambia mama yake, Mama, tazama, mwanao. Kisha akamwambia yule mwanafunzi, Tazama, mama yako. Na tangu saa ile mwanafunzi yule akamchukua nyumbani kwake.”* Yesu iliipa Roho nafasi kubwa zaidi kuliko mwili na kuonesha umuhimu wake hata alipokuwa pale msalabani. Hali yake ya kumaanisha kuhusu umuhimu wa kiroho dhidi ya ule wa familia ya kimwili inafaa kutufanye sisi kama mtu mmoja mmoja au kama ushirika kama kanisa kutafakari tena ni familia gani ni muhimu kwetu na tunalioneshaje hilo.

MASWALI YA KUJADILI

1. Ukweli kwamba hata familia ya Yesu ya kidunia haikumwamini unatuambia nini kuhusu umuhimu wa maombi katika uinjilishaji?

2. “Kumkufuru Roho Mtakatifu” ni nini?

3. Inaonekana wazi kwamba uelewa usio sahihi wa waandishi walivyofikiri kuhusu Yesu na Mungu mwenyewe ndio unaoonekana kuwapelekea kumtuhumu Yesu kuwa amepagawa na Beelezebul na ana pepo mchafu. Ni uelewa gani usio sahihi tulio nao kuhusu Mungu ambao unaweza kutufanya kumuelewa visivyo na/au kumkasirikia?

4. Waandishi walimtazama Yesu kama *mwenye pepo*. Ni matokeo gani (mawazo, maneno, matendo) huwa huwatoka wale wasioelewa au wasiokubaliana?

5. Mwitikio wako ni nini kwa maneno ya Yesu kuhusu familia?

   - Unadhani alimaanisha kwamba tunapaswa kutelekeza familia zetu za kidunia ili kumtumikia Mungu? Kwanini au Kwanini siyo?

   - Unafikiri tunapaswa kuwachukulia waamini na wasioamini kuwa ni toafauti kabisa? Kwanini au Kwanini hufikiri hivyo?

6. Watu walioko nje kanisa letu wanatuona kama familia?

   - Kama sivyo, kwanini hawatuoni hivyo?

   - Kama ndivyo, wanatuona kama familia nzuri iliyobadilika, au kama familia mbaya?

7. Sisi wenyewe tunajiona kama familia, na tunatendeana kama wanafamilia?

8. Tufanye nini kama kanisa kuhakikisha kuwa watu wote katika kanisa letu wanachukuliwa kama wanachama

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

wapendwa wa familia yetu?

4:1-34: ***[1]Akaanza kufundisha tena kando ya bahari. Wakamkusanyikia mkutano mkubwa mno, hata yeye akapanda chomboni, akakaa baharini, mkutano wote ulikuwako juu ya nchi kavu kando ya bahari. [2]Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, akawaambia katika mafundisho yake, [3]Sikilizeni; Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda; [4]ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila. [5]Nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara ikaota kwa kuwa na udongo haba; [6]hata jua lilipozuka iliungua, na kwa kuwa haina mizizi ikanyauka. [7]Nyingine ikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea ikaisonga, isizae matunda. [8]Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri, zikazaa matunda, zikimea na kukua, na kuzaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia. [9]Akasema, Aliye na masikio ya kusikilia, na asikie. [10]Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano. [11]Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano, [12]ili wakitazama watazame, wasione; Na wakisikia wasikie, wasielewe; Wasije wakaongoka, na kusamehewa. [13]Akawaambia, Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje? [14]Mpanzi huyo hulipanda neno. [15]Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao. [16]Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha; [17]ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa. [18]Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno, [19]na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno, likawa halizai. [20]Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu walisikiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia. [21]Akawaambia, Mwaonaje? Taa huja ili kuwekwa chini ya pishi, au mvunguni? Si kuwekwa juu ya kiango? [22]Kwa maana hakuna neno lililositirika, ila makusudi lije likadhihirika; wala hakuna lililofichwa, ila makusudi lije likatokea wazi. [23]Mtu akiwa na masikio ya kusikilia, na asikie. [24]Akawaambia, Angalieni msikialo; kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa. [25]Kwa maana mwenye kitu atapewa, naye asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. [26]Akasema, Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; [27]akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. [28]Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. [29]Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika. [30]Akasema, Tuulinganishe na nini ufalme wa Mungu? Au tuutie katika mfano gani? [31]Ni kama punje ya haradali, ambayo ipandwapo katika nchi, ingawa ni ndogo kuliko mbegu zote zilizo katika nchi, [32]lakini ikiisha kupandwa hukua, ikawa kubwa kuliko miti yote ya mboga, ikafanya matawi makubwa; hata ndege wa angani waweza kukaa chini ya uvuli wake. [33]Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikia; [34]wala pasipo mfano hakusema nao; lakini akawaeleza wanafunzi wake mwenyewe mambo yote kwa faragha.***

mst. 1-34—Yesu anafundisha kwa mifano

Mifano inaweza ikaonekana kama ni aina ya simulizi zenye picha—yaani, simulizi au visa ambamo wahusika au vitu vingine husimama vinachukua nafasi ya vitu vingine, kwa ujumla ni uelezea ukweli wa kiroho wa kimaadili. Mada ya msingi inayounganisha mifano ya Yesu ni ufalme wa Mungu, ambayo upo sasa lakini utakuwa na kilele chake mbeleni. Ufalme ni nguvu ya kiutendaji ya Mungu kujifunua mwenyewe katika kutengeneza jamii ya wale wanaomtumikia Yesu katika kila eneo la maisha yao" (Blomberg 1990: 326). Ufalme unahusisha mabadiliko binafsi na mageuzi ya kijamii. Katika mifano yake, "Yesu kwa wazi ana mada tatu za kuvutia: wema wa Mungu, uhitaji wa uanafunzi na hatari ya kuasi" (Ibid.).

Yesu alitumia mifano "kuchokoza muitikio kutoka kwa wasikilizaji wake, ama chanya au hasi" (Osborne 1991: 241). Njia moja alipofanya hivyo ilikuwa ni kugeuza matarajio ya watu katika kupindisha ile njama katika mifano yake: "Msamaria aliyechukiwa, siyo kuhani wala Mlawi aliyefunga jeraha za mhanga wa majambazi (Lk 10:30-37); kwa kawaida Wasamaria walikuwa watu wa kushambulia siyo kuokoa!); mwana mpotevu ndiye aliyepewa sherehe (Lk 15:11-32); maskini na mlemavu walikaa kwenye sherehe kubwa (Lk 14:15-24); wakili aliyebadilisha hesabu za madeni ya bwana wake ndiye aliyesifiwa (Lk 16:1-13). Kwa kufanya hivyo Yesu anaweza kulazimisha wasikilizaji kupata mtazamo mpya kuhusu uhalisia wa ufalme wa Mungu." (Osborne 1991: 243)

Yesu alitumia mifano kufunua na kuficha, kwa sehemu kubwa kulingana na hadhira yake (angalia **Mat 13:10-17; Mk 4:10-13**). Yesu alifunua kwa: (1) kuelezea jambo kwa namna ambayo litakumbukwa; (2) kutaka mawazo zaidi kwa wale ambao maana yake haikueleweka mapema; na (3) kushawishi hadhira ikubali mambo

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kadhaa ya kiimani kwa namna fulani. Mifano ilificha wakati: (1) wasikilizaji walishindwa kupata maana ya mojawapo ya hadithi za mafumbo; au (2) hata kama alielewa maana, msikilizaji anakataa ushawishi unaomtaka kuleta mageuzi ya namna fulani ya maisha yake. Hivyo, katika **Mk 12:12** viongozi wa Kiyahudi walielewa kuwa Yesu ametoa mfano wa mpangaji mwovu akiwazungumzia wao, lakini hawakuwa tayari kubadilisha njia zao na, badala yake, waliongeza juhudi zao za kumuangamiza.

Ufunguo wa kutafsiri mifano uko katika kutambua matendo ya wahusika wakuu wachache, au alama zinazo wawakilisha. Kanuni ya msingi katika kutafsiri mifano ni "hoja moja kwa mhusika mmoja." "Kila mfano una hoja moja kuu kwa kila mhusika—mara nyingi wawili au watatu kwa kila kisa—na wahusika hawa wakuu huenda ndio sehemu ndani ya mfano inayowakilisha kitu fulani kuliko wao wenyewe, hivyo kuupa mfano husika asili yake ya kiistiari. . . . Wakati huo huo, vitu zaidi ya wahusika wakuu vitabeba rejea za kialama kwa kiwango tu ambacho zinaendana na maana inayokusudiwa na rejea za wahusika wakuu, na tafsiri zote za kiistiari lazima zitokane na kile ambacho kingeeleweka hivyo kwa hadhira ya watu wa karne ya kwanza kule Palestina." (Blomberg 1990: 163) Wahusika wakuu wanawakilisha sehemu mbalimbali za ufalme wa Mungu—kwa ujumla wanahusiana na Mungu, watu wa Mungu, na wale wasio watu wa Mungu.

1. **mst. 1-20—**Mfano wa Mpanzi na aina za udongo

Kwa namna fulani mfano wa mpanzi na aina za udongo ni "mfano wa mifano" kwa kuwa Yesu kwa wazi alitafsiri mfano huu peke yake (**Mat 13:1-23; Mk 4:1-20; Lk 8:4-15**) na mfano ngano na magugu (**Mat 13:24-30, 36-43**). Zaidi ya hayo, katika **mst. 13** alisema, zaidi ya hayo, katika **mst. 13** alisema, *"Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje?"*

Maelezo ya Yesu katika **mst. 14-20** anaufanya mfano ueleweke wazi: mpanzi ni mtu yule anayepanda neno. (injili, yaani mbegu); aina nne za udongo ni aina nne za mioyo ya watu inayofunua mwitikio wao kwa neno. Kwa kuliweka kwa namna nyingine, hali ya mioyo inatangulia katika kupokea injili; mwitikio kwa injili unafunua hali ya moyo. Baadhi ya watu wanafikiri kuwa makundi mawili ya kwanza (wale walioko njiani na walioko kwenye mwamba, penye udongo hafifu) ni wale wasiookoka, lakini kundi la tatu (wale waliosongwa na miiba) ni wale waliookoka lakini ni wakristo "wachanga" au "wa kimwili"[26] Hiyo siyo kweli. Makundi matatu ya kwanza yote yanafanana na hayana faida kwa mpanzi; mtu yule anayemuacha Kristo kwa mambo ya kimwili (kundi la 3) atazungumziwa kwa shida kama ni bora kuliko yule aliyeshindwa na adha (kundi 2). Ni kundi la nne (udongo mzuri) wanawakilisha waliookoka. Maneno anayotumia Yesu katika mfano yanawachukulia makundi yote matatu ya kwanza kuwa sawa lakini yanalitofautisha kundi la nne: (1) Makundi matatu ya kwanza yote yanaelezewa katika umoja; ni kundi la nne tu ambalo linaelezewa katika uwingi, na kuna mbegu tatu njema (30, 60, 100) kuendana na mbegu tatu mbaya za makundi ya 1-3. (2) Makundi matatu ya kwanza yanaelezewa katika neno la wakati uliopita (kiufundi, *aorist*) na hayaoneshi kuwa yanaendelea; ni kundi la nne tu linaoneshwa kuwa linaendelea Yesu anatumia kitenzi kisichokamilika na cha wakati uliopo kuyaelezea). (3) Katika maelezo yake, Yesu anatumia "hawa" kwa makundi matatu ya kwanza (**mst. 15, 16, 18**) lakini anatumia "wale" kwa kundi la nne (**v. 20**)-*tafsiri ya kingereza*. (4) katika **ms. wa. 16** neno "hulipokea" (*lambanō*) ni dhaifu kuliko neno "hulikubali" katika **mst. 20** (*paradechomai*), yaani, kupokea kama tendo la kuhamasika kibinafsi ambalo si lazima limaanishe kuridhika" dhidi ya "kukubali, linalobeba maana ya kutii" (Zodhaites 1993: *lambanō,* 907; *paradechomai,* 1102). (5) Kundi la nne ndilo kundi pekee Yesu analielezea kuwa "zuri." (6) Ni kundi la nne tu linalotajwa kuzaa matunda. Katika huduma yake yote, Yesu alikazia kwamba *"mti hujulikana kwa matunda yake"* (**Mat 12:33**; angalia pia **Mat 7:15-18, 20; Lk 6:43-45; Yh 15:4-5**). Hakika, kusudi hasa kwa Kristo kutuokoa ni ili tuzae matunda, na matunda ni ushahidi wa imani halisi (**Rum 7:4; Ef 2:10**; angalia pia **Gal 5:22-23; Ef 5:8-9; Kol 1:3-6**). Kwa upande mwingine, alisema pia kwamba *"kila mti usiozaa matunda hukatwa na kutupwa motoni"* (**Mat 7:19**; angalia pia **Mat 3:10; Lk 3:9; Yh 15:2, 6**).

Muktadha wa mfano huu ni kwamba Yesu alikuwa ametangaza uwepo wa ufalme wa Mungu katika **1:14-15**. Amekuwa akidhihirisha uwepo wa ufalme huo (na utambulisho wake kama Masihi) kwa njia ya uponyaji wake na miujiza katika **sura za 1-3**. Alikuwa na kundi la wafuasi—wale kumi na wawili—pamoja na kundi "kubwa mchanganyiko" la wasikilizaji, wengine wakiwa hawaamini, baadhi (sehemu ya familia yake mwenyewe) waliofikiri alikuwa na wazimu, na maadui wenye nguvu, waliokusudia (na kupanga njama) kumuua. Katika muktadha huu Yesu sasa anashughulika na *"siri [au 'fumbo'] la ufalme"* (**mst. 11**): kipekee, ufalme wa Mungu hauji kwa namna ambayo watu wengi walitarajia; badala yake, unaonekana sasa kwa njia ya Yesu na unapatikana kwa njia ya mahusiano binafsi na Yesu (kupitia mbegu ya injili iliyopandwa). Anaelezea kwanini, tofatuti na matarajio, ufalme na yeye kama kichwa cha ufalme huo hawakuwa wakikubaliwa kidunia,

[26] Yesu hakusema kuwa robo ya mbegu ilikuwa imepandwa kwa kila aina ya udongo; alikuwa akitumia mfano wa kawaida wa mkulima mwenye kuopanda mbegu, ambapo baadhi ya mbegu ziliangukia katika udongo dhaifu.

badala yake walikuwa wanasababisha mgawanyiko. Anaonesha kuwa Shetani anatenda kazi akipinga kutangazwa kwa injili na baadhi yao walikataa kabisa; wengi huitikia injili kwa namna isiyotosha kuokoa: wengine kwa juu juu tu huonesha kuvutiwa lakini bila kumaanisha kuwa wanafunzi. Matokeo yake, katika **mst. 12** anamnukuu **Isa 6:9-10**, Wito wa Mungu kwa Isaya, ambao ulipelekea wengi kuwa wagumu isipokuwa mabaki. Kama Royce Gruenler anavyoandika, "ujumbe wa Isaya utawathibitisha tu katika uasi wao, kama ujumbe wa Yesu unavyotumika kuthibitisha uasi wao katika kumkataa. Maneno *wasije wakaona kwa macho yao,na kurejea na kuponywa!* Ni muhimu sana, kwa kuwa hawana nia ya kugeuka na kusamehemwa." (Gruenler 1989: 773) Hata hivyo, mkazo wake uko katika ukweli kwamba baadhi yao watakuwa na muitikio mzuri wa imani, utii, na kujitoa, na kutakuwa na mavuno mengi mwishoni. Kadhalika, yatupasa kupanda kama wasiojua ipi itakuwa njema: yatupasa kutarajia baadhi kukataa lakini kwa hakika kutakuwepo na mavuno.

2. **mst. 21-25—**Kilichofichika kitafunuliwa, na kwa kipimo upimacho utahukumiwa

Mistari 21 kiuhalisia unasema, *si nuru imekuja . . ."* Hili linamlenga Yesu na dhima yake:[27] *"Na hukumu ndiyo hii: nuru imekuja ulimwenguni, na watu wakapenda giza badala ya nuru kwasababu matendo yao yalikuwa ya maovu"* (**Yh 3:19**); *"Basi Yesu akawaambia tena akasema, 'Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.'"* (**Yh 8:12**); *"Mimi nimekuja ili niwe nuru ya ulimwengu, ili kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani"* (**Yh 12:46**). **Mistari 22** unatuambia kuhusu hukumu ijayo wakati *"Lakini hakuna neno lililositirika ambalo halitafunuliwa, wala lililofichwa ambalo halitajulikana. Basi, yo yote mliyosema gizani yatasikiwa mwangani; na mliyonena sikioni mwa mtu katika vyumba vya ndani, yatahubiriwa juu ya dari"* (**Lk 12:2-3;** angalia pia **Mat 10:26-27; Lk 8:17; 1 Kor 4:5**). **Mistari ya 21-22** pia inaleta uwiano na **mst. 11-12**, yaani, Yesu ni nuru na alikuja kuifunua nuru katika giza, lakini "walioko nje" hawaelewi kwasababu wanapenda giza kuliko nuru.

Mistari 23-25 inatoa onyo kwa wale "walioko nje." Deffinbaugh anaeleza hivi: "Kanuni iliyoko nyuma ya mfano huu ni hii: 'ukweli unaoshindwa kuutumia, unaupoteza,' au 'Kiuhalisia unamiliki tu ukweli unaoutendea kazi.' Hii ilikuwa ndiyo maana ya Bwana wetu aliposema, 'Angalieni msikialo; kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa. Kwa maana mwenye kitu atapewa, naye asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa' (Mk 4:24-25). Basi isitokee kwa wanafunzi au (sisi) tukashikwa na kiuri kutokana na maarifa tuliyo nayo, wakati wengine wakiendelea kukaa katika ujinga, hebu tutafakari wajibu mzuri tulio nao sisi ambao lililo bora limetufikia." (Deffinbaugh n.d.: The Principle)[28] Kwa kifupi, Kristo ni nuru; ndiye kipimo (angalia **Yh 14:6; 1 Pet 2:6**); wale wanaomkataa watapoteza kila kitu; lakini wale wanaomjua, wanaomtii, na kumfuata watarithi kila kitu (angalia **Mat 5:5; 19:29; 25:34; Mdo 20:32; Rum 4:13; Ef 1:11, 14, 18; Kol 1:12; 3:24; Ebr 1:14; 6:12; 9:15; 1 Pet 1:4; Uf 21:5-7**).

3. **mst. 26-29—**Mfano wa mbegu, kukua, na mavuno

Mfano huu unatuambia kwamba ufalme wa Mungu unaanza kama kwa kificho, unakua kiajabu, unatawaliwa na Mungu, na utaendela pasipo mwisho (angalia pia **1 Kor 3:6-9**). Ufalme wa Mungu umezinduliwa tayari na upo sasa lakini siyo katika utimilifu wake na siyo kulingana na matarajio ya viongozi wa dini.[29] Hivyo, **Lk 17:20-21** anasema, "*Na alipoulizwa na Mafarisayo, Ufalme wa Mungu utakuja lini? Aliwajibu akawaambia, "ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza; wala hawatasema, Tazama, upo huku, au, kule, kwa maana, tazama, ufalme wa Mungu umo ndani yenu."* Rejea ya mundu na mavuno jinsi vinavyoendana na mfano wa ngano na magugu (**Mat 13:26-30, 36-43**) na maelezo ya uvunaji na hukumu ya wakati wa mwisho katika **Uf 14:14-20** (angalia pia **Yoeli 3:13**). Miongoni mwa mambo mengine, hili linatuambia kwamba kanisa litakuwepo duniani siku zote hadi mwisho wakati Kristo atakapokuja tena na kuleta hukumu.

4. **mst. 30-34—**Mfano wa mbegu ya haradali

Mfano huu unakazia tofauti kati ya mwanzo mdogo na mwisho wake wenye kushangaza. Kwa kuwa msingi wa uanachama katika ufalme ni imani yetu katika Kristo, katika **Mat 17:20** Yesu analinganisha imani na *"mbegu ya haradali."* Ukweli kwamba mharadali unakua ili *"ndege wa angani waweze kupata mahali pa*

---

[27] Ingawa baadhi ya tafsiri hutumia sarufi isiyo na mpaka *"mwanakondoo"* [*a Lamp"*], neno la Kigiriki katika **mst. 21** limetumia sarufi (*ho*; yaani sawa na *the*), jambo linaloweka mkazo kuwa Mwanakondoo anayezungumziwa ni Yesu.

[28] Katika *The Screwtape Letters*, C. S. Lewis anatujulisha kwamba, "Neno 'yangu' katika maana yake kamili ya kumiliki haliwe'i kutamkwa na mwanadamu juu ya chochote. Katika hali endelevu ni ama Baba yetu au Adui wanaweza kusema 'yangu" juu ya kila kitu kilichopo, na hasa kwa mtu mmoja mmoja. Usiogope kamwe, mwishoni, watagundua, muda wao, nafsi zao, na miili yao ni mali ya nani—kwa vyovyote siyo *kwao*, haijalishi nini kinatokea." (Lewis 1961: 98)

[29] Kwa majadiliano kuhusu asili ya "tayari" na "bado" ya ufalme wa Mungu, angalia n.2 hapo juu na maandiko yanayoendana nayo.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kuwekea viota vyao katika kivuli chake" unaonesha kuwa ufalme ni nguvu kwa ajili ya mema kwa kila mtu, kama Mungu ambavyo *"huwaangazia jua waovu na wema, na kuwapa mvua wenye haki na wasio haki"* (**Mat 5:45**). Kwa kuwa kanisa ni mwili unaoonekana wa ufalme wa Mungu duniani, inatupata tutambue sura hii ya ufalme na kufanya tuwezayo kumuonesha Mungu wema kwa wote sawasawa wenye haki na wasio haki.

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini Yesu alifundisha kwa mifano? Kwanini aliwaficha ukweli baadhi ya watu (**mst. 11-12**)?

2. Katika mfano wa mpanzi na aina za udongo, kuhusu aina nne za watu ambamo mbegu zilipandwa, ni kundi lipi ambao wameokoka/ walikuwa wameokoka? Kwanini?

3. Unaonaje neno kupokonywa, kuunguzwa, au kusongwa katika maisha yako mwenyewe na katika maisha ya wale walioamini unaowajua? Unakusudia kufanya nini kuhusiana na hili?

4. Unadhani matunda *mara zote* (katika wakati fulani, katika kiwango fulani, na katika njia fulani) huambatana na imani inayookoa?

- Vipi kuhusu yule mwizi pale msalabani?

- Unafikiri baadhi ya matunda yanayodhaniwa ni matunda huwa ni ya "kimwili" tu? Inakuwaje, kama basi ndivyo, unaweza ukayatofautisha?

- Kwa upande mwingine, unadhani kuwa baadhi ya matunda huwa yanaonekana kwa Mungu tu? Kama ndivyo, hii ina maana kuwa *hatupaswi* kuhitimisha kuwa mtu fulani siyo Mkristo kama anadai ni Mkristo, bali mara zote tudhanie kuwa ukiri wa imani yao utakuwa ni wa kweli?

5. Ni kwa namna gani wewe binafsi na kanisa lako mnakuwa nuru katika giza (**ms. wa. 21**)? Unafikiri nini wewe na kanisa lako mnapaswa kufanya kuwa bora zaidi, na kuwa na ufanisia zaidi?

6. Tunaonaje "kipimo cha viwango" ambavyo watu huonesha katika maisha yao?

7. Huwa Kristo anatoa vipimo vigumu na tofauti katika maisha yako ukilinganisha na maisha ya wasioamini unaowajua? Kama ndivyo, kwa namna gani?

8. **Mistari 22-25** inakazia hukumu inayokuja. Unafikiri nini kuhusu hukumu na kwa namna gani, kama ipo, itakavyoathiri namna unavyoishi?

9. Ni kwa namna gani inatupasa tuwe tunapanda katika familia zetu, jamii na dunia?

10. Katika mifano hii, Yesu kwa kurudia anatumia neno "mbegu" na hata kukazia udogo wake katika **mst. 3.** Kwa kuzingatia hili, kwanini Wakristo wanashikwa mno na ukubwa wa mambo (huduma zao, makanisa yao, idadi ya watu waliowaleta kwa Yesu, n.k.)? Kufikiria juu ya ukubwa kunaendana au hakuendani na **mst. 20, 24, 27** na **32** (kuhusiana na hili angalia **1 Kor 3:6-9**)?

- Unawezaje kuwatia moyo wale wanaofanya "vitu vodogo" kwa Mungu?

- Nani unamfahamu anafanya kazi ya ufalme lakini, kwasababu siyo "kubwa" huwa anapuuzwa? Nini unaweza kufanya kuhusiana na hilo?

4:35-41: ***[35] Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia, "Na tuvuke mpaka ng'ambo". [36]Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye. [37]Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. [38]Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto; wakamwamsha, wakamwambia, "Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia?" [39]Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, "Nyamaza, utulie". Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu. [40]Akawaambia, "Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?" [41]Wakaingiwa na***

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

hofu kuu, wakaambiana, "Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?"

mst. 35-41—Yesu atuliza bahari

Baada ya mifano kuisha, Marko anarudi kwenye vitendo vya Yesu. kama ilivyokuwa kweli katika **sura za 2-3,** matukio ya kipindi hiki cha Yesu kutuliza bahari yanatupatia nuru zaidi Yesu ni nani na nguvu kamili na mamlaka aliyo nayo. Tukio hili linakazia mambo kadhaa muhimu. Kwanza, wanafunzi walisha muona Yesu akitenda miujiza mingi. Hivyo, walijua au walipaswa kujua kwamba angeliweza kutuliza bahari. Swali lao, *"Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia?"* (**ms.t 38**) linaonesha kuwa walikuwa wanamkemea, siyo kwa *kutokuwa na uwezo* kutuliza dhoruba, lakini kwa kutokuwajali na kutokuguswa kwa hitaji lao.

Kinyume chake, Yesu anawakemea, *"Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?"* (**mst. 40**) Hili linaibua swala muhimu la imani linalotuhusu wengi wetu. Kwanza, Wanafunzi walikuwa wanajiwazia wao wenyewe tu (nini kitawatokea), siyo Yesu (nini kitamtokea). Pili, Ingawa walimwendea Yesu, hawakuwa na amani, isipokuwa hofu. Walikuwa hawajajifunza bado kweli ya **1 Yh 4:16-18**: *"Nasi tumelifahamu pendo alilo nalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani yake. Katika hili pendo limekamilishwa kwetu, ili tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu; kwa kuwa, kama yeye alivyo, ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu. Katika pendo hamna hofu; lakini pendo lililo kamili huitupa nje hofu."*

Hilo ni kweli hata kwa walio wengi wetu tunapojiangalia wenyewe na hali zetu (bila kujali zinaweza kuwa mbaya kiasi gani), badala ya kumwangalia Bwana (ambaye ni Bwana juu ya hali hizo). Tatu, alikuwa amesema, *"tuvuke ng'ambo"* (**mst. 35**). Ukweli kwamba alikuwa amelala hilo lilipaswa kuwapa wanafunzi hali ya kujiamini na matumaini kwake! Kwa maneno mengine, Yesu alikuwa ana utawala mkononi mwake wa hali ile bila kujali ilikuwa hali ya namna gani, na maadamu unabaki kuwa mwaminifu kutenda alichokuagiza utende, ukimya wa Mungu unapaswa uamshe matumaini yako katika kutenda kile unachotenda. Nne, walipaswa kuwa na matumaini hayo (kama sisi inavyotupasa) kwasababu Yesu alionesha kwamba alikuwa anatawala na ana nguvu juu ya *kila kitu* (angalia **Zab 89:9; 93:4**). Kusema kweli, alitumia maneno yale yale (*phimoō*) katika kuiambia bahari *"tulia"* (**mst. 39**) kama alivyotumia katika **1:25** kuiambia roho chafu *"nyamaza."* Kugeuza vurugu ya ulimwenge wa asili ni mfano mwingine wa uwepo wa ufalme wa Mungu.

Katika **mst. 41** wanafunzi wanauliza swali ambalo kila mmoja wetu anahitaji kulifikiria na kupata jibu, *"Huyu ni nani basi?"* Ni Mungu-mtu, muumbaji, mtoshelezi, na mkombozi wa ulimwengu. Hivyo, yatupata kujiambatanisha na imani na kumtegemea bila kujali zile hali zinazotuletea hofu hasa kwa vile bila yeye, tutaenda wapi? Ni kweli kwamba tunataka tuwe peke yetu wakati hali inapokuwa ngumu na ya kutisha? Tunaweza kumtegemea hata (au hasa) tunapokuwa hatupendi au hatuelewi hali tunayokabiliana nayo, kwasababu siyo tu kwamba ameonesha nguvu zake kamili lakini amethibitisha kuwa anastahili kutegemewa.

Upande unaovutia wa tukio hili ni kufanana kwa tukio hili na Yona. "Yona anaondoka na mashua kuelekea upande ambao ni kinyume na taifa alikotumwa kutoa unabii; Yesu anaingia katika mashua kueleke upande "mwingine' akiwaacha makuatano waliokuwa wakimsonga" (Powell 2007: 160). Muktadha wa matukio yote mawili yanahusu kutoka eneo la Wayahudi kwenda eneo la Wamataifa. "Kama Yona alivyokuwa ndani ya meli ikashikwa na upepo mkali, na kurushwa rushwa na "dhoruba kali ya baharini." 'Bahari ilichafuka kwa upepo mkali' na 'meli ilikaribia kuvunjika.' Katika Mathayo 8:23-27 kadhalika kristo aliingia katika meli katika hali inayofanana na hiyo. Kulikuwa na "dhoruba kubwa baharini,' na 'meli ilifunikwa na mawimbi.' Yona alikuwa amelala chini pembeni mwa meli, fofofo,, wakati mabaharia walipopaza sauti kwa kuogopa na 'kila mtu kumuita mungu wake.' Kristo alikuwa amelala usingizi 'sehemu ya nyuma ya meli' (Mk 4:38) hadi wanafunzi wake walipomwamsha, wakisema, 'Bwana, tuokoe, tunaangamia.' Ni jinsi gani kilio cha Agano la Kale kinafanana, 'amka, muite Mungu wako . . . kwamba tunaangamia.' Katika Yona tunasoma, 'nayo bahari ikaacha kuchafuka,' na katika Marko, 'Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu." (Stanton 1951: 246-47) Baada ya bahari kutulizwa, **Yona 1:16** (LXX) inasema, *"Ndipo wale watu wakamwogopa Bwana mno."* Kadhalika, Kiyunai cha **Mk 4:41** kinasema, *"nao wakaogopa kwa hofu kuu."* Kwasababu Yesu ni "mkuu kuliko Yona," kuna mambo ya kupambanisha kati yao. Katika matukio mawili ya dhoruba baharini, "Yona alikuwa *amechoshwa na* kazi ya Mungu. Yesu alikuwa *amechoka kwa* kazi ya Mungu. Pia, Kristo alifanya kile ambacho Yona asingeweza kufanya [isipokuwa kile ambacho Mungu alifanya kwa habari ya Yona]. Alikemea upepo na kutuliza bahari iliyokuwa imechafuka kiasi kwamba watu walishangaa uwezo wake " (Ibid.: 247)

MASWALI YA KUJADILI

1. Linganisha na pambanisha mitazamo ya wanafunzi na Yesu, vitendo, na muitikio ndani ya safari ya mashua kuvuka kwenda ng'ambo. Tunapata mafunzo gani kutoka katika tukio hili?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

2. Huwa Mungu wakati mwingine (au mara nyingi) anaonekana kama amelala au kama vile haguswi na kile kinachotokea katika maisha yako? Kwanini unafikiri hivyo?

- Huwa tunaitikiaje nyakati kama hizo?
- Unapaswa uitikieje nyakati kama hizo?
- Kama kuna tofauti kati ya vile unavyopaswa na vile usivyopaswa kuitikia, kwanini kuna tofauti hiyo, na utafanyaje na hali hiyo?

3. Kwanini unafikiri kuwa baadhi ya watu wanaamini kuwa maisha yao yanapaswa kwenda "bila vikwazo" wakisha kuwa Wakristo?

- Imani hii inatuambia nini kuhusu uelewa wa watu hawa kwa Kristo?
- Kwa namna gani, kama ndivyo basi, unafikiri wazo hili linapaswa lishughulikiwe wakati unapojaribu kumleta asiye-mkristo kwa Kristo?

4. Katika **mst.40** Yesu alisema*"hamna imani bado?"* Ukitumia kifungu hiki (**mst. 35-41**), imani ni nini?

<u>5:1-20:</u> [1]Wakafika ng'ambo ya bahari mpaka nchi ya Wagerasi. [2]Na alipokwisha kushuka chomboni, mara alikutana na mtu, ambaye ametoka makaburini, mwenye pepo mchafu; [3]makao yake yalikuwa pale makaburini; wala hakuna mtu ye yote aliyeweza kumfunga tena, hata kwa minyororo; [4]kwa sababu alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo, akaikata ile minyororo, na kuzivunja-vunja zile pingu; wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda. [5]Na sikuzote, usiku na mchana, alikuwako makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikata-kata kwa mawe. [6]Na alipomwona Yesu kwa mbali, alipiga mbio, akamsujudia; [7]akapiga kelele kwa sauti kuu, akasema, Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese. [8]Kwa sababu amemwambia, Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu. [9]Akamwuliza, Jina lako nani? Akamjibu, Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi. [10]Akamsihi sana asiwapeleke nje ya nchi ile. [11]Na hapo milimani palikuwa na kundi kubwa la nguruwe, wakilisha. [12]Pepo wote wakamsihi, wakisema, Tupeleke katika nguruwe, tupate kuwaingia wao. [13]Akawapa ruhusa. Wale pepo wachafu wakatoka, wakaingia katika wale nguruwe; nalo kundi lote likatelemka kwa kasi gengeni, wakaingia baharini, wapata elfu mbili; wakafa baharini. [14]Wachungaji wao wakakimbia, wakaieneza habari mjini na mashambani. Watu wakatoka walione lililotokea. [15]Wakamwendea Yesu, wakamwona yule mwenye pepo, ameketi, amevaa nguo, ana akili zake, naye ndiye aliyekuwa na lile jeshi; wakaogopa. [16]Na wale waliokuwa wameona waliwaeleza ni mambo gani yaliyompata yule mwenye pepo, na habari za nguruwe. [17]Wakaanza kumsihi aondoke mipakani mwao. [18]Naye alipokuwa akipanda chomboni, yule aliyekuwa na pepo akamsihi kwamba awe pamoja naye; [19]lakini hakumruhusu, bali alimwambia, Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu. [20]Akaenda zake, akaanza kuhubiri katika Dekapoli, ni mambo gani makuu Yesu aliyomtendea; watu wote wakastaajabu.

<u>mst. 1-20—</u><u>Yesu amponya Mgerasi mwenye pepo</u>

Katika uponyaji huu wa mwenye pepo, Marko anaendelea kufikiri swali lililoibuliwa na wanafunzi katika **4:41**, *"Ni nani huyu, basi?"* Jibu linatolewa kwa wazi katika **mst. 7**, *"Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu." "nchi ya Wagerasi"* (**mst. 1**) ilikuwa upande wa mashariki wa bahari ya Galilaya na kwa sehemu kubwa ilikuwa nchi ya Wamataifa. Kwahiyo, haishangazi kwamba Yesu kuitwa *"Mwana wa Mungu aliye juu,"* kwa kuwa maneno hayo mara kwa mara yalitumiwa na Wamataifa (angalia **Mwa 14:18; Isa 14:14; Dan 3:26; Mdo 16:17**). Kama tulivyoona katika **1:24**, mapepo wanajua Yesu ni nani na yanamuogopa kwasababu yanajua hatimaye atawafanya nini (angalia **Mat 25:41; Yak 2:19**). Mtu aliyekuwa amepagawa na mapepo bila shaka alitambua Yesu alikuwa nani. Baada ya kufunguliwa, Yesu alimwambia, *"Nenda nyumani kwa marafiki zako na uwaambie <u>Bwana</u> amekutendea nini."* Yule mtu alitii na *"akaanza kutangaza kule Dekapoli ni mambo gani <u>Yesu</u> amemtendea."*

Mbali na asili ya kiungu ya Yesu na uweza juu ulimwengu wa kipepo, tukio hili linatuambia mambo mengine yenye umuhimu wa kivitendo. Kwanza, kama ilivyooneshwa hapo juu, *"nchi ya Wagerasi" ilikuwa*

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

upande wa mashariki wa bahari ya Galilaya na kwa sehemu kubwa ilikuwa ni nchi ya Wamataifa.[30] Hivyo, ilikuwa ni nje kabisa ya mazingira ya Yesu. Hata hivyo, kwa makusudi alitoka kwenda nje ili kumfungua mtu mmoja aliyemilikiwa na mapepo. Hii ni sawa na Yesu kutoka katika maeneo yake katika **Yh. 4** kumuingiza mwanamke msamaria katika imani. Hili linaonesha ni kwa jinsi gani Yesu anatoka katika "mazingira yake salama" kwa makusudi Kujipatia watu wa aina mbalimbali (makabila, rangi, uzawa, tamaduni, n.k.). Tuko tayari kufanya hivyo pia?

Pili, yatupasa kumwangalia mtu huyu kabla na baada ya kufunguliwa. Kabla Yesu hajatoa yale mapepo, **Mistari 3-4** inasema, *"Wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda. **4**kwa sababu alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo, akaikata ile minyororo, na kuzivunja-vunja zile pingu. Hakuna yeyote aliyeweza kumfunga tena, hata kwa minyororo."* Ijapokuwa wanadamu walishindwa kumfunga mtu huyu, alikuwa amefungwa kabisa na Shetani na mapepo. **Mstari 5** unaongeza kwamba *"na sikuzote, usiku na mchana, alikuwako makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikata-kata kwa mawe."* Baada ya kufunguliwa, **mst. 15** unatuambia kwamba alikuwa *"ameketi, amevaa nguo, ana akili zake."* Uwepo wa Mungu katika maisha yetu hautuingizi kwenye tabia za kilimbukeni na ukichaa isipokuwa amani, akili njema, kiasi na kumrejesha mtu katika kukaa kwa amani na wengine na Mungu (angalia **Gal 5:22-23**). Nimesikia wahubiri kadhaa wakitoa sauti kama ng'ombe anayechinjwa au mtu mwenye hasira wanapotoa "ujumbe" wao kwa sauti iliyoharibika. Sina hakika hili linatokana na utamaduni kwa kiasi gani au kuiga wengine, lakini inaonekana kwangu kwamba mkao wa aina hiyo ndiyo njia ya kuwashawishi watu (hasa wasioamini) kwamba una kichaa; pia ni hakika lina matokeo hasi kwa mtu ambaye ana mahusiano na mtu kama huyo. Kumbuka: Mungu anataka matunda ya kiroho, siyo wazimu wa kidini.

Pande mbili za mazungumzo ya huyu mtu zinastahili kuangaliwa: (A) Mtu huyu hakuwa na chochote kabisa cha kuchangia wokovu wake. Alikuwa mhanga wa mapepo asiyejiweza kabisa; hakuwa na uwezo kufanya chochote, wala hakufanya juhudi yeyote ya kumsaidia kuongoka. Kuchaguliwa kwake, kuitwa, na kufanywa upya (yaani, kuwa "mtu aliyezaliwa mara ya pili") ilikuwa ni kazi ya neema kamili ya kiungu. (B) *Mwitikio* wake kwa uongofu unatueleza uhalisia wa kuzaliwa kwake mara ya pili: alitaka kumfuata na kumtumikia Yesu (**mst. 19**). Na alifanya hivyo (**mst. 20**), kama alivyofanya mwanamke msamaria katika **Yohana 4**. Yesu alijua kuwa ukichukulia mwitikio wa watu waliobakia wa eneo hilo kuhusu uwepo wake (**mst. 15-17**), kwamba akishaoColewa, yule aliyekuwa amepagawa na mapepeo angeweza kuwa na matokeo makubwa katika eneo lile kuliko hata uwepo wa Yesu mwenyewe.

Mwisho, ni muhimu kuona mwitikio wa watu wengine wa eneo hili na mwitikio wa Yesu. Watu waliogopa (**mst. 15**) na *"kuanza kumuomba Yesu aondoke katika maeneo yao"* (**mst. 17**). Hofu yao inaweza kutokana na sababu kadhaa: walikuwa mbele ya uwepo wa mtu aliyekuwa na nguvu halisi, za kushangaza na zisizo za kimwili. Itikio la kawaida kwa watu mbele za Mungu (au malaika) katika Biblia yote ni pamoja na kuogopa. Kwa nyongeza, walipoona kilichotokea kwa nguruwe, wanaweza wakawa waliogopa kuendelea kupata hasara kama Yesu angeendelea kuwepo. Tena, kwa kuwa walikuwa wamejaribu kumfunga mtu yule aliyekuwa amepagawa na kufungwa kwa minyororo, lakini Yesu sasa amemweka huru, wanaweza wakawa waliogopa Yesu angewafanyaje. Mwitikio wao unafanana na ule wa makuhani wakuu na waandishi katika **Mk 11:18** wakati Yesu alipotakasa hekalu.

"Jambo la kuhuzunisha katika kisa hiki chote ni kwamba Yesu alikubali ombi lao. Kuna wakati mwingine tunaweza kupata majibu ya maombi yetu kutoka kwa Bwana kwa hasara yetu (Zab. 106:15, 'Aliwapa walichomtaka'). Wagerasi walitaka huyu Yesu aliyewatishia usalama wao awaachwe wenyewe tu. Ilikuwa iwe ni uamuzi wao kwamba Yesu awaache na asirudi tena, kwa kuwa hakuna ushahidi, katika Marko wa kuwepo kwa huduma ya Yesu baada ya tukio hili." (Cole 1989: 159) C. S. Lewis anahitimisha kwa kusema, "Mwishoni kuna aina mbili tu za watu: wale wanaomwambia Mungu, 'mapenzi yako yatendeke,' na wale ambao mwishoni Mungu anawaambia 'Mapenzi *yako* yatendeke." (Lewis 1946: 66-67)

MASWALI YA KUJADILI

1. Mgerasi mwenye pepo anakupendaje? Tukio hili ni bora kiasi gani kuwa mfano wa sura ya uongofu wa kweli?

2. Umewahi kutoka nje ya mazingira yako salama na "kuingia katika himaya ya adui" kupeleka injili? Matokeo

[30] Ingawa wafafanuzi wengi hufikiria kuwa aliyekuwa amepagawa na pepo alikuwa Mmataifa kwa msingi wa eneol alimoishi na nguruwe wengi, Rikk Watts anaorodhesha sababu kadhaa zinazoibua mashaka kuhusu nadharia hiyo (Watts 1997: 164-66).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

yalikuwaje?

3. Mwitikio wa watu (**mis.15-17**) unashangaza. Unafikiri ni kwanini waliogopa na kumuomba Yesu aondoke? Umewahi kukutana na hali kama hiyo wakati ulipokuwa umetenda kwa uaminifu kwa ajili ya Yesu?

4. Kwanini Yesu hakumruhusu yule mtu kufuatana naye wakati alimuomba afuatane naye?

- Ni kwa jinsi gani aliyekuwa amepagawa amngeliweza kuwa *shahidi bora* kuliko Yesu mwenyewe (kama Yesu angeendelea kukaa katika eneo lile)?

- Ndivyo ilivyo kwako (kwanini au kwanini sivyo)?

5:21-43: ***[21] Hata Yesu alipokwisha kuvuka kurudia ng'ambo katika kile chombo, wakamkusanyikia mkutano mkuu; naye alikuwa kando ya bahari.[22]Akaja mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo; hata alipomwona, akaanguka miguuni pake,[23]akimsihi sana, akisema, Binti yangu mdogo yu katika kufa; nakuomba uje, uweke mkono wako juu yake, apate kupona, na kuishi.[24]Akaenda pamoja naye; mkutano mkuu wakamfuata, wakimsonga-songa.[25]Na mwanamke mmoja mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili,[26]na kuteswa mengi kwa mikono ya matabibu wengi, amegharimiwa vitu vyote alivyo navyo, kusimfae hata kidogo, bali hali yake ilizidi kuwa mbaya[27]aliposikia habari za Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi lake;[28]maana alisema, Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona.[29]Mara chemchemi ya damu yake ikakauka, naye akafahamu mwilini mwake kwamba amepona msiba ule.[30]Mara Yesu, hali akifahamu nafsini mwake kwamba nguvu zimemtoka, akageuka kati ya mkutano, akasema, Ni nani aliyenigusa mavazi yangu?[31]Wanafunzi wake wakamwambia, Je! Wawaona makutano wanavyokusonga-songa, nawe wasema, Ni nani aliyenigusa?[32]Akatazama pande zote ili amwone yule aliyelitenda neno hilo. [33]Na yule mwanamke akaingiwa na hofu na kutetemeka, akijua lililompata, akaja akamwangukia, akamweleza kweli yote.[34]Akamwambia, Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena.[35]Hata alipokuwa katika kunena, wakaja watu kutoka kwa yule mkuu wa sinagogi, wakisema, Binti yako amekwisha kufa; kwani kuzidi kumsumbua mwalimu?[36]Lakini Yesu, alipolisikia lile neno likinenwa, akamwambia mkuu wa sinagogi, Usiogope, amini tu.[37]Wala hakumruhusu mtu afuatane naye, ila Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye Yakobo.[38]Wakafika nyumbani kwa yule mkuu wa sinagogi, akaona ghasia, na watu wakilia, wakifanya maombolezo makuu.[39]Alipokwisha kuingia, akawaambia, Mbona mnafanya ghasia na kulia? Kijana hakufa, bali amelala tu.[40]Wakamcheka sana. Naye alipokwisha kuwatoa nje wote, akamtwaa babaye yule kijana na mamaye, na wale walio pamoja naye, akaingia ndani alimokuwamo yule kijana.[41]Akamshika mkono kijana, akamwambia, Talitha, kumi; tafsiri yake, Msichana, nakuambia, Inuka.[42]Mara akasimama yule kijana, akaenda; maana alikuwa amepata umri wa miaka kumi na miwili. Mara wakashangaa mshangao mkuu.[43]Akawaonya sana, mtu asijue habari ile; akaamuru apewe chakula.***

mst. 21-43—Binti Yairo na mwanamke mwenye kutokwa na damu

Sehemu hii imekaa kama **3:20-35** ilivyokuwa. Inaanza na mwanzo mfupi kuhusiana na binti wa Yairo, kisha inahamia kwa uponyaji wa mwanamke aliyetokwa na damu, kisha inahitimisha na kufufuliwa kwa binti wa Yairo. Marko amemfunua Yesu kama Mwana wa Mungu mwenye nguvu juu ya asili na mapepo. Hapa anadhihirishwa kama mwenye nguvu juu ya mauti yenyewe. Katika matukio yote yanaendeleza mada ya hali ya mwanadamu kujishindwa kabisa ambayo imeoneshwa katika tukio la kufunguliwa kwa Mgerasi aliyekuwa amepagawa. “Kulingana na shreia za Kiyahudi kugusana na kaburi, damu, au kifo vilimfanya mtu kuwa najisi” (Wessel 1984: 660). Sehemu hii pia inaongeza kitu kipya: imani. Pale ambapo matukio ya awali yalikazia kutokuamini watu (hasa wapinzani wa Yesu), matukio haya mawili yanaangazia imani ya wale wanaomwendea Yesu.

1. **mst. 21-24a**—Yairo anamkaribia Yesu

Yairo anaelezwa kama *“mmoja wa wakuu wa sinagogi”* (**ms. wa. 22**). Watawala wa sinagogi walikuwa watu maarufu wenye sifa njema waliosaidia ujenzi na ibada (Wessel 1984: 660). Kwa vyovyote Yairo alikuwa ameshamsikia Yesu na kuamini kuwa anaweza kumponya binti yake. Hali yake isiyo na njia nyingine ni kubwa mno kiasi cha kuacha kiburi chake chote na kuanguka miguuni mwa Yesu, akiomba aambatane naye. Bila kusema neno, Yesu anakubali.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

2. **mst. 24b-34—**Mwanamke mwenye kutokwa na damu

Mwanamke huyu imesemekana alikuwa *"akitokwa na damu kwa miaka kumi na mbili"* (**mst. 25**). Maneno haya ni sawa na yale ya **Law 15:25** ambayo yanasema, *"Na mwanamke kama akitokwa na damu yake siku nyingi, nayo si katika majira ya kutengwa kwake, au kama anatoka damu kuzidi majira ya kutengwa kwake; siku hizo zote za kutoka damu ya unajisi wake, atakuwa kama alivyokuwa katika siku za kutengwa kwake; yeye yu najisi.* Mlinganisho wa maneno ya Walawi na Marko unaonesha kwamba huyu mwanamke alikuwa na kile ambacho kinazungumziwa na Walawi. Kama hili limeanzia wakati wa kubalehe, basi nusu ya maisha yake ingeishia kuteswa na tatizo hili. Mateso yake yalikuwa mabaya: ameteseka kwa kuhudumiwa na waganga wengi; ametumia mali zake zote alizokuwa nazo; na hali yake iliendelea kuwa mbaya (**mst. 26**). Mbali na hayo, **Law 15:26-27** inasema, *"Kila kitanda akilaliacho katika siku zote za kutoka damu kitakuwa kama kitanda cha kutengwa kwake; na kila kitu atakachokilalia kitakuwa najisi, kama unajisi wa kutengwa kwake. Na mtu ye yote atakayevigusa vitu vile atakuwa najisi, naye atazifua nguo zake, na kuoga majini, naye atakuwa najisi hata jioni."* Hilo lilimaanisha kuwa "asingeweza kuingia katika sinagogi na angetengwa hata na washirika wa familia yake mwenyewe, ambao wangekuwa najisi kama wangegusa chochote ambacho alikalia au kushika" (Cole 2006: 1180). Asingeweza kuolewa. Huenda ndiyo maana alimkaribia Yesu kwa nyuma (**mst. 27**).

Imani yake ilikuwa imara. Alijisemea, *"Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona"* (**mst. 28**). "Mamia ya miaka kabla ya kuzaliwa Yesu, nabii Malaki alikuwa amemtabiri Masihi ambaye atakuja na 'uponyaji katika mbawa zake' [**Mal 4:2**]. Kwa baadhi yao, hilo lilimaanisha kuwa alikuwa na uponyaji katika pindo za vazi lake.' Na nabii Zakaria alikuwa ametabiri kwamba watu kutoka kila taifa watataka kugusa upindo wa vazi lake au vishungi vya vazi la masihi kwasababu wangelitambua kuwa Mungu yuko pamoja naye [**Zak 8:23**]." (Vander Laan and Mrkham 1996: 74) Mguso wa mwanamke kwa vazi la Yesu ulikuwa ni tendo la imani. "Hili lilikuwa ni kuthibitisha kuwa alitambua sifa za kimasihi alizokuwa nazo Yesu na matendo yake. Aliamini alikuwa Masihi. Kwasababu aliamini hivyo—kwasababu ya imani yake kubwa—nguvu za Yesu zilitiririka na kumuingia. Zilimponya mwili wake, na kumrudishia ushirika na jamii ambayo alikuwa ametengwa nayo kwa muda mrefu." (Ibid.)

Imani yake inaweza kuwa kubwa ndani kuliko inavyoonekana kwa nje. Kwake kumgusa mtu (Yesu na wale waliokuwemo katika mkutano ambao alilazimika kuwasukuma apate njia) kungemfanya yeyote aliyeguswa kuwa najisi. Kitendo cha Yesu kutangazia mkutano kuwa ameguswa naye (**mst. 33-34**) kingekuwa ni kutangaza kuwa *ame*shanajisika. Mwanamke huyu aliyajua hayo, na bado imani yake ikaweza kumsukuma kusonga mbele. Hata hivyo, inawezekana kuwa pia alijua kwamba, kama ilivyokuwa katika kisa cha Yesu kumgusa mkoma na kumponya katika **1:40-45**, kwa kuwa Yesu alikuwa ni Masihi na Mwana wa Mungu, uchafu na "unajisi" havikuhamishika kwenda kwake, isipokuwa "usafi" ndio ulihamishika kwenda kwa mtu aliyemgusa au aliyeguswa naye. Kama Vander Laan na Markham wanavyoliangalia hili, "Maajabu haya hayakuwa katika kuguswa na Yesu; yalikuwa katika haki na utakatifu wake. Musa alikuwa ameponya. Eliya alikuwa amefufua mfu. Hivyo matendo hayo, pamoja na kuwa ya miujiza hivyo, siyo yaliyomtofautisha Yesu. Hayo yangalimfanya kuwa mmoja wa manabii wakubwa. Kilichomfanya kuwa tofauti ilikuwa ni utii wake kamili kwa Baba yake." (Vander Laan na Markham 1996: 74) Zaidi ya hayo, yafaa tuone kuwa kumuita yule mwanamke (jambo ambalo ndilo alilofanyika katika **mst. 30**), na kisha kutumia muda kuongea naye, Yesu alikuwa anamthibitisha mwanamke huyu na kuithibitisha imani yake—huenda anaweza akawa hajawahi kuthibitishwa na yeyote kwa miaka hiyo kumi na miwili. Alifanya hivi hata kama alionekana kutumia muda wa thamani wa safari yake ya kwenda kumponya binti wa Yairo.

Kuna upande mwingine wa tukio hili ambao umejificha lakini siyo kwa bahati mbaya. Kuponywa kwa mwanamke huyu, kama pia ilivyopendekezwa kwa habari ya uponyaji wa Mgerasi aliyekuwa na pepo na kama itakavyokuwa katika kumfufu binti wa Yairo, ni alama au picha ya wokovu wa kiroho. **Rum 10:9-10** inasema, *" Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."* (angalia pia **Mat 10:32; Lk 12:8**) Mwanamke huyu alikuwa ameamini katika moyo wake. Alitambua kwamba Yesu alipomuita ajitokeze, alikuwa anamwita ili "akiri kwa kinywa chake," na ndivyo alivyofanya (**mst. 33**). "Tayari alikuwa ameponywa kwa imani yake, lakini kukiri hadharani kulimletea neno la uthibitisho kutoka kwa Yesu.. . . . Kwa upande mwingine hili, lilileta kutambua njia ambayo imemfikisha kwenye muujiza wake (*imani yako* . . .), ahadi ya amani ya Mungu, na kujisikia salama kwa ajili ya yaliyoko mbele." (Cole 1989: 162) Uponyaji wake wa kimwili unaenda sambamba na wokovu: amejaribisha kila njia ali "ajiponye," lakini njia zote hazikufaa; anatambua hali yake isiyo na tumaini na anaona kwamba ni Yesu pekee anayeweza kumponya. Vivyo hivyo kwetu sisi kwa habari ya wokovu. Haipaswi basi kushangaza kwamba Yesu alipomwambia, *"Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena"* (**mst. 34**), neno "uwe mzima" (Kigiriki = *sōzō*) ni neno lile lile linalotumika kwa "uokolewe"

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

(yaani, wokovu kutoka katika mauti ya milele). Yesu kumuita "Binti" kunawakilisha ukweli kwamba tunapokuwa tumeokolewa, tunaasiliwa katika familia ya Mungu (angalia **Yh 1:12; Rum 8:14-17, 23; 9:4; Gal 3:26; 4:5-7; Efe 1:5; 2:19; 1 Yh 3:1**). Kumuambia *"aende kwa amani"* kuna maana ya amani ambayo Yeye tu ndiye huitoa, siyo kama ulimwengu unavyotoa (angalia **Yh 14:27**); kwa maneno mengine, "shwari ya nafsi iliyohakikishiwa wokovu wake kwa njia ya Kristo, haiogopi chochote kutoka kwa Mungu wala matokeo ya yale yanaayoweza kutokea duniani, ya namna yeyote. Haya ni matokeo ya moja kwa moja ya ukombozi wa Kristo." (Zodhiates 1993: *eirēnē,* 520)

Matumizi mojawapo ya tukio hili kwetu ni kwamba "sisi, pia, tunaweza kuwarejesha wengine kwa jamii kwa imani. Kukubalika kwetu, kujitoa kwetu, na ushuhuda wetu kuhusu uhalisia wa Yesu kuwa siyo tu masihi lakini ni masihi wetu kunatufungulia njia za uponyaji wa Mungu na nguvu ya kutufanya upya, iwe ni kwa mahitaji yetu ya kimwili, ya kimhemko, na kuvunjika kwetu kiroho au mahitaji ya wengine." (Ibid.: 74-75)

3. **mst. 35-43—**<u>Yesu amfufua binti wa Yairo</u>

Katika **mst35** Yairo anagundua kuwa binti yake ameshakufa, kwahiyo mtu aliyemletea habari alisema, *"kwanini kuzidi kumsumbua mwalimu?"* Jibu la Yesu kwa Yairo ni kutumia somo la mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu: *"usiogope, amini tu"* (**mst. 36**). Hata miongoni mwa wale kumi na wawili, Yesu alikuwa na wachache wa "karibu zaidi" (angalia **Mat 17:1; Mk 9:2; Lk 9:28**). Wakati Yesu aliposema mtoto "amelala" tu (**mst. 39**), ni sawa na kifo cha mwenye haki kama ilivyo katika **1 Thes 4:14** (angalia **Lk 8:55**). Kama ilivyo kwa mkoma na mwanamke mwenye kutokwa na damu, Yesu hakusita kumgusa mtu ambaye angeweza kumfanya awe "najisi" kwa mujibu wa mapokeo (**mst. 41**). Kuwaambia wazazi wampe msichana kitu ale (**mst. 43**) inaonesha kujali kwa Yesu katika mahitaji ya kawaida ya kibinadamu, ikiwa ni pamoja na hitaji la kujiburudisha baada ya kazi ngumu.[31] Ukweli kwamba Marko anaandika kwamba Yesu alikuwa akiongea kwa kiaramaiki (**mst. 41**) na kuwaambia wazazi kumpatia binti kitu ale (**mst. 43**) ni mambo madogo ya kina ambayo yangaliwezekana tu kutoka kwa mtu aliyeshuhudia kwa macho (huenda akawa Petro) na ukihusisha kuwa hiki ni kisa cha kweli cha kihistoria, siyo jambo la kutungwa. Tukio hili linakamilisha matukio kadhaa ambayo kwa pamoja yanafunua utambulisho wa Yesu kama Masihi na Mungu aliyekuja duniani. Ana nguvu juu ya ulimwengu wa kimwili: madhaifu na magonjwa (**1:30-34; 2:11-12; 3:1-5; 3:25-34**), matendo ya asili (**4:35-41**); ulimwengu wa mahusiano ya kibinadamu, ya kifamilia (**5:19, 43**) na kijamii (**1:40-44; 2:14-17; 5:19-20, 34**); na ulimwengu wa kiroho: dhambi (**2:1-12**), Sabato, sheria ya Mungu, na desturi za kidini (**1:40-41; 2:14–3:6; 5:5, 27-34, 41**), Shetani na Mapepo (**1:24-26, 34, 40-44; 3:22-27; 5:1-13**), na mauti (**5:35-43**). Hivyo tunapata jibu lililosheheni vema la swali la wanafunzi katika **4:41**, *"Huyu basi, ni nani?"*

Kufufuliwa kwa binti wa Yairo kunatupa tena alama nyingine au picha ya wokovu. Msichana huyu alikuwa amekufa na hakuweza kufanya chochote ili ajifufue arudi kwenye maisha ya kawaida, kama na sisi tulivyokuwa *"wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazo tuliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu"* (**Ef 2:1-2**) na hatukuweza kufanya chochote kujifufua ili kuingia katika maisha mapya. Kufufuliwa kwa binti huyu kutoka kwa wafu kulifanywa na Yesu bila mtu au kitu kingine kuhusika; hakuchangia chochote, kama vile sisi pia ambavyo hatukuchangia chochote ili kufanywa upya na kuhesabiwa haki, jambo ambalo hukamilishwa kabisa na Yesu. Kimwili, kwa namna fulani, alikuwa "amezaliwa upya" kama vile na sisi ambavyo ni lazima tuzaliwe upya tuweze kuuona ufalme wa Mungu (**Yh 3:3**). Kama alivyofufuka kimwili na *"kuanza kutembea"* (**mst. 42**), kadhalika uinuke na *"kutembea katika upya wa maisha"* (**Rum 6:4**). Kama ambavyo alitakiwa kupewa kitu fulani ale, kadhalika tunapaswa kufunzwa katika maisha yetu mapya, kwanza kwa "maziwa" kisha kwa "chakula kigumu" cha neno la Mungu (angalia **1 Kor 3:1-2; Ebr 5:12; 1 Pet 2:2**).

<u>MASWALI YA KUJADILI</u>

1. Tukio la mwanamke mwenye kutokwa na damu liliwakilisha kuingiliwa kwa mpango wa Yesu na Yairo. Yesu alionaje na kushughulikia "kuingiliwa" huku? Huwa unaangaliaje na kushughulikia kuingiliwa kwa mipango yako?

2. Kwanini Yesu aliuliza nani aliyenigusa na kuangalia waliomzunguka akimtafua yule mwanamke? Yesu aliitikiaje akionesha upendo wake kwake?

3. Unashughulikiaje wazo la kwamba, kwasababu ya mkazo wa imani katika matukio haya mawili,

[31] Kitu kama hicho kilitokea katika **1 Fal 19:1-8** kwa Eliya wakati alipokuwa anajificha pangoni dhidi ya Yezebeli.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

yanavyotufundisha, kama unaomba kwa ajili ya uponyaji na hujaponywa, ni kwasababu huna imani?

4. Yairo (mwanaume, mtawala, mtu muhimu katika jamii) na mwanamke (asiye na jina, najisi na huenda aliyetengwa) wote wananyenyekea kwa Yesu wakati wa uhitaji mkubwa. Ni aina gani ya watu huwa hupata shida kunyenyekea kwa Yesu?

- Tunawezaje kuwasaidia watu kama hao kujinyenyekesha wenyewe kwa Yesu?

- Unafikiri Mungu anajisikia vibaya wakati watu wanapojitokeza kwake wakati wakiwa na shida tu?

5. Uponyaji wa mwanamke mwenye kutokwa damu na kufufuliwa kwa binti wa Yairo unakuwaje mfano mzuri au fumbo la wokovu?

6. Katika mifano hii, kama ambavyo mara kwa mara ilitokea, Yesu anaonekana kupuuza au hata kutawanya mkusanyiko wa watu (wakati ilikuwa awahudumie) ili kuweka mkazo katika kuhudumia mtu maalumu. Unafikiri kwanini alifanya hivyo na hili linatuambia nini kuhusu Yesu?

- Mifano hii ya Yesu inatuambia chochote kuhusu kipi kinapaswa kuwa muhimu kwetu na namna tunavyopaswa kuzunguka kuieneza injili?

- Kwanini unafikiri Wakristo huangalia sana idadi na ukubwa wa huduma, ushawishi, na kanisa kuliko kina na ubora?

6:1-6: ***[1]Akatoka huko, akafika mpaka nchi ya kwao; wanafunzi wake wakamfuata. [2]Na ilipokuwa sabato, alianza kufundisha katika sinagogi; wengi waliposikia wakashangaa, wakisema, Huyu ameyapata wapi haya? Na, Ni hekima gani hii aliyopewa huyu? Na, Ni nini miujiza hii mikubwa inayotendeka kwa mikono yake? [3]Huyu si yule seremala, mwana wa Mariamu, na ndugu yao Yakobo, na Yose, na Yuda, na Simoni? Na maumbu yake hawapo hapa petu? Wakajikwaa kwake. [4]Yesu akawaambia, Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake. [5]Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. [6]Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao. Akazunguka-zunguka katika vile vijiji, akifundisha.***

mst. 1-6—Yesu kule Nazarethi

Ingawa haitajwi, mji alikozaliwa Yesu ulikuwa Nazareth, kijiji kidogo katika Galilaya, magharibi mwa mto Galilaya (angalia **Mk 1:9, 24; Lk 4;16; Yh 1:46**). Maswali na mawazo ya watu katika **mst. 2-3** yanaonesha kwamba huenda ilikuwa ni mara ya kwanza Yesu kufundisha katika sinagogi la nyumbani kwake. Sifa yake kama mwalimu na mtenda miujiza kwa vyovyote ilikuwa imemtangulia. **Mistari 3** kwa mara nyingine tena anataja familia ya kibaolojia ya Yesu[32] na kazi yake kabla hajaanza huduma yake hadharani.[33]

Tukio hili linafunua mabadiliko ya hatua kwa hatua ya muitikio wa watu kwa Yesu. Unaonesha ni kiasi gani watu siyo wa kutegemea. Angalia akiwa anaongea, watu waliokuwemo katika sinagogi wanahama kutoka "kushangaa" (**mst. 2**) hadi "kukwazwa" (**mst. 3**) na Yesu. Hili linatuambia kuwa mshangao wao ulikuwa na msingi katika ukweli kwamba ni wazi Yesu alikuwa mwalimu mzuri, yaani, watu walishangazwa na *mtindo* wake. Hata hivyo, kukwazika kwao kunaonekana kutokana na kutafakari *mambo* ambayo Yesu alisema.[34] Hilo linaoneshwa katika maneno ya Yesu katika **mst. 4** kuhusu yeye kuwa "nabii" (yataelezewa hivi punde hapa chini) na Luka anavyoandika juu ya hili katika **Lk 4:16-30**. Katika maandiko ya Luka, Yesu anasoma kutoka **Isa 61:1-2**, kifungu cha maandiko ambacho kinarejea mwaka wa Jubilii. Ananukuuu, *"Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za*

[32] Kupata zaidi kuhusu familia ya kibaolojia ya Yesu, angalia majadiliano katika **3:20-21, 31-35**, hapo juu.
[33] Yesu, kama wengi wao katika wakati wake na utamaduni wake, alifuata nyayo za aliyedhaniwa kuwa baba yake kama seremala (angalia **Mat 13:55**).
[34] Hili linapasw akuwa onyo au angalizo kwetu kwamba siyo lazima tupokee tuyaonayo watu wanapokuja mbele na "kumpokea Yesu" wakati wa kampeni za kiinjilisti. Wanaweza kufanya hivyo kwasababu za kimhemko, wakibebwa na "joto la yaliyoko" kuwafurahisha marafiki zao, au kwasababu zingine. Mfano wa mpanzi na aina za udongo (**Mk 4:1-20**) tayari umetuonesha kwamba kuna imani ya muda ambayo siyo imani inayookoa. Imani ya kweli, inayookoa huvumulia, hubadilisha mtu kutokea ndani, na hubadilisha matendo na maisha yao.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kufunguliwa kwao. Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao" (**Lk 4:18-19**). Kisha akasema, "leo hii sehemu hii ya maandiko imetimizwa masikioni mwenu*"* (**Lk 4:21**). Neno "kufunguliwa" katika **Isa 61:1** (**Lk 4:18**) ni neno lile lile katika **Law 25:10**. Kitenzi katika kifungu hiki (*"kuwahubiria injili maskini," "kutangazia kufunguliwa kwao waliofungwa," "kuweka huru walioonewa"*) linahusu "yale yaliyokuwa yameagizwa katika Walawi 25 kuhusu mwaka wa Jubilei, ambapo rasilimali zilizokuwa zimeshikiliwa katika maswala ya kifedha zilirudishwa ili kuruhusu jamii imara na yenye ufanisi. Hivyo, mfululizo wa vitenzi unachukuliwa kuwa ni tangazo la Jubilei." (Brueggemann 1998: 214) *"Mwaka wa Bwana uliokubalika"* unarejea "mwaka wa Jubilei" ambao unafanywa kama alama na matendo yake [Yesu] ya wokovu (Marshall 1978: 184). Katika **Lk 4:14–21**, wakati Yesu aliponukuu **Isa 61:1-2** na kusema, *"Leo hii maandiko haya yametimizwa masikioni mwenu,"* kiuhalisia alikuwa anasema, "mimi ndiye utimilifu wa kile ambacho siku zote kilitarajiwa; katika mimi Jubilei ya mwisho imewafikia hapa."

Yesu alikuwa anatoa madai ya kushangaza ya kimasihi: Roho wa Mungu yu juu *yangu*! Mungu ame*ni*paka mafuta! *Mimi* ndiye utimilifu wa yale ambayo siku zote AK lilitumainisha! Ni katika muktadha huo watu walihoji asili ya hekima ya Yesu na nguvu na kuibua ukweli kwamba alikuwa ni seremala tu kutoka katika familia iliyoko kwenye kijiji kidogo ambacho kila mmoja alikijua. Hawaamini kuwa ndiye kama anavyodai na wanamkataa. Kama tulivyoona, wengi miongoni mwa viongozi wa dini walikuwa wamemkataa Yesu, kama walivyofanya wale wa eneo la Wagerasi, waombolezaji kwenye kifo cha binti wa Yairo, na hata familia yake mwenyewe. Sasa, watu wa mji wake wanamkataa pia. Huu ni mfano wa msemo unaosema, "Kuzoeana kunaleta dharau." Yesu "alishangaa" (Kigiriki = *thaumazō*) kwa kutokuamini kwao (**mst. 6**). Kuna sehemu mbili tu ambako Yesu alisemwa kuwa "alishangaa": hapa na katika **Mat 8:10** ambapo alishangaa imani ya liwali aliyesema, *"Bwana sistahili wewe kuingia katika dari yangu, sema neno tu, mtumwa wangu atapona"* (**Mat 8:8**). Mlinganisho una mashiko: mpagani, Mmataifa wa Kirumi ana imani kubwa, lakini Wayahudi wa nyumbani kwake waliomfahamu, hawana. Huu ulikuwa mfano wa wazi wa **Yh 1:11** (*"Alikuja kwa walio wake, na walio wake hawakumpokea")* jambo ambalo linaashiria kukataliwa kwake mwisho wa safari yake na makutano wasio na msimamo kule Yerusalemu na kusulubiwa.

Yesu mwenyewe kujiita "nabii" (**mst. 4**) siyo tu kunaonesha mshangao wake kwa kutokuamini kwa wale watu lakini kunajenga katika yale ambayo amekuwa akisema ambayo yalisababisha watu kumkataa. Sababu ni hii kwamba katika **Kumb 18:15-19** Musa alisema, *"[15] Bwana, Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye. [16] Kama vile ulivyotaka kwa Bwana, Mungu wako, huko Horebu, siku ya kusanyiko, ukisema, Nisisikie tena sauti ya Bwana, Mungu wangu, wala nisiuone tena moto huu mkubwa, nisije nikafa. [17] Bwana akaniambia, Wametenda vema kusema walivyosema. [18] Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. [19] Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake.'"* Yesu anadai kuwa nabii huyo. AJ, siyo mara moja bali mara nne, humtambulisha Yesu kama nabii aliyetabiriwa. Katika **Yh 1:45**, baada ya kukutana na Yesu, Filipo anampata Nathanaeli na kumwambia, *"Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, — Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti."* katika **Yh 6:14**, baada ya Yesu kutenda alama ya kimiujiza, watu walioshuhudia muujiza ule walisema, *"Hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimwenguni."* "Nabii" pekee anayeweza kuzungumziwa hapa ni nabii aliyetabiriwa katika **Kumb 18:15-19**. **Mdo 3:22** na M**do 7:37** wote wananukuu kana kwamba unabii umetimizwa na Yesu. Mahubiri ya Petro katika **Mdo 3:11-26** yanahusu Mungu kumwinua Yesu ambaye Wayahudi walimuua (na kama pia alivyotabiriwa) na jinsi Yesu alivyotimiza unabii: matokeo yake, watu walitaka kutubu au wataangamizwa Kristo atakaporudi tena. Katika Mdo **7**, Stefano alirejea historia ya Israeli kwa viongozi wa Kiyahudi. Baada ya kunukuu unabii wa Kumbukumbu la Torati anahitimisha kwa kusema, *"kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo. Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwudhi? Nao waliwaua wale waliotabiri habari za kuja kwake <u>yule Mwenye Haki; ambaye ninyi sasa mmekuwa wasaliti wake, mkamwua</u>."* (**Mdo 7:51-52**) "Mwenye haki," hapa , siyo mwingine isipokuwa Yesu ambaye amesalitiwa na kuuwawa kwa njama za viongozi wa Wayahudi.

Tukio hili lote linakazia kutokuamini kwa watu waliomjua Yesu. Hili linasimama katika kulinganishwa na imani kuu ya Yairo na mwanamke mwenye kutokwa na damu katika matukio yaliyofuata baada ya hili. Kwasababu ya kukosa imani kwa watu wa Nazareth, Yesu *"hakuweza kutenda matendo makuu huko,"* (**mst. 5**), pia katika kupambanisha na kile kilichokuwa kimetokea punde kwa mwanamke na binti wa Yairo. Hata hivyo, Walter Wessel anatukumbusha, "Kusema kweli, hivi siyo kusema kwamba, hakuwa na uwezo wa kufanya miujiza mingi kuliko aliyotenda kule Nazareth. Kutokuwepo kwa uwezo huo kulihusiana na hali ya kimaadili. Katika mazingira ya kutokuamini alichagua kutokutumia nguvu yake ya kimiujiza. Moja ya mambo ambayo injili ya Marko inakazia ni kwamba Yesu hutenda miujiza yake kutokana na uwepo wa imani." (Wessel 1984: 666)

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

MASWALI YA KUJADILI

1. Watu wangewezaje kuhama kutoka *"kushangwazwa"* (**mst. 2**) hadi *kukwazwa* (**mst. 3**) na Yesu? Kwa upande mwingine, kifungu hiki kinatoa msingi wa *tumaini* lolote kwetu?

2. Kama chanjo, *mazoea* katika mambo ya Mungu na lugha ya dini ("Mungu huongea") vinaweza kuwa mahali panapostawisha kukataliwa kwa Yesu halisi. Tunaepukaje hatari ya kwamba imani yetu (na watoto wetu) inatosha kutupatia kinga kinyume na kitu halisi?

3. Umekutana na ukweli kiasi kwamba ni vigumu kuwa mtumishi mwaminifu wa Yesu ndani ya familia yako kuliko kwa watu wasio wa familia yako?

- Umeshughulikiaje hali hii tata?

- Tunapaswa kushughulikiaje hali hii tata?

6:7-13, 30-32: *7 Akawaita wale Thenashara, akaanza kuwatuma wawili wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu; 8 akawakataza wasichukue kitu cha njiani isipokuwa fimbo tu—wala mkate, wala mkoba, wala pesa za bindoni— 9 lakini wajifungie viatu; akasema, Msivae kanzu mbili. 10 Akawaambia, Mahali po pote mtakapoingia katika nyumba, kaeni humo hata mtakapotoka mahali pale. 11 Na mahali po pote wasipowakaribisha ninyi wala kuwasikia, mtokapo huko, yakung'uteni mavumbi yaliyo chini ya miguu yenu, kuwa ushuhuda kwao. 12 Wakatoka, wakahubiri kwamba watu watubu. 13 Wakatoa pepo wengi, wakapaka mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawapoza.*

30 Na mitume wakakusanyika mbele ya Yesu; wakampa habari za mambo yote waliyoyafanya, na mambo yote waliyoyafundisha. 31 Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula. 32 Wakaenda zao faragha mashuani, mahali pasipokuwa na watu.

mst. 7-13, 30-32— Kumi na wawili wanatumwa na kurudi

Wakati Yesu alipochagua kumi na wawili, alifanya hivyo ili *"wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, tena wawe na amri ya kutoa pepo"* (**Mk 3:14-15**). Sasa anakamilisha sehemu ya pili ya sababu za kuwachagua. Katika **2 Tim 2:2** Paulo anatueleza moja ya kanuni muhimu nyuma ya hili: *"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* Hii ni kanuni kwamba sisi, kama kanisa, tunahitaji kuifuata. Kazi kuu tatu walizofanya ilikuwa ni kutangaza kuwa watu wapate kutubu, kutoa pepo, na kupaka mafuta wale waliokuwa wagonjwa na kuwaponya.[35] Kazi yao ilifuata kielelezo cha huduma ya Yesu. Yeye na wanafunzi

---

[35] Yakobo anajadili tukio hili la mwisho katika **Yak 5:14-15**, *"14 Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. 15 Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, na Bwana atamwinua; hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa."* "Mafuta ya kupakwa" yalionekana kuwa na uwezo wa kuponya nyakati za biblia (angalia **Lk 10:34**), jambo ambalo limepelekea baadhi ya wafafanuzi kuhitimisha kwamba "Yakobo anatoa maombi na dawa" (Burdick 1981: 204). Hata hivyo, walio wengi na labda walio na mtazamo sahihi wanaangalia mafuta ya kupakwa kama ishara ya kutengwa kwa mgonjwa kwa ajili ya hatua maalumu na uangalizi wa kiungu (angalia Moo 1985: 179; Moo 1989: 1162). Hili linaoneshwa na maelezo kwamba mafuta yatumike *"yatumike katika jina la Bwana"* (**mst. 14**), na mafuta ya kupakwa ni alama ya matendo au uwepo wa Roho Mtakatifu (angalia **1 Sam 16:13; Zab 89:20; Lk 4:18; Mdo 10:38**). "Si mafuta wala mzee anayeponya, bali ni Bwana mwenyewe, kwa kuwa kupakwa huku kunafanyika katika jina lake. Baadhi ya wengine Afrika wanaamini ni mafuta yenye uwezo wa kimiujiza wa kuponya. Wengine wanafikiri kwamba uponyaji unategemea ubora wa mafuta yanayotumika. Watu kama hao yawalazimu kuacha kuyachukulia mafuta kama kitu kilichowekwa wakfu au chenye nguvu maalumu na lazima kiambatanishwe na ahadi za Mungu. Ndiyo maana mwandishi wa waraka huu anashauri maombi (5:15). Ni maombi ya imani badala ya kurudiwa rudiwa kwa kanununi fulani kunakoleta uponyaji wa kimiujiza." (Andria 2006: 1516)

Wakatik **mst. 15** unasema *"maombi ya imani yatamuokoa mgonjwa,"* siyo maombi peke yake yaliyo na nguvu maalumu ya kuponya kama ilivyo kwa mafuta ya kupakwa—ni Mungu ndiye aponyaye. "Maombi ya kweli ya imani, basi, mara zote yanahusisha kutambua kwamba Mungu ndiye mwenye sauti ya mwisho katika kila jambo; Kwamba ni mapenzi ya Mungu ambayo ndiyo yanayopaswa kutendeka. Na ni wazi kwamba kwa vyovyote mara zote ni mapenzi ya Mungu kuwaponya walio na madhaifu (linganisha na 2 Kor. 12:7-9). Kwahiyo, 'imani' ambayo ni kiungo muhimu cha maombi yetu kwa ajili ya uponyaji ili yajibiwe—imani hii ikiwa ni zawadi ya Mungu—inaweza kudhihirika hasa pale tu inapokuwa ni mapenzi ya Mungu kuponya. . . . Katika maisha haya, mara nyingi hatutajua kama ni mapenzi ya Mungu kuponya; mara

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

hawakutenganisha kutangaza mambo ya "kiroho" na mahitaji ya "kimwili" ya watu. Hakika, kuwapatia watu mahitaji yao ya kimwili mara nyingi huwafungua waweze kuipokea injili. Hii ni kanuni pia kwamba kanisa linahitaji kujua na kuonyesha kwa matendo (muingiliano kati ya yale ya "kiroho" na yale ya "kimwili" yanayojadiliwa katika sehemu ya uanafunzi na umisheni katika Menn 2017b).

Yesu kamwe hakuwahi kutuma wanafunzi wake mmoja mmoja, bali mara zote katika makundi ya wawili wawili, labda ni katuka kufuata matakwa ya AK kwamba jambo huthibitishwa kwa *"mashahidi wawili au watatu"* (**Hes 35:30; Kumb 17:6; 19:15**). Kwa hakika kuna sababu za kivitendo kwa hili: wawili wanaweza kutiana moyo, wanaweza kusaidiana, kulindana, n.k. Hawakuhitajika kubeba chochote, bali kumtegemea Mungu kwa mahitaji yao ambayo wangelipokea mahubiri yao miongoni mwa wale waliokuwepo katika vijiji ambamo walikwenda kuhubiri. R. Alan Cole anatuonesha jambo, "Umasikini haujawahi kuwa kielelezo katika biblia, ingawa ikiwa ni lazima yapasa kupokelewa kwa furaha katika utumishi wa Mungu na kwa ajili ya Kristo." (Cole 1989: 170). Baada ya pasaka ya mwisho, Yesu alionesha kuwa wanafunzi walikuwa wameweza kujifunza kumtegemea Mungu kwa mahitaji yao: *"'Je! Hapo nilipowatuma hamna mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlipungukiwa na kitu?' Wakasema,'la'."* (**Lk 22:35**) Ndipo wakati huo akasema kwamba, kwasababu wamejifunza kumtegemea Mungu wangeweza sasa kurudisha mifuko yao ya fedha, mikoba, na upanga watakapotoka tena (**Lk 22:36**). Ni tofauti kiasi gani ukilinganisha na "wainjilisti", wanaosafiri katika ndege zao binafsi, na kuvaa mavazi ya kifahari, na kukaa katika hoteli za gharama kubwa, na kuwa matajiri kutokana na mamilioni ya fedha wanazochukua kutoka kwa watu wasio na uwezo.[36] **Mistari 11** (*"kukung'uta mavumbi kutoka katika miguu yao"*) kunaonesha kuwa kukataliwa kwa injili kuna matokeo mabaya. Paulo na Barnaba walidumisha utaratibu huu (angalia **Mdo 13:51; 18:6**). Injili inaleta wokovu kwa wale wanaoikubali lakini ni hukumu kwa wale wanaoikataa. Kukung'uta mavumbi kutoka miguuni mwao ilikuwa ishara kwamba wale wanaokataa wamejiingiza katika hukumu ya Mungu.

Mistari 30-32 inatuambia kwamba mitume waliporudi, walitoa hesabu ya yale yaliyotokea katika safari yao ya kimisheni. Mahojiano, kujipunguzia mzigo, na uwajibikaji katika huduma ni muhimu, na Yesu na mitume walidhihirisha mambo haya. Zaidi ya hapo, kupumzika, kujifurahisha, na kujiburudisha ni muhimu kwa ajili ya akili na afya ya mwili.Tunapokuwa tumechoka na kimwili kuishiwa nguvu akili zetu haziwi katika utimilifu wake. Zaidi ya hayo, kama tunatumia muda wetu wote katika ajira zetu, maisha yetu hupatwa na hali isiyo na uwiano na mahusiano yetu na familia zetu marafiki hudhoofika. Kudumisha mahusiano imara na watu

---

zote hatutaweza kuhisi kama hiyo 'imani' imepata kile ilichoomba kwa kuwa ni ya wakati uliopo. Wakati maombi yetu yanapokuwa hayajajibiwa, basi inakuwa siyo kwasababu ya imani yetu ina kasoro; muktadha ambapo imani kama hiyo ingeweza kuwepo haukuwepo." (Moo 1985: 182, 186-87)

[36] Kanisa la kwanza walikutana na tatizo kama hilo kwa "manabii" wa uongo na "mitume" wa uongo ambao walifanya hayo kwa ajili ya kupata pesa. Mwongozo wa kanisa la kwanza, *The Didache* (c. 70-110), unakazia umuhimu wa kutathimini msukumo wa mtu na maisha anayoishi ili kuppambanua kama ni nabii au mtume wa uongo. Inasema: "Sasa kuhuisiana na mitume na manabii, ushughulike nao kama ifuatavyo kulingana na kanuni za injili. Kila mtume anayekuja kwako akaribishwe kwa heshima kana kwamba ni Bwana. Lakini asikae zaidi ya siku moja, isipokuwa kuna haja, ambapo anaweza kukaa siku nyingine. Lakini ikiwa atakaa siku tatu, ni nabii wa uongo. Na mtume anapoondoka, asichukue kitu chochote isipokuwa mkate hadi hapo atakapofika katika sehemu yake ya kulala. Lakini kama ataomba pesa, atakuwa nabii wa uongo.

Pia, usimpime au kumtathimini nabii yeyote ambaye ananena katika Roho, kwa kuwa kila dhambi itasamehewa, lakini dhambi hii haitasamehewa. Hata hivyo, siyo kila mtu anayenena kwa Roho ni nabii, isipokuwa anaenenda katika njia za Bwana. Kwa njia hii basi, nabii wa uongo na nabii wa kweli watabainika. Zaidi ya hayo, nabii anayeagiza chakula katika Roho hatakula chakula hicho; kama akila, ni nabii wa uongo. Kama nabii yeyote atafundisha ukweli, na asitende anachofundisha, ni nabii wa uongo. Lakini nabii aliyethibitishwa kuwa wa kweli ambaye afanya jambo linaloashiria hali ya kidunia ya maana ya kanisa (ili mradi hamfundishi mtu kufanya yote anayofanya) hutamhukumu, kwakuwa hukumu yake anayo Mungu. Zaidi ya hayo hata manabii wa zamani walitenda hivyo pia. Lakini yeyote akisema katika roho, 'nipe pesa,' au kitu kingine, usimsikilize. Lakini akikuambia utoe kwa ajili ya mtu mwingine mwenye uhitaji, mtu yeyote asimhukumu." (*Didache* 1989: 11.3-.12)

Maandiko ya zamani ya Kikristo *The Shepherd of Hermas* (c. 95-154) kadhalika yanakazia tabia ya mtu na mwenendo wake katika kumtathimini kama ni nabii wa uongo: "Huamua mtu yupi ana Roho wa kiungu katika maisha yake. jambo muhimu yule aliye na Roho wa kiungu kutoka juu na mpole na mtulivu na mnyenyekevu, na anajiona mwenyewe kuwa maskini kuliko wengine, na hatoi jibu kwa yeyote akiulizwa. Wala haongei kutoka katika nafsi yake mwenyewe (wala Roho Mtakatifu haongei wakati mtu anataka kuongea), lakini huongea wakati Mungu anapotaka aongee. . . . Sasa sikia, alisema, kwa habari ya roho ya kidunia isiyo na faida, isiyo na nguvu bali upumbavu. Mtu anapodhania ana roho na hujiinua na kutaka kuketishwa mahali pa heshima, mara anakuwa mkorofi na asiye na aibu na mwongeaji na anayejua mambo mengi ya anasa na starehe, na hupokea pesa kwa kutoa unabii, na kama asipopewa pesa hatoi unabii. Sasa, roho ya kiungu inaweza kupokea pesa na bado ikatabiri? Haiwezekani kwa nabii wa Mungu kufanya hivyo, lakini roho ya mtu atendaye hayo ni ya kidunia." (*Shepherd of Hermas* 43.7-.8, .11-.12)

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

walio karibu nasi, na kupata muda wa “kuchaji betrii zetu” na kupangilia upya vipaumbele vyetu, ni muhimu ikiwa tunataka kubakia macho, wenye akili na maisha yanayokwenda vema.Yesu alitambua umuhimu wa kupumzika kimwili na kurejesha nguvu upya. Watu wengi katika huduma leo hawaonekani kulitambua hili kama Yesu alivyotambua. Kwa kutokuwa na muda wa kula kwa namna inayofaa na pumziko la kutosha, afya ya miili yetu, mahusiano yetu, na huduma zetu vitadhoofika. Huo siyo uwakili mzuri, na siyo kumheshimu Mungu. Inatupasa kujifunza masomo yanayooneshwa na Yesu na wanafunzi wake.

MASWALI YA KUJADILI

1. Ni *mamlaka* gani ambayo Yesu aliwapa wanafunzi wake? Ni *mahitaji* gani ya *kidunia* waliyotakiwa kubeba?

- Unafikiri kuna uhusiano kati ya hayo mawili?

- Lipi, kama lipo, tunalojifunza kutokana na haya?

2. Wakati Yesu alipotuma mitume wake, hakuna aliyewaona ambaye angeshawishika kuvutiwa na Kristo kwa mali zao au matarajio ya kutajirika. Kwanini unafikiri “wainjilisti” wengi wa kisasa hufanya kinyume chake (wakionesha utajiri wao)?

- Kiroho hali hiyo ina maana gani?

- Kwanini watu wanawasikiliza watu kama hao, wanawafuata, na kuwapa pesa?

- Nini kifanyike dhidi ya hali hii?

3. Umuhimu wa mahojiano na kutoa hesabu ni nini?

- Kwa namna gani, kama ipo, tunachukua hatua hizi dhidi ya wainjilisti na viongozi wa kanisa wa kisasa?

4. Kula kuna umuhimu gani na kupata pumziko sahihi na kurejesha mwili katika hali yake?

- Huwa unakula ifaavyo na kupumzika inavyostahili na kurejesha mwili katika hali yake? Kama sivyo, utalifanyiaje kazi hili?

6:14-29: ***14 Naye Mfalme Herode akasikia habari; kwa maana jina lake lilikuwa kutangaa, akasema, Yohana Mbatizaji amefufuka katika wafu, na kwa hiyo nguvu hizi zinatenda kazi ndani yake. 15 Wengine walisema, Ni Eliya. Wengine walisema, Huyu ni nabii, au ni kama mmoja wa manabii. 16 Lakini Herode aliposikia, alisema, Yohana, niliyemkata kichwa, amefufuka. 17 Kwa maana Herode mwenyewe alikuwa ametuma watu, akamkamata Yohana, akamfunga gerezani, kwa ajili ya Herodia, mkewe Filipo ndugu yake, kwa kuwa amemwoa; 18 kwa sababu Yohana alimwambia Herode, Si halali kwako kuwa na mke wa nduguyo. 19 Naye yule Herodia akawa akimvizia, akataka kumwua, asipate. 20 Maana Herode alimwogopa Yohana; akimjua kuwa ni mtu wa haki, mtakatifu, akamlinda; na alipokwisha kumsikiliza alifadhaika sana; naye alikuwa akimsikiliza kwa furaha.***

21 Hata ilipotokea siku ya kufaa, na Herode, sikukuu ya kuzaliwa kwake, alipowafanyia karamu wakubwa wake, na majemadari, na watu wenye cheo wa Galilaya; 22 ndipo binti yake yule Herodia alipoingia, akacheza, akampendeza Herode na wale walioketi pamoja naye karamuni. Mfalme akamwambia yule kijana, Niombe lo lote utakalo, nitakupa. 23 Akamwapia, Lo lote utakaloniomba nitakupa, hata nusu ya ufalme wangu. 24 Basi akatoka, akamwuliza mamaye, Niombe nini? Naye akasema, Kichwa cha Yohana Mbatizaji. 25 Mara akaingia kwa haraka mbele ya mfalme, akaomba akisema, Nataka unipe sasa hivi katika kombe kichwa cha Yohana Mbatizaji. 26 Mfalme akafanya huzuni sana, lakini kwa ajili ya viapo vyake, na kwa ajili ya hao walioketi karamuni, hakutaka kumkatalia. 27 Mara mfalme akatuma askari, akaamuru kuleta kichwa chake. Basi akaenda, akamkata kichwa mle gerezani, 28 akakileta kichwa chake katika kombe, akampa yule kijana, naye yule kijana akampa mamaye. 29 Wanafunzi wake waliposikia habari, walikwenda, wakauchukua mwili wake, wakauzika kaburini.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mst. 14-29—Hatma ya Yohana Mbatizaji

"Mfalme Herode" ikimaanisha Herode Antipa ambaye alikuwa liwali wa Galilaya na Perea (nchi iliyoko mashariki mwa Yordani) kuanzia mwaka wa 4 KK hadi 39 BK. Kaka zake Herode walikuwa maliwali katika maeneo mengine ya Palestina. Tunahitaji kumtofautisha Herode huyu na baba yake, Herode Mkuu ambaye alikuwa mfalme wa Palestina yote kuanzia miaka ya 40-4 KK. Ni Herode Mkuu ambaye alipanua Hekalu na kuagiza kuuwawa watoto wadogo kule Bethlehemu (angalia **Mat 2:1-23**).

Mwanzo wa **mst. 14** huenda unahusu miujiza ya Yesu ambayo Herode alikuwa ameisikia, kwa kuwa katika **mst. 14b-16** inakazia utambulisho wa Yesu na nguvu zake za kimiujiza. Wazo kwamba Yesu alikuwa Yohana aliyerudi tena katika mwili mwingine, au Eliya amefufuka, au mmoja wa manabii ni wazi lilikuwa limeenea, kwa kuwa wanafunzi wanataja mitazamo hiyo mitatu wakati Yesu alipouliza,*"Watu hunena mimi ni nani?"* (**Mk 8:27-28**)

Ingawa tumezungumzia kurudi kwa wanafunzi kutoka katika safari yao ya kimisheni (**mst. 30-32**) hapo juu, inatupasa kuona kuwa Marko hasa anatuandikia haya kuhusu kifo cha Yohana Mbatizaji *kati ya* Yesu kutuma wanafunzi wake na kurudi kwao. Hili linaweza likaonesha gharama za uanafunzi. Wazo hilo linahusishwa na mambo kadhaa yanayofanana kati ya vifo vya Yohana Mbatizaji na Yesu. Wote waliuwawa na watawala. Maherode na makuhani wakuu walipanga njama kutekeleza hilo lakini awali likashindikana hadi "fursa" ilipojitokeza (**Mk 6:21; 14:11**). Herode na makuhani wakuu wote waliahidi kutoa zawadi (kwa binti Herodia na Yuda) ambao ndio waliofanikisha mauaji (**Mk 6:23; 14:11**) Herode na Pilato hawakutaka kuwaua wafungwa wao lakini walilazimika kutokana na shinikizo la wengine (**Mk 6:26; 15:15**). Yohana alikufa kama nabii; Yesu alikufa kama nabii (**Kumb 18:15-19**). Wote Yohana na Yesu walizikwa na wanafunzi wao (**Mk 6:29; 15:45-46**).

Mambo mengine ya kina yanayozunguka kufungwa kwa Yohana Mbatizaji na kifo chake (**mst. 17-29**) yanatupatia masomo fulani ya kivitendo. Kwanza, namna kifo cha Yohana Mbatizaji kilivyotokea inatuonesha umuhimu wa Yesu kutofautisha familia ya kidunia na famila yake ya kweli, ya kiroho (**Mk 3:31-35**). "Ilikuwa ni kutokana na kupagawishwa kimapenzi na Herodia kulikompelekea Herode amweke Yohana Mbatizaji gerezani: na hivyo hata wenza hutupotosha. . . . Hata utii wa binti kwa mama yake katika hili umegeuka na kuwa dhambi: na hivyo, nje ya Kristo, hata sifa za "asili' zinaweza kupotoshwa na kuwa uovu." (Cole 1989: 174)

Pili, Yohana alikuwa na maadili ya kiwango cha kuweza kumpa ujasiri wa kuikana hadharani ndoa ya Herode kwa Herodia. Ndoa kama hiyo haikuwa halali (**Law 18:16; 20:21**). Kusema kweli kinyume cha wale walioko madarakani kunaweza kutuletea matokeo mabaya, kama Yohana na Wakristo waaminifu katika vizazi vyote walivyokutana na mambo kama hayo (angalia **Yh 15:20; Mdo 14:22; 2 Kor 4:7-11; 2 Tim 3:12**). Kusema ukweli, licha ya hatari kwa usalama na maisha yetu, ni moja ya mtihani wa uaminifu wetu kwa Kristo. Tunahitaji kukumbuka utii wetu wa msingi ni kwa nani na mtawala mkuu ni nani: ni Kristo, siyo watawala wetu wa kidunia. **Zab 2:2-4** inatukumbusha, *"[2] Wafalme wa dunia wanajipanga, Na wakuu wanafanya shauri pamoja, Juu ya Bwana, Na juu ya masihi wake. [3] Na tuvipasue vifungo vyao, Na kuzitupia mbali nasi kamba zao. [4] Yeye aketiye mbinguni anacheka, Bwana anawafanyia dhihaka."* Jenny Cox anahitimisha hivi, "Mifano hii ya kibiblia imetolewa kwetu kututia moyo kuishi maisha ya utauwa katika kutii wito tulioitiwa na Baba. Maisha haya ya utauwa yanahusisha wito wa kinabii wa kutangaza toba kutoka dhambini, na utayari wa kuteseka kutokana na kutangaza huko. Tofauti na wasioamini ambao hawana nguvu majaribu yanapowajia, Wakristo wanaume kwa wanawake wamepewa mafuta ya Roho Mtakatifu ili waweze kusimama siku ya uovu ikifika. Tutahitaji nguvu ya Roho Mtakatifuili tuweze kutembea katika njia hii. Hebu, basi, tuombe nguvu hiyo ya kutuwezesha kutembea katika utii bila kujali gharama binafsi." (Cox 2013: n.p.)

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwanini unafikiri kwamba Yohana Mbatizaji alijiletea matatizo kwa kuingilia maisha binafsi ya Herode?

2. Katika kifungu hiki Herode anaonekana kuonesha kutawaliwa na mihemko na ushawishi (unaopingana wakati mwingine). Ni ipi hiyo?

- Kwa namna gani, kama basi ipo, kutambua mihemko na ushawishi wa watu vinaweza kutusaidia kuwashuhudia?

3. Kifungu hiki kinatuambia nini kuhusu gharama ya uanafunzi iliyoko?

6:33-44: ***[33] Watu wakawaona wakienda zao, na wengi wakatambua, wakaenda huko mbio kwa miguu, toka miji yote, wakatangulia kufika. [34] Naye aliposhuka mashuani, akaona mkutano mkuu, akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji; akaanza kuwafundisha mambo mengi. [35] Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi wake walimwendea, wakasema, Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; [36] uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula. [37] Akajibu, akawaambia, Wapeni ninyi chakula. Wakamwambia, Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula? [38] Akawaambia, Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame. Walipokwisha kujua wakasema, Mitano, na samaki wawili. [39] Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. 40 Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. [41] Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. [42] Wakala wote wakashiba. [43] Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. [44] Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.***

mst. 33-44—Yesu awalisha 5000

Kulishwa kwa watu 5000 ndio muujiza pekee unaosimuliwa katika injili zote nne (angalia pia **Mat 14:13-21; Lk 9:12-17; Yh 6:1-14**). Tukio hili linafunua mengi kuhusu tabia ya Yesu. Mpango wake yeye na wanafunzi wake ulikuwa kuwaacha makutano ili aweze kupumzika baada ya ziara yao ya kimesheni (**mis. 30-32**). Hata hivyo, sasa, anaona kuwa mkutano mkubwa umewakuta walikokuwepo, hivyo anaacha mpango wake wa awali kwasababu *"aliwahurumia, kwasababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji. Akaanza kuwafundisha mambo mengi."* (**mst. 34**) Huruma za Yesu hazikuwa tu hisia za juu juu lakini hisia hai na zinazosukuma kutenda jambo. Tena, tunaona kuwa Yesu siyo tu kwamba anajali hali ya kiroho ya watu (aliwafundisha mambo mengi) lakini pia hata mahitaji yao ya kimwili (aliwalisha). Na linganisha chakula cha Yesu na kile cha Herode (**mst. 21**). Chakula cha Yesu ni cha kawaida, kinatosheleza, kina nguvu, na kina uhai; Karamu ya Herode ilikuwa ya kifahari iliyoleta mauti. Kwa kuwa Yesu aliweza kulisha wanaume 5000 kwa mikate mitano na samaki, mara zote anaweza kujali mahitaji yetu ya kimwili. Kama Yesu alivyosema, *"Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe"* (**Yh 6:35**). Tambua kwamba Yesu alikuwa wakili mwema: hakuruhusu mabaki ya chakula yapotee. Inaweza kufikirika, vikapu kumi na viwili vilivyojaa mabaki vingetumika kama chakula cha wanafunzi baada ya mkutano kutawanyika na waliweza kupata muda wao wa kupumzika na kupata nguvu tena baada ya kuchoshwa na kazi. Vikapu kumi na viwili vilivyojaa vipande pia inaelezea kile ambacho Paulo alisema katika **Ef 3:20-21**: *"Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya milele na milele. Amina."*

Sehemu nyingine muhimu ya Yesu inafunuliwa katika ukweli kwamba alitambua kwamba watu *"walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji."* Maneno hayo yanaonekana kwa mara ya kwanza katika **Hes 27:15-18** Mungu alipomwambia Musa kumteua Yoshua kama mrithi wake: *"[15]Musa akanena na Bwana, akisema, [16] Bwana, Mungu wa roho za wenye mwili wote, na aweke mtu juu ya mkutano, [17] atakayetoka mbele yao, na kuingia mbele yao; atakayewaongoza watokapo, na kuwaleta ndani; ili mkutano wa Bwana wasiwe kama kondoo wasio na mchungaji. [18] Bwana akamwambia Musa, Mtwae Yoshua, mwana wa Nuni, mtu mwenye roho ndani yake, ukamwekee mkono wako."* Yoshua ni "mfano" wa Kristo. Kwa kiebrania, "Yoshua" ni "Yehoshua" au "Yeshua"; jina hili kwa kingereza ni "Jesus." Zaidi ya hapo, **Ebr 4:4, 8** inatumia jina hilo la Kigiriki, *Iēsous,* kwa Joshua na Yesu. Muhimu zaidi, Yoshua aliwaongoza watu kuingia katika ushindi dhidi ya maadui zao na kuingia katika nchi ya ahadi. Hata hivyo, kutimizwa kwa kinachowakilishwa na mfano ni muhimu kuliko mfano wenyewe. Ijapo Yoshua aliwashinda maadui zake na kuwaingiza Israeli nchi ya ahadi, **Ebr 4:8** inatuambia hakuweza kuwapa watu wake "raha" kamili. Pale msalabani, Yesu alimshinda mkuu wa maadui wote—dhambi, mauti na Shetani—na kuwaingiza watu wake katika nchi ya wokovu na uzima wa milele, yaani, "raha" yetu ya kweli; atakapokuja tena, Pamoja na ujio wake ataleta nchi ya ahadi kamili ya mbingu mpya na nchi mpya.

Mada ya "kondoo wasio na mchungaji" inatokea tena katika **1 Fal 22**. Mfalme Ahabu alitaka kufanya vita, lakini nabii Mikaya alisema, *"Naliwaona Waisraeli wote wametawanyika milimani, kama kondoo wasio na mchungaji. Bwana akasema, 'Hawa hawana bwana; na warudi kila mtu nyumbani kwake kwa amani.'"* (**1 Fal 22:17**) Maneno haya yana maana ya watu au, kwa habari ya maelezo ya baadae, taifa zima lisilo mcha Mungu, lisilo na uongozi wa kiroho. Mada hii inafikia kilele chake katika AK katika **Ezek 34** ambapo Mungu anawakataa viongozi wa Israeli: *"Mwanadamu, toa unabii juu ya wachungaji wa Israeli, toa unabii, uwaambie, naam, hao wachungaji, Bwana MUNGU asema hivi; Ole wao wachungaji wa Israeli, wanaojilisha wenyewe;*

je! Haiwapasi wachungaji kuwalisha kondoo? [3] Mnawala walionona, mnajivika manyoya, mnawachinja walionona; lakini hamwalishi kondoo. [4] Wagonjwa hamkuwatia nguvu, wala hamkuwaponya wenye maradhi, wala hamkuwafunga waliovunjika, wala hamkuwarudisha waliofukuzwa, wala hamkuwatafuta waliopotea; bali kwa nguvu na kwa ukali mmewatawala. [5] Nao wakatawanyika, kwa sababu hapakuwa na mchungaji; wakawa chakula cha wanyama- mwitu, wakatawanyika." (**Ezek 34:2-5**) Matokeo yake, Mungu anaahidi, *"Nami nitaweka mchungaji mmoja juu yao, naye atawalisha, naam, mtumishi wangu, Daudi; yeye atawalisha, naye atakuwa mchungaji wao. Na mimi, Bwana, nitakuwa Mungu wao, na mtumishi wangu, Daudi, atakuwa mkuu kati yao; mimi, Bwana, nimesema haya."* (**Ezek 34:23-24**) Unabii huu unatimizwa katika Yesu ambaye alisema, *"Mimi ni mchungaji mwema"* (**Yh 10:11, 14**; ona kwamba **Mat 26:31; Mk 14:27**). Anaitwa *"mchungaji mkuu"* katika **Ebr 13:20** na *"mchungaji kiongozi"* katika **1 Pet 5:4**. *Kutimizwa kwa Yesu kama mchungaji wetu kutadumu milele katika mbingu mpya nan chi mpya, "Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao."* (**Uf. 7:17**)

Haya yote yanadokezwa katika habari za Yesu na wale 5000. Inapaswa itusababishe tulitathimini kanisa na uongozi wake. Hao wanoitwa "watu wakubwa-wa Mungu" wenye sura na matendo kama wachungaji wa uongo wa **Ezek 34** kuliko"mchungaji mwema." Kama hali hii ikiendelea kuruhusiwa, itapelekea kundi kuwa dhaifu na kutawanyika na italeta hukumu ya Mungu kwa watu wake wasio waaminifu.

MASWALI YA KUJADILI

1. Mwitikio wa ndani wa Yesu ulikuwaje kwa wanafunzi wake na kwa mkutano?
   - Mwitikio wa wanafunzi ulikuwaje kwa mkutano?
   - Hili linatuambia nini?

2. Huu ni muujiza pekee wa Yesu unaoandikwa na injili zote. Unafikiri hiyo inatuambia nini?
   - Ni funzo gani tunapata kutokana na muujiza huu?

3. "Alihubiri injili ya kawaida tu?"
   - Jukumu la kuangalia mahitaji ya kimwili ni nini katika ukristo?

4. Muujiza huu, hasa maelezo yanayofuata yaliyotolewa na Yesu katika **Yh 6:26-71**, unaanza kuonesha kile ambacho marehemu Richard Wurmbrand alikiita tofauti kati ya "kuwa mteja wa Yesu" na kuwa "mwanafunzi wa Yesu." Tofauti ni nini na kwanini ni muhimu?

5. Linganisha na kupambanisha chakula cha Yesu katika kifungu hiki na karamu ya Herode katika kifungu kifuatacho.

6:45-56: ***[45] Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande mashuani, watangulie kwenda ng'ambo hata Bethsaida, wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkutano. 46 Hata alipokwisha kuagana nao akaenda zake mlimani kuomba. 47 Na kulipokuwa jioni mashua ilikuwa katikati ya bahari, na yeye yu peke yake katika nchi kavu. [48] Akawaona wakitaabika kwa kuvuta makasia, kwa maana upepo ulikuwa wa mbisho; hata ilipopata kama zamu ya nne ya usiku akawaendea, akitembea juu ya bahari; akataka kuwapita. [49] Nao walipomwona anatembea juu ya bahari, walidhani ya kuwa ni kivuli, wakapiga yowe, [50] kwa kuwa wote walimwona, wakafadhaika. Mara akasema nao, akawaambia, Changamkeni; ni mimi, msiogope.***
[51] Akapanda mle chomboni walimo; upepo ukakoma; wakashangaa sana mioyoni mwao; [52] kwa maana hawakufahamu habari za ile mikate, lakini mioyo yao ilikuwa mizito.
[53] Hata walipokwisha kuvuka, walifika nchi ya Genesareti, wakatia nanga. [54] Nao wakiisha kutoka mashuani, mara watu walimtambua, [55] wakaenda mbio, wakizunguka nchi ile yote, wakaanza kuwachukua vitandani walio hawawezi, kwenda kila mahali waliposikia kwamba yupo. [56] Na kila alikokwenda, akiingia vijijini, au mijini, au mashambani, wakawaweka wagonjwa sokoni, wakamsihi waguse ngaa pindo la vazi lake; nao wote waliomgusa wakapona.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mst. 45-56—Yesu anatembea juu ya maji na kuponya kule Genezareti

Katika injili yake yote, Marko amekuwa akimfunua Yesu ni nani. Matukio yanayojitokeza katika sehemu hii yanaonesha sehenu zaidi na za kina za utambulisho wa Yesu na kutupatia majibu ya kina kwa swali katika **Mk 4:41**, *"Huyu ni nani, basi?"*

1. **mst. 45-52—**Yesu anatembea juu ya maji

Tukio hili linaanza na Yesu kuruhusu mkutano kutawanyika na kuwaagiza wanafunzi wake kuingia katika mashua wakati yeye anakwenda mlimani peke yake kuomba. **Lk 5:16** inasema kwamba mara nyingi Yesu alijitenga ili apate kuomba akiwa peke yake mahali pa faragha. Marko anaandika matukio matatu kama hayo: hili hapa, baada ya hamasa ya awali kule Kapernaumu (**Mk 1:35**), na baada ya chakula cha jioni cha mwisho (**Mk 14:26-42**). Alifunga kwa siku arubaini, na bila shaka alitumia muda huo katika maombi, kabla hajaanza huduma yake kwa uwazi. (**Mat 4:1-2; Lk 4:1-2**). Tunapaswa kuona mlinganisho baina ya maisha ya maombi ya Yesu na yale ya walio wengi wetu. Kama yeye, akiwa Mungu kabisa na mtu kabisa, aliomba mara kwa mara hivyo, kwanini sisi hatufanyi hivyo? Matukio yote ya maombi yake ya faragha yalifuatwa au kutanguliwa na tukio muhimu sana. Maisha yake yote yalikuwa ya muhimu mkubwa. Kwa hiyo mtu anaweza kuhitimisha kwamba maisha yake ya kina ya maombi na kuwa na maisha yaliyokuwa muhimu vilikuwa na mahusiano. Labda wepesi wa maisha wa baadhi yetu vina uhusiano na wepesi wa maisha ya maombi.

Mistari 47-48 inaonesha mlinganisho kati ya Yesu na wanafunzi ambao wako peke yao. Zamu ya nne ya usiku inaweza kuwa kati ya saa 9:00 usiku-6:00 asubuhi, jambo ambalo lina maanisha kuwa wamekuwa wakishindana na upepo bila kupungua, wakitaabika usiku kucha, bila kuonekana kama wanafika mbali. Ukweli kwamba wanafunzi wamekuwa wakishindana na upepo na bahari usiku kucha wakati Yesu hakuwa kwenye mashua pamoja nao, na kwamba upepo ulikoma mara alipoingia katika mashua, Haimaanishi kuwa Yesu kama akiwa Bwana wa maisha yetu, na kama tuna maisha ya maombi ya mara kwa mara ya kina, basi maisha yetu yatakuwa ni "safari ya salama." Kusema kweli hili ni kama picha ya uanafunzi wa maisha ya Kikristo. Wanafunzi walikuwa katika mashua kwa kutii moja kwa moja agizo la Yesu. "Dhoruba haioneshi kuwa wameacha njia ya mapenzi ya Mungu: badala yake, njia ya Mungu kwao ilipita kwenye dhoruba, kwenda upande mwingine wa ziwa" (Cole 1989: 179). Ingawa inawezekana ilionekana kwao (na kwetu) kwamba Yesu alikuwa amewaacha au amewasahau, sivyo. Yesu alituhakikishia kwamba tutakutana na dhiki na nyakati ngumu (**Yh 15:20**; angalia pia **Mdo 14:22; 2 Kor 4:7-11; 2 Tim 3:12**). Anatumia nyakati ngumu kutuzamisha ndani na kutuumba upya. Kama ilivyokuwa kwa wanafunzi, inachukua zaidi ya tukio moja gumu kwetu ili kutuleta mahali pa kuelewa na kumtumaini. Lakini kwa Yesu, maisha yetu yatakuwa na matukio na yanayostahili; bila yeye, maisha yetu yatakuwa hayana thamani na ni bure.

Maneno ya **mst. 48-52** yanachukua kutoka AK kufunua Yesu hasa ni nani. *"kutembea kwake juu ya maji"* na maneno *"akitaka kuwapita"* (**mst. 48**), pamoja na wanafunzi kushindwa kumtambua kuwa ni yeye lakini wakifikiri wanaona mzimu (**mst. 49**) yamechukuliwa kutoka **Ayb 9:8-11**, yakimzungumzia Mungu, *"Ambaye peke yake ni mwenye kuzitandika mbingu, Na kuyakanyaga mawimbi ya bahari."* (**mst. 8**); *"Tazama, yuaenenda karibu nami, nisimwone; Tena yuapita kwenda mbele, nisimtambue"* (**mst. 11**). Kwa nyongeza, Yesu akiwa amekusudia *"kuwapita"*akawakaribia **Kut 33:22** na **34:6-8** Wakati utukufu wa Mungu *"ulipompita"* Musa, na Mungu akafunua asili yake kwa Musa. Hili linathibitishwa katika **mst. 50** ambapo Yesu anawaambia wanafunzi wake *"ni mimi."* Maneno alisi kwa kigiriki ni, *"Mimi niko,"* ambayo ni maneno aliyotumia Mungu kujitambulisha kwa Musa katika kichaka kilichowaka moto: *"Musa akamwambia Mungu, Tazama, nitakapofika kwa wana wa Israeli, na kuwaambia, Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wakaniuliza, Jina lake n'nani? Niwaambie nini? [14] Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO; akasema, Ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli; MIMI NIKO amenituma kwenu.'"* (**Kut 3:13-14**) "NIKO" ikitafsiriwa inakuwa YHWH (yaani, Yahwe; Yehova). Yesu alikuwa akijitambulisha kama Mungu, na kudhihirisha ukweli huo kwa kufanya jambo ambalo ni Mungu peke yake awezaye kulitenda (kutembea juu ya maji), na kuthibitisha hilo kwa kusababisha upepo kukoma mara alipoingia ndani ya mashua (**mst. 51**). Hilo lilipotokea, walilazimika kukumbuka wakati Yesu alipotuliza dhoruba (**Mk 4:35-41**) Hofu yao iligeuzwa kuwa mshangao, lakini bado hawakuweza kuelewa Yesu alikuwa nani

Kuna mambo ya kujifunza kwetu katika hili. Baadhi ya watu wanafikiri, "Kama tu ningeona muujiza, ningeamini." Siyo kweli. Wanafunzi waliona miujiza mingi, bado mioyoni mwao kulikuwa na ugumu hata wasielewe (**mst. 52**). Tutaelewa tu na kuamini wakati Roho Mtakatifu anapotufanya upya na kutupa imani tusiyoweza kuizalisha wenyewe (angalia **Ef 2:8-9**). Kwa nyongeza, usalama wetu, amani, na imani havina msingi katika katika hali zetu. Hali inaweza kuwa nzuri au mbaya; mara kwa mara hubadilika. Lakini hali zinazobadilika hazina uhusiano na ama na kuwapo kwa Mungu au uwepo wake: *"Yesu kristo ni yeye yule jana na leo na hata milele"* (**Ebr 13:8**). Kwa Wakristo, hatupaswi kuangalia dhoruba na magumu ya maisha na

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

kutishwa lakini tunapaswa kumtazama Yesu katika dhoruba na magumu ya maisha yetu na kutambua kwamba yupo pamoja nasi, anatumia dhoruba na magumu hayo kutusogeza kwake na kutufinyanga katika sura yake, na tunapaswa kusogelea uwepo wake na Roho wake atuwezeshe kuwa na amani ya ndani na usalama licha ya dhoruba na magumu.

2. **mst. 53-56—**Uponyaji wa Yesu kule Genesareti

Kule Bethsaida (**mst. 45**) na Genesareti (**mst. 53**) ilikuwa miji iliyokuwa upande wa kaskazini mwa pwani ya ziwa la Galilaya. Yesu anaweza kuwa alibadilisha anakokwenda baada ya kuingia katika mashua. Kitu kikubwa cha kushika **mis. 53-56** siyo uponyaji mwingi ambao Yesu alitenda lakini imani kwa Yesu ambayo watu wa kawaida walikuwa nayo, ukilinganisha na kutokuamini kwa wanafunzi. *"Nao wakiisha kutoka mashuani, mara watu walimtambua, wakaenda mbio, wakizunguka nchi ile yote, wakaanza kuwachukua vitandani walio hawawezi, kwenda kila mahali waliposikia kwamba yupo."* (**mst. 54-55**), ambapo wanafunzi *"wote walimuona wakaogopa"* (**mst. 50**). Ni moja ya alama za ukweli na uhalali wa Biblia kwamba kutokuamini kwa wanafunzi kumewekwa wazi. Kama matukio haya ya kibiblia yangekuwa ya kutungwa karne kadhaa baadaye wakati kanisa lilipopata kibali, ushawishi, na nguvu, wanafunzi wasingeendelea kuoneshwa kama wadhaifu na wasio na imani lakini wangehaririwa na kuonekana mashujaa wa imani kila mahali. Tunaweza kuiamini Biblia na, muhimu zaidi, tunaweza kumtumaini yule ambaye ndiye mada ya Biblia: Yesu Kristo.

MASWALI YA KUJADILI

1. Angalia jinsi ambavyo Yesu alilazimika kuondoka mwenyewe kumuomba Baba. Hili linatuambia nini kuhusu mahusiano yetu na Mungu?

- Unaweza kusema kwamba ni *dhambi* kutokuwa na maombi? Kwa nini?

- Kama ndivyo, dhambi hiyo ni kubwa kiasi gani? Kwanini hali ya kutokuomba mara chache hufikiriwa (au kuhubiriwa) kama ni *dhambil*?

2. Kwa nini maombi ni muhimu?

- Tiba ya kutokuomba ni nini (chochote isipokuwa "kuomba zaidi")?

3. Kulingana na mfano unaoonekana katika kifungu hiki, *kinyume* cha imani ni nini?

4. Kifungu hiki kinaweza kuonekana kama jibu kwa swali la wanafunzi linalopatikana katika **Mk 4:41**. Kifungu hiki kinajibuje swali hilo?

5. Gundua mlinganisho kati ya **ms. wa. 52** na **mis. ya 53-56**. Mkutano ulielewa nini ambacho Marko anataka tukione?

7:1-23: ***Kisha Mafarisayo, na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu, wakakusanyika mbele yake,***
2 wakaona wengine katika wanafunzi wake wakila vyakula kwa mikono najisi, yaani, isiyonawiwa. 3 Kwa maana Mafarisayo na Wayahudi wote wasiponawa mikono mpaka kiwiko, hawali, wakishika mapokeo ya wazee wao; 4 tena wakitoka sokoni, wasipotawadha, hawali; na yako mambo mengine waliyopokea kuyashika, kama kuosha vikombe, na midumu, na vyombo vya shaba. 5 Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza, Mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee, bali hula chakula kwa mikono najisi? 6 Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo Ila mioyo yao iko mbali nami; 7 Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu, 8 Ninyi mwaiacha amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu.
9 Akawaambia, Vema! Mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu. 10 Maana Musa alisema, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Amtukanaye babaye au mamaye kufa na afe. 11 Bali ninyi husema, Mtu akimwambia babaye au mamaye, Ni Korbani, yaani, wakfu, kitu changu cho chote kikupasacho kufaidiwa nacho, huwa basi; 12 wala hammruhusu baada ya hayo kumtendea neno babaye au mamaye; 13 huku mkilitangua neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana; tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo.
14 Akawaita makutano tena, akawaambia, Nisikieni nyote na kufahamu. 15 Hakuna kitu kilicho nje

ya mtu ambacho kikimwingia chaweza kumtia unajisi, bali vile vimtokavyo, ndivyo vimtiavyo unajisi yule mtu. [16] Mtu akiwa na masikio ya kusikilia, na asikie.] [17] Hata alipoingia nyumbani, ameuacha mkutano, wanafunzi wake wakamwuliza habari za ule mfano. [18] Akawaambia, Hivi hata ninyi hamna akili? Hamfahamu ya kwamba kila kitu kilicho nje ya mtu, kikimwingia, hakiwezi kumtia unajisi; [19] kwa sababu hakimwingii moyoni, ila tumboni tu; kisha chatoka kwenda chooni? Kwa kusema hivi alivitakasa vyakula vyote. [20] Akasema, Kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. [21] Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, [22] wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. [23] Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi.

mst. 1-23—Mapokeo na kinachotia watu unajisi

Kama katika **sura za 2-3**, mwakilishi wa waandishi na Mafarisayo kutoka Yerusalemu alikuja kuchunguza na kumhoji Yesu. Mistari yote, **mst. 1-13** (Mahojiano ya Yesu na waandishi na Mafarisayo) na **mis. 14-23** (Maelezo ya Yesu kuhusu nini hasa kinatia watu unajisi) yameunganishwa na dhana ya "unajisi" na "uchafu." Waandishi na Mafarisayo wanaibua swala katika **mst. 2** na **5**, na Yesu anatoa maelezo kuhusu unajisi katika **mst. 15-23** kwa kutumia namna ya matamshi yaliyotumiwa na Mafarisayo.

1. **mst. 1-13—**Mahojiano ya Yesu na Mafarisayo kuhusu mapokeo

Mistari mitano ya kwanza inahusu desturi ya kunawa mikono. Swala hili siyo la kiusafi bali linafuata sherehesho na mapokeo, yaani, *"mapokeo ya wazee"* (**mst. 5**). Wakati wa Yesu, haya yalikuwa mapokeo ya mdomo yalikuwa yameenea kila mahali. Kwenye miaka ya 200 BK mapokeo haya yaliandikwa katika *Mishnah*. Maswala haya ya desturi na usafi yalikuwa muhimu kiasi kwamba sehemu sita za *Mishnah* zilikuwa zimebeba mambo yahusuyo "usafi" na maswala ya uchafu (angalia Neusner 1988: 893-1137). AK lenyewe lilihitaji kunawa mikono tu kwa makuhani na wazee kuhusiana na utoaji wa dhabihu (**Kut 30:18-21; 40:30-32; Kumb 21:6**) au kama mwisraeli alitokwa na damu (**Law 15:11**). Desturi hizi zimekuwa zikiendelezwa na marabi kama nyongeza ya kile hasa kilichosemwa katika AK; "zilikaa kama uzio kuzunguka sheria." Kwa maneno mengine, kama mtu angefuata mapokeo basi asingeweza kuvunja sheria na hivyo ingekuwa ni kumheshimi Mungu (angalia Wessel 1984: 678; Cole 1989:182-83).

Wakati Marko anaelezea baadhi ya mapokeo haya katika **mis. 3-4**, anataja *"kuosha vikombe, na midumu, na vyombo vya shaba. Na makochi ya sehemu za chakula."* Neno halisi lililotafsiriwa kama "kuosha" ni *baptismos,* au "ubatizo." Katika hili, kwa njia ya mapokeo yao, Mafarisayo walibatiza vitu visivyohitajika lakini wakapinga ubatizo wa Yohana Mbatizaji na wa Yesu ambao huo ulitakasa moyo. Yesu mwenyewe anatumia wazo hili anapowajibu Mafarisayo, kwa kunukuu **Isa 29:13** (angalia pia, kwa mfano., **Amosi 5:21-26; Isa 1:10-15; Yer 7:21-26**). Anasema kwamba uchambuzi wa Isaya kuhusiana na ustawi wa kidini kabla ya uhamisho kwenda Babeli uliendana na ustawi wa kidini wakati wa siku za Yesu, pamoja na kwamba Wayahudi walikuwa wamerudi katika nchi yao wenyewe kwa miaka zaidi ya 500. Kwa maneno mengine, hakuna kilichokuwa kimebadilika. Yesu kuwaita "wanafiki" inamaanisha "mtu muovu aliyejitenga na Mungu kwa matendo yake" (Wilckens 1972: 564). Unafiki wao "ulijaa utata mwingi kati ya kile wanachosema na kile wanachotenda, kati ya muonekano wa ndani na kutokuwa na haki ya ndani.

. . . Kwahiyo, unafiki wao ni dhambi; kushindwa kufanya mapenzi ya Mungu kumefichwa katika muonekano wa matendo ya nje." (Ibid.: 567-68) Yesu anakazia umuhimu wa hili katika **mst. 6-7**, *"Watu wananiheshimu kwa midomo yao, lakini mioyo yao iko mbali nami; nao waniabudu bure."* Leo, kila dhehebu lina mapokeo yake. Huwa "tunabatiza" mapokeo yetu, tukifikiri kuwa yako sahihi na ni ya kitauwa. Tunahitaji kujitathimini hasa. Sote tunamheshimi Kristo kwa midomo yetu, lakini je kumwabudu kwetu kumekuwa "bure"?

Katika **mst. 9-13** Yesu alitoa mifano maalumu ya unafiki wa *"mapokeo ya wazee,"*yaani, desturi iliyojulikana kama Korban. Korban ilikuwa ni kuweka wakfu kitu (mfano pesa) kwa Mungu. Ikishawekwa wakfu hivyo, haikutakiwa itumike kwa makusudi mengine. Ijapo desturi kama hiyo inaonekana ya kiroho (*"utafuteni kwanza ufalme wa mbinguni,"* **Mat 6:33**), Yesu alikuwa akionesha jinsi ilivyo rahisi kuitumia desturi hiyo vibaya ili kumwezesha mtu kukwepa wajibu uliomhusu. Mtu anawajibika kuwaangalia wazazi wake. Lakini wanapohitaji msaada, kama wakiambiwa, "Pesa ambayo ilikuwa niitumie kukusaidia nimeiweka wakfu kwa Mungu," unaweza kuepuka kuwasaidia wazazi wako. Anachosema Yesu ni kwamba kiroho cha kweli kimsingi kinadhihirishwa na namna tunavyowatendea watu. Sababu ni kwamba watu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu, na namna tunavyotendea sura ya Mungu inaonesha tunamfikiriaje Mungu. Hivyo, **1 Yh 4:20** inasema, *"Mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, ni mwongo; kwa maana asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hakumwona."* Kanuni hii inapatikana katika Biblia yote (angalia, kwa mfano, **1 Sam 15:22; Yh 13:34-35; Yak 1:27**).

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

2. **mst. 14-23—**Yesu anasema kwamba unajisi unatoka ndani[37]

Katika mistari hii Yesu anaelezea unajisi unakaa wapi kiuhalisia: siyo nje, bali ndani: siyo kushindwa kutekeleza matambiko fulani ya kidini, lakini hali ya moyo. Jambo lake la msingi ni kwamba *kila mmoja* ni "najisi" na "mchafu," kwasababu sote tumezaliwa na moyo ulioharibika na wenye unajisi, na hatuwezi kuubadilisha sisi wenyewe. Dini zote, yakiwemo madhehebu yote ya Kikristo, yana matambiko na desturi zao. Haya yanaweza kuwa mazuri kama yanamuelekeza mtu kwa Mungu. Hata hivyo, matambiko na desturi huwa yanaonesha dini "kwa nje" Kwa hilo, nina maana kuwa watu huwa wanafikiri (kama Mafarisayo walivyofanya) kwamba "kama ninaenenda kulingana na matambiko na mapokeo ya dini yangu (mfano, nahudhuria ibada kila juma; natoa zaka), na kama ninaepuka mahali fulani ambako ni "najisi" (mfano Baa, miji fulani), basi nitakuwa ninakubalika kwa Mungu. Hili linafanya kuhesabiwa haki kuwe mikononi mwangu na pia ina maana kuwa sihitaji kufanya mabadiliko makubwa sana katika maisha yangu ili kupata kibali cha Mungu. Hata moja katika hayo Yesu hakuwa nayo! Kwa kubaini chanzo cha tatizo letu, Yesu anasema kuwa kila mmoja—Myahudi kwa Mmataifa, Mtoza ushuru na Farisayo—wote wamo ndani ya mashua moja. Suluhu pekee ya tatizo letu ni injili, yaani, siyo lile tunalojitahidi kutenda ili kupata kibali kwa Mungu, lakini ni kile ambacho Mungu kwa njia ya Kristo ametenda kwa ajili yetu (angalia majadiliano katika **Mk 1:1**, hapo juu). Hii ni moja ya sababu kwanini Yesu alisema, *"Amin nawaambia, watoza ushuru na makahaba wanatangulia mbele yenu kuingia katika ufalme wa Mungu"* (**Mat 21:31**). Walitambua hali yao ya dhambi na hawakuwa na matambiko ya nje na mapokeo ya kuwadanganya kuwa walikuwa na haki kama Mafarisayo (angalia pia **Lk 18:9-14** na majadiliano katika **Mk 2:13-17**, hapo nyuma, ya kaka mkubwa katika mfano wa mwana mpotevu).

Kwamba Yesu alikuwa anaingia kwenye kitovu cha dini inaonekana katika maneno ya Marko katika **mst. 19**, *"Kwa kusema hivi alivitakasa vyakula vyote."* Sheria ya vyakula ya Kiyahudi, ikiambatana na kutahiriwa na Sabato, vilikuwa ndio kitovu hasa kilichowafanya Wayahudi kuwa wa kipekee (angalia **Dan 1**). Bado Yesu anaweka pembeni sheria zote za kilawi kuhusu vyakula; na aliitikia kwa namna hiyo hiyo kuhusu Sabato (**Mk 2:23–3:6**), na baadaye kanisa lilifanya kitu kile kile kuhusiana na tohara (angalia **Mdo 15:1-29; Rum 2:25-29; 3:30; 4:9-12; 1 Kor 7:18-19; Gal 5:2-6; 6:15**). Haishangazi basi, kwamba viongozi wa Kiyahudi walimuona Yesu kuwa hatari.

MASWALI YA KUJADILI

1. Katika **mst. 10-13** Yesu anatoa jambo muhimu. Hata hivyo, kanuni iliyoko nyuma ya jambo hilo inafunika zaidi ya ule mfano alioutumia. Elezea kanuni muhimu anayotoa Yesu hapa kwa maneno yako mwenyewe.

- Kuna mifano mingine ya kibiblia unayoweza kufikiria ambayo inaeleza jambo kama hili?

2. Unafikiri watu ni wepesi kubebwa na nini katika kutengeneza matambiko na mapokeo, hasa katika maswala ya kidini?

3. Makanisa mengi ya kiinjili na ya kipentekoste hupenda kujifikiria kuwa siyo ya kudesturi (au aghalabu hayafungwi na desturi). Ni mapokeo gani hasa, tunayo, ikimaanisha namna tunavyoendesha ibada zetu na namna tunavyoenenda katika maisha?

- Ni kwa namna gani mapokeo yetu yanatuingiza katika hatari ya kuwa "mapokeo ya wanadamu" yanayoishia kuweka mipaka kati yetu na Bwana?

4. Yesu anaingia katika kiini cha kile kinachosababisha kunajisika, uchafu, uovu na mashindano ndani na miongoni mwa watu: ni kile kilichoko ndani yetu, kilicho sehemu yetu kwa kurithi, vile tulivyo katika asili ya namna tulivyo—siyo chochote kilichoko nje yetu, kinachotutokea au yale tunayokumbana nayo katika maisha yetu. Hata hivyo, huwa tungali tunaweka mkazo katika mambo ya nje kuliko yale yanayotuakisi kwa "ndani"? Kama ndivyo, kwa namna gani? Na kwanini?

5. Maelekezo ya Yesu kwa watu "yanaanza ndani kuja nje" (yaani, kubadilisha *moyo* kwanza ili kuwa na maisha yaliyobadilika badala ya "kuanza nje kuja ndani" (yaani, kubadilisha tabia ili kubadilisha moyo). Kwanini unafikiri hivi ndiyo sawa?

[37] Ingawa baadhi ya tafsiri za Biblia zina **mst. 16**, *"Mtu yeyote akiwa na masikio, na asikie,"* mstari huo hauko katika maandishi ya zamani zaidi: kwahiyo, haukuingizwa.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

- Kama kweli hii ndiyo njia ya Ukristo, kwanini tunashindana na tabia tunazojua siyo sawa na kutaka mabadiliko?

- Lazima tufanye nini ili kubadilisha hasa tabia kama hizo?

6. Kama uchunguzi wa Yesu kuhusu tatizo la wanadamu ni kwamba linapatikana katika moyo wa mwanadamu, na maelekezo yake ni kwamba kwasababu hiyo ni lazima tupate moyo mpya na kubadilisha maisha yetu "kutokea ndani kuja nje," hili lina maana kwamba Ukristo haupaswi kushughulikia maovu ya kijamii, kisheria, kimazingira, kunyimwa haki, umasikini, magonjwa, n.k., bali unapaswa "kuhubiri injili tu" kama njia ya kushughulika na mambo hayo? Kwanini au Kwanini sivyo?

7:24-37: ***[24] Akaondoka huko, akaenda zake hata mipaka ya Tiro na Sidoni. Akaingia katika nyumba, akataka isijulikane na mtu; lakini hakuweza kusitirika. [25] Ila mara mwanamke, ambaye binti yake yuna pepo mchafu, alisikia habari zake, akaja akamwangukia miguuni pake. [26] Na yule mwanamke ni Myunani, kabila yake ni Msirofoinike. Akamwomba amtoe pepo katika binti yake. [27] Akamwambia, Waache watoto washibe kwanza; maana si vizuri kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia mbwa. [28] Naye akajibu, akamwambia, Naam, Bwana, lakini hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya watoto. [29] Akamwambia, Kwa sababu ya neno hilo, enenda zako, pepo amemtoka binti yako. [30] Akaenda zake nyumbani kwake, akamkuta yule kijana amelazwa kitandani, na yule pepo amekwisha kumtoka.***

[31] Akatoka tena katika mipaka ya Tiro, akapita katikati ya Sidoni, akaenda mpaka bahari ya Galilaya, kati ya mipaka ya Dekapoli. [32] Wakamletea kiziwi, naye ni mwenye utasi, wakamsihi amwekee mikono. [33] Akamtenga na mkutano faraghani, akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate, akamgusa ulimi, [34] akatazama juu mbinguni, akaugua, akamwambia, Efatha, maana yake, Funguka. [35] Mara masikio yake yakafunguka, kifungo cha ulimi wake kikalegea, akasema vizuri. [36] Akawaonya wasimwambie mtu; lakini kadiri ya alivyozidi kuwaagiza, ndivyo walivyozidi kutangaza habari; [37] wakashangaa mno kupita kiasi, wakinena, Ametenda mambo yote vema; viziwi awafanya wasikie, na bubu waseme.

mst. 24-37—Yesu anamponya binti wa mwanamke Msirofoinike na mtu kiziwi

Matukio haya mawili katika sehemu hii na kulishwa kwa watu 4000 katika **8:1-10** kunaigiza jambo alilolifanya Yesu katika **mst. 14-23**, yaani, kama vile hakuna *chakula* kilicho najisi, kadhalika hakuna *watu* najisi (yaani Wamataifa). Au, kuliweka kwa namna nyingine, watu wote ni "wachafu" kwa viwango sawa; Wayahudi hawako karibu na Mungu kuliko Wamataifa, kwakuwa watu wote, Wayahudi kwa Wamataifa, wamefanywa kwa sura ya Mungu, na watu wote wamepotea sawa katika dhambi. Mungu alilileta jambo hili kwa Petro katika **Mdo 10**.

1. **mst. 24-30—**Yesu anamponya binti wa mwanamke Msirofoinike

Tiro na Sidoni ilikuwa miji katika pwani ya bahari ya Mediterania na ilikuwa ni sehemu ya Foinike ya zamani. Lilikuwa ni eneo la Wamataifa. Maelezo ya Mathayo (**Mat 15:21-28**) yanatupatia habari fulani zinazojazia maelezo ya Marko. **Ms. wa 24** unaanza na Yesu na wanafunzi wake kwenda eneo la mbali, wanaingia katika nyumba moja, na wakiwa hawakutaka yeyote ajue walipokuwa. Hili linaashiria kuwa alitaka muda wa utulivu wa kupumzika na kurejesha nguvu ya mwili kama katika **Mk 1:35; 3:7**; **6:31-32**, na labda muda wa kufundisha wanafunzi wake mbali na mkutano. Robert Guelich anasema kuwa *"na aliingia katika nyumba asitake yeyote kujua"* inaonesha kuwa "Alitaka faragha mbali na watu. Hili haliweki pembeni shauku yeyote ya Yesu ya kujihusisha na huduma katika eneo hili." (Guelich 1989: 384) Kama ilivyokuwa katika matukio mengine alipojitenga, hata hivyo, watu walikuwa wameshasikia habari zake, walijua alikokuwa, na *"asingeweza kujificha"* (**mst. 24**).

Inaonekana kulikuwa na mazungumzo zaidi na mwanamke Msirofoinike kuliko yaliyojulikana. Kwanza, kitheolojia, matamko ya Yesu katika **mst. 27**, *"Waache watoto washibe kwanza; maana si vizuri kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia mbwa"* yanaakisi kile alichowahi kusema katika maelezo ya Mathayo kuhusu tukio la kukutana na mwanamke Msirofoinike, "*Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli"* (**Mat 15:24**; angalia pia **Mat 10:5-6**). Pia inaakisi ukweli kwamba, katika mpango wa Mungu, utaratibu wa wokovu ni *"kwa Wayahudi kwanza, na pia kwa Wagiriki"* (**Rum 1:16**; angalia pia **Mdo 1:8; 13:46; Rum 2:10**). Sababu ni kwamba "ni Wayahudi tu ndio wangeliweza kuelewa umuhimu wa Yesu. Hakuna Mrumi, Mhindi, au Mjapani angeliweza kumpokea, kwasababu alikuwa ndani ya historia na katika

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

maandiko ya Israeli peke yao." (Nehls and Eric 2010: 116) Kama Paulo anavyoeleza katika **Rum 9:4-5**, ilikuwa ni Israeli *"ambao ni Waisraeli, wenye kule kufanywa wana, na ule utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada ya Mungu, na ahadi zake; ambao mababu ni wao, na katika hao alitoka Kristo kwa jinsi ya mwili. Ndiye aliye juu ya mambo yote, Mungu, mwenye kuhimidiwa milele. Amina."* Wamataifa *"kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani"* (**Ef 2:12**). Hata hivyo, Mungu alikuwa ameahidi kuubariki ulimwengu wote *kwa njia ya Israeli* (angalia **Mwa 12:3; 22:18**). Kwa maelezo haya, "badala ya kuona mtazamo wa Yesu wa kimasihi kwa maana ya *ama au,* mtu anahitaji kuona misheni yake kama ni *kwa* Israeli *kwa niaba ya* mataifa. Kwa maneno mengine, kwa kurudisha shabaha yake kwa Israeli, Yesu anafanya kazi muhimu kwa dunia yote." (Wax 2013: Christ's Mission *to* Israel *for* the World) hivyo, katika mkutano wake na mwanamke Msamaria kisimani, Yesu anasema, *"wokovu watoka kwa Wayahudi"* (**Yh 4:22**) *siyo* "wokovu ni *kwa ajili ya* Wayahudi."

Pili, licha ya utaratibu wa hapo juu wa kitheolojia kama wokovu, Robert Gundry anavyoeleza kwamba matamko ya Yesu kuhusu watoto kulishwa kwanza kinyume na mbwa ambako kimsingi haikuhusiana na utaratibu wa kuwafikia Wayahudi na Wamataifa kwa ujumla, lakini, Yesu akiwa anataka kuwafundisha wanafunzi wake faraghani, na ndiyo maana *"alikwenda maeneo ya Tiro na Sidoni. Na kuingia katika nyumba asikotaka yeyote ajue."* (**mst. 24**) Gundry anaeleza kuwa mahali pengine pekee katika Marko ambako Yesu hakutaka ajulikane ilikuwa katika **Mrk 9:30-31** kwasababu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake kuhusiana na kifo chake kinachokuja na kufufuka kwake. Mfanano wa matamshi ya **7:24** na **9:30** "unatuambia kwamba Yesu anataka faragha ili aweze kufundisha wanafunzi wake hapa, pia. . . . Lakini ikiwa sababu zilizojificha ni sawa na zile za 9:30-31, kuchukua mkate kutoka kwa watoto wadogo na kuwapa mbwa wadogo kulimaanisha kuwanyima wanafunzi uangalizi unaohitaji kufundishwa na badala yake kuutoa kwa binti wa mwanamke yule na watoto wengine wa Wamataifa walioambatana naye. Ms. wa. 27 haupambanishi taifa lote la Wayahudi na Wamataifa wote, wakati huo, bali Wanafunzi wa Kiyahudi wa Yesu na Mtoto wa Mmataifa." (Gundry 1993: 373) Mtazamo huo unaungwa mkono na ukweli kwamba, katika maelezo ya Mathayo, wakati mwanamke kwa mara ya kwanza alipoomba Yesu amsaidie binti yake, kwanza *"hakumjibu neno. Na wanafunzi wake walimjia na kumsihi, wakisema, Muondoe huyu kwa kuwa anatulilia."* (**Mat 15:23**) Zaidi ya hayo, hadi hili limeelezwa na Marko, uponyaji mwingine wote wa Yesu ulifanyika baina yake na mhusika. Hilo lingemaanisha kuwa angependa kwenda pale alipokuwepo yule binti, badala ya kubakia ndani ya nyumba na wanafunzi wake, jambo ambalo lingekuwa kinyume na nia yake ya kuwa na faragha katika nyumba ile na wanafunzi wake, katika nchi ya mbali kwa mara ya kwanza.

Tatu, Pamoja na hayo, Yesu alimhudumia mwanamke yule. Ingawa matamshi ya Yesu, *"acha watoto wale kwanza, kwa kuwa si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa"* (**mst. 27**), yangeonekana kama kejeli, sivyo—wala mwanamke yule hakuyachukulia hivyo. Neno halisi lenye maana ya "mbwa"ni (*kuōn*) lilikuwa na maana hasi ya jumla. Hata hivyo, Yesu hakutumia neno hilo bali *kunaria, au* "mbwa wadogo," na "maana yake haiendani kimatumizi na mbwa tunaofuga nyumbani"; hakika, mbwa wadogo "wanaruhusiwa katika nyumba na unaweza kuwakuta chini ya meza wakati wa chakula tofauti na mbwa wakubwa au mbwa wazururaji wa mtaani" (Lane 1974: 262).[38] Hivyo, matamshi ya Yesu yalilenga "picha nzuri", ya "hivi vimbwa vidogo vya nyumbani vinavyopendwa na watoto" (Robertson 1930: 326). William Lane kwa usahihi anahitimisha, "Huenda inaonekana kwamba mwanamke, kwa uchache, alielewa matamshi ya Yesu katika tukio hili la kivitendo (siyo kitheoloji)" (Lane 1974: 262).

Kulikuwepo na sababu ya kina, na ya kiutendaji kwanini Yesu atoe matamshi aliyoyatoa, yaani, kufunua imani yake na kuthibitisha kuwa Wamataifa wako katika ngazi moja na Wayahudi. Mwanamke Msirifoinike alidhihirisha imani kwa kumjia Yesu, kumwangukia miguuni mwake, na kumsihi amtoa pepo kwa mwanawe. Maelezo ya Mathayo na Marko yanatupatia picha kamili ya utaratibu wa matukio. Alianza kwa kumuita *"Mwana wa Daudi"* (**Mat 15:22**). "Mwana wa Daudi" lilikuwa ni maneno ya Kiyahudi ya Kimasihi. Kwa maneno mengine, yeye, kama, Mmataifa, alikuwa anamjia Yesu kwa maneno ya Kiyahudi. Kwa vyovyote hili ndilo lililopelekea kutamkiwa maneno, *"Sikutumwa isipokuwa kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli"* (**Mat 15:23**). Katika maelezo ya Mathayo baada ya hayo anarudia ombi lake, siyo kwa misingi ya kiyahudi, lakini kwa msingi wa mahitaji ya wanadamu wote, yaani, *"Bwana nisaidie"* (**Mat 15:25**). Yesu anamjibu kwa kumwambia *"Acha watoto wale kwanza, kwa kuwa si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa"* (**Mk 7:27; Mat 15:26**). Matamshi ya Yesu "yanalenga tukio lililopo. Meza imeandaliwa na familia [wanafunzi wake] wamekusanyika. Haifai kuwasumbua chakulani na kuruhusu mbwa wa kufugwa

[38] Kenneth Wuest anaongeza, "Na lazima atakuwa aliongea kwa Kigiriki na mwanamke huyu, kwasabau asingejua Kiaramaiki cha Wayahudi" (Wuest 1973: 152)

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

achukue mkate wa watoto. Katika ngazi hii ya uelewa fumbo linaeleweka kulingana na picha ya kimaisha inayopatikana sura ya 7:24ff. Ina rejea maalumu kuhusu umuhimu wa kupumzika, ambao ndio uliomfanya Yesu awepo katika eneo lile na mwanamke sasa anavuruga kupumzika." (Lane 1974: 262) Itikio lake la kifumbo lilikuwa linaalika kuitikiwa. "Mwanamke hili alilielewa vema na hakusita licha ya kikwazo kilichokuwepo mbele zake. Hakuhisi kama ni kejeli katika mlinganisho kati ya watoto na mbwa wa kufugwa. Badala yake alikigeuza kwa faida yake: Makombo yaliyoangushwa na watoto, hata hivyo hutumiwa kulishia mbwa! Kulinganisha kwa Yesu hakukataliwi lakini kunaendelezwa katika hatua nyingine zaidi, inayobadilisha tukio zima: kama mbwa wanakula makombo chini ya meza, wanalishwa *kwa wakati mmoja* na watoto (na hawahitaji kusubiri, kama maana hiyo inavyothibitishwa na mastari wa 27a). . . . Huku hakuhitaji kuangaliwe kama kuingilia watu wakila chakula [yaani, anaweza kuendelea kubakia ndani ya nyumba na kufundisha wanafunzi wake], kwa kuwa anachoomba siyo mkate wote lakini kipande cha mabaki." (Ibid.: 263) Yesu anasifia imani yake (**Mat 15:28**) na jibu lake (**Mk 7:29**), na kwa mara ya kwanza katika Marko anatoa pepo akiwa mbali.

Kwa kifupi, muingiliano hapa unaonesha Yesu siyo tu ni Masihi wa Kiyahudi, lakini mwokozi wa ulimwengu wote—na Wamataifa hawahitaji kungoja hadi Wayahaudi wapate sehemu yao lakini wanaweza kuanza kupokea sehemu yao kwa wakati mmoja. Ingawa Yesu na Wanafunzi wanaweza kuwa walikwenda maeneo ya Tiro na Sidoni kwa ajili ya kupata faragha, siyo misheni, alikwenda nchi ya Wamataifa na kuingiliwa na mtu wa kwanza anayeelezewa katika Marko kama Mmataifa, na alimtoa yule pepo kutoka kwa binti wa Msirofoinike. Kwa kufanya hivyo, alikuwa anaelezea kile ambacho alikuwa ametokea kukielezea katika **mst. 14-23**, kwamba kama vile vyakula vyote vilivyo safi, kadhalika aina zote za watu. Kusema kweli, tukio hili na mengine mawili yanayofuata, (kuponywa kwa kiziwi kule Dekapoli na kulisha watu 4000) tokea mwanzo Marko aliashiria kuwepo kwa injili kwa Wamataifa; baada ya kufufuka kwake, Yesu anaweka wazi katika vifungu kama vile **Mat 28:18-20** na **Mdo 1:6-8** kwamba hakika, injili imekusudiwa kwa wote—Wayahudi na Wamataifa bila upendeleo.

2. **mst. 31-37—**Yesu amponya mtu kiziwa

Dekapoli ilikuwa ni muungano wa miji kumi ya kigiriki na kirumi iliyoanzishwa (isipokuwa Damaskasi) baada ya kifo cha Alexander Mkuu. "Chini ya utawala wa Kirumi, miji ya Dekapoli haikuwa sehemu ya nchi iliyotawaliwa na ufalme wa Kiherode, nchi zilizorithiwa na majimbo ya Kiherode, au jimbo la Kirumi la Yudea. Badala yake, miji hii ilipewa uhuru wa kisiasa kiasi fulani chini ya ulinzi wa Kirumi. Kila mji ulikuwa kama mji-mkuu, wenye mamlaka juu ya nchi zilizozunguka." ("Decapolis" 2021: "Autonomy under Rome") Miji yote isipokuwa mmoja ilikuwa mashariki ya Mto Yordani. Wakazi wake wengi walikuwa Wamataifa na "kwa sehemu kubwa waliambatana na utawala wa kikoloni katika uasi uliofanywa na jamii ya wazawa" (Overman 1993: 162). Kama inavyooneshwa katika ziara hii katika eneo hili la Tiro na Sidoni, Yesu angeliweza kwenda zake na kutembelea Dekapoli. Kwa kufanya hivyo, alikuwa akiwaendea Wamataifa na kuweka msingi wa misheni kwa Wamataifa ambayo itaanza mara baada ya kufufuka kwake (angalia **Mat 28:18-20; Mdo 1:8**).

Mistari 32 inasema kwamba, pamoja na kuwa kiziwi, mtu huyu alikuwa pia na *"ulemavu wa kipekee"* (baadaye, katika **mst. 37**, watu walimuita "bubu"). Mahali pekee pengine katika Biblia ambako neno la Kigiriki lilitafsiriwa "udhaifu wa kusema" limetumika katika tafsiri ya **Isa 35:6**, ya Biblia Septuagint (LXX) *"Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba;"*[39] Hili lina umuhimu wa kitheoljia na kieskatolojia kwasababu: "Unabii wa kurudi kutoka uhamishoni, na kurudi kwa YHWH Sayuni, hutazama matukio haya kama kurejeshwa kwa uumbaji, kwa kulenga uponyaji wa wagonjwa [mfano, **Isa 35:1-10:** *"Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema ataruka-ruka kama kulungu, na ulimi wake aliye bubu utaimba."*]: . . . Tunaweza kusema kwa kujiamini kwamba Yesu alikusudia 'matendo yake makuu' ya uponyaji yaeleweke kama alama zinazotimiza matarajio haya. . . . Hivyo ilikuwa kwamba, wakati nabii wa kieskatolojia Yohana aliposhangazwa na yale Yesu alikuwa anatenda, na labda kwa yale ambayo hakutenda, Yesu alijibu kwa kuwaamsha wajumbe wa Yohana waone thamani ya alama ya sifa zilizojitokeza (praxis) [yaliyofanyika; vitendo]: 'Nendeni mkamwambie Yohana mnayoyaona: vipofu wanaona, vilema wanatembea, wakoma wanatakaswa na viziwi wanasikia, na wafu wanafufuliwa na maskini wanasikia habari njema. Heri mtu yule asiye kwazwa nami' [**Mat 11:4-6; Lk 7:22-23**, akinukuu kutoka **Isa 35:5** na **61:1**]." (Wright 1996: 428-29) Hivyo, Marko kwa mara nyingine tena anatumia uponyaji huu: (A) Kuonesha kuwa Wayahudi na Wamataifa wako sawa mbele za Mungu; na (B) anamtambulisha Yesu kama Masihi—Mungu aliyekuja duniani kama mtu—ambaye anatimiza unabii wa Isaya, sasa katika nchi ya Wamataifa na

[39] Septuagint ilikuwa ndiyo tafsiri ya Kigiriki ya AK. ilikuwa ikitumika wakati wa Yesu, na Yesu na mitume mara nyingi walinukuu kutoka humo.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

katika nchi ya Israeli pia. Maneno ya mkutano, *"Ametenda mambo yote vema"* (**mst. 37**) ni mwangwi wa *"vema sana"* ya **Mwa 1:31** na ikipambanishwa na tathimini ya Yesu juu ya unafiki wa Mafarisayo, *"Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi"* (**7:6**).

Sehemu nyingine ya uponyaji huu inafaa tuiangalie. Katika **mst. 33** inasema kwamba Yesu alimchukua yule mtu pembeni kutoka katika mkutano faraghani. Hili laweza kuwa ni ili akili zake zisibebwe na vitu vingine lakini pia yule mtu apate kumtazama Yesu kwa akili moja. Yatupasa kukumbuka mkazo wa Yesu kwa yule mtu, na siyo mkutano, mahusiano yetu na mtu mmoja mmoja na makanisa. Hili hasa ni muhimu katika eneo la uinjilishaji na uanafunzi.

MASWALI YA KUJADILI

1. Ni kwa namna gani mpango wa Yesu kuingiliwa na mwanamke Msirofoinike na mtu kiziwi kunaelezea kanuni iliyotajwa na Yesu katika **mst. 14-23** ambako anatamka kwamba vyakula vyote ni safi?

2. Unafikiri kusudi la Yesu lilikuwa nini katika kumwambia mwanamke, *"Acha watoto wale kwanza, kwa kuwa si vema kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa"* (**mst. 27**)?

3. Ni kwa namna gani Yesu alikuwa anamjaribu mwanamke? Yeye aliitikiaje?

- Tunaweza kujifunza nini kutokana na alivyoitikia?
- Kuitikia kwake kunatuonesha sifa gani?

4. Mungu anakujaribu wewe na imani yako?

- Umekuwa ukiitikiaje wakati Mungu alipokujaribu wewe na imani yako?
- Je kuna tofauti kati ya "kujaribiwa wewe" na "kujaribiwa kwa imani yako"?
- Kusudi la Mungu ni nini katika kufanya hivyo?

8:1-10: ***[1] Katika siku zile, kwa vile ulivyokuwa mkuu tena ule mkutano, nao wamekosa kitu cha kula, akawaita wanafunzi wake, akawaambia, [2] Nawahurumia mkutano kwa sababu yapata siku tatu wamekaa nami, wala hawana kitu cha kula; [3] nami nikiwaaga waende zao nyumbani kwao hali wanafunga, watazimia njiani; na baadhi yao wametoka mbali. [4] Wanafunzi wake wakamjibu, Je! Ataweza wapi mtu kuwashibisha hawa mikate hapa nyikani? [5] Akawauliza, Mnayo mikate mingapi? Wakasema, Saba, [6] Akawaagiza mkutano waketi chini; akaitwaa ile mikate saba, akashukuru, akaimega, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; wakawaandikia mkutano. [7] Walikuwa na visamaki vichache; akavibarikia, akasema wawaandikie na hivyo pia. [8] Wakala, wakashiba, wakakusanya mabaki ya vipande vya mikate makanda saba. [9] Na watu waliokula wapata elfu nne. Akawaaga. [10] Mara akapanda chomboni pamoja na wanafunzi wake, akaenda pande za Dalmanutha.***

mst. 1-10—Yesu awalisha 4000

Mfano huu unalingana na ule wa kulisha 5000 katika **Mk 6:33-44**. Baada ya kuponya mtu kiziwi, hakuna dalili kama Yesu ameondoka Dekapoli. Matokeo yake, tunaweza kufikiri kwamba alikuwa angali katika nchi ya Wamataifa. Hili linaweza kuangaliwa, siyo tu kwa kukosekana kwa dalili za Yesu kuondoka Dekapoli, lakini kwasababu zingine zilizoko katika kifungu hiki. Kwanza, Mathayo hahusishi maelezo ya kuponywa kwa kiziwi. Badala yake, baada ya Yesu kukutana na mwanamke Msirofoinike katika maeneo ya Tiro na sidoni, Mathayo anasema, *"[29] Yesu akaondoka huko, akafika kando ya bahari ya Galilaya; akapanda mlimani, akaketi huko. [30] Wakamwendea makutano mengi wakimletea viwete, vipofu, mabubu, vilema, na wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; akawaponya; [31] hata ule mkutano wakastaajabu, walipowaona mabubu wanasema, vilema wanakuwa wazima, viwete wanakwenda, na vipofu wanaona; wakamtukuza Mungu wa Israeli."* (**Mat 15:29-31**) Kwa kuwa Dekapoli ilikuwa mashariki mwa bahari ya Galilaya, maelezo ya Mathayo yanaendana na kuwepo kwa Yesu kule Dekapoli, karibu na bahari ya Galilaya. Kwa nyongeza, Marko na Mathayo wanataja "makutano," na wote wanaeleza makutano kuonesha mshangao wao kuhusu uponyaji aliofanya Yesu. Hakika, maelezo ya Mathayo *"wakamtukuza Mungu wa Israeli."* Lugha hiyo inaonesha kwamba wale waliomtukuza

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

Mungu hawakuwa Wayahudi kutoka Israel, bali walikuwa Wamataifa. Kwa nyongeza, baada ya kulisha wale 400, Marko, anatuambia, *"Mara akapanda chomboni pamoja na wanafunzi wake, akaenda pande za Dalmanutha"* (**8:10**). Maelezo ya Mathayo kuhusu kulishwa 4000 yanahitimisha, *"Akawaaga makutano, akapanda chomboni, akaenda pande za Magadan"* (**Mat 15:39**). "Kutoka katika kurasa hizi mbili inafaa kusema kwamba 'mipaka ya Magadan' na 'sehemu za Dalmanutha' ilikuwa inapakana. Huenda tunaweza kusema kutoka kwa wasimulizi kuwa zilikuwa pwani ya magharibi mwa bahari ya Galilaya. Baada ya kulishwa kwa 4000, Yesu na wanafunzi wake walikuja maeneo haya. Kutokea hapo waliondoka kuelekea upande mwingine' (Mk 8:13), Wanaingia Bethsaida. Kwa ujumla hii inaaminika kuwa ni Bethsaida Julias, Kaskazini mwa bahari." ("Magadan" n.d.: n.p.) Kwa maneno mengine, Yesu alikuwa amelisha Wayahudi 5000 na kisha akavuka kuingia nchi ya Wamataifa; sasa analisha watu 4000 Wamataifa na kuvuka kurudi nchi ya Wayahudi.

Yote haya ni muhimu kwasababu, kama tulivyoona, katika **7:20-23** Yesu alisema kwamba kunajisika siyo kwa nje bali kutokea ndani. Jambo muhimu linalopatikana hapa kuhusu kanuni hiyo ni kwamba watu wote, Wayahudi kwa Wamataifa, ni sawa: wote wamenajisika sawa na wote wanahitaji injili ili kuokolewa. Mara baada ya kutangaza kanuni hiyo, Yesu anathibitisha hilo kwa kuponya Wamataifa wawili nje ya Israeli. Sasa, kulisha kwake watu 4000 kule Dekapoli kunaonesha kitu kile kile, isipokuwa kwamba wakati huu ni kwa kiwango kikubwa, na idadi ya vikapu vya mabaki vilionesha hilo. Vikapu kumi na mbili vya mabaki kutoka kwa watu 5000 kwa hali ya kwaida tunge vilinganisha na makabila kumi na mbili ya Israeli. Hivi saba vya mabaki kutoka kwa watu 4000 ni vya Wamataifa. Kwanini? Kwasababu **Kumb 7:1** inasema kulikuwepo na *"mataifa saba"* katika wakati Israeli walipoingi katika nchi ile! Katika **Yh 6:41-58**, Yesu aliwaambi Wayahudi kwamba alikuwa *"mkate wa uzima."* Sasa, kwa kulisha 4000 katika ardhi ya Wamataifa anaonesha kwamba yeye ni mkate wa uzima kwa watu wote, kila mahali.

Lakini kuna zaidi katika alama za kitheolojia kuliko hayo kwamba, "Vikapu" vilivyojazwa na wale 5000 kwa Kigiriki viliitwa *kophinos*; vile "vikapu" vilivyojazwa na wale 400 ni *spuris.* "*kophinos* vilikuwa vikapu vya kawaida vya Kiyahudi vya safari. . . . Wayahudi walibeba vyakula vyao katika vikapu hivi vya mianzi walipokuwa wakisafiri katika nchi za Wamataifa ili kuepuka unajisi. . . . Vilikuwa na ukubwa mbalimbali, lakini huenda havikuwa vikubwa kama *spurides* (wingi wa *spuris*, vikapu virefu vya mianzi)." (Zodhiates 1993: *kophinos,* 883). *Kophinos* mara nyingi vimetafsiriwa kama "vikapu vya chakula cha mchana" na mara nyingi hutumika kuhusiana na wale 5000; *spuris* mara nyingi hutafsiriwa kama "hamper" (kikapu) na mara zote tafsiri hii imetumika kuhusiana na wale 4000 (Wessel 1984: 690n.19). Tuna ushahidi mzuri wa kibiblia kwamba *spuris* vilikuwa vikubwa zaidi kuliko *kophinos,* kwa kuwa **Mdo 9:25** inatuambia kwamba Paulo aliweza kuepuka njama za kumuua kule Damasca wakati *"wanafunzi wake walipomchukua usiku na kumteremsha kupitia dirisha lililokuwa ukutani, kwa kutumia kikapu [yaani, spuris]."* Hii inaonesha kuwa, ingawa misheni ya Kristo inaweza kuwa ilianza kwa udogo (yaani, mwanamke wa kisirofoinike peke yake aliyepokea "makombo" kutoka chini ya meza), mwishoni Wamataifa wakajaa kupita kiasi na, ukichukulia ukubwa wa vikapu vyao, mavuno ya wamataifa yatakuwa mengi zaidi kuliko ya Wayahudi (kama ambavyo historia imethibitisha hilo). Mwisho, kanisa la kwanza walichukulia namba "saba" kama alama ya utimilifu au ukamilifu. Hivyo, makanisa "saba" [katika kitabu cha Ufunuo] humaanisha kanisa la dunia (Aune 1997: 130; angalia pia Johnson 2001: 14; Schüssler Fiorenza 1991: 53). William Milligan anaongeza, "kila msomaji wa kitabu cha Ufunuo anatambua umoja wa namba unaooneshwa na namba hiyo katika muundo, na kwa kuzingatia ukweli kwamba (isipokuwa kama sura ya xvii. 9 itakuwa tofauti) haikumaanisha hiyo tarakimu peke yake. Ni namba ya umoja katika tofauti. . . . Namba saba —yao—lazima ichukuliwe hivyo kama namba inayowakilisha umoja huo, na makanisa saba yanawakilisha kanisa moja la dunia." (Milligan 1896: 28-29) Kwa maneno mengine, Kwa kutumia vitu vinavyowakilisha na alama, kulishwa kwa 400 kwa vikapu saba vilivyojaa mabaki kunaonesha kuwa Kanisa la Kristo halitakamilika hadi Wamataifa "wamepandikizwa kikamilifu" (angalia **Rum 11:17-24**) kuunda kanisa moja ambako *"hakuna Wayahudi au Wamataifa, hakuna mtumwa au huru, hakuna mwanamme au mwanamke katika Kristo Yesu"* (**Gal 3:28**; angalia pia **Efe 2:13-22; Kol 3:11; Uf 5:9; 7:9**).

MASWALI YA KUJADILI

1. Kwa kuwa Marko tayari ameandika muujiza mmoja wa kulishwa (kulishwa watu 5000 katika **6:33-44**), unafikiri kwanini anahusisha muujiza huu?

- Ni kwa namna gani mtiririko wa simulizi ya Marko inatusaidia kuelewa hilo?

2. Kwanini Yesu alifanya muujiza huu?

- Unatupatia ujumbe gani (au anasemaje) kuhusu yeye mwenyewe na kuhusu wengine?

8:11-21: ***[11] Wakatokea Mafarisayo, wakaanza kuhojiana naye; wakitafuta kwake ishara itokayo mbinguni; wakimjaribu. [12] Akaugua rohoni mwake, akasema, Mbona kizazi hiki chatafuta ishara? Amin, nawaambieni, Hakitapewa ishara kizazi hiki. [13] Akawaacha, akapanda tena chomboni, akaenda zake hata ng'ambo.***
[14] Wakasahau kuchukua mikate, wala chomboni hawana ila mkate mmoja tu.
[15] Akawaagiza, akasema, Angalieni, jihadharini na chachu ya Mafarisayo na chachu ya Herode.
[16] Wakabishana wao kwa wao, kwa kuwa hawana mikate. [17] Naye Yesu akatambua, akawaambia, Mbona mnabishana kwa sababu hamna mikate? Hamfahamu bado, wala hamjaelewa? Je! Mioyo yenu ni mizito?
[18] Mna macho, hamwoni; mna masikio, hamsikii? Wala hamkumbuki? [19] Nilipoivunja ile mikate mitano na kuwapa wale elfu tano, mlichukua vikapu vingapi vimejaa vipande? Wakamwambia, Kumi na viwili. [20] Na ile saba kuwapa wale elfu nne, mlichukua makanda mangapi yamejaa vipande? Wakamwambia, Saba.
[21] Akawaambia, Hamjafahamu bado?

mst. 11-21—Mafarisayo wanataka ishara na wanafunzi hawaelewi

Yesu anapomalizia huduma yake kule Galilaya, akijiandaa kwa safari yake ya mwisho kwenda Yerusalemu, upinzani wa Mafarisayo na kushindwa kuelewa kwa wanafunzi wake kwa mara nyingine tena kunajitokeza.

1. **mst. 11-13—**Mafarisayo wataka ishara

Kejeli katika **mst. 11-13** zinashangaza: Mafarisayo wanabishana na Yesu na kudai *"ishara kutoka mbinguni,"* wakati muda wote, amesimama mbele zao na kuongea nao moja kwa moja akiwa *"mtu aliyetoka mbinguni."* Bila shaka Mafarisayo walikuwa walishasikia miujiza mingi aliyoitenda Yesu, na ndiyo sababu walimfuata. Lakini madai yao hayakuwa na nia njema isipokuwa yalikuwa ya *"kumjaribu"* (**mst. 11**). Tatizo lao lilikuwa hali ya kudhamiria kutokuamini; lilikuwa ni tatizo la utashi, siyo la akili au la kuona kwa macho. Kama Yesu alivyosema katika **Yh 7:17**, *"Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake, atajua habari ya yale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu, au kwamba mimi nanena kwa nafsi yangu tu."* Mafarisayo walikuwa mifano ya (mithali isiyo ya kibiblia), "Hakuna kipofu kama yule ambaye hataona" (angalia pia **Isa 6:9-10; Yer 5:21; Ezek 12:2; Mat 13:13; Mk 4:12**). Maneno, *"Akawaacha"* (**mst 13**) ni moja ya kukataliwa na kuachwa kunakotisha ambako mtu anaweza kufikiri.

Yesu kutumia maneno *"kizazi hiki"* katika **mst. 12**, hasa yakiambatana na kuguna, yanaonesha kwamba anatumia *"kizazi hiki"* kama sifa ya udhaifu, ikimaanisha "kutokuamini, kukataa ubinadamu, kutomuitikia Mungu na kwa vyovyote watakaokabiliana na hukumu yake" (Nelson 1996: 383). Anafanya hivi wakati wote alipokuwa akihutubu mlima wa mizeituni na kungineko (angalia **Mat 12:39-42; 23:36; 24:24; Mk 13:29-30; Lk 11:29-32; 21:31-32**). Neil Nelson anaongeza kwamba, katika hotuba ya mlima wa mizeituni, Mathayo anaonekana kwa makusudi akiweka maneno hayo 'kizazi hiki' sambamba na maelezo kuhusu siku za Nuhu katika 24:37-39 ili kuleta mwangwi wa kizazi kibaya cha gharika (Mwa 7:1 LXX). Kizazi cha gharika ni aina ya 'kizazi hiki' kinachoona ishara za mwisho, kama gharika yenyewe ilivyosimama mahali pa hukumu itakayokuja wakati wa kiama (*parousia)*. 'Kizazi hiki' katika 24:34 inawakilisha kizazi cha muda mrefu cha watu wasioamini, wasioitikia kutoka wakati wa Nuhu hadi mwisho wa nyakati." (Ibid.: 383-84) Kitu kile kile kinatokea hapa.

2. **mst. 14-21**—Wanafunzi hawaelewi

Uzito wa akili, kutokuelewa kwa wanafunzi na hali ya akili kutokuwepo katika sehemu hii vinadhihirika kikamilifu. **Mistari 14** (*"Wakasahau kuchukua mikate, wala chomboni hawana ila mkate mmoja tu."*) hii ni kejeli kubwa: ingawa wanaweza wakawa na mkate mmoja tu halisi, *"mkate wa uzima"* (**Yh 6:35, 48, 51**), ambao si muda mrefu ulikuwa umelisha watu 5000 na 4000 kwa kuzidisha mikate michache iliyokuwepo, ulikuwa umeketi nao kwenye mashua!

Hali yao ya kujisikia hatia kuhusu kutokubeba mikate iliwasababisha wasielewe maneno ya Yesu katika **mst. 15**. Walikuwa wamezama katika dunia yao wenyewe kiasi kwamba hawakuweza kutambua ukweli wa msingi kuhusu Yesu. Tusiwalaumu sana, hata hivyo, hata sisi mara nyingi tunazama katika vidunia vyetu kiasi kwamba tunashindwa kutambua uwepo wa Kristo, uongozi wake na nguvu zake katika maisha yetu.

Matamshi ya Yesu katika **mst. 15** kuhusu *"chachu ya Mafarisayo na chachu ya Herode"* inahusiana na kutokuamini na mafundisho yao. **Mat 16:6** inatumia "Masadukayo" badala ya Herode au Maherode. Chachu mara nyingi inakuwa na maana hasi katika Biblia na humaanisha ushawishi mbaya usioonekana wa mafundisho ya uongo na mitazamo potofu katika maisha. Mafarisayo na Maherode? Masadukayo wanawakilisha pande

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

mbili zisizopatana za upeo mzima wa mafundisho ya uongo. Mafarisayo walikuwa wanadini walioshikilia mapokea na misimamo ya torati, lakini walijali zaidi muonekano wa nje katika kushika *"mapokeo ya wazee"* (**7:3, 5**). Yesu aliwaita "wanafiki" na *"watu wanaoniheshimu kwa midomo yao, lakini mioyo yao iko mbali nami"* (**7:6**). Maherode "walikuwa watu wenye ushawishi ambao walikuwa wafuasi wa himaya ya Maherode," wakivutiwa zaidi na nafasi za kisiasa na kuwa na ushawishi (Hoehner 1992: 325). Masadukayo walikuwa ni wanadini wenye msimamo wa kadiri ambao hawakuamini ufufuo (**Mat 22:23; Mk 12:18; Lk 20:27; Mdo 23:8**). "Maherode kitheolojia walipatana na Masadukayo na kisiasa pande hizi mbili zilikuwa kinyume na Mafarisayo" (Hoehner 1992: 325). Cole anaongeza kwamba Masadukayo "walikuwa na ufahamu, matajiri, watu wa nafasi ya juu kikuhani, na ushawishi wa kidunia ambao ulikuwa hatari sawa tu na misimamo wa taratibu za kidini za Mafarisayo" (Cole 1989: 198). "Chachu" kubwa zaidi ya Mafarisayo, Maherode na Masadukayo ilikuwa kwamba, kwasababu mbalimbali, wote hawakuelewa Yesu ni nani na hivyo hawakumkubali kama Masihi na Mwana wa Mungu. Maonyo ya Yesu kwa wanafunzi wake katika mashua yanafaa hata kwa kanisa la leo. Taratibu za kidini, unafiki, mikazo katika mapokeo badala ya mabadiliko halisi ya mioyo, kujitoa kimsingi kwa ajili ya siasa na uchumi, na upotofu wa kimafundisho mara zote vimekuwa tishio la utakatifu na kanisa kumtazama Yesu kama jamii nzima na Mkristo mmoja mmoja—na inapotokea hivyo, hufunua kwamba hata sisi pia hatujui Yesu ni nani.

Matamko ya Yesu kwa wanafunzi katika **mst. 18**, *"Mna macho, hamwoni; mna masikio, hamsikii?"*ni kama alivyosema katika **4:12-13** kuhusiana na mifano yake na kushindwa kwa wanafunzi kuielewa na kuihusisha na (**Isa 6:9-10; Yer 5:21; Ezek 12:2**). Maswali ya Yesu kwa wanafunzi wake katika **mst. 17-21**, ambayo yanatufaa pia, yanazungumzia matishio haya.

- *"Hamfahamu wala kuelewa?"* (**mst. 17**) ina maana kwamba tunatumia akili zetu. Tunahitaji kuacha na kufikiria kile kilichotokea kwetu binafsi na kama kanisa na kwa nini. Biblia inasemaje kuhusu hali yetu? Wanafunzi walikuwa wanaangalia tu mambo ya kimwili (kusahau mikate) lakini walihitaji *"kugeuzwa kwa kufanywa upya nia zao, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."* (**Rum 12:2**).
- *"Mioyo yenu imekuwa migumu?"* (**mst. 17**) inatutaka tuchunguze hali ya mioyo yetu, yaani, ile sehemu yetu ya ndani kabisa; nafsi yetu halisi. Tunahitaji kuwa wakweli kuhusu kwanini tunafanya tunachofanya. Ukweli unapaswa utushawishi. Kama hatujatenda jambo ambalo tunasema tunaliamini, inaonesha kuwa hatuamini kiuhalisia.
- *"Mna macho hamwoni, na mna masikio lakini hamsikii?"* (**mst. 18**) yalikuwa ni matamshi aliyotumia kwa kurudia rudia alipokuwa akifundisha. Kuna maana ya kina kwa mambo mengi. Chakula alichotoa kwa wale 5000 na wale 4000 kilikuwa ni zaidi ya chakula cha kimwili lakini kilikuwa kinaashiria kuwa wote walikuwa na hitaji kubwa zaidi ambalo ni yeye tu, *"mkate wa uzima,"* anaweza kulitosheleza (aliliweka hili wazi kwa yule mwanamke kisimani katika **Yh 4:9-14**). Kila kitu tunachofanya kitakuwa na matokeo milele. Tunahitaji kuona kiroho zaidi ya kimwili.
- *"Na wala hamkumbuki?"* (**mst. 18**) unatuelekeza katika njia yote ambako Mungu ametenda katika maisha yetu huko nyuma. Hakuna kinachotupata kwa ajali. Anatumia kila kitu tufanane na sura ya Yesu Kristo (angalia **Rum 8:29**). Ukikumbuka ni namna gani alitenda huko nyuma, na uelewe kwamba tu sehemu ya mpango wake mkubwa, inaweza kutupatia kujiamini katika kupokea kutoka kwake kadiri tunavyoendelea na maisha yetu sasa.

Tukitafakari mambo haya sisi sote tunakabiliwa na swali lake la, *"Hamjafahamu bado?"* (**mst. 21**)

MASWALI YA KUJADILI

1. Ombi la kutaka ishara kutoka mbinguni lilikuwaje? (**mst. 11**) siyo uchunguzi wenyewe nia safi ili wapate kuamini, lakini ishara ya mioyo iliyofanywa migumu dhidi ya Mungu?

2. Zipi zilikuwa sifa bayana za (A) Mafarisayo, na (B) Maherode/Masadukayo, ambazo Yesu alikuwa akiwaonya wanafunzi wake? Makundi haya mawili yalikuwa yanafanana kwa jambo gani?

3. Katika **mst. 17-21**, Yesu anauliza wanafunzi wake mfululizo wa maswali, akihitimisha na *"Hamfahamu bado?"*Alikuwa anajaribu kuwasaidia waelewe kitu gani?

4. Katika Yesu kukemea wanafunzi wake (**mst. 17-21**), ananukuu miujiza yake miwili tu ya "kulisha." Miujiza hii miwili iliwapa wanafunzi ujumbe gani (na inatupa sisi ujumbe gani) kuhusu Yesu, maadili yake, na ufalme wake?

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

8:22-26: ***[22] Wakafika Bethsaida, wakamletea kipofu, wakamsihi amguse. [23] Akamshika mkono yule kipofu, akamchukua nje ya kijiji, akamtemea mate ya macho, akamwekea mikono yake, akamwuliza, Waona kitu? [24] Akatazama juu, akasema, Naona watu kama miti, inakwenda. [25] Ndipo akaweka tena mikono yake juu ya macho yake, naye akatazama sana; akawa mzima, akaona vyote waziwazi. [26] Akampeleka nyumbani kwake, akisema, Hata kijijini usiingie.***

mst. 22-26—Yesu amponya kipofu

Hali ya Mafarisayo na wanafunzi ya kutokuona (*"wana macho lakini hawaoni"* **mst. 18**) ilimtengenezea Yesu jukwaa la kumponya huyu mtu kipofu. Tena sisi ambao ndio imani ya wengine (*"wakamletea kipofu, wakamsihi amguse.,"* **mst. 22**). Tunaona tena Yesu akionesha kumjali mtu mmoja kuliko mkutano (*"Akamshika mkono yule kipofu, akamchukua nje ya kijiji, akamtemea mate ya macho, akamwekea mikono yake, akamwuliza, waona kitu,"* **mst. 23**). Kwa mara nyingine tena tunaona Yesu hakutaka kujulikana kwa watu kama mtenda miujiza (*"Akampeleka nyumbani kwake, akisema, Hata kijijini usiingie,'"* **mst. 26**).

Tukio hili ni la aina yake kwasababu ni tukio pekee ambako Yesu anauliza swali wakati wa mchakato wa uponyaji, na uponyaji pekee ambao unafanyika kwa hatua mbili. Kwa kufanya hivi, Yesu anaonesha kuwa nguvu zake haziko kwenye "sanduku," yaani, hakuna "njia moja tu" ya kufanyia mambo. Hapo kuna funzo kwa ajili yetu: mara nyingi huwa tunafikiri kuwa kuna njia moja tu "iliyo sahihi" ya kufanyia mambo,wakati kuna njia malimbali sahihi za kufanyia mambo. Kwa maneno mengine, "tunabatiza" tamaduni zetu wenyewe, au desturi za kanisa letu, au namna ile tuliyojifunza kwamba hiyo ndiyo njia sahihi ya "kufanya mambo". Tunahitaji kutoka katika "masanduku" yetu wenyewe. Pia inaonesha ukweli wa Filipo (**Flp 1:6**): *"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu."*

Katika kiwango kingine, ni mfano wa kuigizwa kwa wanafunzi. Hivyo, haishangazi kwamba kufuatiwa na kutokuelewa na Yesu kuwauliza swali katika **mst. 14-21**. Kipofu hapa ni mwakilishi wa wanafunzi, ambao wana macho lakini hawaoni na masikio lakini hawasikii. Ni kwa taratibu na hatua kwa hatua ndipo wanaweza kuanza kupata uelewa, Yesu ni nani, na program yake inahusu nini. Hivi punde, katika **mst. 29**, Petro atamkiri Yesu kuwa ni Kristo: hata hivyo, hata mpaka hapo haelewi Kristo yupo kwa ajili gani, na Yesu alilazimika kumkemea, *" maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu"* (**mst. 33**). Hata baada ya ufufuo, wanafunzi bado watashindwa kuelewa Yesu na ufalme wake ulihusu nini (angalia **Mdo 1:6-8**). Uponyaji huu pia ni mfano kwetu: *"Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana."* (**1 Kor 13:12**)

Uponyaji huu unatufikisha kwenye hitimisho la sehemu ya kwanza ya kitabu cha Marko ikitarajiwa itafungua macho ya kiroho ya wanafunzi. Ukianzia na **mst. 27** hadi mwisho wa kitabu, mkazo uko katika ufunuo kamili wa Yesu mwenyewe, safari yake kuelekea Yerusalemu, na kifo chake.

MASWALI YA KUJADILI

1. Huu ni uponyaji pekee wenye sehemu mbili. Unafikiri ni kwanini Marko aliandika maelezo haya (siyo kwa namna ulivyoandikwa katika injili zingine)?

- Je muktadha au nafasi katika simulizi ya Marko inakuonesha muunganiko au inakupa dokezo lililopelekea Marko kuandika sehemu hii?

- Tunapata mambo gani ya kujifunza kutoka katika hili?

2. Ni kwa namna gani uponyaji huu ni mfano "ulioigizwa" wa maisha ya wanafunzi wa Yesu? au kwetu?

3. Uponyaji huu hasa unatufikisha mwisho wa nusu ya kwanza ya huduma ya Yesu kama ilivyoandikwa na Marko. Weka kwa mukhtasari mambo makuu tuliyojifunza kuhusu Yesu na ufalme hadi hapa.

BIBLIOGRAFIA

Alexander, T. D. 2008. *FRum Eden to the New Jerusalem: Exploring God's plan for life on earth.* Nottingham, England: InterVarsity.

Andria, Solomon. 2006. "James." In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1509-16. Nairobi: WordAlive.

Anselm of Canterbury. 1903. *Cur Deus Homo.* Translated by Sidney Norton Deane. Chicago: Open Court. Online: http://www.ccel.org/ccel/anselm/basic_works.i.html.

Archer, Gleason. 1982. *Encyclopedia of Bible Difficulties.* Grand Rapids: Zondervan. Online: http://sent2all.com/Archer-Introduction%20to%20Bible%20Difficulties.pdf.

Aune, David. 1997. *Revelation 1-5* (WBC 52A). Dallas: Word.

Barrett, C. K. 1958. *The Holy Spirit and the Gospel Tradition.* London: S.P.C.K.

Bauckham, Richard. 1998. *God Crucified: Monotheism and Christology in the New Testament.* Grand Rapids: Eerdmans.

Beyer, Hermann. 1964. *"Blasphēmeō, Blasphēmia, Blasphēmos."* In *Theological Dictionary of the New Testament,* Vol. 1, ed. Gerhard Kittel, 621-25. Translated by Geoffrey BRumiley. Grand Rapids: Eerdmans.

Blomberg, Craig. 1986. "The Legitimacy and Limits of Harmonization." In *Hermeneutics, Authority and Canon,* eds. D. A. Carson and John Woodbridge, 135-74. Eugene, OR: Wipf & Stock. Online: https://books.google.com/books?id=iVNLAwAAQBAJ&printsec=frontcover&dq=hermeneutics,+authority+and+canon&hl=en&newbks=1&newbks_redir=0&sa=X&ved=2ahUKEwjtg9jAj8zxAhWWaM0KHYiNBXEQ6AEwAHoECAgQAg#v=onepage&q=hermeneutics%2C%20authority%20and%20canon&f=false.

_____. 1990. *Interpreting the Parables.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Bremer, Paul. 1993. "Blasphemy." In *The Oxford Companion to the Bible,* eds. Bruce Metzger andMicahel Coogan, 91-92. New York: Oxford University Press.

Brueggemann, Walter. 1998. *Isaiah 40-66.* Louisville KY: Westminster John Knox.

Burdick, Donald. 1981. "James." In *The Expositor's Bible Commentary,* ed. Frank Gaebelein, 159-205. Grand Rapids: Zondervan.

Burke, Trevor. 2006. *Adopted into God's Family: Exploring a Pauline Metaphor* (NSBT 22). Nottingham, England: Apollos.

Carson, D. A. 1982. "Jesus and the Sabbath in the Four Gospels." In *FRum Sabbath to Lord's Day: A Biblical, Historical and Theological Investigation,* ed. D. A. Carson, 57-97. Grand Rapids, MI: Zondervan.

Carson, D. A., and Douglas Moo. 2005. *An Introduction to the New Testament,* 2nd ed. Grand Rapids: Zondervan.

Carter, John. 2003. "A Perspective on the Distinctiveness of Mrk's Gospel." *American Journal of Biblical Theology* 4: 1-18. Online: https://citeseerx.ist.psu.edu/viewdoc/download?doi=10.1.1.454.9875&rep=rep1&type=pdf.

Cheney, Johnston. 1969. *The Life of Christ in Stereo.* Portland, OR: Multnomah.

Cole, R. Alan. 1989. *Mrk,* rev. ed. (TNTC). Grand Rapids: Intervarsity.

Cole, Victor. 2006. Mrk." In In *Africa Bible Commentary,* ed. Tokunboh Adeyemo, 1171-1202. Nairobi: Word Alive.

Cox, Jenny. 2013. "Parallels between the death of John the Baptist and the Death of Jesus." Online: http://cross-connect.net.au/parallels-between-the-death-of-john-the-baptist-and-the-death-of-jesus/.

Cranfield, C. E. B. 1972. *The Gospel AcKording to Saint Mrk* (CGTC) rev. ed. London: Cambridge University Press.

Danker, Frederick, ed. 2000. *A Greek-English Lexicon of the New Testament and Other Early Christian Literature.* Chicago: The University of Chicago Press.

Davids, Peter. 1982. *The Epistle of James* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

"Decapolis." 2021. *Wikipedia.* Online: https://en.wikipedia.org/wiki/Decapolis.

Deffinbaugh, Robert. Not dated. "26. A Crucial Change of Course (Mrk 3:1-4:25)." Online: https://bible.org/seriespage/crucial-change-course-Mrk-318211425.

Hakimiliki © na Jonathan Menn 2021. Haki zote zimehifadhiwa.

Dennison, James. 1994. “The Gospel of Mrk fRum Beginning to End.” *Kerux* 9. Online: https://www.kerux.com/doc/0903A1.asp.

The Didache. 1989. In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 145-58. Grand Rapids: Baker. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.xii.html.

Eusebius Pamphilus. 1890. *Ecclesiastical History.* Grand rapids: Eerdmans. Online: https://ccel.org/ccel/schaff/npnf201/npnf201.i.html.

Gibson, Jeffrey. Not dated. “The Scribal Charge of Demonic Kollusion in Mk 3:22: Honest Asssessment or Calculated Calumny?” Online: http://www.ibiblio.org/GMrk/afr/MK322.htm.

Goldsworthy, Graeme. 1991. *AcKording to Plan: The Unfolding Revelation of God in the Bible.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Goppelt, Leonhard. 1982. *Typos: The Typological Interpretation of the Old Testament in the New.* Translated by Donald Madvig. Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Gruenler, Royce. 1989. “Mrk.” In Evangelical Commentary on the Bible, ed. Walter Elwell, 761-98. Grand Rapids: Baker.

Grundmann, Walter. 1964. *“Hamartanō, hamrtēma, hamartia.”* In *Theological Dictionary of the New Testament,* Vol. 1, ed. Gerhard Kittel, 267-316. Translated by Geoffrey BRumiley. Grand Rapids: Eerdmans.

Gundry, Robert. 1993. *Mrk: A Commentary on His Apology for the Cross.* Grand Rapids: Eerdmans.

Guelich, R. A. 1992. “Mrk, Gospel of.” In *Dictionary of Jesus and the Gospels,* edited by Joel Green, Scot McKnight, and I. Howard Marshall, 512-25. Downers Grove, IL: InterVarsity.

Faro, Ingrid. 2021. *Evil in Genesis.* Bellingham, WA: Lexham.

France, R. T. 1975. “Old Testament Prophecy and the Future of Israel: A Study of the Teaching of Jesus.” *Tyndale Bulletin* 26:53-78. Online: http://www.tyndale.cam.ac.uk/index.php?page=frame&add=http://www.tyndalehouse.com/TynBul/Library/00_TyndaleBulletin_ByAuthor.htm.

_____. 2002. *The Gospel of Mrk* (NIGTC). Grand Rapids: Eerdmans.

Guelich, Robert. 1989. *Mrk 1-8:26* (WBC 34). Dallas: Word.

Hoehner, Harold. 1992. “Herodian Dynasty.” In *Dictionary of Jesus and the Gospels,* eds. Joel Green, Scot McKnight, I Howard Marshall, 317-26. Downers Grove, IL: InterVarsity.

Hoekema, Anthony. 1979. *The Bible and the Future.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Jesus Film Project. 1995-2021. “What Did Jesus Mean about Putting New Wine in New Wineskins?” Online: https://www.jesusfilm.org/blog-and-stories/what-did-jesus-mean-putting-new-wine-new-wineskins.html.

Johnson, Dennis. 2001. *Triumph of the Lamb: A Commentary on Revelation.* Phillipsburg, NJ: P&R.

“Jose O’Callaghan Martinez.” 2021. *Wikipedia.* Online: https://en.wikipedia.org/wiki/Jos%C3%A9_O%27Callaghan_Mart%C3%ADnez.

Keller, Timothy. 2008. *The Reason for God: Belief in an Age of Skepticism.* New York: Dutton.

_____. Not dated. “The Gospel—Key to Change.” Online: https://www.cru.org/content/dam/cru/legacy/2013/01/Gospel_KeytoChange_TimKeller.pdf.

_____. Not dated. “The Two Prodigal Sons: Reading & Reflection.” Online: https://static1.squarespace.com/static/530e4ef9e4b07ec5e7d89c14/t/57110d6a2b8ddec14befd7b2/1460735338885/The+Two+Prodigal+Sons-+Reading+%26+Reflection+-+by+Tim+Keller.pdf.

Ladd, George Eldon. 1959. *The Gospel of the Kingdom.* Grand Rapids: Eerdmans.

Lane, William. 1974. *The Gospel AcKording to Mrk* (NICNT). Grand Rapids: Eerdmans.

Lewis, C. S. 1946. *The Great Divorce.* London: Geoffrey Bles. Online (a different edition): https://archive.org/details/ebook-lewis-c-s-the-great-divorce/page/n3/mode/2up.

_____. 1961. *The Screwtape Letters.* New York: MacMillan. Online (a different edition): http://www.samizdat.qc.ca/arts/lit/PDFs/ScrewtapeLetters_CSL.pdf.

_____. 1996 (reprint). *Mere Christianity.* New York: Touchstone. Online: http://christiangrads.org/wp-content/uploads/2012/08/Mere-Christianity-The-Book.pdf.

"Magadan." Not dated. *BibleHub: Encyclopedia.* Online: https://bibleatlas.org/magadan.htm.

Marshall, I. Howard. 1978. *The Gospel of Luke* (NIGTC). Grand Rapids, MI: Eerdmans.

McBirnie, William. 1973. *The Search for the Twelve Apostles.* Wheaton, IL: Living Books.

Menn, Jonathan. 2016. *Biblical Stewardship.* Online: https://www.eclea.net/courses.html#stewardship.

_____. 2017b. *The Church: Its Nature, Mission, and Purpose.* Online: https://www.eclea.net/courses.html#church.

_____. 2020. *Christianity and Islam: The Essentials.* Online: https://www.eclea.net/courses.html#islam.

_____. 2021. *Biblical Theology.* Online: https://www.eclea.net/courses.html#theology.

Milligan, William. 1896. *The Book of Revelation.* New York: Armstrong. Online: https://books.google.com/books?id=98DYAAAAMAAJ.

Moo, Douglas. 1984. "Jesus and the Authority of the Mosaic Law." *Journal for the Study of the New Testament* 20: 3-49. Online: www.djmoo.com/articles/jesusandauthority.pdf.

_____. 1985. *James* (TNTC). Grand Rapids: Eerdmans.

_____. 1989. "James." In *Evangelical Commentary on the Bible,* ed. Walter Elwell, 1150-62. Grand Rapids: Baker.

Nehls, Gerhard, and Walter Eric. 2010. *Trainer's Textbook 2: Christian-Islamic Controversy.* Nairobi: Life Challenge Africa. Online:http://answering-islam.org/Nehls/tt2.pdf.

Nelson, Neil. 1996. "'This Generation in Matt 24:34: A Literary Critical Perspective." *Journal of the Evangelical Theological Society* 38: 369-85. Online: http://www.etsjets.org/files/JETS-PDFs/38/38-3/JETS_38-3_Nelson_369-386.pdf.

Neusner, Jacob. 1988. *The Mishnah: A New Translation.* New Haven: Yale University Press.

Osborne, Grant. 1991. *The Hermeneutical Spiral.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Overman, J. Andrew. 1993. "Decapolis." In *The Oxford Companion to the Bible,* eds. Bruce Metzger and Michael Coogan, 161-62. New York: Oxford University Press.

Pippert, Rebecca. 1979. *Out of the Saltshaker and into the World.* Downers Grove, IL: InterVarsity.

Powell, Frank. 1954. *The Trial of Jesus Christ.* Grand Rapids: Eerdmans.

Powell, Mrk. 2007. "Echoes of Jonah in the New Testament." *World & Word* 27: 157-64. Online: http://wordandworld.luthersem.edu/issues.aspx?article_id=979.

Poythress, Vern. 1991. *The Shadow of Christ in the Law of Moses.* Brentwood, TN: Wolgemuth & Hyatt. Online: http://frame-poythress.org/ebooks/the-shadow-of-christ-in-the-law-of-moses/.

Price, David. 2018. "Holy Hebrew Arithmetic: What Age was Jesus when he became Teacher-Priest?" *The Jerusalem Post.* Online: https://www.jpost.com/blogs/truth-beyond-price/holy-hebrew-arithmetic-what-age-was-jesus-when-he-

became-teacher-priest-542343.

Robertson, Archibald. 1930. *Word Pictures in the New Testament,* vol. 1. New York: Harper & Brothers.

Schreiner, Thomas. 1989. “Luke.” In *Evangelical Commentary on the Bible,* ed. Walter Ewell, 799-839. Grand Rapids: Baker.

Schüssler Fiorenza, Elisabeth. 1991. *Revelation: Vision of a Just World* (PC). Minneapolis: Fortress, 1991.

The Shepherd of Hermas. 1989. In *The Apostolic Fathers*, 2nd ed., edited and revised by Michael Holmes, translated by J. B. Lightfoot and J. R. Harmer, 194–290. Grand Rapids: Baker. Online (another edition): http://www.ccel.org/ccel/lightfoot/fathers.ii.xiv.html.

Sidebotham, Bruce. 2002. “New Paradigm for Outreach to Middle Eastern Cultures: Gospel Restores Honor to the Dishonored.” *The Operation Reveille Shofar* 6:1 (First Quarter): 4-5. Online: http://oprev.sidebotham.net/wp-content/back_issues/ShofarPDFs/1stQtr02.pdf.

Smith, William. 2004. “The Sin That Won’t Go Away.” Online: https://banneroftruth.org/us/resources/articles/2004/the-sin-that-wont-go-away/.

Spencer, Michael. 2008. “The Baptism.” Online: https://jesusshaped.wordpress.com/2008/11/21/gospel-of-Mrk-study-4-the-baptism/.

_____. 2008. “The Forerunner.” Online: https://jesusshaped.wordpress.com/2008/11/09/gospel-of-Mrk-study-3-the-forerunner/.

_____. 2008. “The Temptation.” Online: https://jesusshaped.wordpress.com/2008/12/01/gospel-of-Mrk-study-5-the-temptation/.

_____. 2009. “The Calling.” Online: https://jesusshaped.wordpress.com/2009/01/07/gospel-of-Mrk-study-8-the-calling/.

_____. 2020. “Reconsider Jesus – The Bridegroom and the New Wine.” Online: https://imonk.blog/2020/11/09/reconsider-jesus-the-bridegroom-and-the-new-wine-Mrk-218-22/#footnote22.

_____. “Reconsider Jesus – Calling the Tax Kollector.” Online: https://imonk.blog/2020/10/30/reconsider-jesus-calling-the-tax-Kollector-Mrk-213-17/.

_____. 2020. “Reconsider Jesus – The Forgiver of Sins.” Online: https://imonk.blog/2020/10/23/reconsider-jesus-the-forgiver-of-sins-Mrk-21-12/.

_____. 2020. “Reconsider Jesus – The Healer.” Online: https://imonk.blog/2020/10/19/reconsider-jesus-the-healer-Mrk-129-45/.

_____. 2020. “Reconsider Jesus – The Response.” Online: https://imonk.blog/2020/09/21/reconsider-jesus-the-response-Mrk-114-15/.

_____. 2020. “Reconsider Jesus – The Teacher.” Online: https://imonk.blog/2020/10/05/reconsider-jesus-the-teacher-Mrk-121-28/.

Sproul, R. C. 2002. *Saved fRum What?* Wheaton, IL: Crossway.

_____. 2021. “New Wine for New Wineskins.” Online https://www.ligonier.org/learn/devotionals/new-wine-new-wineskins/.

Stanton, Gerald. 1951. “The Prophet Jonah and His Message [part 1].” *Bibliotheca Sacra* 108: 237-49.

Stoops, Robert. 1993. “Baal-zebub.” In *The Oxford Companion to the Bible,* eds. Bruce Metzger and Michael Coogan, 70. New York: Oxford University Press.

Stott, John. 1986. *The Cross of Christ.* Downers Grove: InterVarsity. Online: https://korycapps.files.wordpress.com/2012/11/j-stott-cross-of-christ.pdf.

Tasker, R. V. G. 1982. *The General Epistle of James* (TNTC). Grand Rapids: Eerdmans.

Thompson, Marianne. 1999. "Committing the Unforgivable DSin." *Christianity Today* (June 14): 82.

Vander Laan, Ray, and Judith Mrkham. 1996. *Echoes of His Presence.* Kolorado Springs: Focus on the Family.

Van Iersel, B. M. F. 1980. "The gospel acKording to st. Mrk – written for a persecuted community?" *Nederlands Theologisch Tijdschrift* 34: 15-36.

Venema, Kornelis. 2000. *The PRumise of the Future.* Carlisle, PA: Banner of Truth.

Viljoen, Francois. 2014. "Jesus healing the leper and the Purity Law in the Gospel of Matthew." *In die Skiflig* 48: 1-7. Online: http://www.scielo.org.za/pdf/ids/v48n2/04.pdf.

Vos, Geerhardus. 1979 (reprint). *The Pauline Eschatology.* Grand Rapids, MI: Baker.

Walker, P. W. L. 1996. *Jesus and the Holy City: New Testament Perspectives on Jerusalem.* Grand Rapids, MI: Eerdmans.

Wallis, Arthur. 1968. *God's Chosen Fast.* Fort Washington, PA: Christian Literature Crusade.

Watts, Rikk. 1997. *Isaiah's New Exodus in Mrk.* Grand Rapids: Baker Academic.

_____. 2007. "Mrk." In *Commentary on the New Testament Use of the Old Testament,* eds. G. K. Beale and D. A. Carson, 111-249. Grand Rapids: Baker Academic.

Wax, Trevin. 2013. "Why did Jesus say he came only for Israel?" *The Gospel Coalition*. Online: http://www.thegospelcoalition.org/blogs/trevinwax/2013/01/28/why-did-jesus-say-he-came-only-for-israel/.

Wessel, Walter. 1984. "Mrk." In *Expositor's Bible Commentary, vol. 8,* edited by Frank Gaebelein, 603-793. Grand Rapids: Zondervan.

Wilckens, Ulrich. 1972. *"Úpokrinomai, sunupokrinomai, úpokrisis, úpokritēs, anutokritos."* In *Theological Dictionary of the New Testament,* Vol. VIII, ed. Gerhard Friedrich, 559-71. Translated by Geoffrey BRumiley. Grand Rapids: Eerdmans.

Wright. N. T. 1996. *Jesus and the Victory of God.* Minneapolis, MN: Fortress.

Wuest, Kenneth. 1973. *Wuest's Word Studies fRum the Greek New Testament,* vol. 1. Grand Rapids: Eerdmans.

Zodhiates, Spiros, ed. 1993. *The Complete Word Study Dictionary: New Testament,* rev. ed. Chattanooga, TN: AMG.

MWANDISHI

Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada yake ya B.A. ya heshima ya sayansi ya siasa kutoka katika chuo cha Wisconsin-Madison, mwaka 1974, na baadaye alijumuika na Phi Beta Kappa kwa kuwa na heshima ya kijamii. Tena akapata J.D. kutoka kwa Shule ya Uanasheria cha Cornell, magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akawekwa kwenye mamlaka ya Kisheria ya Coif haki za heshima ya jamii. Akaitumia miaka iliyofuata 28 akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye akashirikiana na Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Alikuwa muumini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Kukua kwa pendo lake katika Thiolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu katika chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Kati ya 2007-2013 alikuwa Mkurugenzi wa Afrika ya Mashariki wa Equipping Pastors International. Sasa Jonathan ni Mkurugenzi wa huduma ya Equipping Church Leaders-East Africa (**www.eclea.net**). Vitabu vyake mbalimbali vya mafundisho ya biblia vinapatikana katika tovuti ya huduma **www.eclea.net**. Unaweza kuwasiliana na Jonathan kwa anuwani hii ya baruapepe: **jonathanmenn@yahoo.com**.